

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

## BUNGE LA TANZANIA

### MAJADILIANO YA BUNGE

#### MKUTANO WA SITA

Kikao cha Nane – Tarehe 9 Februari, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

#### D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kawaida yetu siku ya Alhamis huwa na kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, kwa siku ya leo kipindi hiki hakipo kwa sababu Waziri Mkuu yupo safarini Dar es Salaam na badala yake Mheshimiwa Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ndiyo anashikilia nafasi ile ya kushikilia nafasi ya Kusimamia Shughuli za Serikali Bungeni.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliondoka jana kwa madhumuni ya kwenda kushughulikia mgogoro unaoendelea wa Madaktari. Lakini mtakumbuka pia kwamba karibu toka tuanze Bunge hili wenzetu kadha wa kadha Wabunge hapa walikuwa wanatumia kifungu cha 47 cha Kanuni zetu ili tuweze kujadili suala la mgogoro huu kama ni suala la dharura. Tangu mwanzo tulipoanza walipoanza kuomba hivyo mimi nilikuwa nawaeleza kwamba kwanza tulikuwa na kauli ya Serikali, halafu baadaye nikasema kwamba Kamati yetu ya Huduma za Jamii tumeituma kwenda kufuatilia hili suala. Kwanza kupokea taarifa ya Kauli ya Serikali na kwenda kufuatilia haya mambo.

Kwa hiyo, hata juzi wakati Mheshimiwa Serukamba alipoomba tujadili vilevile Naibu Spika alisema hapa kwamba wenzetu bado walikuwa hawajarudi kutoka kule tulikowatuma kufanya kazi.

Kamati yetu imefanya kazi kwa muda mfupi lakini umefanya kazi kubwa sana na kwa sababu ya udharura yenyewe ilibidi tutumie Kamati ya Uongozi kuipokea Taarifa ile maana na wenyewe wamefika usiku ilibidi tutumie namna yoyote ile ili waweze kufika na kuitolea taarifa Kamati ya Uongozi yale waliyoyaona hata kabla hawajandika taarifa yao yote. Kamati ya Uongozi pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii tumefanya shughuli ya kujadili taarifa hiyo tukiwa tumepata maelezo ya wenzetu waliofika kule, wameongea na Madaktari, wamekagua Hospitali ya Muhimbili, wameongea na watu mbalimbali na wakapata undani wa hali halisi. Kwa hiyo, ushauri wao tumejadili jana usiku mpaka tumemaliza kikao kama saa sita ya usiku. Baada ya saa sita za usiku kwa sababu mambo yenyewe yalikuwa ni haraka wakanituma utafute viongozi wakuu wengine, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu waliko jana usiku.

Kwa hiyo, tumeongea na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wote wanakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na kwamba mpaka sasa hivi hayupo kwa sababu Kamati ilichokuwa inaomba ni kwamba kwanza tuombe kwa dhati kabisa na Bunge hili tunaomba Madaktari warudi kwenye *stations* zao. Mawasiliano mabaya yaliyokuwepo kati ya wao na Wizara yatachukuliwa hatua leo na madai yao mengine ambayo kwa kweli ni ya dharura na ya haraka Serikali ipo huko na Mheshimiwa Waziri Mkuu anaongea nao hivi sasa. Kwa hiyo, naamini kabisa kwa uzalendo walionao Madaktari na uzalendo tunaomba uwepo naamini siku ya leo majibu yatapatikana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo suala hili si dogo limegusa maisha ya watu wetu kufa, sio kugusa tu kufa na wenzetu waliokwenda kwenye Hospitali ya Muhimbili wanasema unalia machozi badala ya kufanya kitu chochote. Kwa hiyo, tusilifanye kama jambo la ushabiki tu. Tuombe leo Serikali ichukue hatua zinazostahili Madaktari warudi kazini.

Kwa hiyo, naomba katika matatizo mazito lazima tuwe na uvumilivu, tuwe na utaratibu na tuwe na uzalendo sisi wenyewe tusifanye kitu cha kisiasa hapa haitusaidii na wenzetu Waandishi wa Habari katika suala hili pia tuwe nao tusichochee ugomvi kati ya watu na watu. Magazeti, Wabunge, Viongozi wa Dini na wananchi wote tuombe Madaktari warudi na mambo yao mengine yatafanyika wanayodai. (Makofi)

Kumbe kulikuwa na utaratibu walitakiwa watumie, kuna chombo cha Serikali kabisa kinaitwa CMA ambacho kinafanya kazi ya kusikiliza kama kuna migogoro halafu watu wanaendelea. Kwa hiyo, vyombo vyote vitatumika. Kwa hiyo, Waziri Mkuu yupo huko kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, tusibiri mchana huu tutapata maelezo yanayostahili na Madaktari pengine watakuwa wamerudi. Nashukuru sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu.

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

#### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):**

Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Usimamizi wa Matengenezo ya Magari ya Serikali (*The Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Management of the Government Vehicles Management*).

Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Usimamizi wa Usambazi wa Maji Mijini (*The Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Management of Water Distribution in Urban Areas*).

Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Usimamizi wa Mapato yanayotokana na Uvunaji wa Misitu (*The Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Management of Forest Harvesting*).

Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Usimamizi wa Mapato yanayokusanywa na Wakala katika Halmashauri (*The Report of the Controller and Auditor General on Performance Audit on the Management of Outsourced Revenue Collection Functions by the Local Government Authority in Tanzania*).

Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Ukaguzi Maalum Uliofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 96

#### **Halmashauri Zinazozalisha Chakula kwa Wingi Kuongezewa Fedha**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Barabara nyingi katika maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi zikiwemo Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma sio nzuri na Bajeti inayotengwa ni ndogo sana:-

Je, kwa nini Halmashauri zinazozalisha mahindi kwa wingi zisiongezewe fedha za barabara ili kuzinusuru barabara hizo za vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa matengenezo na ukarabati wa mtandao wa barabara zilizo chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini ikiwemo zile zinazopita katika maeneo yanayozalisha chakula mkoani Ruvuma. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hizo Serikali kupitia Mfuko wa Barabara imekuwa ikitoa fedha za matengenezo kwa mtandao wa barabara za Halmashauri nchini mwaka hadi mwaka.

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara ilitoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 84.5 kwa matengenezo ya mtandao wa barabara za Halmashauri zenye urefu wa Km. 28,849. Kwa mwaka 2011/2012 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 94 kwa matengenezo ya mtandao wa barabara za Halmashauri zenye urefu wa KM. 28,939 ikiwa ni ongezeko la fedha za matengenezo kwa asilimia kumi na moja (11%).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mkoa wa Ruvuma pekee ulipatiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.012 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zenye urefu wa KM.1274 pamoja na madaraja. Kwa mwaka 2011/2012 Halmashauri katika Mkoa wa Ruvuma zilizopatiwa fedha za matengenezo ya barabara kiasi cha shilingi bilioni 3.565 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa KM.1,127 pamoja na madaraja na makalvati. Hii ni sawa na ongezeko la fedha kiasi cha asilimia kumi na nane (18%). Serikali itaendelea kutoa fedha za matengenezo ya barabara za Halmashauri ikiwamo zile zinazozalisha mahindi kwa wingi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini ni ukweli usipingika nchi hii na taifa kwa ujumla inafahamu Mkoa wa Ruvuma hususan Halmashauri ya Wilaya ya Songea Jimbo la Peramiho limekuwa likipata mvua nyingi na hivyo kusaidia kuzalisha chakula kwa wingi na kuhudumia nchi nzima; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba TAMISEMI huwa inatenga fedha Mfuko wa Dharura wa kuongeza Bajeti ya kusaidia matengenezo ya barabara za nchi nzima katika Halmashauri.

Je, kwa kigezo hicho nilichokisema cha umuhimu wa Mkoa wa Ruvuma kuzalisha chakula na kulisha Watanzania wote haoni kuwa kuna haja kubwa ya kutumia fedha hizo kuziongeza Halmashauri hizo ili ziwe na barabara nzuri kama motisha ya kuendelea kuzalisha chakula na kuwalisha Watanzania wote?

Mheshimiwa Rais wakati alipokuwa anafungua Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji aliahidi kabisa barabara ya kutoka Songea kupitia Matomondo kwenda mpaka Mkenda itajengwa kwa kiwango cha lami na upembuzi yakiniifu umeshafanyika na umeshakamilika. Je, Serikali sasa inaniambia nini? Inaanza kutenga Bajeti ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais na ahadi ya Rais ni agizo kwa Serikali yake? (Makofi)

**SPIKA:** Waziri wa Ujenzi majibu. Ni barabara tu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba tunatambua umuhimu wa kuongeza fedha zinazotokana na Mfuko wa *Road Fund* ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 1998 *Amendment* namba mbili katika maeneo ambayo yanazalisha mazao ya kilimo kwa wingi ikiwemo Ruvuma, Iringa na sehemu zingine.

Lakini kwa taarifa yako tu ambayo kwa kazi nzuri zilizofanywa na Bunge katika Bunge lililopita la kupunguza uchakachaji wa mafuta ya taa na kupitisha Sheria iliyokuwa nzuri ambayo imesaidia kuongeza Mfuko wa Mapato ya *Road Fund*.

Katika mwaka huu zilikuwa zinategemewa zingekusanywa bilioni 316 lakini kwa sasa hivi mategemeo katika mwaka huu zitakusanywa zaidi ya bilioni 400.

Katika *quarter* ya kwanza tulitegemea tukusanye bilioni 78, zimekusanywa bilioni 105; na katika *quarter* ya pili tulitegemea tukusanye bilioni 78.8 tumekusanya bilioni 107.

Kwa hiyo, pana uwezekano patakuwepo na ongezeko la bilioni 90 katika Mfuko wa Barabara na fedha hizi napenda kumhakikishia Mheshimiwa Jenista Mhagama, tutawaelekeza Bodi ya Mfuko wa Barabara inayoongozwa na Mheshimiwa James Wanyancha, fedha zingine zipelekwe kwenye Halmashauri zote katika nchi hii, zikiwemo Halmashauri za Peramiho na Songea na maeneo mengine wanayolima mazao kwa wingi ili ziweze kufanya kazi kikamilifu kulingana na matatizo yaliyopo kule. (*Makofi*)

Kuhusu swali la pili, kazi zimefanyika za upembuzi yakinifu. Katika kazi ya barabara yoyote huwa tunaanza na upembuzi yakinifu, tunakuja na *details design*, baadaye tunakuja na *Construction*.

Baada ya upembuzi yakanifu na *details design* kukamilika tutaendelea kuzingatia ahadi ambayo imetolewa na Rais kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa bahati nzuri kwa sasa hivi *flow* ya fedha imeanza kuwa inakwenda vizuri na kuna miradi mingi kwa sasa hivi yenye thamani ya trilioni 3.88 ambayo inategemewa kuwekewa mawe ya msingi na kufunguliwa katika nchi nzima. (*Makofi*)

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa kwa nyakati tofauti Wabunge na wadau mbalimbali wameishauri Serikali kuhusu kuundwa kwa Wakala wa Barabara Vijijini ili kuboresha maendeleo ya barabara vijijini na Serikali kukubali hayo maoni na mapendekezo.

Kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba itashirikisha TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi ili kuunda huo Wakala. Je, ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa hivi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa *agency* yoyote iko chini ya wajibu wa Sheria namba 30 ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake. Ni matumaini yangu mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge yatajadiliwa ndani ya Serikali kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ili kuona kama kweli kuna uwezekano wa kuanzisha *agency* itakayokuwa inahusika na barabara katika barabara za Halmashauri.

Hili tutaendelea kulijadili lakini *agency* ya barabara ambayo iko chini ya *TANROAD* nayo imeanzishwa kwa Sheria hizo hizo ambayo inahusika kwa Barabara Kuu pamoja na Barabara za Mikoa ambazo ni zaidi ya kilomita 35,000 katika nchi nzima.

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Spika, tafiti mbili zimeonyesha kwamba moja ya tatizo kubwa linalosababisha nchi yetu kutokuondoa umaskini ni miundombinu ya vijijini. Utafiti uliofanywa kati ya Serikali na Serikali ya Marekani, *diagnostic survey* na hata *Report ya Human Development Report* ya mwaka huu inaonyesha hivyo pia.

Wazo la kuanzishwa kwa *Rural Roads Agency* lilitolewa wakati tunatunga Sheria ya Barabara. *Roads Act* ya mwaka 2007. Napenda kurejea swali la Mheshimiwa Mahenge, Serikali imefikia wapi utekelezaji wa pendekezo hili.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika uundwaji wa Sheria au kuanzishwa kwa *agency* yoyote katika nchi hii unasimamiwa chini ya Sheria namba 30 ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake. Serikali inalipitia hili na ndiyo maana katika *agency* nyingi ambazo

zimeshaanzishwa katika nchi hii zipo, kuna TANROAD imeshaanzishwa agency, kuna TEMESA, TBA na agency nyingine katika Wizara mbalimbali.

Nina uhakika wenzetu wa TAMISEMI wanaendelea kuliangalia hili ili kuona ni kwa namna gani tutaweza kuanzisha agency ambayo itakuwa inahusika na barabara za vijijini ambazo ni zaidi ya kilometa 52,000 katika nchi nzima.

Katika hili tunaendelea kushirikiana na Norwegian Road Agency ambao walikuwa wako mbele sana katika kutusaidia namna ya kuanzisha agency za barabara ni kitu kigumu ambacho kinahitaji utafiti wa kutosha kinahitaji pia mipango thabiti ya ku-deal na masuala haya ya barabara yanayohusu vijiji vyote na katika Wilaya zote.

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Zitto aendeleo kuipa nafasi Serikali ili iendeleo kulishughulikia hili suala ambalo ni zito na umuhimu wake huwezi ukalipeleka haraka haraka kama kupika chakula cha mchicha ambacho kinaweza kikaiva haraka haraka. Nataka kumhakikishia ndani ya miaka mitano mambo yakienda vizuri agency itakayokuwa ina-deal na barabara za Halmashauri katika Halmashauri zote nchini inaweza ikawa imeshaundwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, unajua vitu vikubwa namna hii nyie huwa mnasema mengi mengi na Hansard zimejaa. Hoja Binafsi ndiyo zinakuja kwa mambo makubwa kama hayo. Sasa ukishaleta Hoja Binafsi ni kwamba lile swali umetoa katika maneno yote mnayosema hili mnasema tunataka attention.

Sasa nyie mkizungumza mlisema, mlisema, so what? Hoja ndiyo ina single out kwa maneno yenu yote mliyosema sasa tunataka hili litekelezwe. Tunaendelea na swali linalofuata atauliza Mheshimiwa George Simbachawene.

Na. 97

#### **Kuharibika kwa Miradi ya Visima Vifupi/Virefu Mpwapwa**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Miradi ya visima vifupi na virefu iliyotekelezwa kati ya mwaka 2000 hadi mwaka 2010 katika Wilaya ya Mpwapwa karibu yote imeharibika na haifanyi kazi kwa muda mfupi tu tangu ilipokamilika:-

Je, nini chanzo cha tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi mwaka 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitokeleza miradi mbalimbali ya maji ya visima virefu 9, visima vifupi 86, miradi ya maji ya mtiririko, chemchem 3 na skimu za uvunaji maji mvua 15. Kati ya visima virefu 9 vilivyokamilishwa, visima 2 havifanyi kazi. Kati ya visima vifupi 86 vilivyochimbwa, 9 havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, sababu za miradi hiyo kutofanya kazi ni uchangiaji mdogo wa wananchi katika gharama za uendeshaji hivyo kusababisha kukosekana kwa fedha za ukarabati hasa pale panapotokea uharibifu au uchakavu wa miundombinu ya maji. Hali hii imesababisha miradi mingi kutokuwa endelevu na usimamizi usioridhisha kupitia Kamati za Maji za Vijiji na kusababisha miradi hiyo kutokidhi matarajio ya kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, lipo tatizo la uharibifu wa mazingira hasa katika vyanzo vya maji hali inayosababisha upatikanaji wa maji katika maeneo hayo kutokuwa ya uhakika kutokana na ukame. Ni kutokana na sababu hizo,

jenereta iliyokuwa inatumika kusukuma pampu ya maji iliharibika na haikufanyiwa matengenezo katika Kijiji cha Ving'hale, mabomba yaliyopasuka katika mradi uliopo katika Kijiji cha Seluka hayajafanyiwa matengenezo likiwemo tatizo la kutofanya kazi kwa visima vifupi tisa (9) kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na kero hizo za upatikanaji wa maji katika Jimbo la Kibakwe, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 inachimba kisima kirefu katika Kijiji cha Kibakwe kwa gharama ya shilingi milioni 50 na kufanya ukarabati wa mradi wa maji katika Kijiji cha Kazania kwa gharama ya shilingi milioni 60 kwa kuweka pampu mpya, nyumba ya kuhifadha pampu, ununuzi wa jenereta na kujenga njia moja ya maji sawa na kilomita 1.5. Chanzo cha fedha hizo ni ruzuku ya Serikali (CDG). Aidha, Halmashauri katika mwaka 2011/2012 imeidhinishiwa shilingi milioni 730 ambazo zitatumika kujenga mradi mkubwa wa maji ya mtiririko na ukarabati wa mradi wa maji katika Kijiji cha Chenyifukwe kwa kujenga miundombinu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, inapotokea tukatofautiana, maana najua hili jibu limetoka Wilayani kwangu. Nilichokiuliza mimi ni tofauti na jibu analolisema Mheshimiwa Waziri kwa sababu ya takwimu ya hali halisi ya ugumu na ufanisi mbaya ya miradi iliyotekelezwa, ni hatari sana. Lakini mimi ndiye *field officer*, sisi Wabunge ndiyo *field officers* tunaajua mambo halisi kwenye *ground* yakoje. Swali langu sasa, kwa kuwa nilichokiuliza bado uhalisia wake uko vilevile na ndiyo hali halisi ilivyo kwenye *ground*. Je, hawa watalaam wanaosimamia miradi yetu ya maji wakiwepo na wakandarasi, inapotokea hali ya miradi waliyoisimamia na wakandarasi miradi waliyoitekeleza ikawa haijawa *sustainable*, ni hatua gani sasa tuwachukulie maana hali hii sasa inatisha katika nchi? Hilo swali la kwanza. Lakini swali la pili; hali ilivyo katika Vijiji hivyo alivyovitaja wa Vikisima, Unyenzele, Chinyanhuku, Kazania, Ving'ahwe, ni hali ambayo imekuwa hivyo kwa miaka mitano ambayo mimi nimekuwa Mbunge na matatizo yake na fedha zinatengwa na inafanyika, lakini hatutatu tatizo. Je, Mheshimiwa Waziri sasa, anatumia vipi wananchi wa Jimbo la Kibakwe na Mpwapwa juu ya uzembe huu wa usimamiaji mbovu wa miradi hii. Je, hao wanaohusika wanachukuliwa hatua zipi hata kama hawapo? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Simbachawene naomba anisikilize vizuri. Alipouliza swali hili mimi nilipenda. Mheshimiwa Simbachawene anachozungumza hapa anasema *what is the basic contradiction?* Ndicho anachouliza hapa! Nini tatizo la msingi la maji katika Wilaya ya Mpwapwa? Ndilo swali lililoulizwa hapa. Sisi tumemweleza hapa, tumemwambia hapa kwanza kabisa, hali iliyoko Mpwapwa ni kwamba watu wanakata miti hovy hovy, watu wanachoma moto miti.

Tatizo hili hata kama ungeleta *engineer* anatoka Marekani, ukamwambia njoo ukafanye kazi hii, bado utabaki pale pale kwa sababu tatizo la msingi halijatatuliwa. Ukitatua tatizo la msingi (*the primary contradiction*) *the secondary contradiction* inaondoka *automatically*, inaondoka moja kwa moja pale. Kwanza hilo, ameuliza swali hapa, ni nini tatizo la msingi. Hilo la kwanza. Pili ni usimamizi mbovu na tatu hakuna mradi endelevu pale.

Mheshimiwa Spika, tumesema hapa ukitaka maji yapatikane na watu wapate maji hapa, wananchi lazima wachangie sehemu fulani ya nguvukazi au hela ili uweze kusimamia miradi hii. Hivi Vijiji vilivyozungumzwa hapa, tumekwenda kule tumewauliza. Tumewaambia ninyi mnatakiwa hapa mkichota maji kidogo, mchangie kidogo, tukaambiwa kwamba wananchi hawachangii. Sasa bomba likipasuka pale unafanyaje? Ndiyo maana tukajibu hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Simbachawene na mimi nakubaliana naye. Sisi sasa kwa vile hii ni *issue* na hii ni mara yake ya tatu anauliza swali hili, tutatoka pale TAMISEMI, tutakwenda sisi mpaka Mpwapwa, twende tukatafute, huu usimamizi mbovu ni pamoja na zile *trusts* zinazoundwa pale Kijijini. Kama tutakuta humo ndani yake kuna *engineer* ambaye anaonekana naye amesababisha hali hii kama Mheshimiwa anavyosema, kwa sababu amesema yeye ni *number one* pale *which I agree with him* na juzi tulisema hapa, hatutampuuza Mbunge yeyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nikuahidi, Kibakwe ni hapa karibu, tunaweza tukaomba ruhusa hapa haraka haraka, mimi nikaondoka na Mheshimiwa Simbachawene, tukaenda kule tukashughulika mara moja, nimalize kazi hiyo iishe. (Makofi/Kicheko)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imechimba visima virefu 12 katika Jimbo la Longido na visima 8 havikuwa na maji na vinne (4) vilikuwa na maji, lakini havikuendelezwa. Ni lini Serikali itaendeleza visima hivyo ili wananchi wenye kero ya maji waweze kupata maji katika visima hivyo ambavyo vimepatikana na maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Naibu Waziri wa Maji hayupo!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hivi anavyovisema Mheshimiwa Laizer, huwa Mheshimiwa Laizer tunashirikiana wote, kuna wengine kule kwangu Siha tunachota maji kwake na wale wa Longido wanakuja kuchota maji kwetu. Kwa hiyo, najua natakwa niwe mwangalifu.

Mheshimiwa Spika, labda niliweke vizuri hapa liweze kueleweka na Mheshimiwa Lwenge amekuwa anajibu swali hili mara kwa mara. Unapoanzisha mradi huu wa kuchimba maji, kuna mtu hapa anaitwa Mshauri Elekezi. Mshauri Elekezi akishakwambia hapa panachimbwa maji, unaweza ukachimba hapa visima 10, 6 vinatoa maji, 4 havitoi maji. Yule mkandarasi aliyeko pale yeye anakwambia "mimi nipe hela yangu, *whether* maji yanatoka au hayatoki, mimi sijui kwamba ulikuwa unachimba choo au ulikuwa unachimba maji, mimi sijui".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachosema hapa na hili si jambo la ajabu Waheshimiwa Wabunge kwamba eti utakuta mahali kwamba hakuna maji, ni jambo la kawaida kabisa, *Hydrologists* wanafahamu hiyo habari. Ukichimba kama ni visima 10, inawezekana kabisa 8 vikaonekana kwamba vina maji, 2 havina maji, ni jambo la kawaida kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi bado wanahitaji maji, ndicho anachosema Mheshimiwa Mbunge, *whether* yametoka au hayakutoka lakini *the basic contradiction* pale ni kwamba watu hawana maji.

Mheshimiwa Spika, Mimi nataka niahidi kitu kimoja hapa kwamba tutakwenda, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara. Hili eneo ni eneo gumu, ukiwakuta watu wako kule, tukijibu haraka haraka hapa, itatuletea matatizo kwa sababu wanapata tabu kweli kweli wananchi walioko katika maeneo hayo.

Tutakwenda kukaa nao tuone na tutakaa na Mheshimiwa Laizer, tuzungumze vizuri kwa karibu. Unajua nikifanya hivyo na wananchi wangu wa Siha nao watafaidika huko huko kwa sababu wanachota maji humo humo. (Makofi)

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo nitazungumza na Wizara ya Maji na yeye Mheshimiwa Laizer tusaaidiane katika jambo hili.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika majibu yake ya msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba matatizo haya ya maji yanachangiwa na usimamizi mbovu na matatizo kama haya ya Mpwapwa ya kuchimba visima na miradi kushindwa kuendelezwa yako vile vile kwenye Jimbo la Ubungo ambapo kuna visima vingi virefu na vifupi ambapo miradi imekwama maeneo ya Kibwegele, Makoka, Msumi, Bonyokwa pamoja na Goba.

Je, Ofisi ya Waziri Mkuu iko tayari sasa kuchukua hatua za kiseru, kwa kuwa visima hivi na miradi hii ya wananchi ilikuwepo wakati maeneo haya yakihesabika kama ni vijiji na sasa maeneo haya yameendelea na yamekuwa mitaa na ni makazi ya wananchi wengi. Je, Ofisi ya Waziri Mkuu iko tayari sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha sheria ya DAWASA (*DAWASA Act*) inatekelezwa ili maeneo yote haya hii miradi ihame kutoka mamlaka ilizokuwepo awali chini ya Serikali za Mitaa, kuhamia kwa DAWASA pamoja na DAWASCO ili kuweza kusimamiwa kwa uthabiti zaidi na wananchi wakapata huduma ya maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, wazo ni zuri, lakini mimi naangalia kitu hiki tunachokiita *D by D (Decentralization by Devolution)* kwamba una *devolve*, unapeleka madaraka zaidi kwa wananchi ili wananchi waweze kuendesha shughuli zao wao wenyewe. Sisi ndiyo wenye dhamana ya kwamba wananchi wafanye wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukirudi nyuma sasa, najua kwamba kuna *development* mpya ambayo inaizungumzia hapa kwamba ungewapeleka katika DAWASA. Tunachosema hapa, sera inasema kwamba wananchi pale walipo wataunda *trusts* au kitu kinachoitwa *associations* na hizi ndizo zitakazokuwa zinasimamia maji pale. Sasa Mheshimiwa Mnyika, anasema kwamba kwa vile kuna *development* mpya, sasa wale wanatawaliwa na ile sheria ya miji na Wazo hili ni zuri, sisi tutalichukua ili twende tukaliangalie. Kwa mapana hayo ninayoyazungumza hapa na tuone namna ambavyo wananchi bado wanaweza wakashirikishwa katika jambo hili kama anavyojaribu kushauri hapa. Kwa hiyo, tunalichukua Mheshimiwa, tutalifanyia kazi.

Na. 99

### **Kiwanda cha Mbao (TWICO)**

**MHE. SALUM K. BARWANY** alijibu:-

Ziwani *Middle School* – Mingoyo, ilibadilishwa na kuwa Kiwanda cha mbao (TWICO) na sasa hakipo tena.

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kubadilisha matumizi ya shule hiyo ni kudhoofisha elimu ambayo iko chini Mkoani Lindi?
- (b) Je, ni mamlaka gani ilifanya mabadiliko hayo na sheria gani ya nchi ilitumika?
- (c) Je, ni lini Serikali itarejesha shule hiyo na kufanya itoe huduma kwa watoto wa maskini wa Manispaa ya Lindi na maeneo ya jirani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfani Barwany, Mbunge wa Lindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya elimu Mkoani Lindi imeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka hivyo kufanya Mkoa huo kutokuwa wa mwisho kielimu hapa nchini. Mfano mwaka 2010 Mkoa ulishika nafasi ya 11 katika Mfihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kati ya Mikoa 21.

Mwaka 2011 jumla ya wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi walikuwa 20,415 na kati yao, wanafunzi 9,881 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza. Wanafunzi wote hao wamepata nafasi katika shule za sekondari Mkoani humo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi una jumla ya shule za msingi 442, shule za sekondari "O" Level 118 na shule za sekondari "A" Level 5, ikiwa ni jumla ya shule za sekondari 123. Idadi ya shule za sekondari imekuwa ikiongezeka kwa asilimia 2.8 Kitaifa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1950 mpaka 1960, palikuwepo na Ziwani *Middle School* ambayo ilikuwa ni *Boarding School* ikiwa chini ya Serikali. Ziwani *Middle School* ilikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo upungufu mkubwa wa wanafunzi kutokana na mwamko duni wa kielimu katika eneo hilo kwa wakati huo.

Sambamba na hiyo, vita vya Msumbiji viliathiri sana uendeshaji na mahudhurio ya wanafunzi. Pia uchakavu wa majengo ya shule hiyo ulisababisha Serikali kubadilisha matumizi ya eneo. Sheria ya Ardhi ya *Town and Country Planning Act, 1956*, Ibara ya 378 na ambayo



ilirekebishwa mwaka 1961, ndiyo iliyokuwa ikitumika na Mamlaka ya Ardhi kubadilisha matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1967, Serikali ilibadili matumizi ya eneo ya iliyokuwa Ziwani *Middle School* na kujengwa kiwanda cha mbaao (*Tanzania Wood Industry Company Limited (TWICO)*). Aidha, mwaka 1966 TWICO ilibionafishwa kisheria na kuwa *Mingoyo Saw Mills Company Limited*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo hili lina mmiliki halali ambaye ni *Mingoyo Saw Mills Company Limited*, Serikali haina mpango wa kurejesha eneo hili na kuwa eneo la shule kama ilivyokuwa awali. Hata hivyo, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) na kwa kushirikisha nguvu za wananchi wa eneo hilo, wananchi wameweza kujenga shule mbadala ya Sekondari ya *Mingoyo*. Shule hii iliyoanza mwaka 2009 imeweza kutoa fursa ya elimu ya Sekondari kwa watoto wa Kata ya *Mingoyo* na Mkoa wa Lindi kwa ujumla.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Waziri, niseme majibu yasiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba mabadiliko ya mfumo wa elimu kutoka *Standard 8* katika maana ya zile shule za *Middle School*, yalifanyika mwaka 1967 na kurudi tena kuwa *Standard 7*. Hivyo, mwaka huo wanafunzi walihitimu Ziwani *Middle School*. Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba shule hiyo ilikosa wanafunzi, iweje kwamba wanafunzi walihitimu katika mwaka huo wa 1967 na mfumo wa *Middle School* ulivunjwa wake ule? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Majengo ambayo yanatumika leo katika kiwanda cha mbaao cha Ziwani ni yale ambayo yalikuwa ni majengo ya Ziwani *Middle School*, hakuna majengo mapya ambayo yalijengwa kwa ajili ya kiwanda hicho kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza. Je, yupo tayari Mheshimiwa Waziri kufuatana na mimi kujua hali halisi kuliko taarifa hii ambayo wamempa haina ukweli ndani yake? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ni rasmi, lakini hayana ukweli! Hiyo kweli....! Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, suala hili ni la kihistoria, kama nilivyosema, ni wakati wa mwaka 1950 mpaka 1960 mpaka 1970 wakati *Middle School* ilikuwepo huko Lindi. Taarifa za mafaili yetu ofisini kama nilivyosema tumejaribu sana kuwasiliana na Afisa Elimu wa Mkoa wa Lindi, tumejaribu kuwasiliana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi.

Taarifa zilizopo kule ni kwamba, baada ya athari za vita vya Msumbiji kwa wakati ule na baada ya wanafunzi kutohudhuria shule kwa wakati ule, basi Serikali iliamua eneo lile, kwa sababu wakati ule ilikuwa bado ni Serikali, kuweza kulipeleka kuwa kiwanda kwa wakati ule kutokana na mahitaji ya wakati ule kutokana na historia kama nilivyosema. Lakini bado haikuathiri hali ya elimu ya Mkoa wa Lindi kama nilivyosema, shule ni nyingi hata kwa wakati ule hakukuwa na tatizo lolote ambalo lilisababisha suala lifanyike vile. Lakini kuhusu taarifa zingine za kina kama Mheshimiwa Mbunge anao ushahidi wa kina wa kimaandishi na wa kisheria, mimi niko radhi kabisa kufuatana naye kwenda kuangalia hali halisi, tuweze kuchimbua historia kwa wakati ule, kwa sababu naamini miaka ya 1950 hata Wabunge wengine hapa hatukuwa tumezaliwa kabisa na ni wachache sana. Kwa hiyo, tunaweza tukaanza kuivumbua. Kama yeye ana historia nzuri ya wakati ule, basi ningemwomba tu atupatie ili tuweze kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nilifanya makosa, niliacha swali Namba 98 ambalo linaulizwa Ofisi ya Rais – Utawala Bora. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Lucy Owenya, aweze kuuliza swali hilo.

**Serikali Kutohojiwa kwa Matumizi ya  
Mali ya Umma**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Jamhuri ya Muungano inajumuisha pande mbili za Muungano za Tanganyika na Zanzibar:-

(a) Je, ni kweli kwamba Serikali haiwezi kuhojiwa chochote kama vile maamuzi ya kuuza mali ya Umma?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ripoti ya vyombo vya habari vya Zanzibar kwamba Serikali haiwezi kuhojiwa lolote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali haiwezi kuhojiwa chochote kwa maamuzi yake ikiwa ni pamoja na maamuzi ya kuuza mali za umma.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 63(2) inatamka wazi kuwa Bunge ndiyo chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano ambacho kimepewa madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali. Kusimamia na kuishauri Serikali iliyopo madarakani ni pamoja na kuhoji na kwa kuuliza maswali. Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakitekeleza kazi hiyo kwa kiwango cha ufanisi wa hali ya juu kabisa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haioni sababu ya kutoa tamko lolote kuhusu ripoti inayosemekana imetolewa na vyombo vya habari kwamba Serikali ya Zanzibar haiwezi kuhojiwa kwa lolote, mimi binafsi sijaiona ripoti hiyo na sifahamu ilitolewa katika mazingira gani. Ninavyoelewa mimi ni kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wamekuwa wakihoji mambo mengi yanayohusiana na maamuzi ya utendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri kwamba Serikali inaweza kuhojiwa kwa kuuza mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi mwenyewe nilimwona Rais wa Zanzibar akizungumza katika vyombo vya habari kwamba Serikali haiwezi kuhojiwa kwa kuuza mali za Umma ndiyo msingi wa swali langu naomba nimpe taarifa Waziri ajue hilo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa jibu katika swali la msingi kinachoamua ni Katiba, Katiba inasema Bunge na Baraza la Wawakilishi wanayomamlaka ya kuhoji Serikali. Sasa kwa sababu taarifa anayotoa Mheshimiwa Lucy Owenya mimi sikuiona napata tabu sana kutafsiri alichokisema Rais wa Zanzibar. Lakini ninachorudia kusema ni kwamba Katiba ndiyo inaweka Rais, ndiyo inaweka Bunge na ndiyo inaweka utaratibu wa mahusiano kati ya Bunge na Rais. *(Makofi)*

**Wanafunzi Waliofutiwa Mitihani.**

**MHE. SUSAN A. LYIMO** aliuliza:-

Matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2011 yameonyesha zaidi ya wanafunzi elfu tisa (9,000) kufutiwa matokeo ya mtihani kutokana na udanganyifu, ishara ambayo ni mbaya kwa maendeleo ya elimu hapa nchini:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wahusika?

(b) Je, kuna mikakati gani ya kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imesikitishwa sana na udanganyifu uliofanywa katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2011 na hivyo kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali imewafuatia wanafunzi 9,736 matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2011.

(ii) Walimu na wasimamizi katika baadhi ya Mikoa na Halmashauri ambao wamethibitika kuhusika na udanganyifu huo wamechukuliwa hatua zikiwemo kuwashusha vyeo na kuwazuia kuhusika na usimamizi wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi. Aidha, Serikali imeunda Tume ambayo itafanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha tatizo na kutoa ripoti yake mwezi Aprili mwaka 2012. Serikali haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu watu wote watakaobainika kuwa wamehusika na udanganyifu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2011. (Makofi)

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeunda Tume, namsihi Mheshimiwa Mbunge awe na subira na wakati Tume itakapomaliza uchunguzi wake itatoa taarifa na kupendekeza mikakati ya kudhibiti hali hiyo.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Naibu Waziri amenisihia nivute subira kwa kuwa Tume imeundwa na kwa kuwa Naibu Waziri huyu alitoa taarifa kwa Vyombo vya Habari kwamba wanafunzi hawa wamesamehewa.

Je, Naibu Waziri haoni kwamba kauli yake hiyo inatofautiana na majibu anayoyasema. Je, kama sasa wanafunzi hawa wataonekana kweli walifanya udanganyifu, Waziri anatuieleza nini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni jana tu matokeo ya Kidato cha Nne yametoka na udanyanyifu umeendelea kuwa sugu katika Taifa hili. Mwaka huu udanganyifu umekuwa zaidi ya mara kumi ya udanganyifu wa mwaka juzi. Lakini vile vile ni wazi kwamba kumekuwa na ufasidi wa elimu katika Taifa hili kwa muda mrefu, siyo tu kwa Elimu ya Msingi lakini vile vile kwa Elimu ya Sekondari, kwa elimu ya Juu na Vile vile kwa digrii za Uzamivu. Wote tuna taarifa kwamba kuna jamaa aliyeandika kitabu cha ufasidi wa elimu na akatoa majina ya watu waliopata Ph. D. feki. (Makofi)

Je, Waziri anatuambia nini wakati viongozi hao bado wamo na tuna baadhi ya Wabunge ambao pia wamo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Mbunge hakutuelewa katika *statement*. Hatukusamehe kuhusu kufutwa kwa matokeo, kilichofanyika pale, baada ya tamko la kwanza ya kwamba wanafunzi wale wote wamefutiwa matokeo na hawatarudia mitihani, baada ya wiki mbili kutokana na ushauri wa wadau mbalimbali wa elimu na wale wa Haki za Watoto na ninyi Wabunge mkiwemo, mkipiga simu na kuja mpaka

ofisini kuomba angalau wale wanafunzi wafanye mtihani mwaka huu, Serikali ikasema hawatafanya mwaka huu kutokana na mambo mengine ya changamoto ya Bajeti na kadhalika.

Lakini tukasema watarudia mtihani mwaka mwingine ambao kwa mwaka jana maana yake ni sawa na mwaka huu mwezi wa tisa Septemba hilo ndilo lililofanyika. Kwa hiyo, siyo kwamba tumewasamehe, kwa sababu baada ya kitendo cha wanafunzi kufutiwa matokeo kutokwenda sekondari mwaka huu katika mfumo wa kawaida na kufanya mtihani kwa baadaye bado hiyo ni adhabu tosha kama ambavyo Wadau wote mkiendelea kulalamika juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udanganyifu uliojitokeza mwaka huu wa Kidato cha Nne kama ambavyo Katibu wa Baraza la Mitihani jana Dkt. Ndalichako ametangaza matokeo haya na sisi wote tumeyasikia tupo huku Dodoma kwamba ni kweli udanganyifu unaendelea kuongezeka. Ninachotaka kusema ni kwamba naomba tunapokuwa tunatoa hizi adhabu kwa watoto wetu, Wabunge ninyi wenyewe ndiyo mnaokuja mnawatetea. Serikali itaendelea kuwa na mkazo ule ule kwamba tukishawafutia watoto matokeo basi kama Serikali mtuache tufanye kazi ili mambo haya yasiendeleo kujirudia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hili suala tayari wanafunzi elfu tatu(3000) wamedanganya katika matokeo ya mtihani mwaka jana, utashangaa tayari mtaanza kuongea kwenye magazeti hata kwenye redio ooh! wasamehewe. Lakini Serikali jana imetamka kwamba watafanya mtihani huo kama adhabu baada ya miaka mitatu, naomba mtuache tufanye kazi ili tutoe fundisho kwa watoto wanaoiba mitihani. Ndiyo maana hata wale walimu waliodanganya mwaka jana kwenye mitihani ya Darasa la Saba, tumeshawachukulia hatua tayari, Wilaya ya Mufindi tumewachukulia hatua Walimu 8, Mbeya Jiji tumewachukulia hatua walimu 5, Mbarali Mwalimu Mmoja, Kyela Mwalimu Mmoja, Dar es Salaam walimu 18 tumeshawashusha Vyeo na kuwavua madaraka na kuwapeleka TSD, Ruvuma tayari walimu wako kama Nane tumewachukulia hatua na Wilaya zingine ambazo wamefanya udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata *Form Four* kama watu tayari wamedanganya naomba muiache sheria ifanye kazi kwa sababu kwenye Baraza la Mitihani kuna sheria ambayo inasema kwamba Walimu wasijihusishe tena katika Mitihani na wale wanafunzi waendeleo kukaa huko mpaka baada ya miaka mitatu ndipo waje warudie mitihani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Wabunge tuwe na subira hiyo.

Kuhusu swali la *Ph. D.* feki..

**SPIKA:** Hapana ni maswali mawili tu yanatosha. Mheshimiwa Mwaiposa swali la nyongeza.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, pamoja na kundi la udanganyifu ambalo alikuwa ameuliza katika swali la msingi, lipo kundi lingine la wanafunzi ambao badala ya kujibu maswali huandika matusi ya nguoni au nyimbo za bongo fleva na kadhalika katika karatasi zao za majibu ya mitihani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia kuwachukulia hatua wanafunzi hawa ikiwa ni pamoja na kuwapima akili zao kwa sababu siyo jambo la kawaida ili kunusuru na kujua ni kitu gani kinakabili kizazi hiki? (Kicheko)

**SPIKA:** Ahsante, swali lenyewe limetokea jana, Waziri majibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Ni kweli kabisa kwamba haya yanatokea na mimi binafsi pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu tumeoneshwa na Baraza la Mitihani karatasi ambazo badala ya mwanafunzi kujibu maswali ameandika beti za muziki wa bongo fleva kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa karatasi hilo. Lingine ni matusi kabisa yale ya nguoni yameandikwa mle badala ya kujibu lile swali.

Tunatafakari hatua kwa sababu mwaka huu hatukuwafutia matokeo ya masomo yote wanafunzi hao kwa makosa hayo, lakini tunatafakari hatua mahsusi ambazo tutachukua kuanzia mtihani wa mwaka huu 2012 ili tabia hiyo tuiondoshe kabisa katika watahiniwa wanafunzi katika nchi yetu. Ahsante sana.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika nilitaka kuuliza swali alilouliza Mheshimiwa Mwaiposa, ahsante sana.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana. Kwa kuwa, kwa miaka ya hivi karibuni matokeo ya shule zetu yameendelea kushuka na mifano halisi ni mwaka jana katika matokeo ya shule za msingi na mwaka huu katika matokeo ya Kidato cha Nne. Je, Serikali sasa inaweza kutueleza tafsiri ya matokeo haya na thamani ya elimu ya Tanzania inakoelekea?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, tumepata kadhia kubwa hasa kuanzia mwaka jana kwa matokeo ya Kidato cha Nne, yale yalikuwa siyo mazuri kama tulivyotegemea. Lakini jambo la uhakika ni kwamba tumechukua hatua kubwa ya kuongeza nafasi katika elimu ya Sekondari ama access kwa kiwango kikubwa kushinda nchi yeyote katika Bara la Afrika kwa miaka ya hivi karibuni. Bila shaka unapochukua hatua kubwa kiasi hicho kutajitokeza madhara upande mwingine. Tuliyatambua hayo na matokeo yake ni haya ambayo tumeyaona mwaka jana ya wanafunzi wengi kutokufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejipanga kimadhubuti kuhakikisha sasa baada ya kulishughulikia tatizo la access sasa tunapanda kwenye ubora wa elimu na ndiyo nia thabit ya mpango wa maendeleo ya elimu ya Sekondari awamu ya pili, haitoangalia kujenga majengo tena, inakwenda kwenye ubora wa elimu. (Makofi)

Hatua zote tutakazozichukua kwa maana ya Walimu, kumalizia madarasa ambayo hayajaisha, kujenga maabara, na kujenga maktaba na kuweka vitabu, yote hayo na mengine mengi yanalenga katika ubora wa elimu kama tulivyoona mwaka huu 2012 mtihani matokeo yake yamepanda walau kwa asilimia ndogo.

Sasa ufaulu ni asilimia 52 tofauti na mwaka jana asilimia 50. Lakini kuanzia sasa na kuendelea bila shaka Bunge hili litaona mabadiliko makubwa katika shule zetu za *Secondary* ziwe *Functional Secondary Schools*. (Makofi)

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

Na. 101

### **Biashara Nchi za Afrika Mashariki**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imejipangaje katika kutoa elimu kwa wananchi wote nchini juu ya haki ya kuuza bidhaa zao wenyewe bila vikwazo vyovyote katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki?

(b) Je, ni bidhaa zipi zinaruhusiwa na zisizoruhusiwa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa rufusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu kwa swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, lenye vipengele (a) na (b) ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Elimu kwa Umma uliozinduliwa mwaka juzi, Wizara yetu imeendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa za biashara ndani ya Jumuiya kupitia njia mbali mbali zikiwemo mikutano ya hadhara, maonyesho mbalimbali ya Kitaifa, vipindi vya redio, luninga, majarida na vitini.

Aidha, katika kurahisisha utoaji wa elimu ya Umma juu ya masuala ya mtengamano wa Afrika Mashariki katika ngazi ya Halmashauri, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeteua maafisa 140 ambao ni (focal persons) kutoka Halmashauri zote nchini watakaohusika na uratibu wa masuala ya mtengamano katika Halmashauri zao. Katika kuwawezesha Maafisa hawa, Wizara kwa kuanzia imewapatia mafunzo maalumu maafisa 36 kutoka Kanda ya Ziwa na zoezi hilo litaendelea katika Kanda nyingine.

Mheshimiwa Spika, vile vile, nchi wanachama wa Afrika Mashariki zimeanzisha utaratibuwa pamoja wa kutoa elimu kwa Umma ambao unaitwa (*Joint Sensitization Programme*) katika maeneo ya mipakani, utaratibu huu unawawezesha watalaam, wafanyabiashara, wakulima na wananchi wote waishio katika pande zote mbili za mipaka kupata elimu kwa pamoja kuhusu fursa za mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pamoja na hayo pia wanapata fursa ya kujua taratibu zilizo ili kunufaika na fursa hizo. Aidha, wananchi hupata fursa ya kueleza changamoto ambazo zinawakabili katika kufanya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo hizi zikishatokea hufanyiwa kazi na Wizara yetu.

(b) Kulingana na itifaki ya Umoja wa Forodha, bidhaa zote zinazozalishwa ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki huwa zinaweza kufanyiwa biashara katika jumuiya hiyo. Bidhaa zilizo ndani ya jumuiya na zinazokidhi vigezo vya utambuzi wa asilia wa Afrika Mashariki hazitowzi ushuru wa Forodha zinapouzwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Bidhaa ambazo hazikidhi vigezo vya utambuzi wa usilia na bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hutowzi ushuru wa viwango vya aina tatu. Viwango hivyo ni asilimia hizo ni zero kwa malighafi zinazolingia yaani mitambo na bidhaa za metali. Asilimia kumi kwa bidhaa zinazosindikwa kwa kiwango cha kati na kiwango cha asilimia 25 kwa bidhaa za mwisho za mlaji zilizokamilika usindikaji wake.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana, nampongeza pia Waziri wa Afrika Mashariki kwa kutimiza ahadi yake hapa Bungeni, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, Naibu Waziri amesema kwamba amepeleka Maafisa 36 katika Kanda ya Ziwa.

Je, Waziri anaweza kunieleza ni Afisa gani ambaye amepelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe?

Pili, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na Kanda ya Ziwa wamekuwa wakipata shida sana Mpakani hasa mpaka wa Burundi na Rwanda wanapopeleka bidhaa zao wakiambiwa kwamba watoe *Certificate* au cheti cha kuingiza bidhaa katika nchi jirani na kwa kuwa hawajui *Certificate* zinapatikana wapi.

Je Serikali inaweza kutueleza wananchi wetu watapata wapi hivyo vyeti vya kupeleka bidhaa nje?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli kuna watalaam au waratibu 36 ambao walipata mafunzo kule Mwanza Juni, 2011 na katika hao bahati nzuri nilijiandaa upande wa Karagwe kuna Mtendaji ambaye ni Afisa Biashara Mkuu anaitwa Deogratius Kapami, ndiye mhusika mkuu wa uratibu katika Halmashauri ya Karagwe.

Ni Kweli tunapata matatizo mengi katika ziara ambazo tunaenda juu ya usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine. Matatizo haya yamepatikana wakati tulipokwenda Mtukula, Murongo, Lungalunga na sehemu nyingine.

Kwa kweli inabidi tuwaambie wananchi kwamba ili mazao yao yapite kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine ni lazima wapate *Certificate of Origin* na *Certificate* hii inapatikana ofisi za TCCIA katika mikoa ile. Kwa hivyo tunawaomba sana wananchi waende wakachukue *Certificate* za mazao yao kwa sababu tumebaini kwamba mazao ambayo yanasafirishwa siyo mazao ambayo yamesindikwa nusu wala siyo mazao yamekamilika ni mazao ambayo wananchi wanayalima kama machungwa, mananasi, ndizi na mahindi.

Kwa hivyo haya ni wazi kabisa yana uasilia wa Kitanzania kwa hivyo tunawaomba wananchi waende kwenye ofisi za TCCIA mikoani ili wapate *Certificate* na wafanye biashara zao bila ya matatizo yeyote. (Makofi)

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri utaratibu uliotuelezea kuhusiana na mchakato mzima wa kupitisha miradi hii. Je, uko sawa baina ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inahusisha Tanzania kuwa kama ni nchi ya *partner state*. Kwa kuwa Tanzania ni Jamhuri ya Muungano wa Zanzibar na Tanzania Bara ni wazi kwamba huu utaratibu unahusisha sehemu zote mbili. Kwa taarifa yake Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Zanzibar kwamba kule Zanzibar kuna ZCIA ambayo ndio inaratibu upatikanaji wa *Certificate* za *Original*.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niongezee kidogo juu ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba nitoe taarifa tu kwa wafanyabiashara wanaotoka hususan Pemba, kuelekea Mombasa, Serikali ya Kenya imetuletea kama Tangazo hivi la tahadhari kwamba wao hivi sasa wako vitani wanapambana huko Somalia.

Kwa hiyo, wafanyabiashara wanaokwenda Mombasa Shimoni wazingatie kwamba haitakuwa rahisi kutambua maadui hasa nyakati za usiku. Kwa hiyo, wanashauriwa waweze kwenda saa za mchana na biashara zao itakuwa vepesi zaidi.

Kwa hiyo, tumepata tatizo la wavuvi 51 kukamatwa kule Mombasa na hao wametoka Pemba, lakini tumelishughulikia na Ofisi ya Ubalazi Mdogo pale Mombasa tumeweza kulipa faini na wavuvi 51 wote Watanzania wale wamerejeshwa bila tatizo lolote. Lakini sasa tuchukue tahadhari. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante kwa tahadhari.

Na. 102

### **Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi Zanzibar**

**MHE. JUMA SURURU JUMA** aliuliza:-

Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi ni kati ya miradi iliyokuwemo katika mkakati wa sekta ya uchukuzi na programu ya maendeleo ya barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa mujibu wa taarifa za Baraza la Mawaziri la Sekta ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa (T.C.M.) imeridhia miradi mitatu ya Zanzibar kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotafutiwa fedha kuwezesha ujenzi, lakini ule wa Maruhubi bado:-

(a) Je, mradi wa ujenzi wa Bandari ya Maruhubi utagharimu fedha kiasi gani hadi kukamilika na umefikia hatua gani?

(b) Je, Serikali haioni kuchelewa kupatikana kwa fedha za ujenzi wa mradi huo kunarudisha nyuma maendeleo ya Zanzibar?

(c) Je, hadi sasa ni nchi ngapi zimepelekewa maombi kupatiwa msaada wa fedha za ujenzi huo na ni kitu gani kimekwamisha utekelezaji huo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu kwa swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja nitajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Bandari ya Maruhubi ni mmoja kati ya miradi ya sekta ya uchukuzi ambayo ilipitishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kikao chake tena kwa mara ya pili cha Novemba, 2011. Gharama za mradi huo zinakadiriwa kuwa ni jumla ya Dola za Kimarekani baina ya Milioni 200 na milioni 700.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huo wa Bandari ya Maruhubi kama ilivyo kwa miradi mingine ya Jumuiya kunatokana na michakato mirefu ya majadiliano baina ya nchi tano hadi kufikia makubaliano ya kupitisha mradi huo. Aidha, maombi kwa washirika mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya kufadhili mradi wa ujenzi wa bandari ya Maruhubi kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki yatawasilishwa baada ya kukamilika kwa mchanganuo wa mradi huo kutokana na upembuzi yakinifu uliofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, utakaoainisha gharama halisi ya mradi huo kwenye unyambuzi na kazi hiyo, itafanyika mwaka huu 2012.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kujua ni kiasi gani Maafisa Waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanashirikishwa katika mchakato huu?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ambayo inatoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar huwa inakaliwa katika Kikao cha pamoja katika sekta husika kinachoongozwa na Ofisi yetu na Wizara yetu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kwishakutambulika ule mradi kuwa mradi wenye sifa ya kikanda yaani mradi huo uwe unahusisha walau nchi mbili, mradi huo huwa unachukuliwa na kupelekwa kwenye kikao kama hicho lakini kinachohusisha nchi tano. Baadaye baada ya kwishapasishwa ndio huwa unapita ngazi tofauti za maamuzi kufikia Baraza la Mawaziri na kupatiwa mfadhili miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi hizo zote Maafisa Waandamizi na hasa kwa mradi huu ambao umetokea Zanzibar huwa wanajumuishwa kikamilifu katika majadiliano yote hayo na siyo mradi huu tu ni miradi yote mitatu ambayo imepitishwa kutoka Zanzibar katika ngazi ya Afrika Mashariki imehusisha maafisa hao.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru angalau kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mradi wa ujenzi wa bandari ili tuweze kufanikiwa vizuri ni lazima uwepo usafirishaji wa meli na kwa kuwa kuna mipango mingi ya ujenzi wa reli na barabara kwa upande wa Tanzania Bara, lakini mradi huu wa bandari haujahusisha ununuzi wa meli na kwa kuwa katika hata swali lililofuata nyuma kwamba adha ya watu kuuza mazao yao katika Jumuiya ya Afrika Mashariki inatokana pia kwamba hakuna mpaka sasa hivi meli inayofanya kazi baina ya visiwa vya Unguja na Pemba na mwambao wa Tanzania Bara.



Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutueleza sasa kwamba mradi huu wa Bandari ya Maruhubi utakwenda sambamba na ununuzi wa meli ambayo itafanya kazi katika Ukanda wa Pwani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kitaalam mradi unapoandikwa unakuwa na malengo yake na katika mradi huo ambao tumeupata sisi katika Wizara ya Afrika Mashariki na tukauwasilisha kwenye Jumuiya haukuwa na kielelezo cha kusema kwamba tuhusishe usafiri au ununuzi wa meli ndani ya mradi huo. Lakini ni vema na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba unapotengeneza moja basi na nyingine katika *chain* ile liwepo. Kwa hiyo, namshauri tu kwa kushirikiana na ujasiri wake wa kuweza kushawishi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pengine anaweza kushawishi na ununuzi wa meli yakahusishwa pamoja na mradi huu ikiwa kama ni kiungo.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa kunipa nafasi niongezee tu, najivunia sana Naibu Waziri wangu anajibu mambo vizuri sana. (Makofi)

Nataka niongeze kwamba upo mradi wa kivuko *role on role off ferry* ni mradi ambao Serikali ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi tumeuingiza katika shughuli za Jumuiya. Mradi huo sasa, *role on role off ferry* utakuwa ni meli kubwa kabisa ambayo inapakia mizigo, inachukua abiria na itaunganisha bandari za Mombasa, Tanga, Dar es Salaam, Zanzibar na Pemba. Kwa hiyo, sehemu ya mradi huu ni *role on role off ferry* ambao tunaushughulikia hivi sasa. (Makofi)

Na. 103

#### **Uzalishaji wa Chakula cha Kutosha**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aiuliza:-

Shirika la Chakula Duniani (FAO) limetabiri kuwa kutakuwa na uhaba mkubwa wa chakula Duniani kwa miaka 30-40 ijayo:-

Je, Tanzania inajipanga vipi kuhakikisha inazalisha chakula cha kutosha kwa matumizi ya ndani na kuuza ziada kwa nchi zitakazokumbwa na njaa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Hamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika miaka ijayo, nchi yetu kama zitakavyokuwa nchi nyingine duniani itakabiliwa na changamoto nyingi zifuatazo;

- (i) Idadi ya watu inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 42 ya sasa hadi kufikia takribani milioni 82 ifikapo mwaka 2050.
- (ii) Uhaba wa maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi.
- (iii) Upungufu wa nafaka utakaopungua kutokana na nafaka kutumika kutengeneza nishati.
- (iv) Eneo la Mazao ya chakula kugeuzwa kuzalisha mazao ya nishati.
- (v) Msukosuko wa kiuchumi na bei ya mazao ya chakula duniani.

Mheshimiwa Spika, zipo pia dalili za kupungua kwa uzalishaji wa chakula duniani kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokana na ongezeko la joto duniani (*global warming*).

Mpango kabambe wa Taifa wa umwagiliaji wa mwaka 2002 unaonesha kwamba mahitaji ya chakula yataendelea kuongezeka kutoka tani milioni 14,516 za mwaka 2012 kufikia tani milioni 22,897 mwaka ifikapo mwaka 2017. Kwa mchele peke yake mahitaji yataongezeka kutoka tani 785,000 za mwaka 2002 hadi tani 3,373,000 ifikapo mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali pamoja na mambo mengine inachukua hatua zifuatazo:-

- (1) Kuongeza eneo linalomwagiliwa kufikia angalau hekta milioni moja ifikapo mwaka 2015 na kuhakikisha kwamba asilimia 25 ya chakula chote kinatokana na kilimo cha umwagiliaji. Aidha, matumizi ya teknolojia zinazotumia maji kwa ufanisi na ujenzi wa mabwawa na matumizi ya maji chini ya ardhi yatahimizwa.
- (2) Kuhimiza wakulima kuzalisha mazao kulingana na hali ya hewa na kulima mazao yanayostahimili ukame.
- (3) Kufanya utafiti wa mbegu zinazoweza kukinzana na hali ya ukame, magonjwa na wadudu.
- (4) Kusimamia kilimo bora kinachohifadhi mazingira, rutuba ya udongo.
- (5) Kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo, pembejeo na usindikaji wa mazao.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri kwamba katika majibu haya ya Mheshimiwa Waziri sikuona popote mpango mkakati wa muda mrefu ambao unaweza kukabiliana na hali hii ya hatari ya Tanzania na duniani.

Lakini ni dhahiri kwamba Watanzania ambao asilimia 80 ni wakulima wanatakiwa waeleweshwe huu utabiri ili waweze kujipanga vizuri.

(a) Je, Serikali imewashirikisha vipi wananchi ili waweze kukabiliana na utabiri huu ambao utaathiri Tanzania na duniani?

(b) Ikiwa ndani ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika Serikali imemudu tu kuendeleza hekta 400,000 za umwagiliaji na kati ya hizo nyingi miundombinu yake imeshaharibika. Je, Serikali itatumia miujuzi gani kuendeleza hekta milioni moja ndani ya miaka 4 jambo ambalo limeshindikana katika miaka 50 ya Uhuru? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge, anasema hajaona mpango wowote lakini napenda tu nimkumbushe kwamba mbona mipango iko mingi ambayo tumeieleza mara nyingi. Iko *Comprehensive African Agriculture Development Program*, iko mipango ya *NEPAD*, kufuatia mipango hiyo tunayo Kilimo Kwanza, tunayo *ASDP* na sasa tumeingiza katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano ambao tumeueleza na Wabunge wote mnauuelewa. Tumeieleza pia mpango huu *SAGOT* yote hii ni mipango ambayo inaelekea kutoa majibu ya kuongeza uzalishaji wa kilimo katika miaka mingi ijayo. Lakini pia kuna mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo. Yote haya yanalenga kutoa majibu sahihi kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nadhani mifano hii inamwonyesha Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kwamba inaelekea huko ambako tunataka kwenda. Labda tu ni kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango hii.

Lakini la pili kuhusu miujiza itakayofanyika nataka nikubaliane na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kwamba ni kweli mbele huko tunakokwenda hekta milioni moja zinaonekana ni nyingi zaidi. Lakini unajua ni lazima *to aim higher, to think big* tusijirudishe nyuma. Kikubwa zaidi hapa tunachotakiwa kufanya na kuongeza utalaam. Tusipoweza kufikia hekta milioni moja kwa bahati mbaya tukafika hata 500,000. Tutakachokifanya ni kuongeza utaalim ili *cropping intensity* hekta hizo hizo 500,000 zilimwe mara mbili au mara tatu kwa maana hiyo tutakuwa tunaelekea kupata yale tunayotarajia kwenye milioni moja. Lakini lengo twende huko kwenye milioni moja, lakini wakati huo huo tuongeze uzalishaji katika eneo tulilionalo kwa eneo kwa kuongeza *cropping intensity*. (Makofi)

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, Tanzania tumekuwa na kauli mbiu na mipango mingi sana ya kilimo lakini kadri inavyokwenda kilimo kimekuwa kikiendelea kushuka. Kwa mfano mwaka 2007 angalau kilimo kimekuwa kwa asilimia 4.3 lakini mwaka 2009 kilimo kilipungua mpaka kufika asilimia 2.7. Je, Serikali inatambua, itafanya maajabu gani ambayo yatasababisha uzalishaji uendeleo kuongezeka wakati tunaonekana tumeshindwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini kutokana Sauti ya *loud speaker* sikusikia vizuri swali lile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhonga hebu uliza swali tena. Tumia mashine nyingine.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, ametoa majibu ya Serikali ambayo yameonyesha kwamba sekta ya kilimo inaweza ikaongezeka na uzalishaji wa chakula ukawa umeongezeka. Lakini kuna historia ya Tanzania inavyoonyesha kila siku kilimo kinavyozidi kushuka. Kwa mfano, mwaka 2007 kilimo kilikua angalau kikafika asilimia 4.3 miaka ilivyoendelea mwaka 2009 kilimo kilishuka kufika asilimia 2.9 na hali inaonekana kwamba kilimo kinakua *at least* kwa asilimia labda 1 au *zero something*. Je, anatumia kwamba aliyoyasema yatatekelezeka kwa sababu tumekuwa tukipewa mipango mingi lakini miaka inavyokwenda kilimo kinazidi kushuka? (Makofi)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru swali nimelipata.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ukuaji wa kilimo uko chini katika mwaka 2010/2011 kilimo kilikua kwa asilimia 4.2 kwa mwaka. Hiyo ilitoka kukua kwa asilimia 3.2 mwaka ule wa nyuma na asilimia 2.9 kama alivyosema katika mwaka ule uliopita.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ukiangalia hizo takwimu nzuri utakuta kwamba kuna *general trend* ya ukuaji wa kilimo kuongezeka. Ningependa pia niseme kwamba hivi sasa katika mwaka 2010/2011 kama Watanzania tulizalisha asilimia 112.8 ya chakula chetu chote tunachokula sisi wenyewe kutoka asilimia 95 ya chakula tunachokula katika msimu uliopita. (Makofi)

Hivi sasa tumeangalia mipango yetu ambayo tunayo katika kilimo kwa undani zaidi na kwa kupitia *Comprehensive African Agriculture Development Programme*, tumeshirikiana na wadau wetu wa maendeleo na kutengeneza mpango wa uwekezaji katika kilimo au *Tanzania Agriculture and Food Investment Programme*, ambayo tunategemea utatumia shilingi trilion tano katika miaka sita inayokuja. Tunategemea katika mipango ile ambayo inalenga katika kuongeza umwagiliaji, kuongeza uzalishaji na kuongeza ubora wa chakula na kutumia dhana bora kuwekeza katika maeneo ambayo yana uwezekano wa kutoa maendeleo ya haraka; kwa mfano, kama kwenye mbogamboga, kwenye matunda, kwenye maua, kuongeza uzalishaji wa mpunga na nafaka kwa ujumla kwamba katika miaka hii mitano inayokuja, kilimo kitakuwa kwa asilimia sita mpaka nene kwa mwaka.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nina maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Wewe ni swali la nyongeza siyo swali lako hili.

**MHE. MOSHI S. KAKOSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amejibu maswali vizuri lakini sijaona mahali ambapo ameelekeza mpango mkakati juu ya kuwasaidia wakulima kuhakikisha wanasindika mazao yao ambayo naamini yatawasaidia kuboresha au kupandisha mazao yale yawe na thamani. Sijaona mpango mkakati ameeleze vipi, lakini kuna sehemu nyingine ambapo ...

**SPIKA:** Linatosha hilo swali, kuboresha mazao. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakosa, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, sehemu ya mwisho kabisa ya jibu langu nimesema, Serikali itahimiza matumizi ya zana bora za kilimo na matumizi ya pembejeo na usindikaji wa mazao. Sasa siyo rahisi hapa nikaanza kutoa programu nzima ya kusindika mazao katika kipindi hiki kifupi, lakini kwa kifupi tu ni kwamba, lengo letu ni kuhakikisha mazao yetu yote yanasindikwa nchini ili yaongezewe ubora, yapate bei nzuri ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kuanza sasa kutoa maelezo yote katika kipindi hiki.

Na. 104

#### **Bei Kubwa ya Pembejeo**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Azimio la Kilimo Kwanza limerejesha matumaini ya wakulima kwa Serikali yao ingawa zipo changamoto kadhaa zikiwemo za pembejeo kuwa na bei kubwa; kuchelewa kuwafikia wakulima pamoja na tatizo la vituo vya ununuzi wa mazao ya wakulima:-

(a) Je, Serikali inakubaliana na ushauri kuwa ni vyema kuongeza ruzuku katika kilimo ili pembejeo zipatikane kwa bei ya chini?

(b) Je, Serikali inakubaliana na ushauri kuwa pembejeo ziwe zinawafikia wakulima mwezi Julai wakati bado wakiwa na uwezo wa kuzinunua?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianza kutoa ruzuku ya mbolea katika mwaka 2003/2004, kwa lengo la kuhamasisha wakulima kutumia mbolea ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula, hususan zao la mahindi. Aidha, Serikali imekuwa ikiongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo kama mbolea, mbegu bora na madawa ili zipatikane kwa bei ya chini. Kwa mfano, kiasi cha mbolea ya ruzuku kimeongezeka kutoka tani 80,005 za mwaka 2007/2008 hadi tani 141,050 mwaka 2008/2009 kutoka tani 150,000 mwaka 2009/2010 hadi tani 200,000 za mwaka 2010/2011.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali inatoa ruzuku ya pembejeo kwa kiwango cha asilimia 50 ya bei ya soko ili kuhakikisha kuwa mbolea za kupandia (DAP na Minjingu) na mbolea ya kukuzia (aina ya UREA) na mbegu bora ya mahindi na mpunga zinapatikana kwa bei nafuu.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, changamoto kubwa inayosababisha mbolea yenye ruzuku kuchelewa kuwafikia wakulima, *underline* mbolea yenye ruzuku kuchelewa kuwafikia wakulima; ni ucheleweshaji wa kuchapishwa kwa vocha za pembejeo. Ucheleweshaji huu unatokea kila mwaka kwa sababu fedha za ruzuku ya pembejeo

huidhinishwa kila mwaka katika Kikao cha Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaloanza mwezi Juni hadi Agosti. Serikali imeiona changamoto hii.

Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Fedha na Bunge zima ili kupata njia bora itakayoaidia Wizara yangu kupata fedha au mfumo wa kuweza kuagiza mbolea mapema kuliko ilivyo sasa.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Mkoa wa Rukwa na hususan Wilaya ya Nkasi na Jimbo la Nkasi Kusini tumeitikia vilivyo Sera ya Kilimo Kwanza na kutokana na mwitikio huo tumeweza kulima na tunayo ziada ya kutosha. Je, Serikali itatusaidiaje kutoa changamoto iliyoko mkononi ambayo inauwa kabisa afya ya kilimo katika Mkoa wa Rukwa?

(ii) Pamekuwepo tabia ya Serikali kuzuia fursa za masoko yanayojitokeza kwa wakulima kwa kisingizio kwamba yanaweza yakasababisha uhaba wa chakula na hii imedhihirika mwaka jana ambapo palikuwa na soko zuri lakini tulizuiwa na leo tunahangaika na masoko ya mazao ambayo tunayo. Je, Serikali ipo tayari kuacha mara moja tabia ya kuzuia mazao ya wakulima wasipate soko linalojitokeza?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Desderius John Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna ziada ya mazao ambayo bado wakulima wanayo kwenye mikono yao na Serikali inashughulikia suala hili kwa maana ya kutafuta fedha ili kuweza kununua sehemu kubwa ya ziada hiyo ambayo ipo mikononi mwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala la masoko ya ziada ni suala la msingi na tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vizuri tupanue masoko ili wakulima waweze kuuza mazao yao mara tu wanapoyavuna.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba katika msimu wa mavuno uliopita, yapo maeneo ya nchi yetu hasa Ukanda wa Ziwa Victoria, ambayo yalikuwa na njaa kubwa na kwamba tahadhari iliyochukuliwa ilikuwa kujaribu kuwanusuru wenzetu ambao wamepatwa na matatizo ya njaa ili chakula chote kisitoke nje na huku ndani tukawa na maafa ya njaa.

Mheshimiwa Spika, pili; ni ukweli usiofichika kwamba watu wengi waliokuwa wananunua mazao ya wakulima na kuyasafirisha nje kupitia njia za panya, walikuwa wanakwenda nyumbani kwa wakulima na kuwapa bei ya chini sana.

Serikali kwa kuingilia kununua mazao yale kutoka kwa wakulima kwa shilingi 350 kwa kilo, imeweka bei ambayo imekuwa ni msaada mkubwa sana kwa wakulima. Jana tulikuwa na mazungumzo na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani kuangalia kama nchi yetu inaweza kuwa *source country* au nchi ambayo inaweza kutoa chakula kwa muda mrefu kwa watu wenye njaa duniani na tumekubaliana kwamba, mwaka huu watanunua tani 90,000 na mwaka kesho kiasi hiki kitaongezeka kufikia tani 200,000. Tunategemea kwamba katika kipindi cha miaka mitano kiasi hiki kitapanda kifiki tani nusu milioni. Soko hili litakuwa linaweka msingi kwa masoko mengine na bei nzuri kwa wakulima ukichanganya na matumizi yetu wenyewe; hili litatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Sera ya Kilimo Kwanza ni Sera ya Chama cha Mapinduzi iliyohamasisha Wananchi kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi hasa mahindi katika Nyanda za Juu Kusini na hasa Wilayani Ludewa; na kwa kuwa ni Serikali hii ya kwetu iliyozuia wanunuzi binafsi wasinunue mahindi; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Bunge la mwezi Novemba aliahidi kwamba yale mahindi waliozuia Serikali ingenunua; na

kwa kuwa kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Rais mwezi ule ule wa Novemba alifanya ziara Wilayani Ludewa na akawaahidi Wananchi kwamba mwezi Novemba mwaka jana yale mahindi yaliyobaki mikononi mwa wakulima yangenunuliwa; na kwa kuwa sasa hivi ninavyozungumza ...

**SPIKA:** swali, swali.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, mahindi yale ya Wananchi yanaoza mikononi mwao, pembejeo wameshindwa kununua wakati maeneo mengine kama Meatu na Longido kuna njaa. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri umeshindwa kutekeleza ahadi ya Rais ya kununua mahindi kule Ludewa; kwa nini Waziri wa Kilimo na Chakula na Waziri wa Fedha msijuzulu kwa kushindwa kutimiza wajibu wenu? *(Makofi)*

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu nini? Naomba tumalize maswali halafu tuendelee. Mheshimiwa Waziri, maswali ya nyongeza yasiwe marefu kama lilivyoulizwa sasa, naomba Waziri utajibu lakini na wewe jibu kwa kifupi tafadhali tuko nje ya wakati.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu nafasi mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Moja!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, moja. Siyo kweli kama tulizuia watu binafsi wasinunue mahindi ya wakulima, kwa sababu Tangazo la Serikali lilihimiza wanunuzi wa ndani wanunue mahindi kutoka kwenye maeneo yenye ziada na kuyapeleka kwenye maeneo ambayo yana njaa. Ni kweli kwamba, wanunuzi wengi walikuwa wanakwenda nyumbani kwa wakulima, wananunua mahindi kwa bei rahisi sana ...

**SPIKA:** Naomba ujibu swali muda hautoshi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, tunatafuta fedha kwa nguvu sana kwa ajili ya kuyarudia yale mahindi na kuyanunua na nategemea kwamba, katika muda usiokuwa mrefu, tutapata fedha na tutanunua mahindi mengi ambayo yako mikononi kwa wakulima.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu; utaratibu gani?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka utaratibu wa kuuliza maswali ya nyongeza ulioko katika Kanuni ya 45(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili Tukufu ufuatwe na Kanuni yenyewe inasema; swali lolote la nyongeza ambalo linaleta mambo yasiyotokana au kuhusiana na swali la msingi au linakiuka masharti yanayohusiana na taratibu za kuuliza maswali, litakataliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wanauliza maswali ya nyongeza ambayo hayatokani na swali la msingi na wanaruhusiwa; inakiuka Kanuni za Bunge hili Tukufu!

**SPIKA:** Nafurahi imetoka kwenye *floor*. Anachokisema ni kweli, maana unakuta swali la kwa mfano la mwulizaji wa mwisho lilikuwa sahihi pale aliposema mbona unasema utanunua mahindi; kwa nini kule kwetu hamkununua! Lile lilikuwa sahihi, kwa kusema tena watu wengine wajuzulu na vitu kama hivyo, halikuwa sahihi kwa sababu swali la msingi halikudai mtu yeyote kujuzulu.

Alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu ni kweli, unaweza kuuliza swali la msingi, ukaanza kuuliza habari za swali la kwako kule, mimi nasema saa nyingine Mawaziri ni *very brilliant*; maana unauliza swali la Kijiji kingine na Vijiji vingi ambavyo yeye hakujiandaa kwa sababu siyo swali; kwa hiyo mnapata majibu hafifu kwa sababu hawayajui hayo. Ulikuwa unasema ila kwa sababu nimemwambia ajibu atajibu tu lakini siyo sahihi kama anavyosema. Swali la nyongeza lazima liwe la jumla sana kiasa kwamba, Waziri yeyote anaweza kujibu siyo kuingia *specific* na kijiji fulani na kijiji fulani na wewe hili siyo swali lako. Kwa hiyo, alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu ni sahihi na pia Kanuni nyingine inasema kusimamia humu ndani sisi wote tunaweza kusimamia hasa kwa utaratibu. Nashukuru kwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa ninao wageni walioletwa mbele yangu hapa, orodha yao ni kama ifuatavyo:-

Katika *Speaker's Gallery* tunae Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambaye amefuatana na Maafisa kutoka Ofisi yake naye ni Mheshimiwa Ludovick Utuoh; ahsante.

Tunashukuru maana wewe ni mdau wa Wabunge; kwa hiyo, ni vizuri kuwa unakuja mara kwa mara. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine; yupo Ndugu Hussein Bashe, huyu ni Mtendaji Mkuu wa *New Habari Corporation*; yuko wapi? Huyu ni mgeni wa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Omari Nundu, Waziri wa Uchukuzi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka; sasa sijui maji taka yanahusu wapi huko na hawa wageni wako wapi? Ahsanteni sana. Hawa ni Wataalamu nadhani kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka sijui kama ni Dodoma au wapi, lakini karibuni sana. Tuna wanafunzi saba wa Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir kutoka Chuo cha Biashara Dodoma (*CBE*); wako wapi? Ahsante sana. Tuna wageni wengine wanane wa Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, ambao ni Madiwani na Mwenyekiti wa CCM Babati Mjini; wako wapi hawa? Yupo Askofu Mtatu Ihucha; yuko wapi? Ahsante, asifiwe sana. Tuna wageni wengine; kuna mtoto wa Mheshimiwa Anna Kilango anaitwa William John Malecela; yuko wapi? Aah! Huyu hapo. Tuna Ndugu Agnes Stephano; huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Rachel Mashishanga; sijui ni nani? Ahsante sana.

Tuna wageni kutoka Jimbo la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Donald Kelvin Max na Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa Josephine Chagula, ambao ni Madiwani kumi na Mkurugenzi wa Mji Mdogo wa Geita. Mkurugenzi wa Mji wa Geita pamoja na Madiwani wasimame. Hawa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge hapa. Waheshimiwa Madiwani mnakaribishwa. Ahsanteni. Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha St. John's cha Dodoma. Hawa ni majirani zetu hapa; wako wapi wanafunzi wa St. John's? Ahsanteni, endeleeni kukiimarisha Chuo chenu ni kizuri sana.

Tuna Wananchi sita kutoka Dodoma Mjini wakiongozwa na Ndugu Isihack Hamisi Marengu, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Hao nao wako wapi? Ahsanteni sana, karibuni na ninyi Dodoma; ni karibu kwa hiyo mnaweza kupata nafasi mara nyingi. Tuna Maafisa wanne kutoka Shirika la Taifa la Nyumba Dar es Salaam. Wageni wa *National Housing* kutoka Dar es Salaam wako wapi? Tuna wageni wengine waliokuja pia kujifunza hapa ni Ndugu Lainus Mwita na Ndugu Anna Lusobany; ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. Augustine (*SAUT*) - Tabora; hawa wako wapi? Karibuni sana na tunawatakia mafunzo mema.

Naona kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Mwanjale, hawa nafikiri nao ni Madiwani; kuna Mheshimiwa Hamisi Mashang'ombe, Diwani wa Kata ya Ilungu na kuna Ndugu Pendo Kiando, Kata ya Ilungu pia. Kuna Mheshimiwa Fred Mwakwenja, Diwani wa Kata ya Igoma na kuna Jackson Waziri, mwanafunzi wa Chuo cha Hombolo. Kwa hiyo karibuni Waheshimiwa Madiwani, mjifunze shughuli pamoja na wageni wengine wote mnakaribishwa, Bunge lipo wazi kwa kila mtu kuja kulisikiliza. (*Makofi*)

Tunayo matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa D.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, Kamati hiyo itakutana tarehe 9 Februari kuanzia saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231. Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati hiyo wahudhurie. Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Basement hapo chini. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Kabwe Zitto, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Daktari Augustino Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa; mtaelewana huko huko kuna kumbi kama tatu pale.

Mheshimiwa Simbachawene, umeandika mara mbili, nadhani tumeshakubaliana kwamba Kamati Ndogo Ndogo pia zitakaa. Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Chumba Namba 219. Mwenyekiti wa Shirika la Kupambana na Rushwa (APNAC), Mheshimiwa Daktari Mary Mwanjelwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati Kuu ya APNAC kuwa, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa hapo naona mpo watatu, lakini kumbi zinatoshia pale mtajua wenyewe mtakavyojipanga. Mkurugenzi wa Habari, Elimu kwa Umma na Uhusiano wa Kimaifa kutoka Ofisini hapa, kutoka Mezani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Jossey Mwakasyuka, anasema kwamba; Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Mbunge wa Jimbo la Uzini, Zanzibar, ametunukiwa Shahada ya Uzamifu katika Fasihi ya Kiswahili (*Doctor of Philosophy in Literature*) ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwenye mahafali yaliyofanyika mwezi Novemba 2011.

Mada aliyoifanyia utafiti na kuwasilisha andiko inaitwa "Chanjo za Matakwa ya Mwanamume katika mwili wa Mwanamke." Hii hatari! Sasa ulinganisho wa ushairi wa miaka ya nyuma ya Bin Haji na Shaaban Robert, tasnifu yake imechambua kazi za washairi maarufu wa Kiswahili kuhusiana na mwanamke na ni ya pekee kutumia nadharia ya kisiasa, mkazi wa karne nne zilizopita na uhalisia wa kiuandishi ili kuweka bayana tatizo la usawa wa kijinsia katika jamii na pendekezo la utatuzi wa hali hiyo kwa kutumia sanaa ya fasihi hususan ushauri wa Kiswahili. Nadhani hayo maandiko au hicho kitabu atakuwa nacho, atapenda kuuza. Wapo na Madaktari wengine humu ndani tutawataja siku nyingine, yuko Daktari Shekifu hapo naye, yupo Daktari mwingine nimekwishamtaja, wapo wengi tu waliomaliza udaktari. Kwa hiyo, siku nyingine tutawataja, mkikuta nawaita watu madokta mjue wamepanda ngazi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Msitumie muda kuomba mwongozo bila sababu. Haya Mheshimiwa Mussa.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, mimi nina *interest* kidogo kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**SPIKA:** *Interest* haitoshi; unataka kusemaje sasa?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mwongozo wangu Mheshimiwa Spika ...

**SPIKA:** Mwongozo unaoomba?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako; marekebisho ya Sheria yasiendelee leo kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), haya ni marekebisho ya nchi



mbili na wakati tulipokuwa tukiunda Sheria hii ya Katiba, nchi zote zilishirikishwa, lakini leo marekebisho haya yanakuja bila ya kuishirikisha nchi moja! Kwa kuwa Muswada huu unahusisha nchi mbili za Muungano, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwongozo wangu ni kwamba, Muswada unaendelea. Kwanza kabisa, uko nje ya utaratibu. Mimi sijamaliza kazi yangu, umeharakisha kazi ya Spika. Kwa hiyo, hiyo ni sababu ya kiutendaji. Kwa ujumla ni kwamba, tuingie kwenye mwongozo utaeleza wapi hawakushiriki. Maana tuseme tunafunga hivi, tuanze kazi na wewe utapata nafasi ya kuzungumza, utaeleza wapi haukushiriki na unatakiwa ushiriki namna gani. Tunaendelea na kazi yetu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba tujadili kuna jambo la dharura lingine; kuna Wanajeshi walifika kwenye Ofisi ya Mbunge wa Muhambwe, wakilalamika kwamba hawajalipwa maslahi yao toka mwaka 2007. Sasa nimekuwa naomba kwamba, tulijadili jambo hili kama la dharura, kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1), hizi sekta nyeti kama Madaktari na Wanajeshi, kuna Maaskari Magereza kule kwangu wamekosa umeme. Sasa ningepomba tuzijadili sekta hizi muhimu kama mambo ya dharura kabla Bunge hili halijaisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali, Bunge ni mahali pa kujadili jambo mahususi linalogusa watu wengi kwa pamoja na limevunja matatizo ya kisera namna hii. Sasa tukijadili kila dharura, kila mahali na kwa kila mmoja wetu hamtafika. Hili litakuwa siyo Bunge litakuwa sijui ni kitu gani! Sasa nimewaeleza hawa jamaa; Waheshimiwa Wabunge, hawa Mawaziri wako hapa ku-address issues ambazo ni *specific*. Mbunge yeyote mzuri atawatumia hawa kikamilifu; yaani Mbunge yeyote makini atawatumia hawa kikamilifu.

Wale watu wako watafurahi siyo kwa sababu sisi tumejadili hoja, watafurahi kwamba yale madai yao yamepata majibu. Mbona jana Mheshimiwa Machali naye alileta maneno hapa dharura, dharura; kweli tunakumbuka askari waliwapiga watu wakakimbia sijui wakaenda wapi, amekwenda kazungumza na Waziri amepata majibu.

Kazi ya Mbunge ndiyo hiyo na tukikaa hapa sababu hizo ndiyo na ndiyo maana tunapenda Mawaziri wawe *available* kwa Mbunge yeyote. Tafadhali, tusitumie muda vibaya. Kwa hiyo, hilo suala lako hakuna cha dharura wala nini, Mbunge mzuri nenda ukakutane na wenzio Mawaziri hao wakupe majibu. Katibu tunaendelea na hatua inayofuata.

#### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

##### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

#### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

##### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

#### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

##### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

## NOTICE

---

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,  
19<sup>th</sup> December, 2011

**PHILLEMÓN L. LUHANJO**  
*Secretary to the Cabinet*

### **A BILL** *for*

An Act to amend the Constitutional Review Act, 2011.

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

Construction  
Act No.8  
of 2011

**1.** This Act may be cited as the Constitutional Review (Amendment) Act, 2011 and shall be read as one with the Constitutional Review Act, 2011.

Amendment  
of sections 6  
and 18

**2.** The Constitutional Review Act, 2011 is amended as follows:

- (a) in section 6(5), by deleting in paragraph (a)-
- (i) a "comma" and substituting for it the word "and";
  - and
  - (ii) the phrase "or a leader of a political party of any category";
- (b) in section 18, by adding the following provision immediately after subsection (5):
- “(6) For the purpose of this section, the Commission may allow organisations, associations or groups of persons to convene meetings in order to afford opportunity to its members to air their views on the Draft Constitution and forward such views to the Commission.”

## OBJECTS AND REASONS

---

This Bill propose amendments to sections 6 and 18 of the Constitutional Review Act, 2011 for two purposes: first, debarring from appointment as Commissioners members of the public who are not Members of Parliament, Members of House of Representatives of Zanzibar or Councilors. Secondly, it is sought to allow organizations, associations and groups of persons to collect views of their members on the Draft Constitution and forward such views to the Commission.

Dar es Salaam,  
14<sup>th</sup> December, 2011

**CELINA O. KOMBANI**  
*Minister for Constitutional and Legal Affairs*

## TANGAZO

---

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni, unachapishwa kwa taarifa kwa umma pamoja na maelezo ya sababu na madhumuni yake.

Dar es Salaam,  
19 Desemba, 2011

**PHILLEMONT L. LUHANJO**  
*Katibu wa Baraza*

Muswada  
kwa

Ajili ya kufanya marekebisha katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

**Imetungwa** na Bunge la Jamhuri ya Muugano wa Tanzania.

Jina la Sheria Na. 8 ya mwaka 2011

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Marekebisha ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 na itasomwa ikiwa ni sehemu ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka, 2011.

Marekebisha ya Vifungu vya 6 na 18

**2.** Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 inafanyiwa marekebisha kama ifuatavyo:

- (a) katika kifungu 6(5), kwa kufuta katika aya ya (a) -
  - (i) "mkato";
  - (ii) maneno "au kiongozi wa chama cha siasa katika ngazi zote";
- (b) katika kifungu cha 18, kuongeza masharti yafuatayo mara baada ya kifungu kidogo cha (5):
  - "(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume inaweza kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume."

---

## MADHUMUNI NA SABABU

---

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisha katika vifungu vya 6 na 18 vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 kwa sababu mbili. Kwanza kuondoa kizuizi cha kutoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume baadhi ya watu ambao si Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au Madiwani. Pili, kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume

Dar es Salaam,  
14 Desemba, 2011

**CELINA O. KOMBANI**  
*Waziri wa Katiba na Sheria*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani na kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2012 (*The Constitutional Review (Amendment) Act, 2012*).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Waandishi wa Sheria, Kamati na baadhi ya Wabunge kutoka vyama vyote vya siasa. Ninawashukuru sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Namshukuru pia Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo na kupitia kwao Wajumbe wote wa Kamati, kwa mchango na kazi kubwa waliyoifanya kuboresha Muswada huu. Maoni na ushauri wao, kwa kiasi kikubwa vimetusaidia kuuboresha Muswada huu kama inavyothibitishwa katika Muswada unavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, ambalo Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa leo asubuhi. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Na. 8) ya Mwaka 2011, ilipitishwa na Bunge hili katika Mkutano wake wa Tano. Tunaleta mapendekezo ya kufanya marekebisho hayo muda mfupi tu baada ya Bunge kutunga Sheria hii na baada ya Mheshimiwa Rais kuiridhia tarehe 29 Novemba, 2011 na kuanza kutumika tarehe 1 Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Na. 8) ya Mwaka 2011, ilipitishwa na Bunge hili katika Mkutano wake wa Tano. Tunayaleta mapendekezo ya kufanya marekebisho haya muda mfupi tu baada ya Bunge kutunga Sheria hii na baada ya Mheshimiwa Rais kuiridhia tarehe 29 Novemba 2011 na sheria ilianza kutumika tarehe 1 Desemba 2011. Mantiki ya marekebisho haya na kama yatakubaliwa na kupitishwa na Bunge hili, yanalenga kuuboresha Sheria hiyo na kuwezesha kuwepo kwa Mwafaka wa Kitaifa katika kuendesha mchakato wa kuipata Katiba Mpya. Jambo lolote linalotuwezesha kuwa na Mwafaka wa Kitaifa katika jambo muhimu kama mchakato wa kupata Katiba Mpya inayokidhi matarajio, matumaini na mahitaji ya Watanzania wengi ni jambo jema na linalopaswa kupewa nafasi kila inapowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, historia ya kuupitisha Muswada huo kuwa Sheria hii hapa Bungeni inaeleweka na sina sababu za msingi za kuirudia historia hiyo. Kama mnavyofahamu, kabla na baada ya Rais kusaini Sheria hiyo, Mheshimiwa Rais aliendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu namna ya kuuboresha Sheria hiyo ili kuwezesha kuwepo Mwafaka wa Kitaifa. Natumia nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na wale wote ambao walimwona katika mazungumzo na kuafikiana. Maoni hayo yalitolewa na Vyama vya Siasa vyote, Asasi za Kiraia na Jumuiya za Kidini. Kwa kuzingatia baadhi ya maoni yaliyotolewa, Serikali imetoa mapendekezo ya kurekebisha Sheria hiyo kama yalivyoainishwa kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu vya 6, 12, 13, 17, 18 na 21 vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Lengo la mapendekezo haya katika vifungu hivyo ni kuondoa sharti la Viongozi wa Vyama vya Siasa, kwa ngazi yoyote kutoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume; kumruhusu Rais kualika Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu; Mashirika ya Dini, Taasisi, Asasi na makundi mengine ya watu wenye malengo yanayofanana kutayarisha Orodha ya Majina ya Wajumbe ili Rais achague miongoni mwao Wajumbe wa Tume; na kuainisha utaratibu wa kumwondoa Kamishna wa Tume na kuruhusu Wakurugenzi wa Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Manispaa na Makatibu wa Mabaraza ya Miji au Wilaya, kupokea taarifa za programu zitakazoendeshwa katika maeneo yao, badala ya Wakuu wa Wilaya. Aidha, marekebisho hayo yanalenga pia kuruhusu Jumuiya, Asasi, Taasisi au makundi ya watu yenye malengo yanayofanana kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa ajili ya kukusanya maoni juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali la Marekebisho, tunapendekeza kuwa Ibara ya pili ya Muswada ifanyiwe marekebisho kwa kuiandika upya. Lengo la mapendekezo hayo ni kuondoa kizuizi kwa Madiwani kuwa Wajumbe wa Tume. Kwa kuwa Madiwani hawataingia katika hatua ya Bunge Maalum la Katiba, tunapendekeza kuwa wasizuiwe kuwa Wajumbe wa Tume iwapo itaonekana kuwa wapo wenye sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Jedwali la Marekebisho linapendekeza kuongeza masharti katika Ibara hiyo ya pili ya Muswada kwa kuongeza masharti mapya katika kifungu cha sita cha Sheria ya Marekebisho ya Katiba. Masharti

yanayopendekezwa yanalenga kumwezesha Mheshimiwa Rais kuvialika Vyama vya Siasa, Mashirika ya Kidini, Asasi za Kiraia, Jumuiya, Taasisi na makundi mengine yenye malengo yanayofanana, kumpatia orodha ya majina, ambayo miongoni mwao Rais atateua Wajumbe wa Tume. Hii tunaona itasaidia kuweka uwazi na ushirikishi wa Wananchi katika hatua ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume. Aidha, masharti mengine yanayoongezwa katika kifungu hicho yanalenga kuweka bayana kuwa pamoja na kualika Vyama vya Siasa, Mashirika ya Kidini, Asasi za Kiraia, Jumuiya na Taasisi na kuteua Wajumbe kutoka miongoni mwa majina hayo, Rais hatazuiwa kuteua Wajumbe wengine ambao ataona wanafaa kuwemo kwenye Tume. Aya B ya Jedwali la marekebisho inapendekeza kuingiza masharti mapya katika kifungu cha 12 ili kuainisha jinsi Mjumbe wa Tume atakavyoondolewa kwenye Tume. Inapendekezwa kwamba, iwapo suala la kumwondoa Mjumbe wa Tume litajitokeza, basi Mheshimiwa Rais awateue Wajumbe wa Kamati kuchunguza suala hilo. Kamati hiyo itakuwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar atakayeteuliwa na Chama cha Wanasheria cha Zanzibar na Wakili wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society*). Aidha, inapendekezwa kuwa, Kamati hiyo ipewe pia mamlaka ya kutengeneza taratibu zitakazoongoza katika kufanya uchunguzi. Marekebisho mengine yanayopendekezwa katika kifungu cha 13 cha Sheria hiyo katika kifungu kidogo cha (6) kwa azma ya kuifanya Tume kuwa mamlaka ya nidhamu kwa Wajumbe wa Sekretarieti. Sheria ya sasa ilivyo haioneshi mamlaka ya nidhamu kwa Wajumbe hao.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 17 cha Sheria ili kuwezesha Tume kufanya kazi na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa upande wa Tanzania Bara na Mkurugenzi wa Manispaa na Makatibu wa Mabaraza ya Miji au Wilaya kwa upande wa Tanzania Zanzibar katika uandaaji wa mikutano na hadhira zenye kufanana na hizo badala ya Wakuu wa Wilaya walioainishwa kwenye Sheria. Marekebisho mengine yanapendekezwa katika kifungu hicho hicho ili kuruhusu mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana kuendesha Programu ya Elimu kwa Umma kuhusu mabadiliko ya Katiba baada ya kutoa taarifa, kusajiliwa na kuainisha chanzo cha mapato ya kuendesha Programu hiyo kwa Tume. Inapendekezwa pia kuwa Asasi, Taasisi, Jumuiya au vikundi vyenye malengo yanayofanana viruhusiwe kuandaa mikutano kwa lengo la kukusanya maoni ya Wanachama wao kuhusu Katiba na kisha kuyawasilisha kwenye Tume. Hata hivyo, endapo asasi, taasisi, jumuiya au vikundi hivyo vitataka kufanya mikutano au mikusanyiko ya hadhara, watalazimika kutoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa mujibu wa Sheria husika za Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mwisho yanapendekezwa kufanywa katika kifungu cha 21(3) ili kupunguza adhabu kwa watu watakaokiuka masharti ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Adhabu inayopendekezwa ni faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitatu badala ya faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kifungo kwa muda usiopungua miaka mitatu na usiozidi miaka saba inayoainishwa kwenye Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninapenda kupitia kwako, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, waujadili Muswada huu na kuipitisha katika hatua mbili; yaani Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu. Nina imani kwamba, Bunge lako litaridhia marekebisho yote yanayopendekezwa na litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 ili mchakato wa kupata Katiba Mpya nchini mwetu uanze.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora; Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Namba 8) wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa shukrani za dhati na za kipekee kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kusaini Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa 2011, tarehe 29 Novemba 2011. Kwa kweli, bila Rais wetu kusaini Muswada huu kuwa Sheria, Sheria hii isingeweza kuanza kutumika. Hivyo basi, tunamshukuru sana kwa kuruhusu Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba kuanza kutumika na sasa mchakato wa Mabadiliko ya Katiba utaweza kuanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipangia Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 27 Januari 2012, Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mbunge, pamoja na Wataalam wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata ufafanuzi wa Serikali kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilialika Wadau mbalimbali tarehe 27 Januari 2012 kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao juu ya Muswada huu kwa madhumuni ya kuuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani kwa Wadau waliofika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao pamoja na wale waliotoa maoni yao kwa maandishi. Kamati inatambua mchango mzuri wa Wadau hao ambao ni pamoja na Baraza la Taifa linalosimamia Asasi zisizokuwa za Serikali (CONGO), Jukwaa la Katiba, *United Democratic Party (UDP)*, Chama cha NRA, Chama cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Chama cha Wananchi (CUF), Chama cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), Chama cha APPT – Maendeleo na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho, mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu unapendekeza kufanya Marekebisho katika Vifungu vya 6 na 18 vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011, kwa madhumuni ya kuondoa kizuizi kwa baadhi ya watu ambao siyo Wabunge wala Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kutokuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume na pia kuruhusu asasi, taasisi na makundi ya watu kuitisha mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa Wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume. Aidha, baadaye mtoa hoja aliwasilisha Jedwali la Marekebisho baada ya majadiliano na Kamati kwa kuongeza vifungu vingine vipya kama inavyoonekana kwenye Jedwali hilo la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilitumia mamlaka yake kwa kumshauri mtoa hoja kuufanyia Muswada mabadiliko kama inavyoainishwa katika Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Kutokana na ushauri huo wa Kamati, mtoa hoja amewasilisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho ambalo Kamati ilipata fursa ya kulipitia na kufanya maboresho zaidi na kupata Jedwali la Pili la Marekebisho ambalo limezingatia maoni mbalimbali na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, utungaji wa Sheria ni lazima uzingatie masharti ya Katiba na mahitaji ya kisheria kwa wakati unaokusudiwa na kwa kuzingatia masharti ya Katiba iliyopo. Kamati yangu imepitia Muswada huu ili kujiridhisha na masuala ya msingi yanayopendekezwa pamoja na kasoro za kisheria zinazokusudiwa kurekebishwa. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, inatoa maoni na ushauri ufuatao kuhusiana na Muswada huu:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuondoa maneno "*au Kiongozi wa Chama cha Siasa wa ngazi zote*" kutoka katika Kifungu cha 6(5)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Namba 8) ya Mwaka 2011. Kamati ilielezwa na Serikali kwamba, mabadiliko haya yanalenga kuondoa kizuizi kwa baadhi ya watu ambao siyo Wabunge au Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au Madiwani kutoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Hata hivyo, baada ya majadiliano, Serikali ilikubali kufanya marekebisho zaidi kwenye kifungu hicho ili kizuizi kiwe kwa Mbunge na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, sababu za marekebisho hayo ni kutoa nafasi kwa Mheshimiwa Rais kumteua Mwananchi yeyote hata kama ni Mwanasiasa kuwa Mjumbe wa Tume, isipokuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ambao kwa mujibu wa Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Namba 8) ya Mwaka 2011 ni Wajumbe wa Bunge Maalum. Kamati inaamini marekebisho haya yatawezesha Wanasiasa ambao ni Wataalam na wenye uzoefu wa masuala ya Katiba na mabadiliko ya Katiba ambao hawakuainishwa kuwa Wajumbe wa Bunge Maalum kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge, kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume itakayosimamia na kuratibu Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba na hivyo kutumia utaalam na uzoefu wao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza kifungu kidogo cha 6 kwenye Kifungu cha 18 baada ya kifungu kidogo cha (5) kinachosomeka "*kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume inaweza kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa Wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume.*"

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano na Serikali, ilikubalika kufanya marekebisho zaidi kwa kuongeza Kifungu kipya cha 17(9) ili kuruhusu mtu binafsi, taasisi, jumuiya au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana, kuendesha Programu ya Elimu kwa Umma kuhusu Mabadiliko ya Katiba baada ya kutoa taarifa kwa Tume au kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa upande wa Tanzania Bara na kwa Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kusajiliwa kisheria na kubainisha chanzo cha fedha za kuendesha Programu hiyo. Aidha, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kuongeza Kifungu cha 17(10) kitakachoruhusu taasisi, asasi au vikundi vyenye malengo yanayofanana kuruhusiwa kuandaa mikutano kwa lengo la kukusanya maoni ya Wanachama wao kuhusu Mabadiliko ya Katiba na kisha kuyawasilisha maoni hayo kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kamati kuwa, fursa hii iliyotolewa kwa asasi, taasisi na makundi ya watu kuandaa mikutano na kisha kuwasilisha maoni yao kwenye Tume, itasaidia kuongeza ufanisi wa kazi za Tume. Kamati inatoa rai kwa jamii kuwa, pamoja na kutolewa kwa fursa hii, bado ieleweke wazi kwamba Tume ndiyo yenye jukumu na mamlaka ya kisheria katika kazi ya ukusanyaji wa maoni na hivyo taasisi, asasi na watu mbalimbali, wote watafanya kazi hiyo ili kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake na siyo kuchukua jukumu hilo la kisheria la Tume. Pamoja na yote hayo, Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali itoe ufafanuzi zaidi kwa Kifungu cha 17(9) kinachopendekezwa kuongezwa ili kuweka bayana tofauti ya Programu ya Elimu kwa Umma zinazolengwa na mapendekezo haya na mikutano ya hadhara ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322, mikutano ya hadhara hutarifiwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya. Kamati ilihoji endapo mtu binafsi, asasi au taasisi inayotaka kuendesha Programu ya Elimu kwa Umma kuhusu mabadiliko ya Katiba, baada ya kutoa taarifa itahitaji kupata kibali toka kwa Tume au kwa niaba yake toka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa au Katibu wa Baraza la Miji au la; maana kwa namna kifungu kinavyosomeka, hivi sasa haiko wazi ni nini kitafuata au kitatokea baada ya taarifa ya uendeshaji Programu ya Elimu kwa Umma kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza masharti mapya baada ya Kifungu cha 6(5) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho kwamba; "*kwa madhumuni ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3), Rais ataalika Vyama vya Siasa, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi na Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana, kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa Wajumbe.*"

Kamati inaishauri Serikali kuongeza maneno “vyenye usajili wa kudumu” kwenye kifungu hicho baada ya neno “siasa” ili vyama vya Siasa vitakavyodilikwa na Rais kuwasilisha orodha ya majina, viwe ni vile tu vyenye usajili wa kudumu. Kamati inapongeza nia njema ya Serikali, inayolenga kupata Tume bora inayotokana na Wananchi wa Makundi yote kwa kushirikisha Makundi mbalimbali ya watu katika jamii. Kamati inaamini kwamba, huu ndiyo utekelezaji dhahiri wa dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011, kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (4) na (5) katika Kifungu cha 12 cha Sheria Mama ili kuingiza masharti mapya kuhusu ukomo wa Wajumbe wa Tume. Kamati inaamini siyo tu kwamba haki itatendeka, bali itaonekana imetendeka endapo suala la kumwondoa Mjumbe kwa kukiuka Kanuni za Maadili litajitokeza na hivyo kumfanya Rais ateu Kamati itakayochunguza suala hilo. Kamati hiyo itaundwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani, ambaye Kamati imeshauri Muswada utaje bayana kwamba Jaji huyo wa Rufani ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kamishna wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar atakayeteuliwa na Chama cha Mawakili wa Zanzibar na Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania atakayeteuliwa na Chama cha Mawakili wa Tanganyika. Kamati hiyo imepatiwa mamlaka ya kutengeneza taratibu zitakazoiongoza katika kufanya uchunguzi. Aidha, Kamati hiyo ya Uchunguzi ikishamaliza uchunguzi itawasilisha mapendekezo yake kwa Mheshimiwa Rais na endapo Kamati itakuwa na maoni kwamba Mjumbe huyo aliyekuwa akichunguzwa asikome kuwa Mjumbe wa Tume, basi suala la kumwondoa Mjumbe huyo litakoma na Mjumbe huyo ataendelea kuwa Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati inakubaliana na mapendekezo kuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba iwe Mamlaka ya nidhamu kwa Wajumbe wa Sekretarieti kwa sababu itaweka uwajibikaji na kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti kwa Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho yanayopendekezwa na Serikali ya kufuta maneno “Mkuu wa Wilaya” yanayoonekana katika Kifungu cha 17(5)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na badala yake kuweka maneno “Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mtaa.” Aidha, kufuta maneno “Mkuu wa Wilaya” yanayoonekana katika Kifungu cha 17(5)(b) kinachohusu upande wa Zanzibar na kuweka maneno “Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji.” Kamati inaamini mapendekezo haya yamelenga kuufanya mchakato wa ukusanyaji wa maoni ya Katiba Mpya, usimamiwe na Watendaji wa Serikali na Watumishi ambao hawana itikadi ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na uwazi zaidi. Hata hivyo, Kamati inashauri maneno yanayojirudia rudia katika Muswada kama vile “Mkurugenzi”, “Katibu wa Baraza la Mji” na mengineyo, yapatiwe tafsiri ili yaweze kuwa sehemu ya tafsiri ya Sheria Mama; yaani Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kukifanyia marekebisho Kifungu cha 21(3) ili kupunguza adhabu kwa watu watakaokiuka masharti ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Adhabu inayopendekezwa ni faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitatu badala ya faini iliyokuwepo kabla, isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kifungo kwa muda usiopungua miaka mitatu na usiozidi miaka saba kama inavyoainishwa na Sheria ya sasa. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa sababu yanalenga kuoanisha adhabu zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 ziendane na adhabu zinazotolewa kwa mujibu wa Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 (*Penal Code, Cap. 16*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho haya, Kamati inashauri Serikali ilete Bungeni marekebisho mengine kadiri yatakavyokuwa yakihitajika mara kwa mara kwa lengo la kuiboresha Sheria itakayowezesha Nchi yetu kupata Katiba mpya.



Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ambao bila kuchoka na kwa kutumia uzoefu na utaalamu wao katika fani mbalimbali zikiwemo fani za Sheria, Utawala na kadhalika, walifanya kazi hii kwa ufanisi, umakini na uvumilivu mkubwa. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha ushauri huu wa Kamati napenda sasa kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii, waliouchambua Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mwenyekiti wa Kamati, mimi mwenyewe Angella Jasmine Kairuki - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abbasi Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Azza Hilal Hamad, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza, Mheshimiwa Tundu Antiphace Mughwai Lissu, Mheshimiwa Deogratius Aloyce Ntukamazina na Mheshimiwa Rashid Abdallah.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia wewe binafsi kwa kuendelea kutupatia ushauri na miongozo mbalimbali ambayo imetuwezesha kukamilisha kazi hii muhimu. Aidha, napenda pia kumshukuru Dkt. Thomas Kashiilah - Katibu wa Bunge, Ndugu Charles Mloka - Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Peter Magati - Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Bi. Catherine Kitutu - Mhudumu wa Kamati, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA:**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Marekebisho ya Katiba, Sheria Namba 8 ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Novemba 2011, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Siku kumi na moja baadaye, yaani tarehe 29 Novemba 2011, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alitoa kibali cha Muswada huo kuwa Sheria kwa mujibu wa Ibara ya 97(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kanuni ya 92(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007. Kwa mujibu wa kifungu chake cha 1(2), Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Namba 8) ya 2011, ilianza kutumika tarehe 1 Desemba 2011, yaani siku mbili tu baada ya kupata kibali cha Rais.

Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya 73 tangu Sheria hii ipate kibali cha Mheshimiwa Rais na siku 71 tangu ipate nguvu za kisheria ili ianze kutumika. Tumekutana hapa leo hii ili Bunge lako Tukufu lipate fursa nyingine tena ya kuitafakari Sheria hii. Kila mmoja wetu humu ndani na kila Mtanzania anayefuatilia mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya, anafahamu kwamba tendo la kwanza lililoidhinishwa na Sheria hii, yaani kuteuliwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, halijafanyika hadi sasa. Tumekutana leo hii ili kujadili na kama Bunge lako Tukufu litaridhika, kupitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria hii unaopendekezwa na Serikali na hivyo kumwezesha Mheshimiwa Rais kutenda tendo hilo la kwanza kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Novemba 2011, Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), iliunda Kamati Maalum ya Wajumbe saba, iliyopewa jukumu la kuonana na Mheshimiwa Rais kuhusu Sheria hii na mustakabali wa Taifa letu. Siku mbili baadaye, yaani tarehe 22 Novemba 2011, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mheshimiwa Freeman Mbowe, alimwandikia Mheshimiwa Rais, barua ya kumwomba kuonana na Kamati Maalum ya CHADEMA kwa siku na muda atakaoona yeye Mheshimiwa Rais unafaa.

Siku iliyofuata, yaani tarehe 23 Novemba, Mheshimiwa Rais alijibu maombi ya Mheshimiwa Mbowe kwamba, alikuwa tayari kukutana na Kamati Maalum tarehe 27 Novemba 2011. Kamati

Maalum ilikutana na Mheshimiwa Rais na Washauri wake Ikulu, Dar es Salaam, kwa zaidi ya saa tatu siku hiyo na kwa karibu saa nane siku iliyofuata, yaani tarehe 28 Novemba 2011. Mheshimiwa Rais na Washauri wake walikutana kwa mara nyingine tena na Kamati Maalum, siku ya tarehe 20 Januari 2012, wakati Taifa linaomboleza kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Jeremiah Solomon Sumari. Mara hii majadiliano hayo yalichukua zaidi ya saa sita na yalikiwisha majira ya saa sita usiku!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hakukutana na Uongozi wa CHADEMA peke yake; baada ya mkutano wake na Kamati Maalum ya CHADEMA na kwa nyakati tofauti, Mheshimiwa Rais alikutana pia na Wawakilishi wa Chama cha Wananchi (CUF), Chama cha NCCR-Mageuzi, Viongozi wa Taasisi Kuu za Kidini nchini na Wawakilishi wa Mashirika na Asasi zisizokuwa za Kiserikali. Aidha, kama alivyoeleza yeye mwenyewe wakati akihutubia Wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kilele cha kuadhimisha miaka thelathini na tano ya kuzaliwa kwa CCM, Mheshimiwa Rais alikutana pia na Uongozi wa CCM, ambapo alipokea mapendekezo manane ya marekebisho ya Sheria. Ni wazi kwamba, Muswada huu na Jedwali la Marekebisho lililoambatanishwa nao, umefaidika kwa busara za Mheshimiwa Rais, yeye mwenyewe pamoja na mawazo na mapendekezo ya wadau wengine wote ambao nimewataja hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine, Muswada huu hautokani na njama za vikao vya siri kati ya Mheshimiwa Rais na CHADEMA! Ni Muswada unaotokana na mwafaka kati ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake na makundi mbalimbali katika nchi yetu yanayowakilisha maslahi ya kisiasa, ya kijamii na hata ya kidini. (Makofi)

Huu ni Muswada unaoonesha uso halisi wa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimeeleza historia hii kwa kirefu ili Bunge lako Tukufu lipate ufahamu wa background ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ulioko mbele ya Bunge hili Tukufu. Hii siyo tu itawasaidia Waheshimiwa Wabunge kupata ufahamu wa mambo yaliyojiri tangu Sheria hii ilipopitishwa mwaka jana, bali pia inaonesha umuhimu wa Sheria hii na mapendekezo ya marekebisho yaliyoletwa Bungeni na Serikali. Sote tunajua jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais, kama Rais Mtendaji mwingine yeyote, ni mtu mwenye kazi na majukumu mengi kama Mkuu wa Nchi, Mkuu wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu. (Makofi)

Kwa sababu ya kazi na majukumu mengi aliyo nayo, Mheshimiwa Rais hana muda wa kupoteza wala wa kustarehe. (Makofi)

Kwa maana hiyo, Rais anapoacha shughuli zake nyingi nyingine za Kitaifa ili kuzungumza na watu ambao wala hawajibiki kisheria kukutana au kuzungumza nao kwa jambo lolote lile; Rais anapotumia siku nne na saa karibu ya ishirini kuzungumza nao juu ya jambo moja; Rais anapokubali kukaa hadi saa sita za usiku kujadiliana nao juu ya jambo hilo; na Rais anapokubali kuacha shughuli nyingine ili kukutana na Viongozi wa Vyama vingine vya Siasa, Viongozi wa Kidini na Wawakilishi wa Taasisi za Kiraia kujadiliana nao juu ya jambo hilo hilo, yote hayo yanadhahirisha umuhimu wa jambo hilo kwa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumekutana hapa leo kutafakari Sheria hii kwa sababu Mheshimiwa Rais mwenyewe, kwa muda mrefu aliutumia kukutana na kujadiliana nasi pamoja na wadau wengine, ameonesha dhahiri kwamba, Bunge hili Tukufu linahitaji kuitafakari upya Sheria hii muhimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, busara zetu na ufahamu wetu wa umuhimu wa Sheria hii kwa mustakabali wa baadaye wa nchi yetu na uzalendo wetu kwa Taifa letu na kwa kutambua kazi kubwa, mchango na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, vitatuongoza katika kuyajadili na kuyapitisha mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011 ili kumwezesha Mheshimiwa Rais kuunda Tume itakayoanzisha rasmi mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie jambo lingine la mwisho kabla sijafanya uchambuzi wa Muswada wenyewe na Jedwali la Marekebisho lililoambatanishwa nao. Ni kweli kama nilivyosema awali kwamba, Muswada huu unaletwa Bungeni kabla hata ya miezi mitatu

kupita tangu Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilipopitishwa na Bunge lako Tukufu na kupatiwa kibali cha kuanza kutumika na Mheshimiwa Rais. Kama nilivyosema mwanzoni, ni kweli kwamba Muswada huu unakuja Bungeni kabla tendo la kwanza lililoidhinishwa na Sheria yenyewe halijafanyika. Kwa vyovyote vile, hiki ni kipindi kifupi sana kwa Sheria kufanyiwa marekebisho. Kwa sababu hizi, wapo watakaohoji na wana haki ya kufanya hivyo; sababu au uhalali wa mapendekezo ya marekebisho haya katika kipindi hiki kifupi. Aidha, wapo watakaodhani kwamba mapendekezo haya ni ishara ya dharau kwa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa watu hao, nitasema yafuatayo: Kwanza, Katiba yetu haina na haijawahi kuweka muda au ratiba ya kufanya marekebisho ya Sheria yoyote ile. Badala yake, kifungu cha 24 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria (*The Interpretation of Laws Act*), Sura ya Kwanza ya Sheria zetu kimeweka wazi kwamba; "Sheria inaweza kurekebishwa au kufutwa kabisa katika Mkutano wa Bunge ule ule uliopitisha." Kwa maana hiyo, mapendekezo ya marekebisho haya yangeweza kuletwa hata kabla Mkutano uliopita wa Bunge hili Tukufu kumalizika na bado yangekuwa halali kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano wa karibuni kabisa wa jambo hili ni Sheria ya Gharama za Uchaguzi, 2010, iliyopitishwa katika Mkutano wa Thelathini na Nane wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano mwezi Februari 2010. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho katika Mkutano wa Thelathini na Tisa uliofanyika Aprili 2010 na mara mbili katika Mkutano wa Arobaini wa Bunge la Bajeti la mwaka huo. Aidha, Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, 2001 iliyopitishwa tarehe 28 Machi 2001 na kufanyiwa marekebisho katika Mkutano wa Bajeti uliofuatia tarehe 9 Agosti 2001. Kwa maana hiyo, hii siyo na haitakuwa mara ya kwanza kwa Bunge lako Tukufu kufanya marekebisho ya Sheria iliyotungwa katika Mkutano uliopita.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili inatokana na umuhimu wa Sheria inayofanyiwa marekebisho pamoja na umuhimu wa marekebisho yenyewe. Katika hili, ni vyema nikanukuu sehemu ya Waraka tuliomkabidhi Mheshimiwa Rais, siku ya tarehe 27 Novemba 2011. Sheria hii ni muhimu kuliko sheria nyingine yoyote ambayo Bunge la Kumi litapata fursa ya kujadili na kuipitisha. Huu ni Muswada wa kihistoria kwa vile tangu Uhuru wa Tanganyika, miaka hamsini iliyopita na tangu Muungano, miaka karibu arobaini na nane iliyopita, Watanzania hatujawahi kupata fursa ya kujadili na kuamua mustakabali wa Taifa letu Kikatiba kwa utaratibu kama uliowekwa katika Sheria hii." (*Makofi*)

Kama nilivyosema wakati nawasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba katika Mkutano uliopita mwaka jana: "Bunge hili Tukufu lina wajibu mbele ya historia na kwa vizazi vya sasa na vijavyo, kuhakikisha kwamba, tunapata Mwafaka wa Kitaifa juu ya Tanzania tunayoitaka." Muswada huu ni sehemu ya jitihada hizo za kuhakikisha tunapata Mwafaka wa Kitaifa juu ya Tanzania tunayoitaka.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 23 Desemba 2011, wakati majadiliano kati ya Mheshimiwa Rais na wadau wengine yakiwa hayajakamilika. Kama ulivyo sasa, Muswada huu una mapendekezo ya marekebisho ya vifungu viwili tu, yaani kifungu cha 6 na 18 vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Hata hivyo, Jedwali la Marekebisho lililoandaliwa na Serikali na kuwasilishwa Bungeni sambamba na Muswada huu, linapendekeza marekebisho katika vifungu vingine vya Sheria hii. Hii ni kwa sababu ilibidi Muswada uchapishwe katika Gazeti hata kabla mazungumzo kati ya Mheshimiwa Rais na wadau hayajakamilika ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 80(2) ya Kanuni za Bunge inayotaka Muswada kuwasilishwa kwa Katibu wa Bunge siku ishirini na moja kabla ya Kusomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni vyema na ni haki kuweka kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu kwamba, Jedwali la Marekebisho la Serikali ni matokeo ya ushiriki wa moja kwa moja wa Mheshimiwa Rais na Washauri wake; Mheshimiwa William Lukuvi, Mwanasheria Mkuu - Mheshimiwa Fredrick Werema, Mwandishi Mkuu wa Sheria - Ndugu Casimir Kyuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahuasiano na Uratibu) - Mheshimiwa Stephen Wasira na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi. Aidha, kwa upande wa CHADEMA ni vyema na ni haki kutambua kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, ushiriki na kazi kubwa iliyofanywa na

Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Taifa - Mheshimiwa Mbowe, Katibu Mkuu - Dkt. Wilbrod Slaa, Makamu Mwenyekiti (Bara) na Mbunge wa Mpanda Mjini - Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa John Mnyika - Mbunge wa Ubungo na Wajumbe wengine wa Kamati Maalum ya Kamati Kuu, Profesa Mwesiga Baregu na Profesa Abdallah Safari na Mkurugenzi wa Utafiti, Bunge na Halmashauri katika Makao Makuu ya CHADEMA – Ndugu John Mrema.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, sasa naomba niwasilishe uchambuzi wa Muswada wenyewe pamoja na Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Serikali, nikianza na mapendekezo ya marekebisho ya vifungu mbalimbali vinavyohusiana na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niwasilishe uchambuzi wa Muswada wenyewe pamoja na Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Serikali nikianza na mapendekezo ya marekebisho vifungu mbalimbali vinavyohusiana na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 6(5)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa kufuta maneno “au Kiongozi wa Chama cha Siasa wa ngazi yoyote.” Jedwali la Marekebisho la Serikali lililowasilishwa sambamba na Muswada huu linapendekeza marekebisho siyo tu ya kifungu cha 6(5)(a), bali pia kinapendekeza kuongezwa masharti ya ziada katika kifungu cha 6 cha Sheria. Kwanza, inapendekezwa kwamba maneno “Diwani au Kiongozi wa Chama cha Siasa katika ngazi zote” yafutwe na badala yake yabaki maneno “Mbunge na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.”

Mheshimiwa Spika, ili kuelewa maana ya marekebisho yanayopendekezwa ni muhimu kurejea katika kifungu cha 6(5) kinachopendekezwa kurekebisha na Muswada huu. Kifungu hiki kinaweka masharti ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kuwaondolea sifa za kuteuliwa Wabunge, Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Madiwani na Viongozi wa Vyama vya Siasa wa ngazi zote. Kwa mapendekezo ya Muswada huu na Jedwali la Marekebisho la Serikali, watu pekee ambao sasa hawatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ni Wabunge na Wawakilishi wa Zanzibar. Kwa maneno mengine, Madiwani na Viongozi wa Vyama vya Siasa wa ngazi zote watakuwa na sifa za kuteuliwa ilimradi tu wanazo sifa za kitaaluma na nyinginezo zilizotajwa katika kifungu cha 6(3) cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa mjadala wa kupitishwa kwa Sheria hii tarehe 15 Novemba mwaka jana, tuliliambia Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kukataza Viongozi wa Vyama vya Siasa kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume, kifungu cha 6(5)(a) “... kinaondoa kwenye mchakato wa Katiba Mpya kundi kubwa la watu wenye utaalamu na uzoefu katika masuala mbalimbali ya kisiasa, kikatiba, kisheria, kiuchumi, kiutawala, kifedha na kisayansi jamii. Vilevile Viongozi wa Vyama vya Siasa wanawakilisha makundi makubwa ya kijamii yenye mtawanyiko wa watu na wa kijiografia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanawakilisha watu wa umri na jinsia zote kama inavyopendekezwa katika sheria. Pendekezo letu kwamba Wabunge na Wawakilishi wa Zanzibar nao wawe na sifa za kuteuliwa Wajumbe wa Tume halipo katika mapendekezo ya Muswada huu na Jedwali la Marekebisho la Serikali. Hata hivyo, katika kuendeleza moyo wa maridhiano na *give and take*, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaridhika na kuunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 6(5)(a) ili kuwapa Madiwani na Viongozi wa Vyama vya Siasa, sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume.

Mheshimiwa Spika, kuna mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 6(5)(c) ambayo hayapo katika Muswada lakini yameletwa kwa njia ya Jedwali la Marekebisho la Serikali. Kifungu cha 6(5)(c) cha Sheria ya sasa kinawaondolea sifa za kuteuliwa watu waliowahi kuhukumiwa kwa kutenda kosa au ni watuhumiwa katika mashauri ya jinai yaliyopo mahakamani yanayohusu mashtaka ya kukosa uaminifu au uadilifu. Jedwali la Marekebisho linapendekeza na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono, kukifuta kabisa kifungu hicho kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, tayari kifungu cha 6(4) cha Sheria ya sasa kimewaondolea sifa za kuteuliwa kama Wajumbe, watu wasiokuwa “... waaminifu wa hali ya juu na wana tabia inayotiliwa shaka na jamii.” Mtu aliyewahi kuhukumiwa kwa kutenda kosa la kukosa uaminifu au uadilifu anakuwa

*automatically disqualified* na kifungu hicho na kwa hiyo hakukuwa na sababu yoyote kisheria ya kuwa na kifungu cha 6(5)(c).

Pili, mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hiki yanakwenda sambamba na *presumption of innocence* iliyoko kwenye Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba yetu na kwa sababu hiyo yanahifadhi haki za watuhumiwa wa makosa ya jinai ya kupata ulinzi wa sheria hadi hapo watakapopatikana na hatia.

Mheshimiwa Spika, yapo mapendekezo mengine ya marekebisho ya kifungu cha 6 ambayo yameletwa kwa njia ya Jedwali la Marekebisho la Serikali. Kwanza, inapendekezwa kuongezwa kifungu kipya cha 6(6) kinachosema kwamba: "... Rais ataalika Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi na Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana, kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa Wajumbe."

Pili, inapendekezwa katika kifungu kipya cha 6(7) kwamba, katika kualika Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia, Jumuiya, Taasisi zisizo za Kiserikali au Makundi ya watu wengi, kuwasilisha orodha za majina kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu kidogo cha (6), Rais atazingatia umoja unaosimamia Jumuiya au Asasi hizo."

Tatu, kifungu kipya cha 6(8) kinapendekeza kwamba, Rais asizuiliwe na masharti ya kifungu kipya cha 6(6); "... kuteua watu wengine kuwa Wajumbe wa Tume."

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya mapya ni ya kihistoria. Kwanza, tangu tupate uhuru miaka zaidi ya hamsini iliyopita na tangu Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura ya 32 ya Sheria za Tanzania ilipotungwa mwaka 1962, Tume zote ambazo zimeundwa kuchunguza mambo mbalimbali makubwa yaliyogeza taswira ya Kikatiba ya Taifa letu, zilikuwa Tume za Rais kwa maana kwamba Rais alikuwa ni 'all alfa na omega' wa Tume hizo. Rais ndiye alikuwa mteuzi wa Tume hizo, bila mashauriano na makubaliano na mtu mwingine yeyote. Rais ndiye aliyepokea Tume hizo hadidi za rejea na ndiye aliyepokea ripoti za Tume hizo. Rais ndiye aliyeamua kutoa hadharani ripoti za Tume au la na ndiye aliyeamua kipi akikubali na kipi akikatae katika mapendekezo ya ripoti za Tume hizo. Mifano ya Tume za aina hii ni Tume ya Kawawa iliyopelekea kuanzishwa kwa Mfumo wa Siasa wa Chama Kimoja na kupigwa marufuku kwa Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1964/1965; Tume ya Kombo na Msekwa iliyopelekea kuunganishwa kwa Vyama vya TANU na ASP na kuanzishwa kwa CCM mwaka 1977; na Tume ya Nyalali iliyopelekea kuanzishwa tena kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1991/1992. Zote hizi zilikuwa Tume za Rais *par excellence!*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kumwezesha Mheshimiwa Rais kualika Vyama vya Siasa, Taasisi za Kidini, Asasi za Kiraia na makundi mengine ya watu wenye malengo yanayofanana kuwasilisha majina ya watu watakaoteuliwa na Rais kuwa wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, linakata uzi mwekundu ambao umeshonea vazi letu la Kikatiba katika nusu karne ya uhai wetu kama Taifa huru. Wajukuu wa wajukuu zetu na vizazi vyao vitakavyofuata kwa miaka mingi baada ya sisi tuliopo humu ndani kuwa tumeondoka kwenye dunia hii, wataandika kwamba Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa Rais wa kwanza wa Tanzania kuanzisha dhana ya Tume ya Katiba ya Wadau, badala ya utaratibu wa Tume ya Rais aliourithi kutoka kwa Marais waliomtangulia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ambayo katika maoni yake ya tarehe 15 Novemba mwaka 2011 ilipendekeza kwamba "wajumbe wa Tume wateuliwe kufuatana na mapendekezo na makubaliano ya Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, vyama vingine vilivyosajiliwa pamoja na mashirika ya kijamii, taasisi za kitaaluma na za kidini", inayaunga mkono mapendekezo ya marekebisho haya ya kihistoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili muhimu ya nyongeza kuhusu pendekezo hili la kihistoria. Kwanza, kwa kuzingatia wingi wa asasi za kiraia, taasisi za kidini, jumuiya na taasisi zisizo za kiserikali na makundi mengine ya watu yenye malengo yanayofanana, kifungu kipya cha 6(7) kinapendekeza kumrahisishia Rais kazi kwa kumwelekeza azingatie muungano au umoja wa makundi hayo pale anapoyaalika kumpelekea orodha ya watu wa kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume. Pili, kwa kuzingatia kwamba Rais na Serikali anayoingoza pia ni wadau wakubwa na muhimu katika mchakato wa Katiba Mpya, kifungu kipya cha 6(8) kinapendekeza kumpa Rais

mwanya wa kuteua wajumbe wengine kwenye Tume nje ya wajumbe watakaopendekezwa na wadau kwa mujibu wa mapendekezo ya kifungu kipyacha cha 6(6). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na *common sense* iliyoangika mapendekezo yote mawili na inayaunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Marekebisha la Serikali linapendekeza kufanyiwa marekebisha kwa kifungu cha 12 cha Sheria kinachohusu ukomo wa wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Itakumbukwa kwamba katika hotuba yake ya tarehe 15 Novemba mwaka 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza kwamba namna mojawapo ya "... kuhakikisha uhuru wa Tume katika kutekeleza majukumu yake ni kuhakikisha kwamba wajumbe wake wanapatiwa ulinzi wa ajira zao sawa na wanaopatiwa Majaji wa Mahakama ya Tanzania ili kuzuia uwezekano wa wajumbe hao kuondolewa kwa sababu zisizotokana na utendaji wao wa kitaaluma au ukosefu wa maadili."

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili sasa limekubaliwa na Serikali kwani Jedwali la Marekebisha linapendekeza marekebisha ya kifungu cha 12 kwa kuongeza kifungu kidogo kipyacha cha (4) kinachoweka utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya wajumbe wa Tume. Kwa mujibu wa utaratibu unaopendekezwa, endapo suala la kuondolewa kwa mjumbe kwa ukiukwaji wa Kanuni za Maadili litajitokeza, Rais ataunda Kamati itakayochunguza suala hilo na kutoa mapendekezo kwake. Kamati hiyo inapendekezwa kuongozwa na Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania huku wajumbe wengine wakiwa Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kamishna wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Wakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar aliyependekezwa na Chama cha Mawakili Zanzibar (ZLS) na Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania aliyependekezwa na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS). Inapendekezwa kwamba endapo, baada ya uchunguzi wake, Kamati hii itapendekeza kwamba mjumbe wa Tume asiondolewe basi suala la kumwondoa litasitishwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mapendekezo ya kifungu kipyacha cha 12(4), Jedwali la Marekebisha linapendekeza pia kwamba kifungu kipyacha cha 12(5) kiongezwe ili kuiwezesha Kamati kutengeneza utaratibu wake yenyewe wa kufanya uchunguzi. Aidha, inapendekezwa kuongeza kifungu kipyacha cha 13(7) kwa lengo la kuifanya Tume kuwa mamlaka ya kinidhamu kwa wajumbe wa Sekretarieti ya Tume. Kama ilivyo kwa Tume, pendekezo hili vilevile linalenga kuwahakikishia ulinzi wa kisheria watendaji na watumishi wa Sekretarieti ili kuwawezesha kutekeleza wajibu wao kwa uhuru na bila kuingiliwa na mtu yeyote kama inavyotakiwa na kifungu cha 10 cha Sheria hii. Kwa sababu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na mapendekezo yote mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine muhimu yanayopendekezwa na Jedwali la Marekebisha la Serikali yanahusu marekebisha ya kifungu cha 17 cha Sheria kinachoweka utaratibu wa utendaji kazi wa Tume. Kwa mujibu wa kifungu cha 17(5) cha Sheria ya sasa, Tume inaweza kumtaka Mkuu wa Wilaya, Afisa Mtendaji wa Kata au Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kijiji au Sheha kwa upande wa Zanzibar kuitisha mkutano wa wakazi wa mji, kata, mtaa au kijiji au shehia kwa madhumuni ya kukusanya maoni ya wananchi hao kuhusu masuala ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuna hofu kubwa sana juu ya nafasi ya Wakuu wa Wilaya katika mchakato wa Katiba Mpya kama ilivyowekwa na Sheria hii. Hofu hii sio *unfounded* kwani tangu Sheria hii itungwe mwaka jana, Wakuu kadhaa wa Wilaya wamenukuliwa na vyombo vya habari wakitishia kuamuru wawakilishi wa mashirika ya kiraia yanayoendesha elimu kwa umma juu ya mchakato wa Katiba Mpya wakamatwe kama watafanya programu za elimu hiyo katika maeneo yao. Vilevile, kwa mujibu wa Katiba ya CCM na tangu kuanzishwa kwa CCM mwaka 1977, Wakuu wa Wilaya wamekuwa ni wajumbe wa vikao vyote vikuu vya CCM katika ngazi ya Wilaya. Kwa mfano, kwa mujibu wa Katiba ya CCM, Toleo la 1982, Mkuu wa Wilaya ni mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya (Ibara ya 42(3); ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya (Ibara ya 44(3); na ni mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya (Ibara ya 46(3)).

Mheshimiwa Spika, hata baada ya miaka thelathini tangu toleo hilo la Katiba ya CCM litolewe na licha ya miaka ishirini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini, hali bado iko vilevile kuhusiana na nafasi ya Wakuu wa Wilaya katika vikao rasmi vya CCM. Ndio maana, kwa mujibu

wa Ibara ya 76(1)(c) ya Katiba ya CCM Toleo la 2010, Mkuu wa Wilaya ni mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya; ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya (Ibara ya 78(1)(c); na ni mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya (Ibara ya 80(1)(c).

Mheshimiwa Spika, hivi vyote ni vikao muhimu vya maamuzi ndani ya Chama cha Mapinduzi ngazi ya Wilaya. Kuwapo kwa Wakuu wa Wilaya katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kunaleta hofu ya msingi kwamba wanaweza kuhujumu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kwa sababu au malengo ya kisiasa. Kwa sababu hiyo, pendekezo la kuwaondoa Wakuu wa Wilaya na badala yake kuwaweka Wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa - katika mchakato wa kuitishwa kwa mikutano ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba Mpya linajenga imani kwa wadau wengine hasahasa Vyama vya Siasa vya Upinzani. Wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa hawafungamani na Chama chochote cha Siasa ndio maana wamefanywa kuwa wasimamizi wa uchaguzi kwa mujibu wa Sheria zetu za Uchaguzi. Vilevile pendekezo hili linawawezesha Wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa urahisi na Watendaji wa Kata na wa Vijiji ambao pia ni watumishi wa mamlaka hizo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayakaribisha na kuyaunga mkono mapendekezo ya marekebisho haya ya kifungu cha 17(5) ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, moja ya upungufu mkubwa wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kutokuwepo kwa utaratibu wowote wa utoaji wa elimu kwa umma juu ya mchakato wa Katiba Mpya. Ni ajabu kwamba wakati Sheria haijaweka utaratibu wowote, kifungu cha 21(2)(c) cha Sheria hiyohiyo kimetangaza kwamba mtu yeyote atakayeendesha programu ya elimu juu ya mabadiliko ya Katiba kinyume na masharti ya Sheria hii atakuwa ametenda kosa! Hii sio tu inapingana moja kwa moja na hifadhi ya uhuru wa maoni iliyowekwa na Ibara ya 18 ya Katiba yetu, bali pia inaendeleza ujinga wa wananchi katika masuala muhimu ya kikatiba, ujinga wa kutokujua. Jedwali la Marekebisho ya Serikali linapendekeza kuondoa upungufu huu kwa kuweka utaratibu wa kutoa elimu kwa umma juu ya mabadiliko ya Katiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu kipya cha 17(9), inapendekezwa kuwa mtu au taasisi yoyote inayotaka kuendesha programu ya elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Katiba anatakiwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Tume, au kwa Wakurugenzi wa mamlaka za Serikali za Mitaa na Makatibu wa Mabaraza ya Miji kwa upande wa Zanzibar. Mtu au taasisi hiyo sharti iwe imesajiliwa na sharti ibainishe chanzo cha fedha zitakazotumika kuendeshea programu hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayakaribisha na kuyaunga mkono mapendekezo ya marekebisho haya kwa sababu yatawezesha wananchi kutoa maoni yao kuhusu mabadiliko ya Katiba wakiwa na ufahamu mkubwa zaidi wa masuala ya kikatiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuweka utaratibu wa kutoa elimu ya mabadiliko ya Katiba kwa umma, kifungu kipya cha 17(10) kinapendekeza kuhifadhi uhuru wa asasi, taasisi au makundi ya watu "... kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wao kutoa maoni yao kuhusu Katiba na kisha kuyawasilisha kwenye Tume." Mapendekezo haya sio tu yanatambua ukweli kwamba, kutokana na ukubwa wa nchi yetu na wingi wa watu wake, haitawezekana kwa Tume kukutana na kila mtu kwa lengo la kukusanya maoni yake kuhusu mabadiliko ya Katiba. Pendekezo hili pia linaendana na haki na uhuru muhimu wa kufanya mikutano kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Katiba yetu na wa maoni kwa mujibu wa Ibara ya 18. Kwa sababu hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayaunga mkono mapendekezo ya marekebisho haya ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Marekebisho la Serikali linapendekeza kupunguzwa kwa adhabu za watakaopatikana na hatia ya makosa ya kumkwamisha au kumzuia mjumbe wa Tume au Sekretarieti kutekeleza majukumu yake; kumkwamisha au kumzuia mtu au kundi la watu kutoa maoni kwenye Tume; kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi kinyume na Sheria hii; kujifanya mjumbe wa Tume au Sekretarieti; na kuendesha programu ya elimu juu ya mabadiliko ya Katiba kinyume na masharti ya Sheria hii. Makosa haya yako kwenye kifungu cha 21(1) na (2) cha Sheria na adhabu zake, kwa mujibu wa kifungu cha 21(3), ni faini ya kati ya shilingi milioni tano hadi milioni kumi na tano au kifungu cha kati ya miaka mitatu hadi miaka saba au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika waraka wake kwa Mheshimiwa Rais, Kamati Maalum ya CHADEMA ilipendekeza kwamba vifungu vyote vinavyokiuka haki za kimsingi za Kikatiba vifutwe na kuwepo na uhuru kamili wa kujadili, kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi juu ya utungaji wa Katiba Mpya na kuyawasilisha kwa Tume. Pamoja na kwamba vifungu vinavyofanya ukusanyaji na uratibu wa maoni ya wananchi na uendeshaji wa elimu kwa umma kuwa kosa la jinai havikufutwa kama tulivyopendekeza kwa Mheshimiwa Rais, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri, kwa kuzingatia haki zilizohifadhiwa na Ibara za 17 na 18 za Katiba yetu ya sasa, kwamba Bunge hili Tukufu litafakari kama kuna haja ya kuendelea kuwepo kwa makosa haya na adhabu zake katika Sheria itakayotuletea Katiba Mpya na bora kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba, katika kuhitimisha maoni yangu, kwa kusisitiza kwa mara nyingine tena mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika kuletwa kwa Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho lililoambatanishwa, miezi miwili tu baada ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kupitishwa na Bunge lako Tukufu na kupata kibali cha Rais. Naomba nisisitize tena kwamba, katika jambo hili muhimu kwa Taifa letu, Mheshimiwa Rais amekuwa msikivu kwelikweli kwani amejitokea juu ya *the partisanship and factionalism of party politics* na ameangalia maslahi mapana ya Taifa letu. Ni wajibu wetu sasa kuwathibitishia Watanzania kwamba kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais na usikivu wake na uongozi wake katika jambo hili haukuwa wa bure. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafarijika kwamba Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge lako Tukufu imeridhia na kukubali mapendekezo yote ya Muswada huu na Jedwali la Marekebisho la Serikalali. Kwa sababu zote hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni sio tu inaunga mkono Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011, bali pia inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote, bila kujali *the narrowness of our political party affiliations*, tuungane na Mheshimiwa Rais katika kulipatia Taifa letu utaratibu wa kutengeneza Katiba Mpya wenye muafaka wa Kitaifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wasemaji wakuu wa Muswada wetu na bila kusema maneno yoyote yale, hivyo ndiyo inavyotakiwa na kweli kabisa tunaomba na Watanzania wote tuingie kwenye mjadala huu kama wamoja, tubishanie tu hoja na siyo kubishania vyama, hicho ndicho tunachokisema na ndiyo *spirit* ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ameionyesha hapa. Ni kwamba, tujadiliane na tuache uhasama, chuki, hila na kadhalika vyote havihusiki, kweli tujadili na atakapopewa nafasi ya kusaini na kuunda Tume yake, tujadili kama Watanzania kwa sababu *it is about us* siyo juu ya mtu mwingine. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *spirit* ambayo tulikuwa tunaiomba siku zote, hapa hakuna upande, ni kujadili umuhimu na ubora wa mawazo yanayotolewa na mtu mwingine na kila mtu aheshimu mawazo ya mwenzake. Kwa hiyo, unapokuta halingani na wewe siyo uadui ndiyo sababu ya kujadiliana hapa. Kwa hiyo, nawashukuru watoa mada wote wa mwanzo mme-*settle space* na tunaomba na wananchi pia wajifunze hili, wasisikilize hulka za watu za kutaka ugomvi, matatizo na kadhalika kwani hazitusaidii Watanzania, twende mbele tukiwa na amani, umoja na upendo kama inavyostahili. (Makofi)

Sasa kwa sababu wakati hata Muswada haujawasilishwa, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo aliomba kwamba mambo haya yasijadiliwe tena kwa sababu alizozieleza. Naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Engineer Mnyaa kwanza halafu baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela halafu atafuatia Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Said Amour Arfi, nafikiri watatosha kwa asubuhi hii kabla hatuja- *adjourn*. Lakini napenda niwasomee Kanuni moja hapa kwa sababu huu Muswada ni *very trick*, hatuanzi kutunga Muswada wa mabadiliko ya Katiba bali tunafanya *amendment* katika baadhi ya vifungu. Kwa hiyo, Kanuni ya 60(9) inatuelekeza hivi:-

*"Kila Mbunge atalisemea jambo ambalo liko katika mjadala tu na hatarudiarudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wabunge wengine na iwapo itatolewa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja inayojadiliwa, mjadala sharti uwe juu ya hoja hiyo ya mabadiliko mpaka imalizike ndipo mjadala urudie kwenye hoja ya msingi".*



Nimeyasema haya kwa makusudi kwa sababu ninyi mliomba hapa mko kama hamsini. Hapa kwa hesabu zangu za muda mnaweza kufikiwa kumi tu. Kwa hiyo, mjue hapa habari ya kurudia kama mnaanza kutunga Muswada haitakubalika.

Kwa hiyo, tunaanza na hao niliowataja, Mheshimiwa *Engineer Mnyaa!*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kwanza kutoa mchango wangu katika Muswada huu au marekebisho ya Muswada wa Marekebisho ya Katiba ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba tulipopitisha Sheria hii, sisi tuliunga mkono pamoja na kwamba ulikuwa na matatizo tukaweza kupeleka *schedule of amendment*, nyingine zilikubaliwa na nyingine zikakataliwa, lakini hiyo ndiyo katika utaratibu wa demokrasia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hivi leo nichukue nafasi hii baada ya kuona kuna baadhi ya mambo hatukukubaliana nayo mwanzo, nikiri kwamba Chama changu kilikuwa ni kimoja katika Vyama vilivyokwenda Ikulu kumuona Mheshimiwa Rais. Baada ya kukubali ombi letu, tulikwenda kule pamoja na hapa tulikubali Muswada ule. Vipengele vilivyokuwa vina matatizo na tukaweza kuwasilisha malalamiko yetu, vilikuwa ni vipengele kama saba na nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kutukubalia kwenda kule na leo hii yote ambayo tulikuwa hatukubaliani nayo yamerekebishwa kwa 90%. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kusema kwamba na mimi naunga mkono hoja ya mabadiliko ya Sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika hoja hii ni kukubali Viongozi wa Vyama vya Siasa kushiriki au kuwemo katika Tume ile. Kitu hiki ni muhimu na kikubwa sana kwa sababu Katiba ya Nchi ikiwa Vyama vya Siasa visingekuwepo au Viongozi wa Vyama vya Siasa wasingekuwepo ingeweza kuleta matatizo makubwa sana kwa sababu wangejiona siyo *part and parcel* ya Katiba ile. Kitendo cha Mheshimiwa Rais kukubali marekebisho haya yakaletwa leo na Viongozi wa Vyama vya Siasa wakiwemo kutoa mchango wao yaani wakiwemo katika ile Tume, ni jambo kubwa sana na linalotia faraja. Baada ya kukamilisha mchakato wote sidhani kama kutatokea Chama cha Siasa ambacho kitasema hakikushirikishwa au hakikubaliani na mabadiliko hayo ya Katiba au na Katiba Mpya itakayoundwa. Kwa hiyo, hili ni jambo kubwa na zito sana ambalo Mheshimiwa Rais ameliona na kupitia Serikali kuleta marekebisho hayo ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo pia ni zito ni pale ambapo makundi ya kijamii na ya kidini na wao kuruhusiwa. Hili nalo ni jambo ambalo linatoa faraja kubwa na ni kitu ambacho leo hii kitatusaidia kwa sababu Watanzania wote wa asasi zote na wa dini zote watajijikia na wao ni miongoni mwa walioshiriki katika mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa mabadiliko haya mawili makubwa ukiacha mabadiliko mengine madogomadogo, ni mabadiliko ambayo tunaweza kufanikisha wananchi kutoa maoni yao kwa njia salama na ya amani na Watanzania wote kwa ujumla leo wataona wameshiriki na hapa ndiyo pale ambapo maana ya Katiba ni Sheria Mama na Katiba ni ya wananchi itakapoleta maana. Kwa hiyo, hilo nalo nalipongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mambo yote yamekwenda vizuri na sasa tumefarijika sote na kitendo kile cha Kamati kuonana na Vyama vya Kisiasa na Jumuiya za Kiraia kama walivyotoa katika ripoti yao, ni jambo lingine la faraja kwamba sasa hatatokea Mtanzania yeyote ambaye atasema kwamba hakushirikishwa katika Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, bila kuchukua muda mrefu, kuna kitu kimoja tu ambacho Chama changu kilipendekeza na hiki hakimo katika marekebisho haya kwamba, matokeo ya kura ya maoni kwa mujibu wa Sheria hii bado inatamka ni 50%. Leo katika kura za maoni endapo itapatikana asilimia 49.9 ya waliosema 'hapana' kwa upande wa Tanzania Bara au upande wa Tanzania Visiwani au pande zote zikapata asilimia 49.9 ya waliosema 'Hapana', asilimia 50.1 wakakubali, kwa mujibu wa sheria hii ni kwamba Katiba hiyo mpya itapita. Lakini ukitizama asilimia

49.9 na asilimia 51.1 kimantiki ni sawa kwa sawa. Kwa hivyo, kukosekana kwa rekebisha hili hapo Katiba itakuwa bado haijajenga ustawi wa kukubalika kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chama cha Wananchi (CUF), kilipendekeza ni lazima angalau iwe zaidi ya asilimia 60. Kwa taarifa nilizonazo, Serikali imekubali kwa kuwa mpaka sasa Sheria ya Kura ya Maoni hakuna kwa upande wa Tanzania Bara na Serikali italeta Sheria hiyo ya Kura za Maoni hapa Bungeni na wataweka kipengele hicho kwamba Kura ya Maoni iwe ni zaidi ya asilimia 50, itamkwe zaidi ya asilimia 60 au na zaidi. Mchakato wa Katiba ikiwa utaungwa mkono na zaidi ya asilimia 60 ni kweli itakuwa ni Katiba halali ambayo imekubalika na Watanzania walio wengi. Kwa hivyo, naiomba Serikali kutokana na ahadi zake na mazungumzo yaliyofanywa, walete Sheria ya Kura ya Maoni ya Tanzania Bara na katika Sheria hiyo ya maoni ni lazima itamkwe ni zaidi ya asilimia 60, ilivyo hivi sasa haiwezi kuleta maana ikiwa asilimia 51.1 wata kubali na asilimia 49.9 watakataa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niseme naunga mkono hoja ya Mabadiliko ya Sheria hii, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Ninavyoona kama mki-*stick to the point* za Muswada wote nyie mnaweza kupata nafasi lakini mkiongea habari nyingine, kwanza sitawaruhusu.

Kwanza kabisa pale kwenye *Speaker's Gallery* kuna Mheshimiwa George Nangale ambaye ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, naomba usimame wakusalimie. Ahsante, karibu sana. (Makofi)

Nimwite Mheshimiwa Anne Kilango Malecela halafu atafuatia Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Said Arfi atafikiwa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumefikia siku nzuri sana, siku ambayo Watanzania wengi walikuwa wanaisubiri.

Pili, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusaini Muswada wa Sheria ambao tuliuzungumzia hapa ndani mwezi Novemba 2011 na leo hii tuna Sheria ambayo iko mkononi ambayo imeletewa marekebisha na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumza, nakiri kuwa na uhakika kwamba Vyama vya Siasa vilikwenda kumwona Mheshimiwa Rais, nimeyasikia kutoka upande wa Kamati iliyochambua Muswada huu na pia tumesikia alivyowakilisha Msemaji wa Kambi ya Upinzani Rasmi Bungeni, Mheshimiwa Tundu Lissu amewasilisha kistaarabu sana na nampongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Vyama hivi vilivyokwenda ni NCCR-MAGEUZI, CHADEMA, CCM, CUF na asasi zote, ni kweli vilitoa mapendekezo lakini ni vyema Watanzania wote tukaelewa kwamba unatoa mapendekezo, lakini mapendekezo yale hayaji hapa kama mapendekezo yako, yanataifishwa na Serikali, yanakuwa ni mapendekezo ya Serikali, hakuna mapendekezo ya Chama cha Mapinduzi, CHADEMA haya ni marekebisha yanayoletwa na Serikali iliyopo madarakani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze jambo lililonifurahisha sana. Kuna Kiswahili kinachosema 'ndani ya tumbo la shari, humohumo ndani kwenye shari kuna kheri pia'. Kwa nini nasema hivyo? Shari hii, tulivyovutanavutana hapa kwenye Mabadiliko ya Katiba, imetuletea kheri kubwa sana labda watu wengine hamjaiangalia. Kwa sababu nimeweza kuona nikiwa naangalia luninga, wenzetu ambao walikuwa hawamtambui Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani ya shari hii tumepata kheri kwamba sasa wote tunamtambua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo shari hii imetuletea kheri, tumwambie Mwenyezi Mungu ahsante sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye kazi. Bunge ni mhimili anayejitegemea. Serikali ni mhimili anayejitegemea, Mahakama ni mhimili anayejitegemea, Serikali inapoleta marekebisha

yoyote haitushinikizi kwamba lazima tukubali. Kama Bunge hatushinikizwi kwamba Serikali ikileta marekebisho, sisi tukubali, tunatoa mawazo yetu kama Wabunge inapoonekana inafaa Wabunge mnaunga mkono hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba ni-move *amendment*, naomba nizungumzie kuhusu kifungu cha 17(c), najua wengi hiki mnataka kunisikiliza.

**SPIKA:** Kifungu gani?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Kifungu 17(c) katika hili jedwali la *amendments* za Serikali, ambapo anaondolewa Mkuu wa Wilaya katika kusimamia zile shughuli zote za Tume, analetwa Mkurugenzi. Hapa naomba nipaongeele kidogo. Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya ni watu wawili tofauti katika utendaji kazi wao na hata katika nyadhifa zao. Mkurugenzi wa Wilaya anasimamia maendeleo ya Halmashauri yote ya Wilaya, ndio kazi yake kubwa licha ya kwamba atakuwa ni *Returning Officer* wakati wa Uchaguzi. Mkuu wa Wilaya sasa ni mtawala katika ile sehemu aliyoko yeye kama Mkuu wa Wilaya, ile Wilaya yeye ndio mtawala, yeye ndio dola, yeye ndio mwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mkurugenzi hana Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba itakwenda sambamba na Sheria ya Polisi. Mwenye Polisi ni Mkuu wa Wilaya. Sasa wakati Tume inakwenda kwenye Wilaya ambako ndiko wananchi walipo, Tume hii inahitaji kuwe na Kamati ya Ulinzi na Usalama ili mambo yote yaende vizuri katika kazi ambazo watafanya ndani ya Wilaya ile. Sasa tunaona umuhimu wa kumhitaji Mkuu wa Wilaya kuliko Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya yule atasimamia shughuli zote zitakazofanywa na Tume hii ziende vizuri na kuwe na usalama. Yeye ana dola, yeye ndiye mwakilishi wa Rais katika Wilaya ile mfano Wilaya ya Same. Kwa hiyo, pale Mkuu wa Wilaya atahakikisha mambo yote yanakwenda vizuri kuliko Mkurugenzi ambaye anasimamia maendeleo ya Wilaya ile bila ya kuwa na dola na wala yeye si mwakilishi wa mtawala wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba ku-move *amendment* kwamba tumrudishe Mkuu wa Wilaya na kumtoa Mkurugenzi nje. Hapa nitaomba kumwondoa Mkurugenzi katika kifungu cha 17 kuanzia (a), (b) na (c), mahali popote anaposomeka "Mkurugenzi awe anasomeka Mkuu wa Wilaya", Waheshimiwa Wabunge naomba mniunge mkono kwa faida ya Taifa letu. (Makofi)

**SPIKA:** Labda nikusahihishe kidogo, hapa unatoa taarifa kwamba unakusudia kufanya hivyo. Sasa maoni yako watayajadili ili tukifika kwenye Kamati ya Bunge Zima ndipo utaleta *amendment* na nategemea umeziandika. Sasa unatoa taarifa, na wenzio watajadili hoja yako pia.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naleta taarifa kwenye kikao hiki ndani ya Bunge hili kwamba nitaleta *amendment* ya kumwondoa Mkurugenzi katika kifungu hicho cha 17 (a), (b) na (c) na ninamrudisha Mkuu wa Wilaya kwa sababu ambazo nimeziong'ea. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono wakati mnalizungumza hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na nitaomba wenzangu mniunge mkono katika marekebisho yangu. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya halafu Mheshimiwa Arfi atafuata.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata fursa hii tena ya kujadili marekebisho machache katika Sheria ambayo ina vipengele zaidi ya 30 na kwa ajili ya kuboresha Sheria yetu ya Mabadiliko ya Katiba Mpya ili iweze kufanya kazi kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza kaka yangu, Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa hotuba yake nzuri, kwa hotuba ambayo imeonyesha umoja na mshikamano, hotuba iliyoonyesha kwamba Rais Jakaya Mrisho Kikwete ana busara na hotuba iliyoonyesha kwamba ukiwa na tatizo

huna sehemu nyingine yoyote ya kwenda kulia shida yako zaidi yake kama ambavyo alivyotambua wazi wakati anafungulia Bunge hili na leo limeshirika hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo ambayo tunapaswa kufanya kama Wabunge. Unapotaka kufanya marekebisho yoyote yanayohusu Sheria, hakuna sehemu nyingine yoyote utakayokwenda, ni humu ndani na ndio maana hata nilivyokuwa nikichangia Muswada huu wa Katiba niliwaambia wenzangu waliokuwa wanatoka, kutoka sio *solution*, *solution* kubaki na kujadili matatizo, marekebisho ili kuboresha sheria hii, ndicho mnachofanya leo, ndicho ambacho kinafanyika leo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye marekebisho yenyewe, kwanza kabisa naunga mkono rekebisho la kwanza ambalo ni kifungu cha 6, kinachopendekeza asasi za kiraia, vyama vya siasa kwenda kupeleka orodha ya majina ili Mheshimiwa Rais pamoja na kwamba hafungwi kama kifungu cha 7 kinavyoweka angalizo mbali na kwamba atapelekwa orodha ya majina kutoka Taasisi mbalimbali, Rais hafungwi kuteua Wajumbe wengine, hilo naunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuzungumzia kifungu cha 17 kwenye mabadiliko ambapo ni kifungu cha 9, kinachohusu Programu ya Kuendesha Elimu kwa Umma. Hapa napenda Serikali itoe ufafanuzi wa kutosha, kwa sababu unapozungumzia elimu kwa umma, kuna vipindi vya redio, unapozungumzia elimu kwa umma kuna makongamano na unapozungumzia elimu kwa umma kuna mikutano ya hadhara. Sasa tunajua taratibu za mikutano ya hadhara kwamba lazima pia utapata kibali kutoka kwa Jeshi la Polisi, lakini Sheria hii haijaonyesha wazi. Sisi humu tunajua sio wakamilifu, kuna wengine wanaweza waka-*take advantage* ya kukaa kimya kwa kipengele hiki kwenda kufanya mikutano ya hadhara kwa kisingizio cha kutoa elimu kwa umma, angalizo langu ni hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye kifungu hicho hicho cha 17 kwenye marekebisho ya kifungu cha 9(1) ambacho kinasema "Mtu unapotaka kwenda kutoa elimu kwa umma unapaswa kutoa taarifa". Taarifa tu lakini kifungu hiki hakimpi mamlaka huyo mpokea taarifa kukupa kibali au kukuzuia kutokana na mazingira.

Mheshimiwa Spika, tuna *experience* hapa ya chaguzi mbalimbali na tunajua kabisa kunakuwa na Sheria za Uchaguzi, tunajua kabisa wadau wanaitwa ambao ni Vyama vya Siasa, lakini tunashuhudia wengine wanakiuka ratiba kwenda kufanya mikutano katika sehemu ambazo hawapaswi kwenda, hili ndilo angalizo langu. Kwa hiyo, hiki kifungu kieleze kabisa mbali na kwamba unatoa taarifa lakini lazima upewe kibali, lazima huyo mpokea taarifa ajiridhishe kwamba kule sehemu ambayo labda Mheshimiwa Lissu anakwenda hakuna mtu mwingine, tuesday hii migongano. Tunajua kabisa hili zoezi lina utashi wa kisiasa. Sasa kukaa kimya kwa kifungu hiki kitakuja kuleta *contradiction* mbele na mwisho watu wataanza kulumbana, hilo ndio angalizo langu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia naungana kabisa na Mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango kuhusiana na suala la Wakuu wa Wilaya, tusidhalilishie nafasi kwa hisia za kisiasa. Huku tunasema tuna wasiwasi na Mkuu wa Wilaya, hapa hapa tunafanya marekebisho ya wanasiasa kuingia kwenye Tume, huku tunasema Mkuu wa Wilaya, *may be* ana itikadi, je, hawa wanasiasa watakuwa hawana itikadi zao, tusijikanganye. Mkuu wa Wilaya ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama. Mkuu wa Wilaya ana mamlaka ya Wilaya yake ya kutoa vibali hili hatuwezi kuliepuka. Mimi nadhani sheria ile ilikuwa sahihi ya kuwaacha Wakuu wa Wilaya na mimi pia hili nali-*support* kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sina tatizo la Tume kupewa mamlaka ya kuwaruhusu Taasisi za Kiraia, Vyama vya Siasa Makundi mbalimbali kwenda kutoa elimu kwa wanachama wao na kuchukua maoni lakini angalizo langu katika mabadiliko haya je, tunajuaje kama labda hii NGO itaenda kweli kule kwa wanachama? Isije ikawa Ester Bulaya hapa anajifungia nyumbani, anaandika mawazo yake kwa kisingizio kwamba ni mawazo ya watu fulani. Natoa angalizo hilo lakini na mimi naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais na naendelea kusema kwamba sheria

nzuri itatungwa Bungeni na kamwe hakuna mhimili wenye mamlaka ya kuingilia mhimili mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante, kwa mtindo huo, wengi watapata nafasi. Mheshimiwa Said Arfi atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hii muhimu inayohusu mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuungana na maneno yako ya utangulizi kabla ya kuruhusu mjadala huu, ni maneno ya busara, maneno ya hekima na Watanzania takriban zaidi ya milioni 40 leo wanatungalia, wanatusikiliza, ni namna gani busara na hekima tulizonazo zitatuongoza katika kulifanya jambo hili kuwa la Kitaifa. Niwaombe tu ndugu zangu kwamba tutangulize kwanza maslahi ya Taifa letu, twende mbali zaidi ya itikadi ya vyama vyetu na maslahi ya mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ya pekee kabisa kwamba angeweza kunyamaza, angeweza kuiacha hii Sheria ikaendelea kubakia kama jinsi ilivyokuwa lakini amekuwa ni msikivu sana. Alisikia kelele nyingi zilizokuwa zinapazwa nje ya kuta ya jengo hili kutoka katika makundi mbalimbali ya Watanzania akaamua kufungua milango ya Ikulu yake na kuwasikiliza wadau, akakusanya maoni na mapendekezo mbalimbali, akayakabidhi kwenye Serikali yake wakayapitia na hatimaye wamekuja na mapendekezo waliyoyawasilisha kupitia kwa Mwanasheria Mkuu. Mimi binafsi ninaunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyoletwa na Serikali yametokana na mashauriano mengi aliyoyafanya Mheshimiwa Rais na wadau mbalimbali na mashauriano pia aliyoyafanya ndani ya Serikali yake. Jambo hili kama litakwenda kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nina hakika kabisa tutafika huko tunakotaka kwenda kama wamoja, kama Watanzania lakini kama hekima na busara hazitasimama, hazitatamalaki katika Mkutano huu tunaweza kuligawa Taifa hili vipande vipande. Nchi nyingi zimeingia katika machafuko kutokana na Katiba. Majirani zetu Kenya ni mfano. Ni namna gani waliweza kuvurugana kwa sababu ya kutokukubaliana katika mambo ya msingi. Katiba ni jambo la msingi kwa maslahi yetu na vizazi vyetu na Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali, ni mapendekezo ambayo yamepitiwa kwa kina, yamechambuliwa na wataalam, sio tu kwamba ni kwa ajili ya kupendezesha kikundi fulani kilichotoa maoni lakini yameangalia sana maslahi ya Taifa letu. Kwa heshima kubwa sana, napenda kutokukubaliana na Mheshimiwa aliyekuwa anakizungumzia kifungu namba 17(c). Tumelitafakari sana jambo hili kwa uzito wake na sisi wote ni sehemu ya jamii ya Watanzania na tuna mahusiano na Wakuu wa Wilaya. Tunawajua kabisa ni namna gani wanavyofanya kazi zao. Ninachotaka kukisema hapa ni kwamba *spirit* au dhamira au utashi uliopo ni kufanya Katiba si mali ya Chama chochote. Katiba itokane na Watanzania kwa kumpa Mamlaka na dhamana Mheshimiwa Rais kusimamia mchakato huu. Ndiyo maana likaja pendekezo la hiyo Tume litokane na makundi mbalimbali ya jamii ambao ninafurahi kwamba pendekezo hilo lilitolewa na makundi mbalimbali, Mheshimiwa Rais akaona hoja ndani na leo wamewasilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kama alivyotangulia kusema msemaji mwingine kwamba Watanzania sasa wataona Katiba ni ya kwao. Wanaimiliki Katiba, wanauwakilishi ndani ya chombo ambacho kitasimamia kukusanya maoni, kuandika Rasimu ya Katiba na hatua zake zote. Kwa maana hiyo, hakuna mtu atakayesimama na kudai kwamba Katiba hii ni ya kwake. Katiba hii itakuwa ni ya Watanzania. Kwa dhamira hiyohiyo na kwa utashi huohuo ndiyo maana limekuja pendekezo la kuwaondoa Wakuu wa Wilaya katika mchakato huu. Kwa bahati mbaya sana, Wakuu wa Wilaya wanaonekana moja kwa moja ndani ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwaombe tu tuwe wakweli kwa nafsi zetu. Kama kweli tunalipenda Taifa hili, kama kweli tunalipenda nchi hii na mchakato huu uende vizuri basi tukubaliane na mapendekezo ya Serikali. Laiti Mkuu wa Wilaya angekuwa hakuonekana ndani ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi, tusingekuwa na tatizo na hilo lakini ukiangalia Katiba ya Chama cha Mapinduzi, Toleo la Mwaka 2010, Ibara ya 78(1)(c) na 80(1)(c) inaeleza bayana nafasi ya Mkuu wa Wilaya ndani ya Chama cha Mapinduzi. Hatuhitaji huko mbele tukaanza tena kulumbana kwamba hii ni Katiba ya Chama cha Mapinduzi. Tunataka kusema hii ni Katiba ya Watanzania imetokana na Watanzania kwa makubaliano waliyokubaliana. Niwaombe kwa unyenyekevu mkubwa sana, tukubaliane na mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali kama kweli tuna mapenzi mema na Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania watatuhukumu, Watanzania watatupima burasa zetu na hekima zetu katika kudumisha umoja na mshikamano wa Taifa hili. Ni sisi wachache tuliobahatika kuingia katika jengo hili, takribani watu 350 au chini ya 350 ndiyo pekee tunaweza kulifanya Taifa hili likabakia kuwa moja lisilogawanyika kama tutakuwa tayari kukubali hata kama tunajua linatumiza kwa mstakabali na maslahi ya Taifa hili. Tuache mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali yaende kama jinsi yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo ilikuwa rai yangu katika suala hili kwa sababu hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani imeeleza haya na mimi ni mmoja kati ya wale ambao walishiriki katika mazungumzo ya awali. Kwa hiyo, nirudie tu kuwaomba ndugu zangu wapendwa Wabunge, maslahi ya vyama vyetu tuyaweke pembeni, tutangulize maslahi ya Taifa letu. Tuunge mkono utayari aliouonyesha Mheshimiwa Rais, vinginevyo tutahukumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi, najua ni nafasi adhimu sana lakini nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake nzuri za kutaka kuona kwamba mchakato huu wa kupata Katiba mpya, Katiba ya Watanzania na sio Katiba ya Vyama vya Siasa, sio ya kundi moja katika jamii na sio Katiba ya kabila moja. Katiba ya Watanzania, ya wananchi wote kwamba tunaenda kule tukiwa tunatembea kifua mbele, tukiwa tumeshikamana na Tanzania ibakie kuwa nchi yenye amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ni viongozi wa Taifa hili. Tunapokuja humu Bungeni, ni lazima historia na matukio mbalimbali tusiyasahau. Mimi naheshimu sana Kambi Rasmi ya Upinzani humu Bungeni lakini kwa yale yaliyotokea katika Mkutano wa Tano kusema kweli kwa Watanzania walio wengi hatukuwatendea haki kwa sababu mawazo yote mazuri ambayo mlikuwa nayo, mngeweza kuyasema humu Bungeni, Watanzania wakawasikia na Bunge lako likapima yapi ambayo yanafaa yachukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema, kila Mhimili unasimama kivyake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazitungwi nje ya Bunge hili. Nawashukuruni sana wale mlioliona hilo. Mimi sitaki kurudi sana huko nyuma lakini mimi iliniuma sana kusikia kwamba Bunge limekiuka Kanuni za Bunge kwa kutokusomwa Muswada ule kwa Mara ya Kwanza. Niliumia sana kwa sababu Kanuni za Bunge ninazifahamu na sisi wengi humu tunazifahamu. Muswada huo hatukukiuka Kanuni, haukupaswa Kusoma Mara ya Kwanza na nashukuru wewe ulisimama kidete, ukasoma Mara ya Pili na Mara ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Sheria hii tunayoitunga leo, haiwezi ikawa kamili. Tutaendelea kuifanyia marekebisho kama tunavyofanya kwa Sheria zingine na tusiwe na wasiwasi. Niseme hakuna Katiba wala Kanuni ya Bunge inayoweka utaratibu, ni kiwango gani cha kuwashirikisha wananchi katika kutoa maoni yao. Hakuna Sheria au Katiba inayotamka hivyo. Sisi Wabunge

tumepewa dhamana hiyo kwa niaba ya wananchi hata kwa masuala mazito kama haya ya Katiba, tufanye kazi hiyo kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme mambo mawili, matatu tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, naishukuru Serikali kwa kuleta haya marekebisho lakini mimi nilisema na viongozi wengine humu na Wabunge walisema, mantiki ya kuwazuia Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haina mashiko. Ukishafungua kundi lote hilo, sasa hivi wamo katika hatua ya pili katika Bunge Maalum la Katiba, ndiyo maana nilikuwa naomba na nimeona Mheshimiwa Mbunge ameleta marekebisho hayo, Waheshimiwa Wabunge nataka tuone sura hiyo. Hakuna mtu anayeweza kusema kwamba Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ambaye amechaguliwa na wananchi kwamba yeye sio mwanasiasa, itakuwa ni ajabu na kituko cha hali ya juu sana. Nafasi hizi ni 16 kwa Bara na nafasi 16 kwa Tanzania Zanzibar. Sasa mantiki hainijii kichwani kwamba Mheshimiwa Rais eti ataingiza Wabunge wote, nafasi ziko wapi? Lakini tunasema iwapo yupo Mbunge Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kweli anasifa zinazostahili, aingie! Tusifunge mlango huu. Mimi nitaunga mkono ile hoja ya marekebisho hayo ambayo nimeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niisaidie Serikali. Nimegundua kwenye marekebisho ya Serikali kwenye kifungu cha 21, kwenye makundi yale yanayoingiza, labda nisile muda wako, nitakuja kusema tutakapofika kwenye Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu, mimi naunga mkono hoja lakini katika mapendekezo ya Serikali, kifungu cha 6 nimekisemea, kifungu cha 12 sina tatizo kwa sababu ni utaratibu tu wa kumwondoa Mjumbe wa Tume kama atakiuka Kanuni za Maadili, Tume hii kuwa na mamlaka kwa watumishi wa Sekretarieti. DC, hata mimi nina tatizo na Mkurugenzi kwa sababu ya Mfumo wa Utawala wa Sheria. Ni Sheria ya nchi. Mimi sipendi tufike katika Katiba ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu hata Rais kama tukienda namna hiyo naye ametajwa lakini nataka wote tuone kazi ya DC ambayo imo kisheria na kwa kazi ambayo tunataka tuianze, mimi nasema ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tuliangalie hilo kwa makini sana na wala sio kuwagawa Watanzania. Hakuna suala la kuwagawa Watanzania, hawa ni viongozi wa nchi hii, wanamwakilisha Rais katika eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu zile, mimi nakubaliana kabisa na Serikali. Yawezekana Waheshimiwa Wabunge kidogo tulikuwa na munkari lakini tumeshuka kidogo na nashukuru kwamba sasa tunazifanya ziwe sare na Sheria za nchi zingine. Mimi hilo nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeshukuru sana kwamba wenzetu sasa wemeanza kutambua. Ule ukakasi tuliouona kwa jina la Rais katika mchakato huu na Rais wa Zanzibar, sasa wenzetu wemeanza kukubali kwamba lazima mchakato huu umuhusishe Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar katika mchakato mzima. Mimi hilo limenipatia faraja kubwa sana kwa sababu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye kielelezo cha Taifa hili kama Kiongozi wa nchi, Mkuu wa nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi niunge mkono marekebisho haya yaliyoletwa na Serikali na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuyaunge mkono lakini pale ambapo kunastahili kuyafanya maboresho zaidi, tusingope kufanya maboresho, ndiyo kazi ya Bunge hili. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru na mimi kupata nafasi hii adimu. Nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza kwa kukubali kuridhia kuwapokea wananchi wake na kupokea maoni. Nitumie pia nafasi hii kusema kwa mujibu wa muundo wa Bunge letu, katika Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimsingi Bunge linakamilika linapokuwa na Rais. Inasema Bunge la Tanzania lina sehemu mbili, Wabunge na Rais. Kwa hiyo, kitendo cha kwenda kule ni sahihi kabisa na tumepata maoni mazuri kabisa ambayo asubuhi ya leo yapo mbele yetu na sisi inabidi tuyapitie na kuyatolea maoni.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa kusema ni kutambua powers za Rais. Huko nyuma kulikuwa na *debate* sana lakini sasa Muswada huu umetambua sana power za Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati yangu ambayo imekuwa ikifanya kazi usiku na mchana na watu kutumia taaluma zao hadi leo hii tumefikia hapa. Vilevile nimpongeze Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kusoma taarifa ya Kamati vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulioko mbele yetu umetambua sana nafasi ya Rais. Umesema Rais ataalika Vyama, Rais atazingatia umoja unaosimamia Jumuiya na Asasi, kwa hiyo, lazima tutambue kwamba nchi yetu inaongozwa na Kiongozi anaitwa Rais na kama nchi nyingine zilizvyo mfano Ghana, Kenya Rais aliunda Tume ambayo ilishughulika na Mchakato wa Katiba. Kwa hiyo, nawashukuru sana wadau, Watanzania wote kwa kuridhia kwamba Rais is the one who is having the authority ya kuunda Tume na hapo kwa kweli wote tunaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo linalohusu wanasiasa kuwemo kwenye Tume. Nitumie nafasi hii kusema kwamba tulikuja tukajadiliana hapa na tukatafakari sana suala la wanasiasa kuwemo kwenye Tume. Wabunge tulisema kwamba wanasiasa wawemo, wengine wakasema tuwaache na tukazungumza sana hapa habari ya wanasiasa. Zilikuwepo sababu zilizopelekea mwanzo wanasiasa wasiwemo kwenye hiyo Tume lakini baada ya kutafakari kwa kina, sote tunakubaliana kwamba wanasiasa wawemo. Miongoni mwa sababu hizo ni ule utamaduni wa wanasiasa badala ya kuweka maslahi ya nchi kwanza, Tanzania kwanza, tunaweka maslahi yetu binafsi kwanza na itikadi zetu. Sasa ikifikia hatua hiyo hapo ndipo tuliposema kwamba kama hivyo ndivyo kwa sababu Tume hii kazi yake ni kukusanya maoni, wanaozungumza ni Watanzania basi wanasiasa wasiwemo. Kama nchi nyingine waliunda Tume pasipo wanasiasa, kama Ghana ni *Committee of Experts*, lakini leo tumeridhia wanasiasa wawemo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba sana wanasiasa watakaoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba, kwa heshima zote na unyenyekevu na itifaki zote, muweke maslahi ya Watanzania mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeridhia wanasiasa wawemo kwa kutafakari kwa kina sana na kwa changamoto nyingi. Kwa hiyo, wanasiasa mtakaokuwemo, mtakuwa mmepewa heshima, tunaomba sana Watanzania maslahi yao na nchi yawe ya kwanza, itikadi, *interest* binafsi zije baadaye. Utaratibu wa ku-walk out kwenye hii Tume usiwepo. Tuzungumze, tubadilishane mawazo, jambo linapokuwa gumu, tunaahirisha, tunasema tukutane kesho mpaka tunafikia muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanasiasa, tafadhali sana, tunawaomba sana, mtaapishwa kuwa Wajumbe wa Tume, mtakuwa wajumbe 30 na wanasiasa wakiwemo lakini mtafanya kazi kwa niaba ya Watanzania milioni 40 ambao watakuwepo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunawaomba sana wanasiasa, tumieni njia zozote kuendesha zoezi letu la kukusanya maoni ya Katiba na Katiba yetu Mpya ipatikane ndani ya muda muafaka, kusiwepo na mabishano. Hilo napenda liingie vizuri kwenye *Hansard* na hata Tume yenyewe itakapokuwa kwenye migongano, basi waseme Wabunge walijadili nini kuhusiana na suala zima la wanasiasa. Naomba sana mfuata kanuni na taratibu, *interest* binafsi zitafuata baadaye.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni kifungu cha 12(4) kinachosema endapo suala la kumwondoa mjumbe wa Tume atakayekuwa amekiuka maadili litajitokeza, Rais atateua Kamati itakayokuwa na Jaji, Kamishna wa Tume n.k. Ushauri wangu kuhusu kipengele hiki cha 12(4) isiwe kwamba, endapo suala la kumwondoa mjumbe kwa kukiuka kanuni za maadili litajitokeza, mara Rais atakapounda Tume, sambamba na hiyo Tume, aunde hii Kamati ambayo itachukua *disciplinary measures* kwa wajumbe na ielezwe wazi kwamba Kamati hii ambayo itaangalia masuala ya taratibu za wale Wajumbe wa Tume, itafanya kazi sambamba



kwa muda ambao Tume ile itafanya kazi. Kwa hiyo, eneo hilo ningepomba sana liboreshwe, muda wa Kamati uelezwe, iwe Rais ataunda, siyo atateua, aunde sambamba.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala zima la kifungu cha 17(5)(a) kinachohusu Mkuu wa Wilaya. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na utamaduni sana wa kukusanya maoni. Tumekusanya maoni tulivyotoka kwenye chama kimoja kwenda vyama vingi mwaka 1992. Kwa kutumia chama tawala, tukaulizana, asilimia 80 wakasema tubakie na chama kimoja, asilimia 20 vyama vingi. Wakati tunakusanya yale maoni kwenye *White Paper*, tumewashirikisha wanasiasa hawahawa na ma-DC.

Mheshimiwa Spika, tumekusanya maoni ya Shirikisho la Afrika Mashariki, timu ile ya Shirikisho la Afrika Mashariki imeenda kila Wilaya, kila Kata, Wakuu wa Wilaya waliombwa wawakusanye watu. Ikaandikwa ripoti ya Shirikisho la Afrika Mashariki, twende kwenye *political federation*, Watanzania wakasema *no, it is too early* kwa *political federation* ya East Africa, tuungane kiuchumi kama *European Union* lakini, *fast tracking of political federation* ya East Africa bado ni mapema. Kwa hiyo, huo utamaduni wa kukusanya maoni, Watanzania tunao, tuna uzoefu na ni wataalam sana na leo tunaingia kwenye kukusanya maoni juu ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana kama wengine walivyosema, pale kwenye Mkuu wa Wilaya, abaki vilevile na yule Mkurugenzi asiwepo. Mkurugenzi hana *machinery*, Mkurugenzi ana Wakuu wa Idara, *Council Management Team*. *Council Management Team* ina Mkuu wa Idara ya Kilimo, sijui DMO, atakukusanyia mkutano wapi lakini DC ana *mandate*, ana vyombo, *machinery* zipo za kutosha, iweje leo tuwe na hofu? Hilo ni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine, hofu hiyo ya DC inaondolewa na kura ya maoni, ile taarifa wanakusanya, tunachosema sisi, *they have no room to doctor*. Ile Tume haina nafasi ya ku-doctor chochote kwa sababu ile ripoti itaenda Bunge la Katiba, lakini baadaye kila Mtanzania, mimi na wewe na huyu na yule, tutakwenda kupiga kura ya maoni.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. PINDI H. CHANA:** Nadhani kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye Kura ya Maoni tutasema haya maoni tuliyatoa sisi au yamekuwa *doctored*. Kwa hiyo, *safety valves* zipo za kutosha. Tuheshimu sana nafasi hizi ambazo ziko kwenye Katiba. Kama kuna jambo, ndiyo tukatoe maoni. Kwenye hiyo Katiba tutakapokuwa tunatoa maoni ndiyo tutaelezea hao Wakuu wa Wilaya waweje, Wakuu wa Mikoa waweje lakini leo hii kumwacha Mkuu wa Wilaya eti kwa sababu labda yuko katika vyama fulani na kadhalika nchi yetu haina *private candidate*, lazima uwe na Chama! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni habari ya taarifa. Katika kifungu cha 17 kuna mahali inasema kwamba yeyote atakayetaka kuendesha programu ya elimu atatoa taarifa. Naomba taarifa ile atakayotoa iwe na *time* (iwe na muda) kwamba hiyo elimu itaendeshwa wapi, iwe na tarehe, iwe na eneo, huwezi kutoa taarifa tu. Iwe na tarehe kwamba nataka kutoa elimu tarehe fulani, eneo fulani. Sasa sisi watu wa Iringa au *Kunjombe*, unataka kutoa elimu wapi, kwenye uwanja gani, *Wizoba*, unaelezea pale au Iringa au hapa uwanja wa Madela, uwanja wa Jamhuri, lazima useme nataka kutoa elimu Jamhuri au ukumbi fulani, wa Pius Msekwa na ni muda gani, unataka kutoa elimu. Sasa huwezi kusema tu nataka, ni mwaka mzima, maana Tume yenyewe inakusanya maoni miaka minne. Sasa taasisi inayotaka kutoa elimu itafanya na yenyewe miaka minne au mwaka mmoja au miwili. Kwa hiyo, ile taarifa lazima tui-*qualify*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye taarifa pale tuseme kwamba kuwepo na muda, tarehe, eneo na aina ya elimu ambayo inatakiwa kutolewa. Ni vema sana masuala haya yakazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, sambamaba na hilo, katika kifungu cha 10, nacho naunga mkono kama kilivyo lakini pamoja na maoni yangu haya, naungana asilimia 100 na maoni ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala. *(Makofi)*

## **T A A R I F A**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, unachangia, hakuna cha taarifa hapa. Unachangia, zamu yako imefika, changia! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja ambacho ninahitaji kumkumbusha dada yangu Mheshimiwa Pindi Hazara Chana katika mchango wake ambao alikuwa anatupatia kwa maslahi ya Watanzania, binafsi inasikitisha sana kuona mchangiaji ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Sheria na Katiba. Nikinukuu taarifa yao ambayo imesomwa na Mheshimiwa Kairuki hapa, inasema...

**SPIKA:** Naomba nikusahihishe kidogo. Naomba ukae kidogo. Kwa niaba ya Kamati, alishasoma Mheshimiwa Angellah Kairuki, haya ni maoni yake. Kwa hiyo na wewe changia maoni yako kwa uhuru kabisa, wala usisikitike, wala usihangaika, wewe sema tu. Usisikitike hata kidogo, wewe sema tu unachotaka kusema! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini *message sent*, atakuwa anajua, ahsante. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, basi nami naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Chama changu cha NCCR – Mageuzi pamoja na Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge letu hasa wapinzani halisi, kuweza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kukubali kufanya mabadiliko na kuyaleta ndani ya Bunge letu kwa kuangalia maslahi ya Watanzania bila kujali itikadi za Vyama vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, nakumbuka kwamba ulitokea mvutano mkubwa sana hususan katika Bunge la mwezi Novemba mwaka jana lakini wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mpaka dakika hii wanaendelea kulaumu kwamba watu fulani walitoka nje. Naomba Waheshimiwa Wabunge nichukue fursa hii kuwaombeni, huu siyo muda wa kulaumiana na kulalamikalalamika sana haitatusaidia. Tunataka tuwe wamoja kwa maslahi ya nchi yetu. Vinginevyo, mimi Machali nikisimama na kuanza kunyoosha kidole, haitopendeza hata kidogo na wala haitotusaidia. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Nenda kwenye vifungu!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye vifungu, subiri nakuja. Naomba niwaeleze kwa sababu hata ninyi mlizungumza pia, ni wakati wangu wa kuweza kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kuomba tuungane na Serikali na tuungane na mawazo ambayo yametolewa na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, tuungane na maoni yaliyotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu hasa tukijielekeza kwa mfano, kuna *issue* moja hapa ambayo imachangiwa na Waheshimiwa Wabunge, hasa nikianza na mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, anasema kwamba tuwaondoe Wakurugenzi na badala yake ma-DC ndiyo waweze ku-take zile nafasi za Wakurugenzi. Mimi binafsi naomba niseme kwamba siungi mkono suala hilo la watu kuipinga Serikali tena kwa maana nyingine naweza nikawaita kabisa watu hawa ni waasi dhidi ya mapendekezo ya Serikali. Kwa nini? Naomba nisisitize tena kwamba watu hawa watakuwa ni

waasi dhidi ya Serikali. Serikali naomba muwe na msimamo huohuo na sisi Wabunge tunawaunga mkono. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kuna vigezo ambavyo wameweza kuvianisha kwa mfano, moja, wanasema ma-DC ndiyo wa-*take* hizo nafasi za Wakurugenzi eti tu kwa sababu ma-DC ndiyo wenye dola, ma-DC ndiyo wanamiliki Polisi na kama tutaweka ma-DC basi sheria hii itakuwa imekidhi matakwa ya Sheria za Polisi. Tena wanakwenda mbali kabisa, wanazungumza bila aibu eti kwamba Wakurugenzi wao siyo *machinery*, jamani, hata Wakurugenzi wetu wanaongozwa kwa sheria na sheria tumezitunga hapahapa Bungeni na wana watendaji mpaka kwenye Vijiji na Kata huko. Ni haohao Wakurugenzi ambao ndiyo waajiri wa Maafisa Watendaji wa Kata pamoja na Vijiji, siyo Mkuu wa Wilaya ambaye ni mwajiri wa hao Watendaji wa Kata pamoja na Vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa inasikitisha sana kuona Waheshimiwa Wabunge tunazungumza kwamba Wakurugenzi wetu siyo *machinery*, kivipi? *Does it mean* kwamba hawa Wakurugenzi *just* wamekaa pale tu *from nowhere*? Ni lazima tujaribu ku-*stick* na turudi nyuma kwenye utaratibu wetu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tukija katika *structure* ya utawala wa nchi yetu, hawa Wakurugenzi watakuwa ni sehemu ya Tume na watakuwa kwa maana nyingine ni wasemaji kwa niaba ya Tume ambayo itakuwa imeundwa na Mheshimiwa Rais. Chukulia kwa mfano hata Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi ni nani msemaji katika *rank* ya Majimbo yetu au kwenye Wilaya zetu? Ni Wakurugenzi. Sasa, kuna tatizo gani hapa Waheshimiwa Wabunge wenzangu iwapo tutakubaliana na mapendekezo ya Serikali, shida ni nini? Hapa binafsi naona kabisa kwamba kuna watu wana *interest* za kisiasa ambazo zitakuwa hazina tija kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunasisitiza tena toka mwanzo na wengine ambao wamechangia huko nyuma wamesema tusichanganye wanasiasa pamoja na watendaji, tena wakasema kwamba tuangalie *professionals*...

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu!

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 64(d). Katika kujadili jambo hili, kuna lugha ambayo hasa msemaji aliyekuwa anasema ametumia lugha ya kuudhi. Kwanza, anawaita wengine wasiokubaliana na Serikali kuwa ni waasi. Mbona humu ndani tumeahirisha mambo mawili, wote tena tukakubaliana! Kwa hiyo, waasi tulikuwa wote kwa sababu ni ya uasi, siyo kwa sababu ya jambo la haki! Ninasema, hapa tunazungumza, kila mtu atoe maoni yake, lakini kuwaita wengine waasi siyo sahihi. Katika fasili hii inasema "hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine". Mimi naomba afute. Kama ni uasi waliufanya wao mwaka jana, siyo sisi. Ahsante Mheshimiwa Spika. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge Machali, yalikuwa siyo lazima yale maneno ya uasi na nini, maana kujadili hapa, ni kujadili tu. Kwa hiyo, kama ungeweza kuyaondoa maneno ya uasi wa wenzio, basi yaondoe tuendelee na kazi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi nayafuta maneno hayo, lakini pia nimwombe naye ayaondoe maneno yake kwamba mwaka jana sisi tuliasi!

**SPIKA:** Aaah...

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kwa sababu ameyatumia hapa! Kwa hiyo mimi nayaondoa maneno haya, sina tatizo kabisa.

**SPIKA:** Jamani, akishasema Spika, yeye anatoa mfano, sasa yatoke yote. Ukitoa wewe na yale yanafutika. Ukiyatoa wewe na yale yanakuwa siyo! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Mimi nayaondoa maneno hayo. Sioni tatizo binafsi kuweza kuyaondoa maneno hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Endelea kujadili hoja!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kwa hiyo, niombe kwamba tukubaliane na mapendekezo ya Serikali juu ya suala zima la Wakurugenzi wetu kwenye Halmashauri zetu waendeleo kubaki kama ilivyoletwa na Serikali ndani ya Bunge letu ili kuhakikisha kwamba kutakuwa na *checks and balances* katika mchakato mzima wa kuratibu zoezi la kukusanya maoni kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni lazima ifike mahali tuangalie kwamba tunataka kufanya nini. Lengo letu leo tunataka Katiba Mpya. Mambo mengi ambayo pengine yalisababisha huko nyuma tukaweza kutofautiana kwa sababu ya *interests* za vyama vyetu ilikuwa ni mambo hayahaya ya kisiasa. Kwa kiasi kikubwa naweza kusema kwamba kila watu na vyama vyao walitaka kubaka au kuchukua ajenda ya Katiba ionekane ni ya chama fulani. Niombe hebu tujaribu ku-*shift* mitazamo yetu, tutoke huko ambako tulikuwa na badala yake sasa tujiweke katika *position* ya kwamba wote sasa tunarudi kuwa kama Bunge moja katika jambo hili. Njia peke ya kurudi katika *position* hiyo ni kukubaliana na maoni au mapendekezo ya Serikali juu ya mabadiliko ambayo wameyaleta kwenye Bunge letu leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenda tofauti na mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali, tutakuwa tunaua ile dhana nzima ya ushirikiano na mshikamano wa Bunge letu katika *issue* hii. Kwa nini? Ni vitu ambavyo viko wazi, ukijaribu kuangalia, haya ambayo leo hii pengine yanatufanya kwamba tuanze kutofautiana, ndiyo yale ambayo pengine ilifikia mahali yakatufanya baadhi ya watu tukatoka ndani ya Bunge hili. Sasa tusifike huko, hapa mahali ambapo tumefika ni mahali ambapo ni pazuri. Niombe hebu tuweze kupaimarisha na tuhakikishe kwamba Muswada huu unapita.

Mheshimiwa Spika, hata Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu amesema kwa mara ya kwanza anaunga mkono hoja hii na mimi naomba nizungumze kwamba kwa mara ya kwanza ninaunga mkono hoja hii na yeyote ambaye atapingana na hoja hii...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza! Yeyote ambaye atapingana na hoja hii atakuwa ni muasi. Naomba nimalizie, naka chini. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Kwa kweli unaunga mkono hoja hii kwa sababu hata maneno mengine ya kusema hayapo isipokuwa uasi tu! *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda umepita, ngoja niwataje watakaochangia mchana. Bahati mbaya kama nilivyosema, wote hamtaweza kupata nafasi ya kujadili, muda wetu umekwisha, kwa hiyo, mchana tutakaporudi, watajadili watu sita tu. Atakuwa Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Anastazia James Wambura. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukael!

Nilikuwa nadhani Kiongozi wa Kambi ya Upinzani angekuwepo hapa ili kusudi nimpe nafasi lakini sasa simwoni, kwa hiyo, naendelea na orodha niliyoitaja Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili nichangie Muswada huu muhimu sana wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema leo nimefarijika sana kama Bunge lako kwa kweli tumeandika historia mpya, tulikuwa tumeanza vibaya kidogo lakini sasa nadhani leo tumeelewana na tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuunda Katiba duniani kote hata tutakapounda Katiba yenyewe huwa kuna wakati mnaifika mnaangalia mnakuta kuna mambo hamjaenda vizuri mnaifanya *amendments*, juzi nchi ya Kenya wametengeneza Katiba mpya lakini leo wameshafanya marekebisho zaidi ya mara 107. Kwa hiyo, lililofanyika leo ni jambo la kawaida sana na niwashukuru Serikali kwa kwenda na kuangalia na kuona mambo upya na wakaona sababu ya kuleta haya mabadiliko waliyoyaleta leo na kwa kweli mabadiliko mengi yaliyoletwa leo ni ambayo kwa kweli hata wakati ule tunachangia Wabunge wengi waliyasema, walitamani yafanyike lakini Serikali tunamshukuru Rais Jakaya kwa kwenda kuangalia na kutafakari upya na kuleta mabadiliko haya ili angalau sheria hii iwe nzuri na hatimaye itupatie Katiba nzuri sana na itakuwa muhimu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nina jambo moja dogo sana, wapo watu wanaamini kwamba tuwe waangalifu, Katiba isiwe ya chama kimoja, lakini nadhani Mungu atatusaidia Katiba hii itakuwa ya Watanzania, kwa sababu Muswada huu unauona utakuwa ni wa Watanzania. Ndiyo maana kila mtu amepewa nafasi ya kusikilizwa, amepewa nafasi ya kutoa maoni yake, hata pale ambapo kuna watu hawakupenda kusikilizwa lakini bado wamepewa nafasi. Kwa hiyo, nina hakika yanayofanyika ni mambo muhimu kwa nchi yetu na niwaombe Watanzania kwamba kwa vyovyote vile mabadiliko haya leo siyo ya mwisho, kadri tunavyozidi kwenda kila Serikali itakapona lipo jambo yanatakiwa mabadiliko ninaamini wataleta mabadiliko ili hatimaye sheria yetu iwe nzuri zaidi na iweze kutupatia Katiba nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshaleta mapendekezo ya kufanya *amendment* kwa kifungu kimoja ambacho nimeona ni muhimu tukifanyie mabadiliko na hii natoa taarifa tu. Watu wanasema kufanya mabadiliko siyo jambo jema basi tutakuwa hatufanyi kazi ya kuwa Wabunge, kazi ya Bunge ni kutunga sheria, kazi yetu ya kwanza ni kutunga sheria. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile sheria itakayoletwa hapa hatuwezi kupiga makofi tu, tunalo jukumu la kutoa maoni na tunalo jukumu la kufanya mabadiliko, na hii ndiyo kazi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningewashauri Wabunge, Serikali imeleta yes, lakini kama yapo mambo ambayo unadhani na unayo maoni na unaamini kwamba maoni haya yanaweza yakatusaidia siyo vibaya kuwaomba Wabunge wenzako ili tuweze kufanya mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(7) ukiangalia Kifungu kidogo cha 6 labda nisome ili iweze kueleweka vizuri; *"For the purposes of subsections (1), (2) and (3), the President shall invite fully registered political parties, religious organisations, civil societies, associations, institutions and any other group of persons under whatever name having common interest to submit to the President a list of names of persons for appointment as a members."*

Hili ni jambo jema, naishukuru Serikali kwa kuamua sasa tuunde Tume ambayo kwa kweli sisi sote tutakuwa tumeshiriki. Lakini wameenda pale sehemu ya saba:-

*"In inviting religious organisations, civil societies, associations, institutions or any other group of persons to submit lists of names of persons for appointment as members as provided in subsection (6), the President shall have regard to their respective umbrella organisation."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninachokiona kwa kweli ni *duplication* ya kile kifungu cha 6. Kwa sababu zipo *organisations* nyingi sana nchini ambazo hazina *umbrella organisation*, kwa hiyo, tutakuwa tunazinyima hizi nafasi, kwa sababu Kifungu cha 6 tumekubaliana kwamba *institutions, civil societies* kila watu walete majina ili Rais apate wigo mkubwa zaidi wa kuchagua hiyo Tume, nina hakika itakuwa Tume nzuri kwa sababu itakuwa imeshirikisha watu wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwa Wabunge kwamba Kifungu cha 7 tukifute na sasa kilichokuwa Kifungu cha 8 ndiyo kiwe Kifungu cha 7 ambayo sasa itasomeka, *in deleting subsection (7) appears in paragraph (b), deleting subsection (8) and substituting it for following new subsection.*

*“Subsection (6) shall not be construed as precluding the President from appointing the member or person out of the list of names submitted to him as provided in subsection (6) and renumbering them eight as name as subsection (7).* Kwa hiyo, baadaye tukishafuta cha saba sasa kile cha nane kiwe cha saba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu nchi hii tunazo *organisation* sana, lakini siyo nyingi zina *umbrella*, kwa hiyo, ni vizuri kwa sababu *subsection (6)* ime-*provide* kwa vikundi vyote vya dini, *civil societies* na kila makundi hata mtu mmoja mmoja, basi tumwachie atapeleka *list* na Rais atachagua pale na kile kifungu cha nane kinampa Rais wigo mpana zaidi kwenda popote atakapoona kuna Mtanzania ambaye anaweza akafanya vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niunge mkono mawazo yaliyotolewa kuhusu kurudisha DC, na niwaombe Wabunge hili ni jambo jema sana kwa sababu tumekuwa na Tume nyingi sana hapa Tanzania na kwa kweli Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakifanya kazi hiyo. Tunaamini Rais ana nia njema, haiwezekani sasa anaowateua tusiseme hawana nia njema. Kwa hiyo, watu wote wateuliwa wa Rais kwa maana ya Mawaziri wetu wana nia njema kwenye Muswada huu, ninaamini Wakuu wa Mkoa wana nia njema, Wakuu wa Wilaya wana nia njema na Wakurugenzi wana nia njema, kwa sababu ya muundo wa Kiserikali ni vizuri twende kama tulivyokuwa tunakwenda tumrudishe Mkuu wa Wilaya akasimamia jambo hilo ili tuwaache Wakurugenzi wa Wilaya wetu waendeleo kufanya kazi za maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani sasa nchi nzima tukae miaka karibia mitatu watu wote tunahangaika na jambo moja, tuwaache Ma-DED waendeleo na shughuli ya kuleta maendeleo ya watu na kazi hii ya kukusanya maoni, shughuli hii ya kuandika Katiba tuwaachie watu wa Serikali kwa maana ya Serikali Kuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo leo nimefarijika sana, ninaunga mkono hoja hii na kwa kweli hata hii ya kurudisha wanasiasa kwenye Tume hata wakati ule tunapitisha Muswada huu kama mtakumbuka, mimi nilishauri *strongly* kwamba hata Katibu wa Tume hii siyo lazima awe Mwanasheria kwa sababu jambo la Katiba haliwezi kuwa la wanasheria peke yake, bali nilishauri ni vizuri sana jambo hili tuangalie uwezekano wa kuleta wanasiasa. Nawashukuru sana upande wa Serikali, namshukuru Rais kwa kuliona hilo na kuleta mabadiliko, ninaamini mwisho wa siku tutapata Katiba nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba jambo moja, wale Watanzania wenzetu watakaopata bahati ya kuingia kwenye Tume ambao ni wanasiasa wajue wana kazi moja ya kwenda kutengeneza Katiba ya Watanzania, siyo Katiba ya vyama wanavyotoka ama vyama wanavyovipenda, ama asasi wanazotoka, tunaenda kutengeneza Katiba ya Watanzania. Hili ni jambo la msingi sana lakini nina hakika tunaenda vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na baadaye wakati wa Kamati nitaomba mniunge mkono ili tuweze kufanya mabadiliko katika Muswada huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante, nilisema nitamwita Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Seleman Jafo ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie katika Muswada huu wa Marekebisha ya Sheria ya Katiba yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika michango mingi ya waliotangulia, wengi wameunga mkono, lakini katika kuunga kwao mkono kuna maeneo ya vipengele ambavyo wamevizungumzia ambavyo ndivyo tunaweza kusema wameona kwamba vina tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, hali ya kisiasa nchini siyo nzuri, naomba lieleweke wazi. Watanzania wakati tukiwa nje baada ya Bunge la asubuhi message nyingi walizokuwa wanatutumia wanasema ninyi Wabunge ni watu wa kupitisha kila kitu, sisi Watanzania tunawashangaa. Yaliyo mazuri tunayakataa na yaliyo mabaya tunayakubali kuyapitisha ili mradi yamesemwa na mtu mwingine kayaacha mwingine ni message kutoka kwa Watanzania wanatushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maamuzi yoyote ya kiongozi bora ni lazima yawe na busara na hekima na kiongozi yeyote mwenye maamuzi bora ya busara na ya hekima anapolekwa mabadiliko ya sheria ya namna hii hawezi kukaa na kupinga kwa sababu lengo na nia yetu ni kusaidia Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama chombo cha Watanzania, Watanzania wanajua ukweli, Watanzania wanatusikiliza kwamba malengo ya Muswada wa Sheria ni lazima yapitie njia sahihi kufikia Katiba sahihi ambayo ni safi. *Machiavelli system* inasema ukitumia njia mabaya kupata Katiba bora siyo halali katika mazingira yoyote ya kiuhalisia, kwa sababu huwezi kuiba fedha halafu ukapata utajiri ukasema ule utajiri ni halali, ni kitu ambacho hakiwezekani. Lakini tunachoweza kukifanya ukitumia njia bora kufikia Katiba bora utapata Katiba iliyo bora zaidi, hicho ndicho Watanzania wanakitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro mdogo tu uliopo na mimi ningependa kuuchangia kidogo, tuna kifungu cha 17 kinachohusu maana yake sheria ya awali iliyopitishwa inazungumzia kuwaondoa Wakuu wa Wilaya katika nafasi za kuitisha maoni kwenye masuala mazima ya kuitisha maoni kuelekea kutengeneza Katiba mpya, lakini mgogoro uliopo sasa hivi wengine wanasema waingie na wengine wanasema watoke, lakini kwa mtazamo wa Rais pamoja na washauri wake ambao walikaa naye wakashauriana wakaona inafaa kuwaweka Wakurugenzi na walikuwa na sababu zao kwa nini waliruhusu kuwarudisha Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi zote nchini na sheria za uchaguzi inazungumza wazi kwamba Wakurugenzi kipindi cha uchaguzi ndiyo wanaohusika na masuala yote ya uchaguzi na Wakuu wa Wilaya wapo lakini hawahusika, kwa nini waliwaondoa Wakuu wa Wilaya katika chaguzi na wasiwaruhusu washirikishe kuunda Tume za Uchaguzi? Mantiki ya pale ni kwa sababu wanajua hapatakuwa na haki sahihi ya kuwatendea haki Watanzania kama endapo mtangazaji wa matokeo ya mwisho angekuwa ni Mkuu wa Wilaya ni wazi kabisa na inaeleweka wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo tunasema sawa tuwarudishe, Watanzania wanafahamu kabisa ni kweli Wakuu wa Wilaya katika Wilaya zetu ni Wajumbe wa Kamati za Siasa kwa mujibu wa Ibara za Katiba ya Chama cha Mapinduzi Toleo la mwaka 1982. Ukisoma Ibara ya 42(3), 44(3), 46(3) zote zinazungumzia Mkuu wa Wilaya kama Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa, Mjumbe wa Kamati ya Siasa katika Wilaya ya CCM. *(Makofi)*

Leo Watanzania wanajua kwamba tunataka kuwaweka Wakurugenzi ili kujenga umoja wa Kitaifa ile dhana ya Kitaifa kuondoa hofu ambayo ipo miongoni mwa Watanzania, ni maoni ya taasisi za kidini wameyapeleka kwa Rais, yamezungumzia hilo suala, ni maoni ya taasisi zisizo za Kiserikali, ni maoni ya vyama vya upinzani wamelizungumzia hilo suala, lakini leo mwingine anakuja na dhana kwamba jamani tukiwatoa hawa itakuwa siyo *fair*, tutaweka Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *machinery* ya Halmashauri, Mkurungezi ndiye mwenye Mtendaji wa Kata, Mkurugenzi ndiye mwenye Mtendaji wa Kijiji, Mkurugenzi ndiye mwenye Mtendaji wa Mitaa, hivyo ndivyo Halmashauri inavyoeleweka, lakini katika *machinery* ya Mkuu wa

Wilaya inaishia kwa Katibu Tarafa tu ndipo anapoishia na hii inaeleweka, Afisa Tarafa ama Katibu Tarafa inaeleweka wazi na Watanzania wote wanajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachohitaji kukifanya hapa jamani Tanzania ndiyo tunayohitaji kuiangalia na sisi tupo tayari tunawazungumzia kabisa Watanzania, tupo tayari kutumia busara za Suleiman ndicho ambacho tunajaribu kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatumia busara ya Suleiman alipokuwa anaamua juu ya wanawake wawili waliokuwa wanagombea mtoto mmoja kwamba huyu anasema mtoto wangu na huyu mtoto wangu akasema haya leteni panga achanwe katikati, busara za Suleiman ndizo zinazotumika hapa na ndizo tunazojaribu kukaa na kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiki ndicho ambacho tunakihitaji, mazingira yoyote yanayoweza kutengeneza wasiwasi hayatatupelekea kupata Katiba nzuri. Mimi namuunga mkono Rais, namuunga mkono Mwanasheria Mkuu, nawaunga mkono Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, nawaunga mkono Wabunge wa CHADEMA, nawaunga mkono CUF, NCCR Mageuzi, TLP na UDP na wote waliopeleka mapendekezo yao, kwa sababu lengo na nia ni kuhakikisha kwamba tunalisaidia hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwalimu wangu alipokuwa ananifundisha wakati nikiwa Chuo Kikuu anasema ukizungumza jambo ambalo wengi hawalipendi ni lazima patakuwa na walakini lakini kinachotakiwa ni kuzungumzia ukweli. Mantiki ya kuleta Katiba ni kutaka kuhakikisha kwamba Watanzania wanaweza kujijongoza na sisi kama Wabunge hatuhitaji kuwa watu wa mwisho kabisa kusema kwamba ninyi Watanzania sisi tunavyofikiri mnapaswa kuongozwa hivi, mamlaka ya kuongozwa Watanzania wanayahitaji wenyewe na watu wote wanapozungumza historia itatuhukumu, historia ni hii ambayo tunaitengeneza leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukishindwa kuchukua maamuzi sahihi juu ya vizazi vyetu historia itatuhukumu na kutuhukumu si kwamba utakwenda jela wakati utakapofika, Watanzania watakapofika na kuamua kuchukua hatua zao wenyewe ndipo ambapo sheria itakuwa inatuhukumu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea kujadili Muswada, umuhimu na ubora hizo za akhera, tutafika huko huko. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu kingine ambacho kimejaribu kuzungumziwa kuhusiana na kuondoa baadhi ya wanasiasa kwa maana ya Wabunge na Wawakilishi na kuacha wanasiasa wateuliwe, lengo ni kuongeza wigo mpana, wale wataingia kwenye maamuzi lakini hawataingia kwenye *finalization* yaani hatua ya mwisho juu ya hii Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hata sisi tunasema kwa hili tunaungana mkono na wenzetu na tuwaondoe hofu kabisa kwamba lengo la Muswada katika vifungu vyote ambavyo vimekuwa na wasiwasi ni kuwasaidia Watanzania, tunachokihitaji sasa hivi sisi kama wamoja tukubali kabisa kwamba tuangalie mamlaka za umma, tuangalie Katiba ya nchi ya sasa ambayo tunakwenda kuirekebisha inazungumza nini juu ya vifungu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza maneno hayo machache mimi pamoja na kwamba ninaunga mkono kama alivyozungumza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani lakini ningependa kuwaomba Wabunge wote kwamba sheria hii iliyopo nawaomba tuiipitisha kwa maslahi ya Taifa. Kwa sababu katika mazingira tu ya kawaida kuna mwingine anasema kabisa kwamba hii ipo wazi kabisa kwamba sisi tunasema kwa sababu Rais amepitisha basi Bunge linaweza likafanya maamuzi vinginevyo ili tusimlaumu Rais, lakini tuwe na dhana ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*



**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninapenda nitumie fursa hii kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na kama Mwenyekiti wa chama kutoa maoni yangu binafsi na misimamo au maelekezo mengine kwa Watanzania wenzetu ambao wako chini ya mamlaka ya kutusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba aliridhia kutupa fursa ya kumuona na kwa kweli tulimuona kwa mazungumzo ambayo yalikuwa na maslahi ya Taifa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Tunawashukuru vilevile washauri wake na Serikali yake ambao aliambatana nao katika mazungumzo yetu ya mara kwa mara. Vilevile nawashukuru wadau wengine wote ambao walipewa fursa na Mheshimiwa Rais ya kushauri namna ya kurejesha Sheria hii Bungeni tuifanyie maboresho ili hatimaye ikidhi kiu ya Watanzania ambayo ni Katiba mpya yenye muafaka wa Kitaifa. Kwa hiyo, nawashukuru sana wote waliohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba leo ni mara ya kwanza Taifa letu linakwenda kujadili kwa pamoja uundaji wa Katiba mpya. Kwa hiyo, hatuwezi kusema kuna Mbunge yeyote ndani humu bila kujali chama chake ambaye ana uzoefu wa kuandika Katiba mpya. Ni mara ya kwanza sisi kama Taifa kwa pamoja tunashirikishwa kama Watanzania wote. Kwa hiyo, lazima tukubaliane kwamba tutafanya makosa hapa na pale na tutamhitaji kila mmoja wetu katika nafasi yake binafsi na kila mmoja kama mdau wa chama cha siasa ama taasisi nyingine yoyote ile ile hatimaye kulirejesha Taifa katika umoja ambao wote tunaukusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba katika hatua za awali palikuwepo na hofu kubwa sana kuhusu suala hili. Kulikuwepo na kutokuaminiana kwa kiwango kikubwa mno ambako pengine kungeweza kukalipelekea zoezi zima ambalo lina nia njema likageuka likawa shubiri kwa Taifa letu. Ni dhahiri kwa hatua tuliyofika leo tumeweza kupunguza hofu ile na tutegemee kwamba basi wadau wengine wote wataendelea kutuunga mkono na kila mmoja kwa nafasi yake acheze au afanye kazi kwenye nafasi yake ili hatimaye malengo yetu ya pamoja kama Taifa yaweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hili zoezi ni la muda mrefu na litatuchukua muda mrefu kwa maana hiyo ni lazima kutaendelea kuwepo mabadiliko mengine ya sheria kadri uzoefu na kadri matatizo yanavyojitokeza yatakavyokuwa yanaonekana katika mchakato mzima. Kwa hiyo, ukitazama maudhui ya mabadiliko haya yamelenga zaidi katika awamu ya kwanza ambayo inazungumzia zaidi masuala ya Tume na kukusanya maoni. Nina hakika vilevile wadau wengine wataendelea kutoa mawazo, tutaendelea kupata uzoefu katika muda huu mfupi wa kuanza kazi hii na hatimaye tutaleta marekebisho mengine ya Katiba hatua kwa hatua tuweze kuhakikisha kwamba mwisho wa siku tunapata Katiba njema kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni tulidai sana kuhusu ushirikishwaji wa umma. Pengine hatukueleweka vizuri na pengine wengine vilevile hawakueleweka vizuri. Lakini baada ya Mheshimiwa Rais kuchukua busara za kushirikisha umma katika jambo hili tunaweza tukaona wote leo tunajipongeza katika Bunge hili wote kila mmoja leo anamuona mwenzake siyo adui. Basi ningependa na utamaduni huu wa kutokuonana maadui ueleweke na pasionekane kama pengine kuna mtu ambaye ni jasusi katika mchakato huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile napenda kusema lazima tuwe na uvumilivu wa kisiasa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu naomba hili tuliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, tunapoamua kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge kupeleka ujumbe wetu hatutoki kwa nia mbaya, tunaomba utamaduni huu ueleweke na uzoeeke Tanzania kwamba upo na ni utaratibu wa kidiplomasia na utaendelea kuwepo kama vile tutakavyoona kwamba pengine kwa kufanya hivyo itatusaidia kufikisha message yetu kule kunakohusika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru wote ambao walituvumilia katika hilo na tunaomba waendeleo kutuvumilia, tutaendelea kufanya hivyo kadri zoezi zima la kuboresha sheria au kutengeneza Katiba itakavyozidi kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nijikite kwenye kifungu cha 17, kinachomzungumza Mkuu wa Wilaya. Ni vyema wenzangu tukaelewa kitu kimoja kama kuna kitu kitaharibu mchakato huu wa Katiba ni kufanya miliki ya chama chochote cha siasa ama kufanya miliki ya chombo chochote kingine kile. Katiba hii siyo mali ya CHADEMA, Katiba hii siyo mali ya Chama cha Mapinduzi, Katiba hii haitakuwa mali ya mtu mwingine yeyote kama kikundi. Lakini kila mmoja wetu kwa chama chake ana maslahi katika Katiba hii kwa sababu sisi kwa pamoja ndio tunaunda Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hofu inayotokana na mpango mzima huu ni pale panapoonekana pengine kuna dhamira ya kukifanya chama fulani kiwe kina fursa zaidi katika mchakato huu mzima. Nikijaribu ku-echo mambo ambayo wamezungumza wengine nikirejea Katiba ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 1977 inaoonyesha *categorically* nafasi ya Mkuu wa Wilaya katika siasa za Wilaya. Kifungu namba 76 cha Katiba hiyo kinasema; Mkutano Mkuu wa Wilaya utakuwa na Wajumbe wafuatao: mjumbe namba (c) ni Mkuu wa Wilaya ambaye anatoka katika Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Sasa hii ni dhana kwamba hili suala tukilipuuza na nina hakika napenda kuweka hili suala bayana kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge kama Mwenyekiti wa Chama na Watanzania wote wanisikie, tukilipuuza hili suala huku Bungeni kwa sababu tunazidiana uwingi tunaingiza hofu tena kwa wananchi ambao tumejaribu kuiondoa. Tusiangaliane huku ndani ya Bunge kama kundi ambalo tunaweza kuwa na uamuzi bila kujua kwamba tunapozungumza hapa hatuzungumzi kwa niaba yetu wenyewe, tunazungumza kwa niaba ya mamilioni ya Watanzania wanaotusikiliza huko nje. Nawaomba, chonde chonde Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa vyama vyote vya siasa tulione kwa makini sana hili, tuone hofu ambayo tunaweza kujenga katika Taifa kama tutamrudisha Mkuu wa Wilaya kuwa sehemu muhimu sana katika mchakato mzima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini katika kulizungumza hilo nizungumze masuala ya kiutendaji. Tukirudi katika hii *schedule of amendment* hili Fungu la 17 *role* ambayo inakusudiwa kupewa Mkurugenzi naomba na hapa *nili-clarify* hili maana yake hili suala nalo lilikuwa la ubishi mkubwa katika vikao vingine ambavyo tumekaa, katika kifungu cha 17 kumpa Mkurugenzi mamlaka yale siyo kumpa Mkurugenzi mamlaka yale kama mtu binafsi (*individual*), ni kumpa Mkurugenzi Mamlaka yale kama *institution* na vema Wabunge vilevile tukakubaliana kwamba Mkurugenzi wa Wilaya ana *machinery* pana katika Wilaya yake kuliko Mkuu wa Mkoa. Mkurugenzi wa Halmashauri katika mamlaka yake ana watendaji wengi zaidi katika *control* yake kuliko Mkuu wa Wilaya. Vilevile katika hatua za awali tutakapokwenda kwenye kura ya maoni Mkurugenzi atakuwa anawajibika moja kwa moja chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambaye ataratibu zoezi la kufanya kura ya maoni.

Sasa kwa mujibu wa *schedule of amendment* ambayo tunaizungumza kuhusu majukumu ya Mkurugenzi basi inasema nini? Kwa mfano kifungu namba 17(c)(9) kinasema: "Yeyote atakayetaka kuendesha programu ya elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Katiba atalazimika, endapo ni:-

(a) mtu binafsi, kutoa taarifa kwenye Tume kwa maandishi, au kwa niaba yake, kwa Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa au Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya; au

(b) taasisi, Jumuiya au kikundi kingine chochote cha watu wenye malengo yanayofanana, kitahitaji:-

(i) kutoa taarifa kwa Tume kwa maandishi au kwa niaba yake, Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa au Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya."

Sasa maana yake hii ni nini hii ni mambo ya kiutendaji. Mkurugenzi huyu atapokea mambo chungu nzima maombi atayapeleka *machinery* ya Halmashauri kutumika. (Makofi)

Ndugu zangu lazima tukubaliane kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri kwa maana ya DED huyu ndiye ambaye ni Katibu wa Baraza la Madiwani. Kumkataa Mkurugenzi asishiriki tendo

hili ni kwamba tunakubaliana kwamba tusim-disfranchise Madiwani wote katika process hii, kumkataa Mkurugenzi asiweze kuchukua role yake hiyo ina maana tunawa-disfranchise Makatibu Watendaji, Ma-WEO na Ma-VEO na vilevile machinery nyingine yote ya Mkuu wa Idara katika Halmashauri. Ni hakika Mkuu wa Wilaya hana nafasi hiyo. (Makofi)

Kwa hiyo, niombe sana kwa ajili hiyo kuona kwamba ni muhimu sana DC bado ni Kiongozi wa Serikali na bado ana nafasi nyingi kubwa ya kushiriki katika suala hili. Ni dhahiri kwamba hata katika Halmashauri zetu za Wilaya haiondoi ukweli kwamba DC mara nyingi anashirikishwa kwenye vikao vya Halmashauri na anatoa ushauri wake vilevile. Sasa ni lazima tukumbuke kwamba wale wanatoa mfano kwamba hata Rais anatoka kwenye chama cha siasa, ni kweli Rais anatoka kwenye chama cha siasa, lakini Rais anachaguliwa na kura za Watanzania wote bila kujali wanatoka chama gani cha siasa tofauti na DC ambaye ni appointment ya mtu mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Watanzania wenzetu watuelewe, wasione kwamba CHADEMA wakati wowote tuliamua kulipuuza Bunge, hatuwezi kulipuuza Bunge tunapotoka Bungeni. Ila CHADEMA kwenda kumuona Mheshimiwa Rais ilikuwa ni sehemu ya kutambua kwamba Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtambua Rais kama sehemu ya Bunge. Kwa hiyo, tukaona hata kwenda kumuona Rais ni sehemu vilevile ya pili ya Bunge, kujaribu kuleta busara kwa pamoja ili hatimaye Taifa lipate kile ambacho wote tunakihitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na wengine wote waliohusika, niombe Watanzania wenzangu na niwatake wana CHADEMA wote nchi nzima washiriki zoezi hili kwa sababu kuna nia njema katika hatua ya sasa tukiamini kwamba wenzetu wote tutaona nia njema hii na wote tukaendelea kushiriki katika zoezi hili. Lakini kwa sababu safari ni mwendo na safari ni mchakato tukitumaini kwamba huko mbele ya safari hatutawekeana tena mizengwe ya kutufanya tutoke tena nje katika suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nalitakia Taifa hili Katiba njema. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Uzuri wake humu ndani mnatunga sheria, tungeni sheria hapa zungumzeni kwa nguvu zenu zote kwa hoja nzito halafu mtafika wengi, mtapiga kura kufuatana na utaratibu. Kwa hiyo, naomba kabisa mjipe imani yaani hapa ni mahali pa kutunga sheria jamani, zungumzeni, bishaneni mpaka mtakapoweza wenyewe. Kwa hiyo, mimi nipo kimya nawasikiliza. Sasa nitamuita Mheshimiwa Selemani Jafo kwa sababu nilikuwa nimemuita kwa sababu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akawa ameingia kwa hiyo ndio utaratibu wetu lakini. (Makofi)

**MHE. SELEMANI S. JAFU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na awali ya yote kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. (Makofi)

Leo hii kwa mara nyingine inanirejesha siku chache tulizopita katika mwezi wa kumi na moja wakati ajenda hii ilivyokuja hapa mbele yako na mbele ya Bunge hili Tukufu lakini kwa busara kubwa kwa watu waliokaa hekima wakasababisha mpaka leo hii hatujadili Muswada wa Sheria isipokuwa tunajadili amendment ya sheria ambayo imepita mwezi wa 11. Hii inanipa nguvu sana kuona kwamba leo hii tunajadili vifungu vichache sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia Muswada uliwasilishwa mwezi wa 11 ulikuwa na vifungu 38. Kama kulikuwa na vifungu 38 leo hii tunajadili sehemu mbili tu ina maana kwamba mwanzo Wabunge walifanya jambo sahihi kwa ajili ya mustakabali wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kwamba Bunge lile lilifanya kazi kwa hekima ya hali ya juu kweli kweli. Lakini kwa mjadala ule ule na kwa hekima ile ile namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwathamini Wabunge na kutia sahihi sheria ile na ikawa Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi napenda kushukuru sana nchi yetu imeonyesha ustaarabu wa hali ya juu kweli kweli. Maana ustaarabu wa kwanza unaanzia kwa kiongozi wa nchi. Kama kiongozi wa nchi ameamua kuwakaribisha watu wa maoni mbalimbali kuchukua

maoni katika idara mbalimbali vyama vya siasa kikiwemo Chama chetu cha Mapinduzi, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na vingine lakini wakiwepo na viongozi wa kiroho hasa wa kidini imeonyesha hekima kubwa sana kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hii inanipa nguvu kwamba Watanzania hawakukosea kumpa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kura zote katika uchaguzi uliopita. Ndio maana wenzetu hii leo wamebaini kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nimefarijika sana kwa sababu ukisoma *Hansard* iliyopita nilizungumzia suala zima la ushiriki wa vyombo mbalimbali, suala zima la kushiriki mpaka asasi, mimi nilizungumza kwamba hata asasi mbalimbali na vyama vya siasa viweze kushiriki katika suala zima la mchakato wa siasa. Leo hii nafarijika niseme kwamba ombi la Jafo katika *Hansard* ukirejea utalikuta kwamba leo hii Serikali inalileta hapa kumbe ni mawazo yetu sote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nizungumze jambo moja kubwa kwamba hii kama Watanzania inaonyesha ni hekima kubwa ya Tanzania tuliyokuwa nayo. Kwa bahati mbaya kulikuwa na upotoshaji ulikuwa unataka kufanyika lakini Watanzania leo wanaelewa kwamba Serikali imeleta Muswada huu lakini kwa ajili ya kufanya *amendment* kwa sababu naomba niwaambie ndugu zangu, haya tunayotenda hapa siyo Misahafu, Mwenyezi Mungu ndio alisema hiki ndio kitabu kisichokuwa na shaka kwa watu basi Mwenyezi Mungu ndio kitabu chake hakina shaka. Lakini haya tunayozungumza yote leo hii tunafanya *amendment* kesho tutafanya *amendment* tena. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli kwa nguvu zote naunga mkono hoja hii iliyokuja na iliyoletwa na Serikali hasa ukiangalia jinsi gani wadau mbalimbali watashiriki na wanasiasa katika mchakato huu wa Katiba tunaondoka nao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, namshukuru kaka yangu Mbowe hapa amesema bwana ma-DC wasiwepo kwa mujibu wa kifungu namba 17 na sentensi kubwa alizungumzia suala zima la hofu na hii hofu naomba niwaambie ndio iliyosababisha Watanzania mpaka tulikuwa hatuelewani kwa ajili ya hofu tu. Watu tulikuwa hatuelewani kwa ajili ya hofu. Lakini hofu yetu sasa hivi kila mtu anajua mamlaka ya Rais yana mipaka gani. Lakini bahati nzuri mimi kwa kweli kwa sababu hapa naona ma-DC wamezungumzwa kwa lugha kana kwamba ma-DC hawafai kabisa kwa mujibu wa michango ya watu walivyokuwa wanachangia. Ndugu zangu vile ni vyombo vya ulinzi na usalama katika Wilaya zetu, sisi wote tunaielewa. Bahati nzuri huyo ambaye tumemuamini leo hii ameleta hoja hapa kwa ajili ya kujadiliana ndio aliyewateua Mheshimiwa Rais kuwateua ma-DC. Sasa mimi naona kwamba tutakuwa tunajipa shaka sisi wenyewe kwamba yule tunayemuamini ni msikivu na kila kitu ameteua watu halafu tunasema hawa watu hatuwaamini hata kidogo. (Makofi)

Mimi naomba Watanzania kwa jambo hili tutajipa sisi mashaka, Wazaramo tunasema; "zilongwe mbali, zitendwa mbali" kwamba huku Rais tunamuamini lakini huku tunasema aliyewateua hawa hawafai. Lakini tunasema hawana *machinery* kumbe tunajua polisi wote wapo chini ya DC pale na yeye ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama katika kila Wilaya. (Makofi)

Mimi kwa wale watu walioleta *amendments* zao mimi nitaziunga mkono zile *amendments*. Kuziunga mkono kwangu maana yake hapa nimeunga mkono hii hoja ni kwa sababu lengo letu ni kuweza kuboresha Watanzania waweze kufaidika na mchakato tunaondoka nao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo hii mimi nina imani Watanzania wote wamefurahi. Haya tunayojadili maana yake kila kitu tunajazia nyama pale kulipokuwa na wasiwasi maana hata haya mambo ya DC yawepo maana yake ndio nyama zinajazwa ili mradi Serikali itoke na chombo hapa ambacho tunajua ni sheria ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesema mimi hapa nimeelemewa na furaha lakini furaha kubwa iliyojaa leo mimi ni kwa ajili nimeona busara za Watanzania sasa zimeshafika mahali pake. Katika hili maana yake ni tujifunze jinsi gani Taifa letu hili tunaweza kuliendeleza kwa utaratibu huu wa busara si kitu kingine chochote. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mwenyezi Mungu ampe

nguvu nina imani sote kwa pamoja Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wote tutalipokea jambo hili ambalo linapitisha leo hii kwa nguvu kubwa kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuunga mkono hoja, ningependa kutoa nafasi kwa wengine waweze kuzungumza maana kila mtu ana hamu anataka kujimwaya mwaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa hii nafasi ya kujadili suala ambalo ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu. Kama ambavyo walitangulia wengine nichukue fursa hii kwa dhati kabisa...

**SPIKA:** Hama, naona huo mstari una matatizo. (Makofi)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nadhani hapa nasikika. Kama ambavyo nilitangulia kusema nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika alikuwa na uwezo wa kukataa maombi, lakini akayakubali kwa kushirikiana na wataalum wake tukaletewa marekebisha ya ile sheria tuliyoipitisha. Lakini inawezekana kabisa dhamira njema ya Rais ambayo imeonekana kutokana na marekebisha yaliyoletwa leo tusipokuwa makini tunaweza tukaya-dilute, kwa nini nazungumza hivi? Kuna mambo mawili; jambo la kwanza kuna marekebisha yameletwa, marekebisha ambayo inaonekana kabisa tusipoangalia kwa umakini, tunaweza tukajikuta tunarudi hatua tatu nyuma badala ya kusonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, rekebisha la kwanza ambalo naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anisikie na ile *team* ya Rais ambayo ilishirikiana kuleta haya mambo mema waiangalie. Hofu moja kubwa ya wadau marekebisha ya Mheshimiwa Peter Serukamba, hofu moja kubwa ya wadau ilikuwa ni mamlaka makubwa aliyopewa Rais kuteua Tume na hofu hiyo ikatibua kwa namna nzuri sana na *team* ya Rais aliyokuwa ikikutana na wadau. Ikasema vyama vya siasa na wadau wengine kama ambavyo wametambulishwa na mabadiliko wanaweza wakampelekea ama wanatakiwa wampelekee mapendekezo ya majina na Rais atatakiwa katika uteuzi wake, azingatie yale mapendekezo ya vyama na wadau mbalimbali, lakini mabadiliko haya yakienda mbele zaidi, ili tusimuondolee Rais wetu mamlaka ikasema pamoja na hao kuleta, Rais kuwateua wale haimzui yeye kuongeza wajumbe wengine anaodhani wanafaa. Hiyo ndiyo ilikuwa *spirit*, lakini kwa mabadiliko haya maana mwisho wa siku Chama Tawala ndiyo wengi kwa hiyo, hatujui kwa kiasi gani mmejipanga kupitisha haya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya ambayo yanaletwa na Mheshimiwa Serukamba yanasema; "*subsection (6) shall not be construed as precluding the President from appointing the member or person*" kingereza chenyewe sijui kimeandikwaje *outside the list of names*. Huu ni mgogoro wa fitina. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Rais na timu yake walikubali kwamba wadau wengine mtaleta *list* katika wale wajumbe 30 naweza nikachukua 10 au watano lakini hawa wengine 20 ama 25 nitawateua mimi kwa mamlaka yangu. Kwa marekebisha haya, yataturudisha kule kule na ndiyo uasi aliouzungumza Mheshimiwa Machali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, so mimi nilikuwa na ombi, kama tuna hiyo dhamira tunayoizungumza, dhamira ambayo imeonyeshwa na Mheshimiwa Rais, dhamira ambayo imeonyeshwa na wajumbe ama wadau walioenda kule ikiwemo wajumbe wa Chama cha Mapinduzi, haya mabadiliko tukiyapitisha *back to square one*, hilo la kwanza. Hizo *amendments* za Serukamba tukizipitisha, tunarudi kule kule. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili suala la DC, suala la Mkuu wa Wilaya. Kwanza mimi leo nashangaa imekuaje Wabunge wa CCM wanaogopa sana Wakurugenzi ambao waliwapitisha, nashangaa. (Makofi)

Kama hakuna ajenda ya siri ya kichama kama ambavyo wazungumzaji waliopita wamezungumza, lazima tuseme ukweli mkitumia wingi kupitisha, kuvuruga *its fine* mnayo hayo mamlaka, lakini leo Wakurugenzi ambao walitutangaza sisi na mfumo hadi kule chini Mkuu wa Wilaya hana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina Sheria ya Tawala za Mikoa hapa. Sheria hii ya Tawala za Mikoa inatoa mamlaka ya Mkuu wa Wilaya na ndugu zangu kupitishwa kwa Sheria hii haizuii Sheria zingine kuendelea kufanya kazi, kwa hiyo, kama ni suala la ulinzi na usalama jukumu lake lipo hapa, kama ni suala la kuwa-*facilitate* jukumu lake liko hapa hofu ya nini? Eti Mkuu wa Wilaya amezoea kuitisha mikutano, nimepitia hii Sheria sijaona sehemu hata moja waliosema jukumu la Mkuu wa Wilaya ni kupitisha mikutano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, dhumuni la kumuweka Mkurugenzi kama walivyozungumza waliotangulia ana mfumo kuanzia juu mpaka chini, Mkuu wa Wilaya hana mfumo, Sheria yake hii hapa. Sasa kama tuna dhamira njema kama tunavyosema hatuwezi kupitisha mabadiliko. Ngazi ya chini ya Mkuu wa Wilaya ni Katibu Tarafa na *worse enough* nimeona marekebisha ya Mama Anne Kilango Malecela, namheshimu sana anaenda *further* ukiacha hili la Mkuu wa Wilaya ambae ni kada na ana vyeo vyake sisi tuliogombea kupitia *opposition* ndiyo tunajua adha za Wakuu wa Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kwenye *campaign* Mkuu wa Wilaya ana uwezo wa kumbeba mgombea wa CCM akaenda kuwatisha watu wampigie sembuse kwenye hili? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna watu asubuhi, nadhani alikuwa Mwenyekiti wangu wa Kamati nasikitika kwa sababu Kamati tulipitisha hii kitu kwa *consensus* sasa yeye sijui alikuwepo huko sijui Rukwa sijui huko tulipitisha Kamati kwa ujumla wote anasema anafanya *reference* ya ile taarifa ya Tume ya Nyalali wakati tunajua katika ile Tume ambayo iliwahusisha hawa hawa japo kuwa asilimia 20 walisema tunataka kwenye vyama vingi katika wale asilimia 80 ambao walisema wanataka mabadiliko walionyesha wanataka chama kimoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, walionyesha kwamba wanataka mabadiliko makubwa sana *to the effect* kwamba ni kama vile wanasema wamechoka na mfumo wa chama kimoja, lakini kibaya walioenda kuhojiwa walikuwa ni wana CCM kwa asilimia 95 ndiyo maana kwa busara za Mwalimu zinasema kama wenzangu wamesema haya, lazima nchi nzima inataka mabadiliko. Kwa hiyo, tusitoe *reference* za uongo kwa madhumuni ya kupotosha. (Makofi)

Lakini mabadiliko ya Mama Kilango yanazungumzia kumingiza DAS, kwanza kuna kipengele kimoja cha "b" amesema wale Wakurugenzi waondolewe, wale watu wanaowakilisha kule Zanzibar waondolewe lakini hajatoa *alternative 17(c)(b)* anasema ondoa hii hajatoa *alternative*, sasa sijui kipengele kinabakiaje hapo nadhani Mwanasheria Mkuu utakuwa umeliona hilo kama upo.

Lakini kingine, unamuingiza DAS achukue nafasi ya Mkurugenzi kumpa jukumu la kwenda kutoa ruhusa ama kwa vyama au asasi za kijamii ama mtu mmoja mmoja ambaye anataka kwenda kutoa elimu ya uraia. Katika Sheria Tawala za Mikoa DAS ni nani? Ni *Principal Advisor* wa Mkuu wa Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *this is a joke, this is a joke*. DAS ana *hairachy* gani kufika huku chini? Hana mtu yeyote *just a Principal Advisor* anapewa mamlaka ambayo mabadiliko yaliyoletwa na Serikali yalikuwa na dhamira ya kumpa Mkurugenzi kwa sababu ndiyo ana *machinery*, ana utaratibu kama ambao tunatumia kwenye Tume za Uchaguzi. (Makofi)

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana, nilikuwa naomba sana ndugu zangu kama tuna dhamira ya kufanya ama kuleta ama kuwa na Sheria njema tufanye hivyo, kuna mabadiliko

mazuri yameletwa lakini inasikitisha yale mabadiliko ya msingi ambayo ndiyo core na kiingereza chake cha kuweza kupata wananchi kukusanya maoni kwa ajili ya kuja kujua Katiba yetu itakuaje tunawapa Wakuu wa Wilaya, kuna hoja ya makada, kuna hoja ikaibuka eti kwa nini mnasema huku hamumtaki Mkuu wa Wilaya kwa wataalamu mnataka wanasiasa waingizwe, jamani someni hii Sheria. Sheria inasema hata kama mwanasiasa ataingizwa lazima atimize vigezo vya kitaalum vilivyotolewa kwenye Sheria kwa kuzitumia rungu la DC kujaribu kuzuia utaratibu ambao utaisaidia nchi kupata Katiba nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi mabadiliko haya yaliyoletwa naomba yaangaliwe kwa makini, maana *amendment* ya *amendment* tuyaangalie kwa makini. Rais ana dhamira njema akaweza kutuliza *temperature* ya kisiasa iliyokuwa nje, Bunge tusitumie kuja kuirudisha ile *temperature* iliyokuwa imetulia, tutekeleze wajibu wetu. (Makofi)

Baada ya kusema hayo, ahsante sana ninaunga mkono hoja bila hivyo vipengele vyao, vikilewa sitaunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Kwanza kabisa nichukue tena nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake ambazo ametujalia siku zote lakini zaidi sana kwa kutuwezesha kuuona mwaka huu wa 2012. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nijunge na wenzangu waliotangulia kusema kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza ku-sign Muswada ule ambao tuliupitisha hapa mwezi Novemba. Lakini zaidi sana nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake ambao aliufanya wa kukutana na vyama mbalimbali vya siasa kikiwemo Chama cha Mapinduzi na kuweza kuridhia marekebisho ya sheria yetu ambayo tulikuwa tumeitunga kipindi kile. Kimsingi Mheshimiwa Rais ameonyesha mambo makubwa kama matatu au manne. Kwanza ameudhirishia umma wa Watanzania kwamba yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala si Rais wa CCM. (Makofi)

Lakini vilevile Mheshimiwa Rais ametaka kudhirisha kwamba Katiba hii ambayo tunaitunga si Katiba ya Rais ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile Mheshimiwa Rais ameonyesha jambo lingine ambalo ni la msingi sana, ambalo limekuwa likiwapa wengi sana wasiwasi kwamba Katiba itakapokuwa imetungwa itakuwa ni Katiba ambayo itakuwa sawa na Msahafu, haitaweza kubadilika, lakini kwa kuridhia marekebisho haya, amedhirisha wazi kwamba hata Katiba itakayokuwa imetungwa sio Msahafu, Katiba hii atakuwa tayari kuifanyia marekebisho wakati wowote atakapona inafaa. Kwa hiyo, mimi nadhani niwaombe tu wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuondoe wasiwasi hapa sioni kama kuna sababu kubwa sana ya kufanya malumbano kwa sababu fursa hiyo tunayo kwamba wakati wowote tutakapona kwamba kuna makosa au dosari fulani, marekebisho yatafanyika kwa hiyo hakuna sababu malalamiko yale ambayo tunayasema kwamba vurugu itatokea na nini, mimi sioni kama kuna msingi wa vurugu yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niendeleee tena kusema kwamba Katiba ya nchi ni siasa, lakini wakati huo huo mchakato wa kuipata Katiba ya nchi ukigeuzwa kuwa mchakato wa kisiasa kwa vyovyote vile matokeo yake hayawezi kuwa mazuri na kama tunavyoona katika Sheria yetu inaonyesha wazi kabisa mchakato huu ni wa kisayansi na tutakapoushikilia mchakato huu wa kisayansi, tukauendesha vizuri basi ni dhahiri kwamba tutapata matokeo mazuri na hatutaweza tena kuwa na vurugu katika nchi yetu, wasiwasi wangu ni kwamba tunapotaka kupindisha pindisha na kuingiza siasa katika utungaji wa hii Katiba tunayotaka kuitunga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sheria inazungumza wazi kwamba Tume itaundwa na Tume imepewa baadhi ya majukumu, ina majukumu mengi, lakini baadhi ya majukumu kwanza ni kukusanya maoni ya wananchi, lakini vilevile ni kuchambua maoni yale na kutengeneza rasimu ya Katiba na

baadae kuunda Baraza la Katiba ambalo litahalalisha ile rasimu ya Katiba na baadae Tume hii itatengeneza *report* na kuipeleka kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba ninaunga mkono marekebisho yale ya kifungu cha 6(5) ambayo yanaondoa pingamizi la kuwahusisha viongozi wa vyama vya siasa katika ngazi mbalimbali. Ninaunga mkono, lakini naomba nitoe tu angalizo kwa vyama vya siasa pengine madhehebu ya dini na asasi mbalimbali ambazo tunaona kwamba wataweza kupeleka mapendekezo kuhusiana na ni nani wateuliwe na Mheshimiwa Rais kuingia katika Tume ambayo ataiteua. Ninatoa angalizo kwa sababu moja kwamba wajumbe wa Tume watakuwa ni wachache sana kama tulivyoona ni wajumbe 30 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sidhani kama ni kweli kwamba vyama vyote vya siasa au asasi zote au taasisi za kidini, majina yote yaliyopelekwa kweli Mheshimiwa Rais anaweza akayateua kwa sababu tunaona kwamba Tume hii inahitaji wataalamu zaidi, si wanasiasa wala si viongozi wa dini, wala si viongozi wa asasi. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Rais atazingatia sana vigezo ambavyo vimewekwa katika kuteua wajumbe wa Tume.

Kwa hiyo, angalizo langu ni kwamba wanaweza kuteuliwa watu wachache sana kutoka yale mapendekezo, wanaweza wakawa wawili, anaweza akawa mmoja, wanaweza kuwa watatu sasa swali linakuja tutakuwa wavumilivu? *(Makofi)*

Mimi nadhani hapa kuna swali la msingi la kujjuliza kila mmoja wetu, kila chama cha siasa, kila taasisi kwamba tutakuwa wavumilivu? Tumepeleka majina yetu, mapendekezo yetu halafu baadae tunaambiwa kwamba hakuna aliyeteuliwa, mimi nadhani kazi kwenu. Baada ya kutoa angalizo hilo, mimi niombe tu kwamba tuwe wavumilivu kwa matokeo yoyote yale ya Tume ambayo Rais atatuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho katika kifungu cha 17(5)(a) na (b) ambacho kimekuwa kikizungumziwa na wasemaji wengi waliotangulia kuhusiana na Mkuu wa Wilaya awe ndiyo msimamizi au asiwe msimamizi, kumekuwepo na mabishano mengi sana, kimsingi mimi sikubaliani na suala la kumtoa Mkuu wa Wilaya kuwa msimamizi katika suala hili. Sababu yenyewe ni kwamba siridhiki na sababu ambazo zimetolewa na baadhi ya wachangiaji na sababu moja ni kwamba Mkuu wa Wilaya yuko katika Katiba ya Chama cha Mapinduzi, ameandikwa mie ndani kwenye ile Katiba, lakini nadhani tunafahamu kwamba zipo Katiba za aina mbili, kuna Katiba iliyoandikwa, kuna Katiba isiyoandikwa sasa cha kujjuliza je, hawa Wakurugenzi tunaosema wao ndiyo wawe katika usimamizi huu tuna uhakika kwamba wako katika Katiba ambazo hazikuandikwa pengine wako katika Katiba bubu, tuna uhakika huo? Ndiyo lazima tuwe wakweli kwamba tuna uhakika au tuna uhakika kwamba sio wanachama wa Chama cha Mapinduzi au chama fulani? Kwa nini tunang'angania hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ule uamuzi wa mwanzo kwamba Wakuu wa Wilaya wawe ndiyo wasimamizi wa mikutano hii, mimi naunga mkono ile hoja ya mwanzo na nimhakikishie Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba nitamuunga mkono katika marekebisho yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba Wakurugenzi tutawaona watajitokeza katika ule uchaguzi katika upigaji wa kura za maoni watajitokeza kwa sababu kura za maoni hizi zitafuata ule utaratibu wa uchaguzi mkuu kwa hiyo, lazima watajitokeza kule. Sioni sababu ni kwa nini tulumbane kwamba hapa awe Mkurugenzi hapa awe Mkuu wa Wilaya. Kwa nafasi hii tumwachie Mkuu wa Wilaya, nafasi ya mwisho ya kura za maoni tuwachie Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho katika kifungu cha 17(10) ambacho kinaruhusu asasi, vyama vya siasa, makundi ya watu fulani fulani, taasisi mbalimbali kwamba wao wanaweza wakafanya utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi na kuyapeleka kwenye Tume. Hili mimi nina mashaka nalo sana, nina mashaka nalo kwa sababu moja, Tume hii itakayoundwa ni Tume ya wataalam itakapoundwa itaapishwa.



Lakini vilevile itakaa yenyewe na kupanga kuona kwamba ni utaratibu gani iutumie kuweza kukusanya maoni. Vilevile itapanga utaratibu ambao utawawezesha kufanya *analysis* ya yale maoni. Sasa tutakapowapangia kwamba watumie mtindo gani wa kukusanya maoni wakati mwingine inaweza ikapelekea ugumu wa uchambuzi wa yale maoni kwa sababu tukumbuke kwamba hawatafanya uchambuzi wa juu juu tu, watafanya uchambuzi wa kisayansi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani kama Tume hii tayari ingekuwa imeshaundwa, tungeweza kuwauliza kama hili jambo kwao linawezekana au laa. Kwa hiyo, nilidhani ni vizuri tungewaachia uhuru wao wenyewe waamue ni jinsi gani ambavyo wanaweza wakakusanya maoni ya wananchi, na ninalisema hili kwa sababu kwenda kukusanya maoni si jambo rahisi lazima wawe wamejiwekea mwongozo na tutakaposema asasi, vyama na kadhalika waende, wao watakuwa na miongozo yao tofauti. Sijui na hadidu za rejea watafanyaje na vilevile watakuwa hawajaapishwa kama Tume ambavyo imekuwa imeapishwa. (Makofi)

Lakini vilevile niseme kuna mfano mmoja unapokwenda hospitali, ukifika kule ukampa Daktari vipimo kutoka hospitali nyingine, havikubali vile vipimo, atakuambia lazima wapime kwenye hospitali yao. Sasa sijui kama hii Tume inaweza ikatumia maoni yaliyoletwa na kukindi fulani cha watu kwamba imekusanya maoni kutoka kwa wananchi na ipeleke kwa Tume na Tume ikayategemea hayo maoni kwamba inaweza yakatoa matokeo ambayo ni sahihi. Mimi nadhani matokeo yale hayatakuwa *reliable* sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu niseme kwamba ndugu zangu Watanzania, Waheshimiwa Wabunge sioni kama kuna haja ya kuwa na wasiwasi sana na kulifanya jambo hili kuwa ni jambo ambalo linaweza likatuletea ugomvi mkubwa kiasi hicho. Kwa sababu mchakato wenyewe ukiangalia ni mrefu na mchakato huo unapitia maeneo mbalimbali. Wakikusanya wananchi maoni pia yatakuja yale mabaraza, yale mabaraza ndiyo yatahalalisha ile rasimu ambayo Tume imeandaa. Sasa pale sijui kama tunaweza tukashindwa kugundua kwamba hapa kuna mahali fulani ambapo udanganyifu umefanyika au vipi. Sidhani kama kitu kama hicho kikawezekana kwamba tusigundue. Lakini baadaye itakuja hatua nyingine ya Bunge la Katiba ambapo pia tutakaa na kuyajadili kama tunavyojadili sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Bunge lile litakuwa na watu mbalimbali na wawakilishi mbalimbali. Lakini baadaye na sisi wenyewe zitapigwa zile kura za maoni. Sasa sijui kwa nini tung'ang'anie sehemu moja tu kwamba hii sehemu ndiyo inaweza ikaleta matatizo. Lakini isitoshe mwisho wa siku Mheshimiwa Rais anaweza akaangalia. Kwa sababu tunaambiwa kwamba Bunge la Katiba litavunjwa *immediately* baada ya kuwa Katiba ile imekubalika, lakini Tume haitavunjwa wakati huo huo. Ile Tume itaendelea kufanya utafiti kuhusiana na ile Katiba. Kwa hiyo, sidhani kama Mheshimiwa Rais kwa moyo huu ambao ameuonyesha sasa hivi anaweza akawa tena mgumu kukubali kufanya yale marekebisho ambayo yatahitajika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwanza wewe kwa makubwa mawili, la kwanza kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji jioni ya leo, lakini la pili kukushukuru kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu kwa viwango na kwa hekima ya hali ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuungana na wenzangu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa uhakika na bila kigugumizi kutamka kwamba ninaunga mkono hoja hii. Mtakumbuka na Watanzania watakumbuka kwamba Serikali iliyopo madarakani ya Chama cha Mapinduzi iliwasilisha Muswada wa mabadiliko ya Katiba mwishoni mwa mwaka jana. Kwa hekima ya Mheshimiwa Rais kwa busara ya Mheshimiwa Rais, kwa uzalendo wa Mheshimiwa Rais, Serikali yake ilileta Muswada ambao una vifungu 38 ambavyo tulipitisha ndani ya Bunge lako hili Tukufu, wale tuliobaki humu ndani lakini na hata wale waliotoka nje nao walishiriki kwa maombi na kwa mchango wao wa mwisho na hatimaye tukapata Sheria ambayo Rais aliiridhia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini tulikuwa hatuandiki Msahafu, tulikuwa tunaandika Waraka unaoishi, Waraka ambao unaweza kubadilika kulingana na wakati. Ndiyo maana wenzetu walitambua hili, vyama vya siasa, asasi za kiraia, taasisi za dini zilikwenda kutoa maoni yao kwa kukutana na yule ambaye sote tulimchagua kwa kwenda kwenye jengo lao Ikulu wakakutana na Mheshimiwa Rais na mimi nawapongeza sana kwa kutumia haki yao hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Katibu Mkuu, Dokta Wilbrod Slaa, viongozi wa vyama vingine NCCR-Mageuzi, TLP, CUF na chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kupeleka maoni yao kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wenzangu, viongozi wa vyama hivyo vya siasa na wanasiasa wenzangu kwa kupeleka maoni yao na hii haki kabisa na mimi namshukuru zaidi kwamba ameyazingatia. Lakini kipekee namshukuru sana rafiki yangu mpendwa, mwanaharakati mwenzangu wa zamani Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa hotuba yake nzuri na ya kihistoria. *(Makofi)*

Mimi yule namheshimu sana kwa sababu upeo wake ni mkubwa sana katika masuala ya Sheria, lakini katika msimamo wa mambo ya msingi, Mheshimiwa Tundu Lissu huwezi kumdharau. Unaweza ukatofautiana naye kwenye mambo mengine. Mheshimiwa Tundu Lissu nakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa dhati ya moyo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu watu wajue kwamba busara ya JK si ya jana wala hekima yake si ya jana. Kwa hiyo, leo watu ambao wanazungumza kwa uchungu na mapenzi ya dharura ambayo hata Watanzania wana mashaka nayo kwamba tukitumia nafasi yetu ya Wabunge ya Kikatiba ya kutunga Sheria nafasi ambayo si lazima tukubaliane na Serikali hata kama ni ya Chama changu, wengine wanachukua nafasi hiyo kama ni uasi na kana kwamba wao wana mapenzi makubwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Sasa inafika mahali najiuliza mapenzi haya ya dharura yametokea wapi? Yametokea wapi? Lakini Watanzania wanajua kabisa kwamba aah, Wakristo wanasema ukishajua kweli na hiyo kweli itakuweka huru. Ni vizuri kwamba mmejua na dunia nzima wale ambao walichelewa kujua nao wamejua kwamba Watanzania hawakufanya makosa kwa vipindi viwili kumchagua Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Endeeleni na tuendeleo kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka mapenzi haya yaendeleo yasiwe ya leo tu. Nakuja kwenye hoja kwamba ukiangalia muktadha na mawanda ya Muswada tulionao leo una mambo siyo mengi madogo sana, maana Sheria yenyewe ina vifungu 38 (Sheria ya Mabadiliko ya Katiba). Tunachobadilisha leo ambayo imeleta mapenzi ya dharura na wala hakuna siyo kifungu kamili. Ni vifungu vidogo vidogo, ndiyo marekebisho yaliyoletwa na Serikali. Katika vipengele hivyo kipengele kimoja ambacho ndicho cha msingi ni kuwaondolea kizuizi cha kisiasa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuingia katika Tume ya kukusanya na kuratibu maoni Tume ya kukusanya maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo unaondoa kizuizi na kwa mujibu wa mapendekezo ya Serikali maana yake ni kwamba yeyote ambaye si Mbunge, si Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, anaweza Rais ikimpendeza ama kwa kumuona yeye au kwa kupendekezwa na asasi na vyama anavyotokana navyo au na asasi zingine za kiraia anaweza kumteua mtu yeyote ambaye siyo Mbunge wala si Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, hii ndiyo hoja moja iliyoko hapa. *(Makofi)*

Sasa mimi sina tatizo nayo japo nimeleta mabadiliko kidogo ya kuboresha kwa sababu ukisema ondoa Wabunge, ondoa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini bakiza viongozi wa vyama vya kisiasa, Wabunge ni wanasiasa. *(Makofi)*

Mimi nataka kusema kwa busara hii hii ya Mheshimiwa Rais ambayo anajua wazi kwamba Ole-Sendeka ni Mbunge, hataniteua kuingia kwenye Tume. Lakini ikimpendeza akaona vyama ambavyo vina wanachama wachache, sio wengi sana akaamua kumteua mmoja ambaye ni Mbunge katika jengo hili wala hatabadilisha muundo wa Tume wala ukubwa wa Tume, kwa hiyo,

nakusudia kuleta mabadiliko baadaye wakati wa vifungu. Kwa hiyo, hilo naliacha maana nitapata nafasi ya kulisemea vizuri nitakapoleta hoja yangu. (Makofi)

Sasa nakuja kwenye jambo ambalo linawapa watu taabu. Mwanzoni tulikuwa na *allergy* na neno Rais, hilo limepata chanjo au limepata tiba. Leo *allergy* tuliyonayo ni ya mtu anaitwa Mkuu wa Wilaya. Lakini kazi ya DC kwa mujibu wa Sheria hii ni nini? Ukienda kwenye Sheria ukurasa wa 17 ukaenda kwenye Ibara ile ya 17(5)(a) inasema kwa Tanzania Bara, inasema Tume inaweza kwa Tanzania Bara kumtaka Mkuu wa Wilaya, Afisa Mtendaji wa Kata au Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kijiji kuitisha mkutano wa wakazi wa Mji, Kata, Mtaa ikaendelea. Kwa hiyo, kazi hii hapa ambayo Tume inaweza kufanya ni kumtaka Mkuu wa Wilaya kuitisha mkutano. (Makofi)

Sasa mimi nasema taabu iko wapi? Kwa sababu kama umekubali kuwaingiza wanasiasa ambao ni Wabunge na tukapiga makofi hapa kwamba upo uwezekano wa Mheshimiwa Warioba kuingia, Dokta Slaa kuingia, Baregu kuingia na Mbatia kuingia. Lakini wanasema waingie kwenye Tume ambayo itazunguka na kukusanya maoni. Unasema hawa wanaweza kuingia lakini anayekuitia mkutano ambaye unapata *allergy*, *allergy* hii ya dharura nyingine inatoka wapi? (Makofi)

Huyu mtu anaitwa Mkuu wa Wilaya, huyu jamani ni vizuri mkajua, hapa kinachofanyika ni kupanua wigo. Hatuna tatizo na Wakurugenzi, Wakurugenzi watapata maelekezo, ukimweka Mkuu wa Wilaya maana yake unaongeza na Ofisi ya DC, Mkurugenzi ana kazi kubwa ya maendeleo, lakini atapata maelekezo kwa DC. Mkurugenzi hawezi kumpa maelekezo DAS, wala DC. Tunataka tutumie muundo mzima wa Kiserikali, wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika kuhakikisha kuwa zoezi hili linafanyika kwa wakati na kuwepo na mtu anayeweza kuratibu mambo haya. (Makofi)

Ningependa sana niseme kwamba ningekuwa na muda ningetoa chanjo zaidi ili watu waweze kupona, tatizo hili tena la *allergy* la Mkuu wa Wilaya. Lakini kwa leo nataka niishie hapa hasa ukizingatia kwamba nataka kufika ambapo tunataka tupate Katiba ya nchi, Katiba ya nchi ambayo itakuwa ni zao la Watanzania wote na siyo la chama chochote cha siasa lakini ni Katiba ambayo kwa kweli itakuwa ni fursa ya aina yake ambayo kila mtu akiitumia vizuri tunaweza tukapata Katiba inayoweza kutuvusha kwa miaka mingine ijayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwasihi wenzangu na nimsifu sana Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, aniunge mkono baadaye, atuunge mkono kwenye hili la DC kwamba asiwe na taabu na Mkuu wa Wilaya aweze kuingia katika eneo hilo. Kwa hiyo, nasema kazi kubwa iliyopo mbele yetu sasa kwa dhamira hii hii ambayo tumeanza nayo na kwa kujua kwamba wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yoyote kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(a) na kwamba Serikali itapata madaraka na mamlaka kutoka kwa wananchi. Ni vizuri sana tukahakikisha kwamba tunatumia nafasi hii ya kuwapa Watanzania, kuwatengenezea mazuri ya kuweza kutupa mamlaka katika mihimili yote mitatu ya dola. (Makofi)

Kwa hiyo, nataka kusema kwa kuwa sitaki kupigiwa kengele maana ya kwanza imeshapigwa, nataka niseme ninaunga mkono hoja. Lakini nitawaomba sana Wabunge wenzangu bila kujali chama cha siasa mtuunge mkono katika mabadiliko haya madogo ambayo yanakusudiwa kufanywa. Hii itaonyesha umoja na ukomavu wa kisiasa. Lakini tujue pia kwamba kazi ya Serikali huko ni kuleta mapendekezo. Kazi ya kutunga Sheria ni ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na inatungwa hapa ndani, haitungwi mahali pengine. Huko mengine yote ni mapendekezo tu. AG anaweza kuleta mapendekezo tu lakini hawezi kutunga Sheria, anakuja kama anataka kushiriki, anashirikiana na sisi humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaleta mapendekezo tu, sisi ndiyo tuna mamlaka ya kutunga Sheria hii. Naomba tukalie viti vyetu, tukae tujae ili tuweze kuwatendea Watanzania haki kwa kutunga Sheria itakayotuvusha. (Makofi)

Baada ya hapo naunga mkono hoja na nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi. Ahsanteni sana. (Makofi)

**SPIKA:** Msemaji wangu wa mwisho anakuwa Mheshimiwa Diana Chilolo, nyie vipi? (Kicheko)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa heshima uliyonipa ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Kwanza naomba unisamehe kwa kuchelewa kuingia kwa sababu nilikuwa na vikao vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyofanya kupokea Muswada wetu wa Sheria ya Marekebisho ya Mabadiliko ya Katiba. Kazi aliyofanya kubwa ni kuhakikisha amepitia mapendekezo yetu yote, vifungu vyote tulivyopendekeza Mheshimiwa Rais amevipitisha. Kama ni mabadiliko ni madogo sana sana. (Makofi)

Vilevile nimpungeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavo amekuwa mstaarabu wa hali ya juu, kwa sababu mlango wake uko wazi. Hana ubaguzi, anatambua kwamba yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anawaongoza Watanzania wenye itikadi mbalimbali. Hana sababu zozote za kuelemea upande mmoja bali anapaswa kuwasikiliza Watanzania wote pamoja na itikadi zao. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwapongeze wenzangu wa Upinzani, Novemba, 2011 wakati tunajadili Muswada huu wenzetu baadhi ya wapinzani walitoka nje, mimi nilisikitika sana. (Makofi)

Ndugu zangu, Wabunge wezangu wakati wowote unapotafakari jambo kwanza wakumbuke waliokuingiza hapa, unapoamua kutoka nje utafakari je, walionileta hapa ndani nitakuwa nimewatendea haki ama sijawatendea haki, ndugu zangu anayezila ni mtoto na mtoto anazila kwa sababu anatambua wazi kwamba nikizila mama atanibembeleza, baba atanibembeleza, mtu mzima ukizila nani atakumbeleza? (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana kwa sababu mmeenda mmetafakari, mmeona wajibu wenu ni kuwatumikia Watanzania, mmefanya jambo la kiuungwana sana, hii ndiyo kazi ya mwanasiasa.

Mheshimiwa Spika, leo hii tupo hapa kama timu kuhakikisha tunapitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba kwa manufaa ya Watanzania, Watanzania wanaohitaji Katiba ambayo itawalinda, itawatumikia, italinda maslahi yao barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi sina wasiwasi na maeneo yote, kwanza uwakilishi wa wananchi upo wazi kwenye Sheria hii. Wana nafasi kubwa na pana tena nawatangazia wananchi wote wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Singida, wanawake wa Mkoa wa Singida, wana CCM wenzangu na Watanzania kuwa Tume itakapokwenda kwao, wajitokeze kwa wingi ili waweze kutoa mawazo yao ili haki zao za msingi ziweze kulindwa ndani ya Katiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi sina wasiwasi na idadi ya Wajumbe wa Tume. Idadi hiyo ya Wajumbe 32 mimi naiafiki kabisa na inatosha kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kitu kimoja tu! Naungana na Wabunge wenzangu wote wanaohoji suala la Wabunge pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuenguliwa kwa wanasiasa. Mimi nashangaa! Unaposema kwamba, Mheshimiwa Rais, atapokea majina ya viongozi kutoka Vyama vya Siasa! Unaposema wanasiasa, Mbunge unamwondoa wapi? Mbunge bado ni mwanasiasa! Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi bado ni wanasiasa! Hata hivyo, hofu zetu ni nini Waheshimiwa Wabunge, majina yanaweza yakapelekwa na bado Mheshimiwa Rais, anaweza asichague Mbunge wa aina yeyote wala asichukue Mjumbe yeyote wa Baraza la Wawakilishi. Lakini *formality* ni vizuri tunaposema wanasiasa, Wabunge wawemo na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawemo. Hao ni wanasiasa, hawana sababu yoyote ya kubaguliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vile vile kipengele kingine ambacho naungana na dada yangu hapa Mheshimiwa Mama Malecela, kuhusu Waheshimiwa ma-DC. Mwakilishi katika ngazi ya Wilaya,

Mwakilishi wa Mheshimiwa Rais ni Mheshimiwa DC! Kiongozi Mkuu katika ngazi ya Wilaya ni Mheshimiwa DC! Leo utamchukuaje Mtendaji wa chini umuache mwenye nyumba? Kiongozi Mkuu ni DC, uniambie anayepaswa kupokea wageni! Huyu ndiye msimamizi wa masuala yote ya kiseru. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzetu watuelewe, hatuna sababu yoyote au hila yoyote! Tunachotaka ni kwamba, Mheshimiwa DC apeperushe bendera yake kwa nafasi yake kwa kumwakilisha Mheshimiwa Rais. Hapo ndipo tutakuwa tumetenda haki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Ndugu Mkurugenzi ana kazi zake za kiutendaji! Waacheni Wakurugenzi wasimamie miradi ya maendeleo! Tutawaondoa kwenye kazi za utendaji tuwaingize kwenye kazi za kiseru! Wao sio wasimamizi wa Sera. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge, waelewe DC yuko palepale ndiye mwakilishi wa Mheshimiwa Rais, huwezi ukamweka Mkurugenzi ambaye hana Bendera ukamuacha mtu mwenye Bendera! Kazi iliyosainiwa na Rais, lazima isimamiwe na watu wanaomwakilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina imani wenzetu hawa watakuwa wametuelewa kwamba, sisi hapa hatuko kwa maslahi ya watu wachache! Tuko hapa kwa maslahi ya Watanzania wote. Tunachokifanya ni cha Watanzania wote; hatuna sababu yoyote ya kugombana, tunachotakiwa ni kuungana kama tulivyoingia leo, wote tuko hapa, viti vimejaa! Tufanye kazi moja, tutengeneze Sheria itakayofanya kazi ya kusimamia maandalizi mazima ya mabadiliko ya Katiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono kabisa Muswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnachozungumza ni kile kile! Mnazunguka humo humo mnazunguka humo humo! Halafu kama nilivyowaambia asubuhi, walioomba kuzungumza ni sitini! Sasa tabia ambayo iko humu ndani, nisipoitwa mimi basi wengine wowote hawana haki ya kuitwa!

Nilichokifanya hapa ni orodha ilipopatikana, nimekwenda kwa mtiririko huo huo tu, basi. Niliyemuigiza katikati ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu, kwa mujibu wa Kanuni zetu ni utaratibu. Kwa hiyo, ni lazima hapa, lakini kwangu Wabunge wote mnakuwa sawa! Sasa katika mazingira haya ningefanya nini? Kila mtu nimekwenda kwa orodha yangu na hii kazi inakwisha leo kwa sababu, mnachokifanya hapa ni kurudiarudia tu! Kwa hiyo, kwa mamlaka niliyonayo nimeshafunga majadiliano. (Makofi)

Namwita Mheshimiwa Lukuvi, kwa dakika nilizonazo. Nina dakika zangu nilizopanga. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Muswada huu kwa marekebisho. Kwanza niruidie kama walivyosema wenzangu, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kutuleta pamoja katika kuhakikisha jambo hili limekuja hapa na limejenga umoja wa Taifa, kupitia marekebisho haya. Nampongeza sana kwa kweli, kama walivyosema wenzangu na Mheshimiwa Tundu Lissu, ameandika vizuri kwa maana tulikuwanaye. Nampongeza sana kwa nguvu, jitihada na uwezo wake mkubwa wa kutafakari mengi yaliyokuja kwake na mpaka yakachujwa, yakaja haya machache ambayo leo tunayapitia katika Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Rais amekutana na Makundi yote yaliyotajwa kwenye hotuba yake. Na maoni yaliyotolewa ni mengi sana lakini kwa uchache busara ilitumika, kwanza tuanze na haya ambayo yanahusiana na Tume. Na ndio maana Serikali kwa kushirikiana na wadau haohao tulikaa na kuamua kuleta haya tuliyoyaleta.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia maeneo machache, kwanza, nianze na eneo moja ambalo aliligusa Mheshimiwa Mnyaa, yeye alizungumzia habari ya kura ya maoni na ni kweli walizungumza kwenye kikao. Lakini nataka kumwambia habari ya kura ya maoni hapa, kwanza ni lazima tukumbuke wote, maana hili naona hata Dada yangu Halima kama amelizungumza. Habari ya kura ya maoni itatungiwa Sheria yake, maana hata siku ile tulizungumza, maoni ya

wadau wengi wanasema hawaiamini Tume ya Uchaguzi, lakini maoni ya Mheshimiwa Rais, anasema itakapokuja wakati wa kutunga Sheria ya Kura ya Maoni, mtasema ni chombo gani kisimamie! Kwa hiyo, nafikiri habari ya kura ya maoni isubiri wakati huo.

Mheshimiwa Spika, Mzee Mnyaa hapa anasema kuna hamsini kwa hamsini, nafikiri wakati huo ukifika wa kura ya maoni, tuzungumze. Nasema Mheshimiwa Halima amechanganya hili kwa sababu ya Wakurugenzi kusimamia uchaguzi. Wakurugenzi hapa kwa vyovyote vile kama Sheria itawataka Wakurugenzi kwa mtandao wao kusimamia uchaguzi wa kura ya maoni, tutatunga Sheria. Sheria ya Kura ya Maoni itakuja na itaainisha, itasimamiwa namna gani na nani na nani atashirikishwa. Kwa sasa tumezowea Wakurugenzi Tume ya Uchaguzi inawashirikisha, lakini hatujui Sheria tutakayoitunga itawashirikisha akina nani katika kusimamia kura za maoni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kusema kwamba, pamoja na hizo pongezi, kwa kweli ukiuangalia huu Muswada, mambo mengi sana yamebadilishwa na haya yote ni kwa sababu ya nia njema ambayo iligubikwa katika mijadala yote na wadau. Katika Sheria utakuta kuna mambo mengi ambayo kulikuwa na watuhumiwa, hawaruhusiwi kushiriki katika maeneo mengine! Kulikuwa na adhabu kubwa sana zimewekwa humo ndani!

Mheshimiwa Spika, lakini hata uteuzi wa Tume ukiangalia kwenye Sheria ya mwanzo, ilikuwa ni Rais akishirikiana na Rais wa Zanzibar, peke yao, wanateua! Lakini kutokana na busara hii, Serikali leo inaleta Muswada unaoamta sasa Mheshimiwa Rais, ingawa niwaambieni yaliyo ya ukweli, busara ya Mheshimiwa Rais hata bila Sheria hii kwenye kifungu hiki cha sita (6) nia yake ilikuwa hiyo hiyo. Nia ya kushirikisha wadau katika kuunda Tume alikuwa anafikiria, kwani Watanzania angewapata wapi? Watanzania utawapata kwenye Vyama vya Siasa, kwenye Asasi Zisizo za Kiserikali, kila mahali. Lakini hata hivyo, Serikali imekubali basi kuhalalisha hiyo nia njema ya Rais, kwa kuiandikia Muswada.

Mheshimiwa Spika, hapa, kifungu cha sita (6) kinasema: "Kwa madhumuni ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3), Rais ataalika...". Hili ni jambo kubwa sana! Rais, akiamua kuunda Tume aalike, ataalika au atatoa mialiko kwa Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi Zisizo za Kiserikali na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kuwasilisha orodha, hili ni jambo kubwa sana. Ninavyoona hapa, hakuna hata Mbunge mmoja amelipinga, kifungu cha sita (6)! Hakuna hata mmoja amelipinga, hili ni jambo kubwa. Kwa hiyo, nafikiri hili jambo midhali limebaki, litatunganisha sana na pengine kwa kuwa, lazima Rais atachomoa kutokana na zile orodha, busara yake itatawala tu! Haiwezekani basi, hata kama kuna kifungu cha nane (8) kinachosema asizingatie, halafu majina yote yaje asichukue hata moja! Siamini! Vinginevyo asingekubali jambo hili. Kwa hiyo, nafikiri nia njema ya hili ipo hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa suala la uteuzi wa wanasiasa. Wanasiasa hapa, nataka Watanzania watujue sio kwamba sisi tunajipendelea! Maana wasije wakasema eeh, kumbe marekebishi ya Sheria hii ni kwa sababu wanasiasa wanataka waingie! Sio nia hiyo na wanasiasa wanaoingia hapa sio ilimradi mwanasiasa! Ni mwanasiasa ambaye ametimiza matakwa ya Sheria katika Ibara ya 6(3)(a), (b) na (c); ni mwanasiasa mwenye sifa, sio ilimradi mwanasiasa. Kwa hiyo, ingawa wanasiasa wataingia, lakini ni wale wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nichangie hapa ni kuhusu hili ambalo limetuchukua muda mrefu sana. Naona kuna ubishani mkubwa katika kifungu ambacho Mheshimiwa Sendeka, amekisema vizuri sana, kifungu kidogo cha (5). Kama kuna mtu ana sheria, Serikali inasema, hata mimi nilikuwa naamini hivyo. Kwa kweli, tofauti ya Mkurugenzi na Mtendaji, yaani kwa maana ya kwamba anaweza akatumwa na Tume sioni tatizo lolote. DC kutumwa na Tume sioni tofauti yoyote, kwa sababu, hapa ni *discretion* ya Tume, yaani Tume yaweza. Tume hailazimiki kwenda Wilayani na kuomba kibali kwa mtu kuitisha Mikutano na kwa utamaduni wa sasa haya ni mambo ya kizamani.

Mheshimiwa Spika, leo Tume hii ya kisayansi ambayo ndani yake sasa tuna *Watchdogs*, tuna Viongozi wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, watakaokubali hiyo Tume iburuzwe na DC ni Tume gani hiyo? Ndani humo tuna macho ya watu. Tume inapanga ratiba, inakwenda Mkoa wa Iringa, itazungumza Mkwawa, inatangaza kwenye ma-TV, magazeti, ili watu wajitayarisha.

Unaweza kukuta hapa huyu DC na DED ni *redundant!* Tume inaweza ikapanga ratiba yake kwenye magazeti, ikatangaza, ikaenda zake, hata Mkurugenzi isiwe na shida naye. Kwa sababu, Tume ina madaraka kuliko wote hawa, ila imesema inaweza, ni *discretion*.

Mheshimiwa Spika, lakini ukisoma Sheria hii na Dar-es-Salaam tuna uzoefu, leo mashirika mengi sana yana mikataba na makampuni binafsi na ndio yanayoitisha hata mikutano. Kifungu hiki msishangae Tume ikatumia hata makampuni binafsi kuitisha mkutano kwa sababu, imeruhusiwa, sio lazima imtumie DC au Mkurugenzi. Kifungu hiki namba saba (7) kinasema: "Tume inaweza kumshirikisha mtu yeyote au kumtumia Mtaalam Mwelekezi yeyote kama itakavyokuwa lazima kwa ajili, ya utekelezaji bora wa majukumu yake". Inaweza ikaajiri kampuni moja kutoka Mkoa wa Dar-es-Salaam yenyewe ndio ina-organise conferences na nini, kwa ratiba yake inavyopanga tu! Kwa hiyo, leo hapa tunatoa jasho habari ya DED, habari ya Mkurugenzi, habari ya DC wanaweza wasimtake tu kwa haja ya kuitisha mikutano, TVs zote hizi, Radio zote hizi! Nataka kuwaambieni Tume ikiwa na ukakasi wa Mkurugenzi au DC inaweza ika-opt kifungu cha saba (7). Ikaamua kuajiri Meneja, wakatanguliza Managers wa kuitisha Mikutano huko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri tusigombane, mimi sina *objection*. Tukisema DC na DED wote wawili waingie, sawa. Tukisema Mkurugenzi abaki, sawa. Tukisema DC, lakini ninavyoiona hapa hana kazi. Kwa sababu, hana fursa ya kukataa wala kukubali na ni maagizo ya boshi, Tume ndio yenye Sheria hii. Lakini mtu akiona kwamba, aah, Tume hii ikiona vyovyote vile inaweza ikaamua. Ninachosema ufunguo uko kwenye Tume kwa sababu, ndani ya Tume mle kuna jicho la kila mmoja. Haitakuwa Tume bila Vyama vya Siasa kuwemo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Haya ahsante. Taarifa!

#### TAARIFA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kutoa Taarifa ili *Hansard* isijie ikarekodi vibaya. Mheshimiwa Lukuvi, wakati anazungumza suala la Kura ya Maoni, ali-link na hoja yangu mimi ya ma-DC. Sasa mimi sijazungumza lolote kuhusiana na kura ya maoni! Nimezungumza kile kipengele ambacho kinawapa mamlaka ma-DC kukusanya maoni, hayo ni mazingira mawili tofauti. Kwa hiyo, nitasema niliweke sawa, kuna kukusanya maoni na kura ya maoni ambayo ni hatua ya baadaye baada ya mchakato wa kwanza kabisa kupita. Kwa hiyo, nikasema niliweke sawa, kwa sababu hoja ya kuwapinga ma-DC imeshaelezwa na unapowaambia waende kuitisha mikutano *impact* yake kama ikiwa mbovu hata kura ya maoni itakayokuja kufanywa baadaye na Sheria nyingine vile vile itakuwa mbovu. Kwa hiyo, nilitaka niweke *record clear*.

**SPIKA:** Haya tundaendelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa juu ya Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nataka nimwombe dada yangu. DC hahusiki na kukusanya maoni hapa! Hawezi kukusanya maoni. (Makofi)

**SPIKA:** Aah, nimeshamaliza tutaingia kwenye vifungu, sio mnaanza kubishana nyie wawili! Kwa nafasi gani? Mtoa hoja!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba *Hansard* isichukue aliyoyazungumza kwa sababu ni uwongo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, nimeshaamua, nakuomba sana ukae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, anatoa Taarifa juu ya Taarifa halafu ana-mislead!

**SPIKA:** Tumeshamaliza tutafika...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kama hasomi Sheria sio utaratibu wangu mimi!

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, naomba ukae chini! Tutafika kwenye vifungu, pale kila mtu atapata tena nafasi nyingine.

#### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya marekebisha ya Sheria ya mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 kwa sababu mabadiliko haya yanalenga kushirikisha watu muhimu sana katika jamii ambao ni wanasiasa kutoka vyama mbalimbali. Kwa kuwepo ushiriki wa wanasiasa, nina uhakika kwamba mchakato mzima wa kupata Katiba Mpya utaweza kupata mafanikio makubwa kwa kuzingatia kuwa wanasiasa ndiyo wawakilishi wa wananchi. Nikitolea mfano Wabunge kwa Sheria ya zamani Wabunge wasingeweza kushiriki katika Tume hii kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili ninachopinga ni kule kufuta Mkuu wa Wilaya na kuweka badala yake Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Napendekeza Mkuu wa Wilaya abaki katika mpango mzima wa kuandaa mikutano katika Wilaya yake kwa kuzingatia kwamba Katiba iliyopo sasa inampa mamlaka yote ya kuwa msimamizi na mkuu wa ulinzi na usalama katika eneo lake na siku zote uandaaji wa mikutano katika maeneo ya Wilaya husika, uratibu wote ulitoka katika mamlaka ya Mkuu wa Wilaya kwa mfano Uchaguzi Mkuu na chaguzi zote, mikutano hiyo inaratibiwa na Mkuu wa Wilaya na mambo yote yamekuwa yakifanyika vizuri kabisa. Hivyo basi ninazidi kupendekeza kuwa katika Ibara ya 3(c) kifungu cha 17(a) kwamba maneno Mkuu wa Wilaya yasifutwe yabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini mapendekezo yangu mawili yazingatiwe.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, kifungu 12(4) na (5), kuhusu masharti ya ukomo wa wajumbe. Badala kuwahusisha Mawakili kutoka Vyama vya Mawakili, wateuliwe Mawakili wa Serikali ili kuepusha kuingiza ushabiki kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(5) kuhusu Rais kualika wanaharakati wote walioorodheshwa kuwasilisha orodha kwa dhana ya kuifanya Tume kuwa ya wadau, Tume si ya wadau ni ya Watanzania na Watanzania wamemchagua Rais sio wadau.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja, mimi nachukua nafasi hii kuishauri Serikali kurejesha matumizi ya "White Paper" katika hatua ya utungaji sheria, hii itaondoa matatizo ya kurekebisha Sheria hata kabla haijaanza kutumika na itaondoa malalamiko ya vikundi vingi vinavyodai "public hearing".

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya marekebisha ya Sheria ya *the Constitutional (Amendment) Review Bill*.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja hii. Pili, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi sahihi na wa busara kuleta Muswada huu hapa Bungeni.



Mheshimiwa Spika, Katiba ambayo inatarajiwa ni ya wananchi wote. Hivyo marekebisho haya yanaleta muafaka na imani kwa wadau wote pamoja na wananchi. Inafahamika kwamba, Wakuu wa Wilaya ni sehemu ya Uongozi wa Chama cha Mapinduzi kama Wajumbe wa Kamati za Siasa. Hivyo kuwaondoa katika ushiriki wa moja kwa moja, ni jambo la busara na la kuwajengea moyo wa imani na ushiriki mzuri wananchi wote wasio wanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika marekebisho yanawaingiza Wanasiasa katika kuwahamasisha wananchi. Uamuzi huu pia ni wa kupongezwa sana. Wanasiasa ni wahamasishaji na wako karibu sana na wananchi. Kuwahusisha kutawapa wananchi nafasi ya kupata elimu toka kwa wanasiasa kuhusu mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo muhimu ni kwa wanasiasa hao kuwa wazalendo na kuzingatia maslahi mapana ya Taifa badala ya ubinafsi na vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2011 Muswada ulisomwa kwa Mara ya Pili Bungeni kwa kuzingatia Kanuni za Bunge zinazohitaji Muswada Kusomwa Mara ya Tatu kabla ya kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Vyama vya Upinzani walisusia kujadili Muswada wa Sheria ya Katiba (Wabunge wote 48 wa CHADEMA na wawili kati ya wanne wa NCCCR Mageuzi). Hata hivyo kwa mshangao wa kila mtu, Waziri Kivuli wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliwasilisha maoni ya Kambi hiyo ndani ya Bunge kabla ya kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge kupitisha Muswada wa Sheria, Wabunge wa CHADEMA, CUF, NCCCR na NGO'S kwa wakati tofauti walikwenda kumuona Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo ambalo mimi naunga mkono. Hata hivyo Rais baada ya majadiliano na Vyama hivyo aliscaini sheria hii ambayo sasa ni sheria kamili.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyoletwa ni muhimu lakini naomba Wakuu wa Wilaya waendeleo kusimamia na siungi mkono Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia mchakato huu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, vilevile naunga mkono wanasiasa kushirikishwa katika mchakato huu na kuteuliwa kuwemo ndani ya Tume ya Rais.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono marekebisho yote.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia mjadala wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 2, Mheshimiwa Rais anapewa mamlaka ya kuteua Tume itakayokuwa na wajumbe kutoka makundi mbalimbali ambayo yana maslahi ya karibu na Katiba. Wafuatao naona inafaa wawe miongoni mwa watakaoitwa:-

- (i) Wanasiasa;
- (ii) Viongozi wa Dini;
- (iii) Wanasheria wa Serikali za Mitaa – *Local Government*, ipo karibu na wananchi;
- (iv) Wanasheria wa AG;
- (v) Wawakilishi kutoka Vyuo Vikuu vyenye mchepuo wa Sheria;
- (vi) Wanasheria kutoka Mahakamani; na

(vii) Mawakili kutoka Kampuni binafsi na Taasisi binafsi kama *Tanganyika & Zanzibar Law Society*.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha Hadidu za Rejea ziwekwe kwenye Muswada zijadiliwe ili kumpunguzia Rais kazi pamoja na kumwondolea lawama.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni wajumbe watokao pande za Muungano hususani Tanzania na Zanzibar wajadili mambo ya Muungano tu na mengineyo wawaachie Watanganyika wajadili kwa kuwa ni mambo ya ndani ya Tanganyika na kwa kuwa masuala yanayohusu Zanzibar tu Watanganyika huwa hawayaingilii.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 6(3)d kimetaja jinsia na sio uwiano na kwa kuwa mwanamke wa Tanzania ametokea kwenye shida baada ya kukandamizwa na Sheria na Sera za muda mrefu toka kipindi cha Ukoloni, napenda uwiano uwe sawa ili kuepuka lawama hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 13, Katibu wa Sekretarieti awe ni Mtumishi wa Serikali, nafasi itangazwe, sifa zitolewe na Tume ya Utumishi isimamie zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 21(3) kipo kinyume na Katiba kwa kuwa kinayang'anya uhuru wa mawazo. Tunataka Serikali ituambie kwamba kukwamisha na kuzuia kwa makusudi Mjumbe wa Tume inamaanisha nini na vitendo gani vikifanywa vina-associate kosa hilo, watoe orodha ya vitendo hivyo.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba awali nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie kwenye hoja ya marekebisho ya Sheria ya Katiba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa ukomavu wa kisiasa uliophelekea kukubali kuonana na vyama vya siasa kuhusu suala hili na kuimarisha umoja na utulivu wa kisiasa nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, Ibara ya 17(9)(a) inayopendekeza kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa badala ya Mkuu wa Wilaya, wazo hili sio muafaka kwani ndani ya Wilaya, Mkuu wa Wilaya ndiye mwenye dhamana kuu za utendaji na sio Mkurugenzi. Pendekezo hili ninalikataa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, tatu, kifungu 17(10), pia sikiungi mkono kabisa na ni hatari kuonekana kwenye sheria hii. Kuruhusu vikundi na asasi vikiwemo Vyama vya Sheria ni kuwapora wananchi haki yao. Fursa hii inaweza kutumika vibaya kwa mtu au kikundi kuandaa ripoti ya vikao ambavyo havikufanyika au kuyaghushi maoni ya wananchi. Nashauri uratibu wa vikao ufanywe na Tume kama iivyoelekezwa na Sheria hii. Hili ni hatari kwa vyovyote halikubaliki na wazo hili liondolewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Serikali kwa kuwasilisha mapema Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 ili usomwe Mara ya Pili na Bunge letu Tukufu kujadili.

Mheshimiwa Spika, vilevile nakubaliana na yote yaliyopendekezwa kwenye Muswada huu wakati uliposomwa Mara ya Kwanza na kujadiliwa na Bunge hili. Sina wasiwasi na ushirikishwaji wa wananchi katika kutoa maoni yao juu ya kupata Katiba Mpya ambayo tunategemea itaondoa kero mbalimbali ambazo zinawakumba watu wa kada mbalimbali mfano vijana, wanawake, wazee wakulima madhehebu ya dini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge Maalum la Katiba. Hili nalo sina wasiwasi kwani Wajumbe karibu 600 wataotsha sana kujadili na kuunda Katiba Mpya wakiwemo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wengine 160 watakaoteuliwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu kupitia makundi

mbalimbali tuliyoyaainisha kwenye Sheria ya Katiba Mpya inayoandaliwa. Hivyo idadi yote itakaribia 600.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakuu wa Wilaya kuondolewa kwenye maandalizi ya Katiba Mpya. Nimesikitika sana kuona Wakuu wa Wilaya wameondolewa kwenye Sheria hii ya maandalizi ya Katiba Mpya kwani Katiba ni Sheria Mama inayolinda, kuongoza mambo yote ya kijamii na kisiasa na wakati uleule Wakuu wa Wilaya ni uteuzi wa kisiasa na wanamwakilisha Mheshimiwa Rais kwenye ngazi ya Wilaya. Hivyo kuwaondoa kwenye maandalizi ya kukusanya maoni ya Katiba ni kuvunja daraja la Mheshimiwa Rais kwani mtiririko wa uwakilishi wa Mheshimiwa Rais ni Mtendaji wa Kijiji/Mtaa, Mtendaji wa Kata, Afisa Tarafa, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa ndipo unafika wa Rais wa nchi. Naomba Wakurugenzi wa Halmashauri waondolewe kwenye Sheria itakayotumika kuandaa Katiba Mpya wao wabaki kama watendaji tu wa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuondolewa kwenye orodha ya wanasiasa. Ni kweli usiofichika kuwa katika orodha ya wanasiasa huwezi kuwatoa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hivyo unaposema kuwa Mheshimiwa Rais anaweza kuteua Wajumbe wa Tume ya Katiba Mpya kisha ukawatoa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, hapo tayari umepotosha maana ya wanasiasa. Naomba Bunge likubaliane nami kuwa kati ya wanasiasa, Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapo kwenye kundi hilo. Hivyo ni vema ieleweke kuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawe ndani ya wanasiasa wanaoweza kuteuliwa kuingia kwenye Tume hii ya kukusanya maoni ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nimefarijika kuona sheria inampa uhuru Mheshimiwa Rais kuteua wajumbe wa Tume hii kadri atakavyoona inafaa ili mradi wajumbe wote ni 32. Vilevile mimi naona idadi hii inatosha sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuwapongeza Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Jaji Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wote walioshiriki kuandaa Muswada wa Sheria ya Katiba Mpya. Hata hivyo sioni sababu ya Wabunge wa Chama cha CHADEMA kumsumbua Mheshimiwa Rais Ikulu wakati kwa hiari yao walikataa kujadili Muswada huu uliposomwa Mara ya Kwanza wakatoka nje wote.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono Muswada wa Sheria hii ya mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 kwa asilimia mia kwa mia nikiwa na imani kuwa mawazo yangu yatasikilizwa.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuchukua jukumu kubwa la kushirikisha wananchi kwa kina kabisa katika kutengeneza Katiba Mpya itakayoongoza nchi yetu. Huu ni mfano wa kuigwa na hakuna nchi hata moja inayoshirikisha wananchi kwa kiwango hiki. Hongera sana Rais Kikwete.

Mheshimiwa Spika, pili, tumepata picha, kwa nafasi tuliyopewa na Chama Chetu (CCM) kwenda kwa wananchi kuwaelewesha kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya nchi, kubwa lililojitokeza ni kiu ya Watanzania kutaka kujua na kuelewa Katiba ya sasa ili waweze kushiriki vizuri katika kutoa maoni yao kwa Tume itakayoundwa. Napendekeza Serikali ifanye lifuatalo, nchi yetu ina maktaba kila Mkoa na pia katika Wilaya nyingi. Wananchi wahamasishwe kwenda kwenye maktaba za Mikoa na Wilaya kujisomea Katiba ya sasa na pia hali hii itawajengea Watanzania tabia ya kujisomea na kupanua elimu yao ya uelewa.

Mheshimiwa Spika, tatu, utungaji wa Sheria kuanzia kwenye Muswada ni suala linalofuata Kanuni za Kudumu za Bunge letu, kwa kuwa Sheria zote zinatungwa na kupitishwa kwa utaratibu maalum na Bunge, nilisikitishwa na hatua ya Wapinzani kususia Muswada Kusomwa kwa Mara ya Pili na kutoka nje ya Bunge. Ni dhahiri hawakuwa wamesoma Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 86(1)(2)(a)(b) na (c). Ibara hii imeweka bayana uhalali wa Muswada huo Kusomwa kwa Mara ya Pili kwa kuwa ulikidhi vigezo vyote vya Kusomwa kwa Mara ya Pili. Aliyewasilisha kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa kuwa ni Mwanasheria anastahili kuadhibiwa na Bunge kwa kukiuka Kanuni hii ya 86, ikizingatiwa kuwa pia alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, Kamati

iliyofikisha Muswada mbele ya Bunge zima. Katika kuficha aibu yao hiyo, walikimbilia Ikulu ili kuwachanganya Watanzania wasiwagundue na uzembe wao huo.

Mheshimiwa Spika, Bunge letu lisishushwe hadhi na watu wachache wenye nia ya kuvuruga tu Serikali iliyoko madarakani. Nasema hivyo kwa sababu Wabunge tuna *forum* yetu na mahali mahsusi pa kujadili mambo, kufanya marekebisho ya mambo mbalimbali na kukubaliana au kutokubaliana – yote yanapaswa kufanyika ndani ya Bunge na wananchi wakitusikia. Sote tupo Bungeni tukiwawakilisha wananchi na Wapinzani waelewe kuwa Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge. Majadiliano yetu yote Rasmi ni ndani ya Bunge na siyo Barabarani (Maandamano) wala Ikulu kwa Rais tena kwa sirisiri, haifai. Hakuna majadiliano ya siri kwa mambo yanayohusu Bunge na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayotengenezwa nje ya Bunge yasiruhusiwe kuja Bungeni na tasnia hii ya kumsumbua Rais wetu ikomeshwe ili apate fursa ya kufanya mambo mengine. Haya ni ya Bunge lako Tukufu na Bunge linaweza. Wapinzani kukimbilia Ikulu kwa Agenda zao za siri (ikiwepo kufuta aibu yao mbele ya Watanzania) iwe mwisho kama ni masuala ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nashauri Serikali kwamba, sambamba na marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wote tuelimishwe pia kuhusu Katiba ya Zanzibar ya 1984 iliyofanyiwa marekebisho 2010. Kuna Wanasheria na watu waliosoma vizuri Katiba hizo zilizopo (zote mbili) ya Muungano na ya Zanzibar wameona kuna vipengele vinahitilafiana na wamefikia hatua ya kushtaki Mahakamani. Nimesoma haya kwenye Gazeti la *The Citizen* la tarehe 7 Januari, 2011, ukurasa wa 1 na 3, nina nakala yake.

Mheshimiwa Spika, suala hili limenishtua na hivyo naomba kushauri Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Kuangalia upya Katiba zote mbili zisihitilafiane na kuleta mtafaruku hasa kwa kipindi hiki cha kufanya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

(ii) Tunataka Wabunge na Watanzania kujua kilichopo kwenye Katiba ya sasa ya Serikali ya Kitaifa ya Zanzibar ambapo Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi CUF wanashirikiana kuongoza Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba suala hili liendeshwe haraka ipasavyo ili ifikapo mwaka 2014 nchi yetu iwe na Katiba Mpya.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe na Ofisi yako kwa kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria hiyo. Baada ya utangulizi huu, napenda kuchangia kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu masharti mapya, Kifungu Kidogo cha 5 na 6. Mabadiliko haya yatasaidia kuondoa shaka kwamba Mheshimiwa Rais anaweza kuteua watu wanaoweza kuwa upande fulani tu wa umma. Napongeza sana kwa mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu kualika Jumuiya za Kidini kuleta mapendekezo, natahadharisha kwamba kwa kawaida Dini zote Kuu nchini zina migawanyiko mingi kwa mfano Wakristo wana Katoliki, Lutheran, Anglican, Pentekoste na kadhalika, upande wa Waislam wana Suni, Hamadiya, Ismailia na kadhalika. Utafutwe utaratibu wa mwakilishi wa ujumla ambao hautasababisha makundi mengine waone kama wamebaguliwa au kupuuzwa maoni yao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa wajumbe wa Tume. Kifungu cha 6(1) kilichokuwa kinampa Rais wa Jamhuri ya Muungano akishirikiana na Rais wa Zanzibar, kilikuwa na matatizo ya kumpa

Rais madaraka makubwa sana ambayo kama binadamu yangeweza kuleta mtafaruku mkubwa katika jamii lakini kwa kufanyiwa marekebisho na kwamba sasa Rais atapokea majina ya wajumbe toka makundi na asasi mbalimbali za kiraia, inaleta matumaini ya mchanganyiko maana watakuwa ni Wawakilishi halisi wa wananchi katika makundi hayo na hivyo kutoa maoni yanayowakilisha kada mbalimbali pamoja na matakwa yao wanayotaka yafanyiwe marekebisho katika Katiba Mpya itakayoandikwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu 6(5). Kifungu hiki kilichokuwa kinakataza viongozi wa kisiasa wakiwepo Wabunge na Madiwani kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume, kilikuwa na matatizo makubwa. Kifungu hiki kwa kufanyiwa marekebisho sasa kitatoa wigo mpana kwa viongozi wa Vyama vya Siasa na Madiwani kuweza kukusanya maoni ya wananchi wanaoawaongoza kwa undani zaidi maana wao ndio wanaowawakilisha wananchi katika Kata na Majimbo yao na hivyo kuwa na uwezo mkubwa wa kuyatambua mambo muhimu yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho kwenye Katiba ya sasa. Viongozi wa Vyama vya Siasa na Madiwani ndio watu muhimu ambao wana nafasi ya kuwaelimisha wananchi upungufu uliopo kwenye Katiba ya sasa na hivyo wananchi kuwa na uwezo wa kuleta maoni ambayo yataboresha Katiba itakayoandikwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu 17(a) na (b) kinachoeleza kwamba Wakuu wa Wilaya wawe na mamlaka ya kuitisha mikutano kutoa maoni, kilikuwa kinatia shaka. Ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania ni nchi ya mfumo wa Vyama vingi na ni ukweli kwamba Wakuu wa Wilaya ni Wateule wa Rais ambaye naye ni Mwenyekiti wa Chama Tawala, haiwezi kuingia akilini kwamba Mkuu wa Wilaya ambaye anateuliwa na Rais awe ni mtu ambaye si mfuasi wa Chama chake. Mifano iko hai kwamba wengine ni viongozi wa Chama Tawala na hapohapo ni Wakuu wa Wilaya. Katika hali hii, mikutano itakayoitishwa haitakuwa na usawa kwa sababu kuna uwezekano mkubwa kwa watu watakaoitwa kutoa maoni wawe ni wa Chama Tawala ambao watatoa maoni ambayo yatafurahisha watawala na si maoni ya wengi. Hivyo basi kwa Wakuu wa Wilaya kuondolewa kwenye kazi hii, italeta usawa na uhuru wa watu wote kuitwa bila ubaguzi ili kutoa maoni yao kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pia kifungu kilichoruhusu haki ya kutoa elimu, ya kutoa maoni ili kuweza kufikia Katiba tunayoitaka. Kwa maana hiyo kuruhusiwa kwa asasi na makundi mbalimbali katika kukusanya maoni, kutapelekea Rasimu ya Katiba itakayoandikwa kuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo ambapo makundi haya yalizuliwa kukusanya maoni. Tukumbuke kwamba asasi hizi ni muhimu katika nchi yetu maana zinafanya kazi katika kuleta maendeleo na kuboresha upungufu unaojitokeza katika nyanja mbalimbali za kiongozi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naunga mkono kufutwa kwa mamlaka ya Rais ya kufukuza wajumbe wa Tume na badala yake kazi hii kufanywa na Kamati Maalum. Hili jambo ni jema kwani litamuondolea Rais lawama ya kufukuza wajumbe kwa upendeleo. Tafsiri itakayofuata baada ya mjumbe kufukuzwa na ikiwa kama mjumbe huyo alikuwa anaonekana kutofautiana na aliyemteua hasa katika uendeshaji wa kukusanya maoni ni kwamba hakutendewa haki na hivyo kuzua mtafaruku mkubwa kwenye uso wa jamii. Hivyo Kamati Maalum kwa kujumuisha watu mbalimbali, ni muafaka kwani itatenda haki kwa wajumbe wote wa Tume.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kwenye jambo moja tu katika marekebisho ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pongezi zangu za dhati pamoja na shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa hekima na busara zake zote na wale wote waliofanya kazi na mashauri kupelekea marekebisho ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Spika, napenda kusesitiza juu ya kifungu cha namba 17 ambacho kinapendekeza kuondolewa kwa Mkuu wa Wilaya na badala yake kuwaweka Wakurugenzi wa Wilaya. Hii itaondoa fikra ambazo zinawezajengeka na hata kuondoa imani juu ya Tume ya

Uchaguzi kwani ni dhahiri kuwa hawa Wakuu wa Wilaya ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi (Makada).

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwa na maridhiano kwa kila Mtanzania basi ni vyema tukaunga mkono mabadiliko haya ambayo Mheshimiwa Rais ameyabariki hivyo na sisi Wabunge tuunge mkono kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu uwazi wa ni jinsi gani elimu ya juu ya Katiba itatolea. Je, kuna mikutano ya hadhara au kuna mikutano ya ndani, inazungumzia hili nikijua dhahiri kuna Watanzania wengi hawana elimu ya uraia pamoja na elimu juu ya Katiba ya zamani ili waweze kujua ni wapi kuna mapungufu na hivyo kuweza kutoa mapendekezo yenye kuboresha kupata Katiba mpya kuna manufaa kwa kizazi tulichonacho na kile kijacho miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kama kumetolewa muda maalum kwa ajili ya Tume kukusanya maoni na je, ni kwa kuwaajiri Watanzania wa sehemu zote, bila kujali itikadi, umri, jinsia, kabila na uwezo wa kiuchumi vilevile uwezo wa kielimu. Hivyo basi ingekuwa vyema kama haya yangeainishwa bayana, kwa maana ni kwa muda gani na kwa kutumia jinsi gani ya kukusanya maoni kwa maana ya *methodology* itakayotumika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Mungu ibariki Tanzania, Mungu wabariki watendaji wote kwenye mchakato huu wa Katiba, na mwisho wa siku tuone Katiba mpya ambayo ni kilio cha Watanzania wote.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, katika hatua ya Bunge kuingia kama Kamati, Serikali na Bunge wazingatie kuwa marekebisho yaliyowasilishwa na Wabunge wanne juu ya Jedwali la Marekebisho ya Sheria kwa kutumia Kanuni ya 86(10)(b) hayapaswi kuzingatiwa kwa kuwa yanawasilishwa kinyume na Kanuni.

Kanuni ya 86(10)(b) inamhusu mtoa hoja ambaye ni upande wa Serikali mwenye wajibu kwa mujibu wa Kanuni 86(10)(a)(b) ni mtoa hoja ndiye ambaye anaruhusiwa kufanya marekebisho au mabadiliko ya Jedwali la Marekebisho la tarehe 23 Januari, 2012.

Pia kumejitokeza baadhi ya michango kwamba kwenye kifungu cha 17 kwamba mapendekezo ya Jedwali la Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya kuondoa Mkuu wa Wilaya na kuweka Wakurugenzi yasikubaliwe. Ni vizuri Serikali ikazingatia kwamba suala la kuwaingiza Wakurugenzi ni la msingi sana katika kujenga muafaka wa Kitaifa. Ni vizuri Serikali ikazingatia kwamba kazi zitakazofanywa na Wakurugenzi Watendaji wa Kata, Watendaji wa Mitaa/Vijiji ni kufanya kazi kwa niaba ya Tume katika kuitisha mikutano, kupokea taarifa za wote wenye kutaka kutoa elimu juu ya mabadiliko ya Katiba na kupokea taarifa za vyanzo vya fedha za kutoa elimu husika.

Mheshimiwa Spika, kazi kama hizo wakati wa chaguzi zote kuu Tanzania zimekuwa zikifanya kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi na Wakurugenzi na Watendaji, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya Fedha za Uchaguzi. Hivyo, Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011, kuwapa mamlaka ya kuratibu mikutano, kupokea taarifa juu ya elimu ya mabadiliko ya Katiba na kupokea taarifa za vyanzo vya fedha haitakuwa kitu kipya. Mapendekezo ya Serikali kuwatoa wakuu wa Wilaya na kuingiza Wakurugenzi yamezingatia sheria nyingine.

Pia ni vizuri Serikali na Bunge likazingatia kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 imezungumzia dhana ya kupeleka madaraka kwa umma kupitia Serikali za Mitaa. Mchakato wa Katiba mpya ni mchakato wa umma na watendaji katika Serikali za Mitaa ni Mkurugenzi na Watendaji wake wa Kata, Mitaa na Vijiji.

Ibara ya 145 inaeleza kwamba Serikali za Mitaa ndizo zenye wajibu wa kuwaungaisha wananchi katika masuala ya maendeleo. Tume ikitumia Mkurugenzi na Watendaji wengine wa Serikali za Mitaa itaweza kuwaunganisha vizuri zaidi wananchi kabla mchakato na kukusanya maoni na kutoa elimu juu ya mabadiliko ya Katiba. Kadhalika, kwa ajili ya *chain of command*, Mkurugenzi aingizwe kwa kuwa ndiye atakayeweza kuwasimamia watendaji wa Kata na

Mitaa/Vijiji ambao tayari wameshatajwa kwenye kifungu cha 17 cha Sheria. Wakuu wa Wilaya ni watendaji na kisiasa wa Serikali Kuu ambao chini yao ni Maafisa Tarafa ambao hawako kwenye kifungu cha 17 cha Sheria kwa sasa.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuleta marekebisho haya ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Namshukuru na kumpongeza Rais Mheshimiwa Jakaya kikwete kwa kuyashirikisha makundi ya dini, asasi za kiraia, vyama vya siasa na hatimaye Serikali kuunganisha mawazo yao na kuleta marekebisho yapitishwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni viongozi wachache duniani na nchi ambazo wanatumia hekima aliyotumia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatonya wenzetu wa upande wa pili (wapinzani) ya kuwa mwanasiasa mahiri hakimbii changamoto za majadiliano, badala yake anapaswa ayakabili, awe na ujasiri wa kujadili, hatimaye pande mbili kukubaliana au kutokukubaliana. Naamini kabisa sheria zitafungwa na Wabunge ndani ya Ukumbi wa Bunge na sio mahali popote pengine.

Mheshimiwa Spika, nitajadili kuhusu Ibara 4 katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6(5)(a), Katiba kawaida inaandaliwa na wataalam/wanasheria. Lakini Katiba yoyote ya nchi ina uhusiano kwa kiasi fulani na siasa ya nchi hiyo. Ni vyema Wabunge, Madiwani, wanasiasa mashuhuri wapewe nafasi ya kuteuliwa kuwa Wajumbe katika Tume.

Mheshimiwa Spika, asasi za kiraia, asasi za dini ni vyema wawepo katika Wajumbe wa Tume. Lakini angalizo Ibara ya 37(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuwa huru na hatalazimika kuchukua ushauri wa mtu yeyote. Mheshimiwa Rais katika eneo hili asipangiwe.

Mheshimiwa Spika, zipo asasi kama Jukwaa la Katiba ambalo kabla ya Muswada kuwekwa sahihi na Rais, midahalo yao mingi ilikukwa na upotoshaji mkubwa kwa umma. Inawezekana pia asasi kama hizi zikipewa fursa zikaendelea kupotosha raia.

Mheshimiwa Spika, Ibara 17(5)(a) ya Sheria ya Marekebisho inataja Wakurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kusimamia zoezi la kuita mikutano wakati wa mchakato wa kutoa kura za maoni, badala ya Wakuu wa Wilaya. Ibara 36(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja kuwa Mheshimiwa Rais atakuwa na madaraka ya kuteua viongozi kusimamia utekelezaji wa sera za Idara na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mkuu wa Wilaya ni katika viongozi hao na ni mhimili katika eneo alipo akisaidiwa na Katibu Tawala na Makatibu wa Tarafa. Ana mamlaka na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na hakika kupata umma mkubwa kutoa maoni, ni muhimu yaje Halmashauri ya Wilaya aite mikutano. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ni mtendaji na ana watu pale tu penye mradi anaousimamia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17(9) mtu au taasisi inayotaka kutoka elimu ya kura za maoni sharti asajiliwe na aonyeshe chanzo cha fedha zake. Wiki iliyopita tumepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu, 2012.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kifungu hiki kiwepo kwa sababu inawezekana sana kifungu hiki kikatumiwa na wanaojiita wanaharakati kwa maslahi yao binafsi, wakatumiya fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Ibara ya 21(3) kama ilivyowasilishwa na Serikali, atakayevuruga mchakato awe na kifungu na faini au mojawapo ya adhabu hii kwa upotoshwaji uliowahi kufanya na *media* na Jukwaa la Katiba kuhusu Muswada wa Kurekebisha Katiba. Kifungu hiki ni muhimu kuzuia ukiukwaji wa taratibu na kanuni, katika mchakato wa kura za maoni. Kwa namna hiyo hadhi ya Tume italindwa, haki ya raia kutoa maoni kwa uhuru na mchakato kumalizika kwa wakati bila kuvurugwa na watu wenye nia mbaya.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali idhibiti na kutaka vyombo vya habari na magazeti yanayotoa taarifa za uongo na upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii.

Kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu baada ya kusikiliza hoja na maoni ya wadau mbalimbali.

Kuhusu Tume ya kukusanya maoni kuhusisha wanasiasa hilo naliunga mkono; angalizo ni kwamba wanasiasa hao wawe wenye sifa ya kuwa na ujuzi, uzoefu na uelewa mpana wa masuala ya Sheria, Katiba na uongozi.

Kuhusu usimamizi wa zoezi hili Wilayani kuwe chini ya DC na sio DED. Zoezi hili linahitaji mazingira ya amani na utulivu. Ofisi inayoweza kusimamia mazingira hayo ni ofisi ya DC kwani ndiye mwakilishi wa Rais na ndiye mtawala wa Wilaya na ndiye msimamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama Wilayani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa uamuzi wake wa kuanzisha mchakato wa Katiba mpya ili Tanzania inapoadhimisha miaka 50 iwe imewahusisha Watanzania kutoa maoni ya Katiba wanayoitaka.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na marekebisho ya kuwaongeza viongozi wa kisiasa kuwaelimisha wanachama wao, lakini ninaomba mikutano teleweke na isiwe mikutano ya fujo na malumbano.

Nakubaliana na marekebisho ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuwarudisha Wakuu wa Wilaya katika kusimamia maamuzi haya. Wakuu wa Wilaya ni viongozi ambao ni wasimamizi wa ulinzi na usalama katika Wilaya zao, hivyo Wakuu wa Wilaya ni muhimu katika kusimamia. Naelewa kwamba Wakurugenzi ni Watendaji, watashiriki kusimamia wakati wa kupiga kura za maoni kuhusu kukubali au kukataa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, tuwe makini katika kujadili suala hili bila kuingiza ushabiki wa kisiasa na kutoa taarifa za upotoshaji. Historia itakumbukwa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuweza kuleta Muswada ambao tuliupitisha kuwa sheria na kupitishwa na Rais. Tuna uhakika wa kuwa na Katiba ambayo imeshirikisha wananchi wengi kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuipongeza Serikali.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Chamna cha Mapinduzi kwa kuwa chama sikivu na kwa kuweza kuisukuma kwa haraka na umakini hoja na Muswada ambao unatokana na Sheria ya Katiba ya mwaka 2011.

Kwa hatua hii ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa mabadiliko ya Katiba kwa maana ya kuwa na Katiba mpya itakayoendana na umri wa Tanzania ya miaka 50 baada ya Uhuru wake.

Naunga mkono hatua hii ya Serikali kuleta Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 ili kuweza kupata fursa ya kuitazama tena sheria hii na kufanya marekebisho ili hatimaye kuweza kuongeza ufanisi hususan wa chombo kitakachotekeleza jukumu zito lililopo mbele yetu kwa mustakabali wa Watanzania.



Mheshimiwa Spika, katika marekebisho yaliyoletwa na Serikali yanakusudia kubadilisha kifungu cha 17 kwa kufuta na kumuondoa Mkuu wa Wilaya kwenye jukumu la kuitisha mkutano wa wakazi wa mji, kata, mtaa au kijiji kama atakavyokuwa ametakiwa na Tume ya Rais.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Mkuu wa Wilaya ndiye Kiongozi Mkuu anayeisimamia na kuiwakilisha Serikali katika Wilaya husika, na kwa muundo huo ndiye anayebeba dhamana ya usalama wa raia yaani wa Tanzania katika eneo analolitawala. Vilevile ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, hivyo vyombo vyote vya ulinzi na usalama vipo chini ya mamlaka yake na hivyo hata watu wako kwenye mamlaka ya Mkuu wa Wilaya. Hivi kuna haja gani ya Mkuu wa Wilaya kuondolewa kwenye majukumu yake ya kila siku ya kuwasiliana na kuzungumza na wananchi? Kazi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ni kutekeleza kazi zinazohusu maendeleo kama vile ujenzi wa shule, zahanati, barabara na kadhalika. Hivyo maoni yangu ni kwamba kumuondoa Mkuu wa Wilaya ni kumnyima jukumu lake la kuzungumza na kujadiliana na kuwasikiliza wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hekima na busara zake nyingi zilizopelekea leo Muswada huu kujadiliwa tukiwa wamoja, haya ni mafanikio makubwa kwa mustakaabli wa Taifa letu. Ni pongezi nyingi kwa Rais na Mungu atamlipa kwa wema wake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 2(b)(c) ya Muswada irekebishwe, Tume iondolewe mamlaka ya kuruhusu asasi kuandaa mikutano na iwe kuwa ni wajibu wa asasi kutoa taarifa kwa Tume juu ya mikutano waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebisho ya kifungu kidogo cha 9 kuwa yeyote atakayetaka kuendesha programu ya elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Katiba atalazimika, endapo ni mtu binafsi, taasisi, jumuiya au kikundi kingine chochote cha watu wenye malengo yanayofanana, kitahitajika kutoa taarifa kwa Tume kwa maandishi.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali pendekezo letu la kuwashirikisha wanasiasa nao kuwepo kwenye Tume hiyo ili kuwakilisha kundi la wanasiasa, sambamba na hilo Mbunge na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wawemo kwenye huo mchakato wasitolewe kwani nao ni *part* ya wanasiasa. Hivyo basi, kwa mapendekezo ya Muswada huu na Jedwali la Marekebisho la Serikali kuwa watu pekee ambao sasa hawatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ni Wabunge na Wawakilishi wa Zanzibar, sikubaliani na mapendekezo hayo, naomba Wabunge na Wawakilishi wawe na sifa ili tupate uwakilishi kwenye hiyo Tume.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na marekebisho mengine yote. Nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa hekima na busara zake kubwa na naomba wote tumuunge mkono. Ahsante.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda sana kumshukuru Mungu kwa kunipa fursa na nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza kuwa nyama haramu ya kuchinjwa haiwi halali kwa kupikwa. Katiba nzuri ni kuanza mchakato wake.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa shukurani zangu za dhati kwa vyama vyote vya siasa, taasisi za kidini na asasi zisizo za Kiserikali.

Napenda pia kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kukubali kupitisha na kukubali mabadiliko ya Muswada wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri ieleweke kuwa tunatengeneza Katiba ya nchi na siyo Katiba ya chama chochote cha siasa wala kanuni ya asasi.

Mheshimiwa Spika, inajulikana kabisa Katiba ya nchi iliyo nzuri ni lazima itungwe na makundi yote.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sana Wakuu wa Wilaya basi wasiwe katika hatua za mwanzo za ukusanyaji maoni kwani ni wazi kuwa wakuu hawa ni Wajumbe wa CCM wa Kamati ya Siasa ya Wilaya. Kuweka Wakuu hawa katika hatua hizi kutafanya Watanzania wengi hasa wasio na vyama kuamini kuwa mchakato wa kuitunga Katiba umeporwa na Chama Tawala (CCM).

Mheshimiwa Spika, napenda sana kushauri basi kila jambo katika hatua hizi kuwe cha busara sana. Basi wazo la kuwapa Wakurugenzi nafasi katika kifungu cha 17 ni sawa na hatua hii ni nzuri iliyochambuliwa vyema na itaondoa hofu za kiitikadi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia katika mchakato wa kuchukua maoni ya uundwaji wa Katiba mpya basi kundi la mahabusu na wafungwa ambao watakuwa Magerezani, kuwa mfungwa hakuna maana kuwa mawazo yako hayana maana kwa Taifa hili. Nimeyasema haya mapema ili baada ya kutunga Bunge la Katiba na Kamati ya ukusanyaji wa maoni basi pia wafungwa wachangie.

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru sana kwa kupata fursa hii na ninaunga mkono hasa pale ambapo wanasiasa na Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kubwa anazofanya ili kuimarisha mchakato wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kweli Rais amekuwa mwepesi kuwasikiliza watu wote wenye nia ya kuboresha mchakato wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kizuizi cha kutoteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume baadhi ya watu ambao si Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au Madiwani (Kifungu 6(5) na 28).

Kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume (kifungu 9(5) na (18)).

Katika kifungu cha 17(c) kufuta maneno Mkurugenzi wa Halmashauri na kuweka Mkuu wa Wilaya. Maeneo yote ambayo yanaonesha Mkurugenzi wa Halmashauri na kuweka Mkuu wa Wilaya. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kunijalia afya na kunipa uwezo na hekima wa kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya marekebisho ya Muswada huu ila nashauri Wabunge wenye sifa zifaazo kuwa Wajumbe wa Tume washirikishwe.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine wana upeo, uzoefu na uadilifu mkubwa, si busara kwa sababu tu ya kuwa ni Wabunge watengwe katika Wajumbe wa Tume. Ni vema na ni busara kwa Wabunge wakiwemo iwapo Rais ataona wapo wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17 nashauri Mkuu wa Wilaya awepo badala ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa Wakurugenzi wengi wamekuwa wakifanya kazi zao kwa ubinafsi na kupelekea Halmashauri nyingi kupata hati chafu. Uzoefu huu unatufia wasiwasi katika ushiriki wao katika jambo hilo kubwa na zito kama hili la mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 nakubaliana nacho ila pia nashauri Kamati ya maadili iliyoelezwa ndani ya kifungu hiki Mheshimiwa Rais aiunde sambamba na Tume ili kuweka utaratibu kamili wa nidhamu.

Mheshimiwa Spika, uundwaji wa Kamati ya nidhamu sambamba na uundwaji wa Tume, kutapelekea Tume itakayoundwa kufanya kazi kwa nidhamu kuanzia mwanzo wa mchakato.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu namshukuru na nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa makini katika kusimamia kwa umakini, umahiri, weledi na uadilifu mkubwa. Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara na weledi.

Ewe Mwenyezi Mungu Ibariki Afrika, Ibariki Tanzania na watu wake. Ahsante sana na ninashukuru.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyotajwa hapo juu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kuungana na wachangiaji wengine kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake nzuri ya kuweza kuona kuwa kuna umuhimu wa kuleta mabadiliko ya sheria hii kwa wakati huu. Kwanza napenda pia kuunga mkono hoja hiyo pamoja na maoni ninayoleta kwako.

Kifungu cha 17(5)(a) mimi kwa maoni yangu nashauri maneno ya Mkuu wa Wilaya kuwa katika Kamati au Tume ya kukusanya maoni.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya ni mtu muhimu sana katika mchakato huo haswa kutokana na majukumu yake ili kumwacha Mkurugenzi wa Wilaya akiendelea na kazi yake na majukumu yake ambayo yanahusu maendeleo ya Manispaa lakini unapounganisha na Mkuu wa Wilaya katika jambo hili yeye atatusaidia zaidi katika mchakato huu wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie kwenye kifungu cha 6.18 kwamba Tume inaweza kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu ili kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki kikitumika vibaya kinaweza kuharibu utaratibu na nia njema ya kupata maoni toka kwa wananchi. Ni lazima Tume iwe makini kufuatilia mikutano hii ili kuhakikisha kuwa kweli inakusanya maoni hayo na siyo vinginevyo. Pia isije ikatokea watu wakajifungia mahali na kutoka na mawazo kwa hisia au itikadi zao na kuyafanya ya wanachama wao.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingi nasema marekebisho hayo nayaunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. SAMIA HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa ila sikubaliani na kifungu cha 7 kinachopendekeza kumwondoa Mkuu wa Wilaya na kumweka Mkurugenzi wa Halmashauri. Kifungu kibakie kama kilivyo kwenye Sheria inayorekebisha.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Rais kwa kukubali kukutana na wadau mbalimbali na vyama vya siasa kuwasikiliza na kukubali kuleta marekebisho haya. Pia naipongeza Serikali kwa kukaa na Mheshimiwa Rais hatimaye kukubaliana na kuleta marekebisho haya na ninayaunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naamini mia kwa mia Mheshimiwa Rais amefanya au amekubali kuleta marekebisho haya kwa wewe kushiriki kikamilifu na kuamini marekebisho yaliyoletwa ni ya msingi sana. Kama ulivyokaa na Mheshimiwa Rais na Serikali kwa

ujumla nilivyoona marekebisho haya ni muhimu, nakuomba uendelee kuyajengea hoja ndani ya Bunge hili Tukufu ili marekebisho haya yapite kama yalivyopendekezwa katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amani ya nchi hii ipo mikononi mwenu. Mkikubaliana na hoja ya kutaka kuwarudisha ma-DC katika Tume hakika amani itavurugika na maana ya Katiba kuwa ya Watanzania itafutika itakuwa ni Tume itakayoleta Katiba itakuwa ni ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mmetumia busara sana, nakuomba simamia hali hii isije ikabadilika kama nilivyosema amani ya nchi hii mnayo mikononi mwenu. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, katika mchakato mzima si busara Wakuu wa Wilaya ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi na Wajumbe wa Kamati ya Chama hicho kuwa katika Tume ya kuratibu mchakato wa mabadiliko ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, tushirikishe Taasisi Zisizo za Kiserikali, asasi za kiraia na taasisi za kidini tukijumuisha maaskofu, mapadri na masheikh ili kuleta haki sawa. Kusiwepo na upendeleo wa aina yoyote katika kuteua Wajumbe wa Bunge la Katiba ili kuleta usawa katika kuratibu utaratibu mzima wa mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iondolewe katika kusimamia mchakato mzima kwani hata wakati wa uchaguzi ilionyesha udhaifu mkubwa.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Naunga mkono hoja kuwa Mkuu wa Wilaya ndiye aliye na wananchi wote, ndiye anayemwakilisha Rais Wilayani, ndiye mteuliwa wa Rais. Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama na ulinzi katika Wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, uzoefu katika Uchaguzi wa 2010 Wakurugenzi wali-side na waliwaelekeza watumishi wote wa Serikali katika Idara zao na hasa walimu na walimu wakatoa maelekezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na vyuo vya aina zote kuwa kinyume na CCM. Lakini pale ambapo wafanyakazi hawakutii kwa siri wallichagua CCM. Mkurugenzi anasimamia watumishi ngazi ya Wilaya, Kata, Kijiji tu. Lakini watumishi wote katika ngazi hizo lakini pamoja na wakulima, wafanyabiashara, wanaume kwa wanawake, vijana, wazee, watoto, wagonjwa kwa wazima, vichaa, walemavu wote wapo chini ya Mkuu wa Wilaya na kwa lolote lisilo la usalama, Mkuu wa Wilaya ndiye anawajibika ndiye anayetoa majibu kwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika kushirikisha asasi za kiraia napendekeza wanaharakati wafuatao washiriki Bibi Ananilea Nkya, Bibi Hellen Bisimba, Jukwaa la Katiba na TAWLA.

Mheshimiwa Spika, na wengine ma-catalyst wa migomo na fujo maana wanafahamika.

Mheshimiwa Spika, baada ya masahihisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Aidha, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kuonyesha ukomavu wake wa uongozi na uvumilivu uliotukuka. Rais wetu ana nia njema hususan dhana ya utawala bora. Hili amelitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, vifungu vilivyoletwa vina mantiki kubwa na vitasaidia kuboresha ufanisi na utekelezaji wa Sheria hii. Naomba sasa niingie kwenye kutoa maoni yangu kuhusiana na marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 6(5) kuna mapendekezo ya kuongeza vifungu vidogo vya (6) mpaka (8). Kifungu cha 6(6) kina lengo la kuwaruhusu wanasiasa kuweza kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume, kwani inawezekana kukawa na wanasiasa wenye sifa za kuteuliwa

kuwa Wajumbe wa Tume. Aidha, katika kufungu cha 12, naipongeza Sheria kwa kuleta marekebisho kwani katika kufungu hicho kilikuwa hakijabainisha utaratibu utakaotumika katika kumwondoa Mjumbe wa Tume atakayeshutumiwa kukiuka kanuni na maadili. Kwa kutambua hili, Serikali inapendekeza kuongeza kufungu kipya kidogo cha 4 ambapo Rais anapewa mamlaka ya kuunda Kamati itakayofanya uchunguzi dhidi ya Mjumbe huyo wa Tume.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mapendekezo ya kuongeza kufungu kidogo cha 5 ambapo kinaipa Tume mamlaka ya kusimamia nidhamu ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Tume. Ni vyema majukumu ya Tume yakazingatiwa katika kufungu cha 18 kinapendekeza kuongeza kufungu kipya kidogo cha 6 kitakacho ruhusu asasi, taasisi na makundi mengine ya watu kukusanya maoni toka kwa wanachama wake. Serikali na Tume wawe makini ili kuhakikisha kwamba maoni yatakayotolewa ni halisi na hayajatolewa kwa kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia mapendekezo ya kuongeza kufungu kipya cha 17(a) ambapo yanalenga kuruhusu mtu binafsi, taasisi, jumuiya au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana kuendesha programu ya elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Katiba baada ya kutoa taarifa kwa Tume au kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa upande wa Tanzania Bara au Katibu wa Baraza la Mji kwa upande wa Zanzibar. Kinaendelea mbele zaidi kuzitaka taasisi au vikundi hivyo vitakavyotoa elimu kwa umma vinapaswa kuwa ni vile vilivyosajiliwa kisheria na vitatakiwa kubainisha vyanzo vyao vya fedha vitakavyotumika kwa ajili ya gharama hizo.

Natoa angalizo kwamba ni vyema Muswada ueleze wazi kama kutakuwa na kibali kitatolewa kwa mtu au taasisi au laa. Lakini pia Muswada haujaweka wazi nini kitatokea endapo ruhusa ya kuendesha programu ikishatolewa itakapojitokeza wanaendesha programu wanafanya upotoshaji kwa walengwa wanaopewa elimu hiyo ya umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hekima kubwa aliyoonyesha na kuhakikisha kuwa tunaendesha zoezi kwa amani na salama na nchi yetu kubaki kioo cha dunia kwa kuwa sasa vyama vyote na asasi zote, dini zote zitashiriki kwa usawa katika mchakato wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hekima na busara ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete leo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linajadili kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kufungu cha 17 kurejesha Mkuu wa Wilaya na kumwondoa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Nina wasiwasi vyama vya siasa na asasi za kiraia siji iwapo watapeleka mawazo ya wanachama/wananchi au yao binafsi. Mimi bado naamini Tume ndiyo iwe mchukuaji wa maoni ya wananchi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa busara na hekima aliyotumia katika kusikiliza makundi mbalimbali pale walipomuomba, jambo ambalo limesaidia sana kuweka utulivu na amani nchini. Hali hii itasaidia kupata Katiba mpya ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja ya kuwashirikisha wanasiasa katika Tume ya kukusanya maoni ili kupata Katiba yenye mtazamo wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa wapo viongozi wastaafu ambao ni wanasiasa wenye uzoefu na weledi mkubwa katika masuala ya kisheria, kidiplomasia na kisiasa. Hata hivyo nashauri kama yupo Mbunge au Mwakilishi mwenye sifa zinazostahili, basi hao nao wafikiwe katika Tume. Aidha, Mheshimiwa Rais asilazimike kufuata orodha yote ya vyama vya siasa au asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani na marekebisho ya Serikali kuwa kufungu cha 17(5) kifanyiwe mabadiliko ya kumwondoa DC na kumwingiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya. Kiutawala

DC ndiye mwakilishi wa Rais kule Wilayani na ndiye mtawala. Vilevile ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, DC abaki kama sheria ya sasa ilivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kumpongeza Rais kwa kutia saina Muswada mara tu baada ya Bunge kupitisha mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja pamoja na marekebisho hayo niliyoyataja.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara kubwa aliyoionyesha kwa kukubali kukutana na makundi mbalimbali kusikiliza maoni yao kuhusiana na Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mapendekezo ya kuwatoa Wakuu wa Wilaya kwenye Tume ya Katiba, siridhiki/siafiki pendekezo hilo. Wakuu wa Wilaya wawepo (B. 3 section 17(a)(b).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii nami niweze kuchangia kwa maandishi.

Kwanza naanza na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria na Katiba kwa maoni na ushauri waliotoa kuhusu Muswada wa haya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Namba 8 ya mwaka 2011. Nampongeza sana pia Rais katika hili.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Wizara ya Katiba na Sheria kwa Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kilichonipa faraja zaidi ni kwa jinsi ambavyo katika hili kumekuwa na mawazo na ushauri wa pamoja pasipokujali tofauti za itikadi za vyama. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja kwa sababu zifuatazo; kwanza mabadiliko au utungaji wa sheria ni lazima uzingatie masharti ya Katiba na mahitaji ya kisheria kwa wakati unaokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inayojihusisha na mambo ya Katiba imepitia Muswada huu na kuona mapendekezo ya Serikali yana mashiko nami naunga mkono sana.

Mheshimiwa Spika, yote nayaunga mkono isipokuwa kifungu cha 17(a) kinachomuondoa Mkuu wa Wilaya na kumweka Mkurugenzi wa Halmashauri. Napingana na pendekezo hilo kwani kama walivyoongea wachangiaji wenzangu, Mkuu wa Wilaya ndiye mtawala katika Wilaya husika na hivyo kumwondoa Mkuu wa Wilaya katika Tume si sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini Mkuu wa Wilaya awepo katika zoezi zima la upatikanaji wa Katiba mpya.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa utaratibu wote alioutumia katika mchakato mzima wa marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa rai kwa wanasiasa wasitumie mchakato huu kufanya siasa zao. Napenda kusema Katiba ya Watanzania ni ya wananchi wote, hivyo nashauri Watanzania wote twende tumeshikana katika hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa Wabunge au Wawakilishi ambao watakuwa na sifa ya kuweza kuteuliwa kuingia kwenye mchakato huu, naomba wasifungwe, wasinyimwe nafasi katika hili.

Mheshimiwa Spika, pili, nashauri kwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Mheshimiwa Rais wote wapo chini ya Chama cha Mapinduzi, kama hoja Mkuu wa Wilaya yupo chini ya Chama cha Mapinduzi, hata Rais yuko chini ya Chama cha Mapinduzi. Hivyo basi, naomba tusidhalilishie nafasi ya Wakuu wa Wilaya kwa hisia za kisiasa. Hivyo, naomba Wakuu wa Wilaya waingie kwenye mchakato huu ili kurahisisha mchakato mzima wa kukusanya maoni katika suala hili la mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutia saini Muswada na kuwa sheria ya mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya 41 tangu Rais aisaini na kuwa sheria. Hivyo ni wajibu wetu kikanuni sisi Wabunge kupitia na kuifanyia marekebisho kwa kujadiliana kwa mawazo mbalimbali na hatimaye kupata muafaka na kupitisha mapendekezo yake katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kawaida katika kazi za utungaji sheria zinazokwenda kuwa mwongozo wa kazi za Serikali na mambo muhimu kama hili la marekebisho ya Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katiba ndiyo moyo wa nchi yetu, ndiyo unaoongoza na kusimamia mambo yote ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Sasa ni wajibu wetu sisi kuwa makini na wamoja katika mambo ya msingi hususan katika hili tusiweke tabaka la kubaguana na ndio itakuwa chanzo cha kutengeneza Katiba itakayobagua watu wetu. Ni wajibu wetu kuheshimu na kusimamia kwa pamoja mawazo ya kujenga badala ya kuyapa nafasi mawazo yatakayotutoa katika mhimili wetu wa kihistoria wa umoja ni nguvu na kila Mtanzania ana haki sawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza sana Rais kwa hatua alizochukua kukutana na makundi mbalimbali ya kisiasa na kijamii kwa minajili ya kujenga umoja na kutoa fursa pana ya mawazo nje ya Bunge. Amefanya kazi nzuri, nawapongeza wale wote walioshiriki na kutoa mawazo yao na leo tupo katika hatua hii ya kufanya marekebisho ya kuboresha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, nasifu wanasiasa na wananchi, tulichukulie suala hili ni la kwetu sote, tofauti za kiitikadi tuziweke pembeni, tuitunge Katiba yetu tukiwa wananchi na wazalendo wa Tanzania kwa mustakabali wa nchi yetu. Tanzania yenye neema tele inawezekana.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

(a) Ibara ya 2(6), (3) Kifungu kinaeleza kwamba Rais ataalika Jumuiya za Kidini, makundi na Taasisi nyingine kama zilivyotajwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Jumuiya za Kidini zifutwe, zisiwepo kwa sababu kwanza katika nchi yetu tuna madhehebu mengi ya dini zikiongozwa na imani zao tofauti. Aidha, hakuna chombo chochote kinachounganisha madhehebu yote kitaifa, hivyo itakuwa vigumu kufikia madhehebu yote ya dini. Pia itakuwa vigumu katika uteuzi wa majina yatakayowakilisha Taasisi zote za Kidini kwani mfumo uliopo hauruhusu wao kukaa pamoja na kuteua Wawakilishi wao ambao kupitia uteuzi huo ndiyo Mheshimiwa Rais atateua kati yao kuwawakilisha kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, aidha, mahitaji ya madhehebu ya dini yanatofautina. Mfano Waislam hitaji lao kuu kitaifa ni kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi, Wakristo nao wana mahitaji yao, kila dhehebu lina hitaji lake.

Mheshimiwa Spika, ikizingatiwa kwamba idadi ya Wajumbe wa Tume ni 32 tu, naamini kabisa ni vigumu kwa Rais kuteua Mjumbe kwa kila kundi. Hivyo, kwa kushindwa kutekeleza hayo, inaweza kuleta mgogoro wa kijamii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, kwa vile Serikali haina dini, ila wananchi wake wakiwemo sisi Wabunge tuna dini zetu, basi niwaombe Mashehe, Maaskofu, Wachungaji na

Viongozi wote wa Taasisi za Dini kutumia watu wao kuwasilisha maoni yao na kuwasaidia Tume iweze kuwafikia kwa urahisi.

(b) Kifungu cha (9) kinaeleza utaratibu wa kuendesha *program* ya elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kifungu hiki kwani kwanza itasaidia watoaji elimu wasigongane kwenye eneo moja na kuepusha vurugu zisizo za lazima kutokea. Aidha utoaji taarifa kwa viongozi na Watendaji wa Serikali za mitaa/miji lazima izingatiwe na kusisitiza.

Mheshimiwa Spika, aidha ni lazima Taasisi, Jumuiya au kikundi kitakachotoa elimu kwa umma vizingatie viwe vimesajiliwa, lakini lazima sheria iseme endapo taasisi imepatikana inatoa elimu kwa umma na imebainika haijasajiliwa? Je, ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa? Lazima sheria itamke adhabu kwa Taasisi hizo ambazo zinafanya kazi kinyume cha sheria.

(c) Kifungu cha (10) kinatoa fursa Taasisi, Jumuiya au makundi ya watu kuandaa mikutano ili wanachama wao kutoa maoni na kisha kuwasilisha kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na kifungu hiki, ila nashauri kwenye mikutano hiyo lazima awepe mwakilishi wa Serikali awe katika Serikali za Mitaa/Kijiji ikiwezekana ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu isije ikatokea viongozi wa Taasisi fulani kujifungia wao wenyewe kuandika maoni yao halafu waseme ndiyo maoni ya kikundi au Taasisi zao na kusababisha kuwanyima haki ya kuchangia na kutoa maoni wanachama wao na Tume kupelekewa maoni yasiyo na uwakilishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais baada ya kujadiliana na wadau ameivzesha Serikali kuleta marekebishi ya kuboresha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, na kwa kuwa zoezi zima la kuandika Katiba mpya linahitaji muda wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja na kuhimiza kazi ianze mara moja. Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini wanasubiri wataalam na asasi mbalimbali kuwapa elimu ya uraia na utungaji wa Katiba ili waweze kushiriki kikamilifu.

Mwisho, naomba Baraka za Mwenyezi Mungu kuendelea kumpa Rais wetu hekima ya kuongoza na kusimamia zoezi hili la kihistoria. Nasi wananchi tutambue kwamba kazi hii inahusu mustakabali wa Taifa letu na watoto wetu na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, mshikamano, maono, uvumilivu na hata sadaka/*compromise* ili muafaka upatikane.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALLA:** Mheshimiwa Spika, awali nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutia saini sheria hii ambayo ni muhimu sana kwa mustakabali mwema wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kuwaondoa Ma-DC, sioni muafaka kwa kuwa Mkuu wa Wilaya ndiye mhusika mkuu wa usimamizi wa mwenendo wa siasa, amani na utulivu katika sehemu husika. Kwa hiyo, nahisi badala ya kumwondoa DC, ni vyema wakaongezwa Wakurugenzi/Makatibu ndani ya sheria. Siyo kweli kabisa kuwa Wakurugenzi/Makatibu kuwa hawana itikadi yoyote. Pili hawana amri ya kuwa na mamlaka ya kusimamia amani/siasa na wataalam wa mwenendo wa utawala kiujumla.

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukaainisha ni nani mwenye mamlaka ya kutoa elimu na sifa gani. Ambaye anastahiki sifa hizi lazima ziainishwe, la si hivyo, kutakuwa na hatari ya badala ya



kuelimisha ukweli kutakuwa na upotovu wa elimu hiyo lakini pia ukusanyaji wa maoni lazima uratibiwe na Tume au wakala wake waliopewa kwa mujibu wa “*Defined Criteria*”.

Ni imani yangu jambo hili litaleta utulivu katika ukusanyaji wa maoni. Siyo vyema kabisa kila mtu, kila kikundi, kila asasi au taasisi kuingia mtaani na kukusanya maoni. Huo ni unyimaji wa haki za mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa jambo hili, siyo vyema kupunguza kiwango cha adhabu kwa yeyote atakayesimamisha hatua za kupinga hatua za mchakato wa kusimamia utoaji wa elimu au ukusanyaji wa maoni. Maoni yangu, adhabu kali itumike kwani ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, Katiba ili ipitishwe ni lazima iwe kwa *simple majority* ya asilimia zaidi ya 50. Siyo vyema kutokana na hali ya kisiasa hasa ZNZ ikiwekwa zaidi ya asilimia 60. Basi kutakuwa na mvutano wa kudumu ambao hata unaweza kuondoa amani na kuletea kurejewa kwa kupiga kura mara kwa mara utakaohusisha mirengo ya siasa zaidi badala ya uhalisia wa kitaifa.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa J. M. Kikwete kwa uadilifu na upendo mkubwa aliouonyesha kwa kukubali kukutana na Viongozi wa Vyama vya Upinzani na kuweza kujadiliana juu ya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Rais, Mheshimiwa Kikwete kwa kukubali mapendekezo yaliyotolewa na upande wa vyama vya upinzani na hatimaye kuyaingiza katika Muswada huo hatimaye kukubali kusaini marekebisho ya Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wajibu wetu kutii kilichoridhiwa ili kutoa fursa kwa wananchi kuwa tayari kutoa maoni yao, ni namna gani wangependa Katiba iwe na mwekeleo gani, kwa manufaa ya ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Katiba ni mchakato muhimu kwa maendeleo ya nchi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuandikwa kwa Katiba mpya ni fursa muhimu ya kujenga muafaka wa kitaifa na kuweka misingi muhimu ya mustakabali wa Taifa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, kwa nyakati mbalimbali tangu mwaka 2000 mpaka 2010, nimeungana na wadau mbalimbali kwa njia ya amani katika kutaka Katiba mpya. Tarehe 17 Desemba, 2010, Waziri Mkuu – Mheshimiwa Mizengo Pinda alipofanya Mkutano na Wahariri wa Vyombo vya Habari na kueleza kwamba anakusudia kumshauri Rais aunde jopo shirikishi la kuratibu mapitio ya katiba; tarehe 19 Desemba, 2010 nilifanya mkutano na Waandishi wa Habari na kutaka suala muhimu la Katiba kuanzia Bungeni kupitia maazimio na hatimaye sheria maalum ya mabadiliko ya Katiba, na kueleza kusudio la kupeleka hoja binafsi ili Serikali ifuate mkondo husika; na tarehe 27 Desemba, 2010 nilipeleka kwa Katibu wa Bunge taarifa ya hoja husika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Desemba, 2010, Rais Jakaya Kikwete akaliambia Taifa alikubali kuanzisha mchakato wa mapitio ya Katiba lakini akatangaza kusudio la yeye mwenyewe kuunda Tume na hatimaye Katiba iliyofanyiwa mapitio (*review*) kupitishwa na vyombo vya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Januari, 2011, nilitaka bado suala husika kuanzia Bungeni ili Tume iundwe kwa mujibu wa sheria na badala ya vyombo vya kikatiba ambayo kwa Katiba ya mwaka 1977 inayotumika sasa, ni Bunge kwa mujibu wa ibara ya 98. Hivyo nikataka Serikali ipeleke Bungeni sheria maalum ili vyombo vya mchakato wa Katiba viwe ni pamoja na Bunge Maalum la Katiba. Hatimaye tarehe 5 Februari, 2011, Serikali ilitoa kauli ya kukubali kupeleka Bungeni Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama nilivyoeeza tarehe 30 Machi, 2011, Muswada wa Sheria uliochapwa tarehe 11 Machi, 2011 (GN.1VOL.92), kulikuwa na kasoro ambazo zilihitaji wadau kuzishughulikia. Kasoro hizo ziliendelea hata katika Muswada uliopitishwa Bungeni mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Serikali imewasilisha marekebisho kwa Muswada No.8 wa 2011 (23/12/2011 kupitia GN 51 Vol.92) pamoja na jedwali la Serikali la tarehe 23 Januari, 2012. Marekebisho haya ni ya hatua ya kwanza kuhusu ukusanyaji wa maoni na kuandaa rasimu. Bado katika hatua za baadaye kunahitajika kufanyika marekebisho ya hatua ya pili ya Bunge la Katiba na utungaji wa Katiba na hatua ya tatu ya uhalalishaji wa Katiba hususan suala la kura ya maoni kusimamiwa na Tume ya sasa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sehemu kubwa ya mapendekezo yaliyotolewa kwenye jedwali la marekebisho na nashauri msingi uwe ni mapendekezo ya jedwali la marekebisho. Hata hivyo, katika kifungu cha 17 kama kilivyoeezwa kwenye sehemu (b) ya jedwali la marekebisho, ni muhimu kuongeza kwenye kifungu kidogo cha 9(a) na (b); ni muhimu wakaingizwa Watendaji wa Kata kama walivyotajwa kwenye sheria Kifungu cha 17.

Mheshimiwa Spika, pia kifungu cha 21 kama marekebisho yalivyopendekezwa kwenye sehemu C, bado adhabu ziko juu, hivyo, kuna haja ya kutenganisha kati ya makosa ya kijinai na makosa ya kawaida ya wananchi kuhusu elimu juu ya mabadiliko ya Katiba na kukusanya maoni juu ya mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya utekelezaji, kwenye Mkutano wa Saba wa Bunge, Aprili, 2012 Serikali izingatie bajeti na ratiba ya mchakato wa ukusanyaji wa maoni kwenye mwongozo wa bajeti na mpango wa mwaka wa Taifa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa busara yake, hekima na usikivu wake wenye nia njema ya kuendeleza mustakabali wa Taifa letu katika suala zima la amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza, naomba kueleza kipengele cha kumwondoa Mkuu wa Wilaya kutohusika na kuitisha mikutano ya majadiliano ya Katiba mpya hakiwezi kuleta ufanisi wa Mikutano kutokana na Wakuu wa Wilaya kuwa ni nafasi muhimu kutokana na kazi yake, uzoefu katika kusimamia uhuru wa mawazo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo, iondolewe nafasi ya jina la Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya arudie nafasi yake ya kuhusika na kuitisha Mikutano ya Katiba ili kuleta amani ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais pia kukubali kuhusisha wanasiasa katika Kamati ya kupokea maoni ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusaini Muswada wa Sheria ya Tume ya Marekebisho ya Katiba. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kusudi langu ni kuomba kuwa Mkuu wa Wilaya ni budi pia awepo katika Tume hiyo. Katika sheria hiyo, imeonyesha kuwa Mkuu wa Wilaya ametolewa. Kwa nini? Mkuu wa Wilaya awepo katika Tume ili asimamie suala lote la ulinzi na usalama kwa shughuli yote ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya zamani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni lazima isambazwe mapema ili wananchi waweze kwanza kuielewa vizuri ili waweze kuchangia vizuri katika kutoa mawazo ya Katiba mpya itakayokuja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuusaini na kubariki Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Katiba hii tunayoikusudia kuiunda ni mali ya wananchi, tena ni mali ya Watanzania wote. Hivyo basi, hekima iliyotumika na Serikali ya kuamua kuongoza na kupanua wigo kwa Mheshimiwa Rais kuweza kuteua Wajumbe wa Tume kutokana na Vyama vya Siasa, kwa kuzingatia taaluma yake, sifa, uwezo, pamoja na uzoefu kwenye mambo ya msingi, hivyo kutumia utaalamu na uzoefu wao katika kuratibu mchakato mzima wa mabadiliko ya Katiba ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Serikali, kuleta mabadiliko katika kuziruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuitisha mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni juu ya rasimu. Hii itasaidia zaidi kupanua wigo wa majadiliano, na itasaidia zaidi kupata mawazo mazuri ambayo kupitia katika Tume iliyoundwa ndipo itakapowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubaliana na suala zima la utoaji wa elimu baada ya kupata ridhaa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Tanzania Bara na Katibu wa Baraza la Mji kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Serikali lazima ijue kwamba kwa uwezo zaidi fedha za kuendesha hiyo elimu inatoka wapi, kwa maana ya ufadhili, tusije tukaingiza maadui zetu wasiotutakia mema nchi yetu, na nchi ikashindwa kutawalika.

Mheshimiwa Spika, bado naona kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwaacha Wakuu wa Wilaya kuendelea na usimamizi wa mchakato katika maeneo yao, kwani hao ndio wawakilishi wa kweli wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB S. OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza tumpongeze Rais na Serikali kwa jumla kwa kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono mapendekezo hayo. Mapendekezo haya yamesaidia sana kuleta maelewano baina ya vyama na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, nami nakubali kuwa kifungu nambari 17(c) Mkuu wa Wilaya aendelee badala ya Mkurugenzi. Sababu kubwa ni kwamba Mkuu wa Wilaya ndiye mwenye mamlaka makubwa zaidi katika Wilaya na yeye pia ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama katika Wilaya. Hivyo, ni dhahiri kuwa yeye ndiye anayefaa kukabidhiwa kazi hii.

Mheshimiwa Spika, sina pingamizi na mapendekezo ya mabadiliko yaliyobakia.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwapokea viongozi wa vyama na kuwasikiliza. Kweli Serikali yetu ni sikivu. Nampongeza pia Mwanasheria Mkuu kwa uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yamepanua wigo wa washiriki kwa kuwahusisha viongozi wa vyama, viongozi wa dini na wa asasi. Hii, itawafanya kuona kabisa kwamba wao pia ni sehemu ya mchakato mzima wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mapendekezo ya wengi wa Wabunge kuwa Ma-DC na sio Wakurugenzi ndio wahusishwe na mchakato wa Katiba.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Muswada huu, ila naomba kutoa marekebisho ya kuboresha Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na kifungu namba (6) kuingiza wanasiasa ili kuifanya Tume hiyo iwe na uhai kabisa na kuondosha kelele ya vyama kutengwa katika Tume, lakini Mbunge na Wawakilishi wawemo kama sifa wanayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu Namba 17, katika kuboreshwa zaidi, bora Mkuu wa Wilaya kuendelea kusimamia mchakato na kusimamia Wilaya zao katika mchakato na Mikutano ya Mabaraza katika sehemu ya nyakati mbalimbali kama itakavyoamuliwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mikutano ya Tume na wananchi lazima kuangalia Kijiji fulani kipo wapi ili kuondoa malumbano ya jamii. Lazima kuwe na kifungu kinachoeleza kwamba wanaokwenda kupokea maoni ya wananchi, lazima kuwe na mipaka ya viongozi kutopewa nafasi ya kwenda sehemu moja kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha adhabu ni sahihi kwamba tunafuata sheria za nchi. Sina pingamizi, kifungu hicho kipite.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, napongeza na kuunga mkono marekebisho ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na kuunga mkono, nafurahi kuwa wadau wote waliotoa maoni wamemtambua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kumpa mamlaka zaidi tofauti na ule Muswada wa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna kifungu (6) sehemu ya III - Uundaji wa Tume 6 (6). "Rais ataalika Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu, Jumuiya za Kidini, Asasi na kadhalika kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume".

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Isipokuwa 6(7) ninakipinga kuwa Rais atazingatia umoja unaosimamia jumuiya au asasi hizo.

Swali: umoja huu uko wapi? Maana umoja mwingine hauko registered kwa Registrar of Political Parties. Mfano Babu wa Loliondo ni Mchungaji, yeye ni Kanisa gani? Umoja upi? Lakini tukisema Rais atazingatia umoja unaosimamia Jumuiya au asasi hizo, zipo taasisi njema ambazo hazipo kwenye umoja huo.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu 12 kwa kuongeza kifungu, endapo suala la kumwondoa Mjumbe kwa kukiuka kanuni za maadili litajitokeza, Rais atateua Kamati.

Mheshimiwa Spika, ushauri, wangu ni kwamba, Rais ataunda Kamati na siyo atateua Kamati, aidha ushauri huu. Taasisi inayotaka kutoa maoni, itoe taarifa. Naomba taarifa hiyo iwe na *time, duration place and venue* na majibu ya taarifa. Aidha, taasisi inayotoa maoni lazima iwe na sifa, ridhaa baada ya taarifa ni muhimu. Mfano mtu anataka kukusanya maoni au taasisi lakini sio Mtanzania.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Serikali ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali hasa Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete kwa kuleta Bungeni marekebisho haya yenye nia ya kuhakikisha mchakato huu mkubwa na muhimu kwa nchi yetu unafanyika kwa amani, utulivu na kuwashirikisha wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja kwa kifungu cha 18 (6) ni kwamba, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali yenye nia ya kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wao kutoa maoni yao juu ya rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni yao kwa Tume.

Mheshimiwa Spika, nashauri Kanuni zitungwe kwa ajili ya kutoa mwongozo wa jinsi ya asasi, taasisi na mashirika zitakavyoweza kutoa elimu na kukusanya maoni. Ni vizuri Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba Mpya ikatoa mwongozo ambao utatumiwa na Taasisi hizi katika kukusanya maoni kama pale ambavyo Tume ya Uchaguzi (NEC) inavyotoa mwongozo kwa taasisi jinsi ya kutoa elimu ya uraia wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza wakati wa utekelezaji wa sheria hii Serikali iagize/ishauri wafadhili na wadau wa maendeleo kuratibu misaada/pesa zao zitakazotolewa kwa ajili ya kusaidia elimu kwa umma na ukusanyaji maoni utakaofanywa na taasisi, mashirika yasiyo ya kiserikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali na hasa Mheshimiwa Rais kwa hekima na busara na mapenzi aliyoonesha kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya marekebisho yanayopendekezwa na Serikali, kwamba Mheshimiwa Rais atapokea orodha ya majina kutoka makundi mbalimbali ili miongoni mwake ateuwe wajumbe wa Tume ya kukusanya maoni, kuchambua na kuratibu, nashauri Rais wetu awe huru kufanya uamuzi unaofaa. Yawezekana majina yote atakayopelekewa yakawa hayafai.

Mheshimiwa Spika, sehemu B ibara ya 3(17)(a) kuhusu kufuta Wakuu wa Wilaya kuwa wasimamizi wa kuratibu zoezi la kukusanya maoni. Nashauri Wakuu wa Wilaya ambao ndiyo Wenyevidi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama katika maeneo yao ya utawala wapewe dhamana hiyo. Wakuu wa Wilaya iwapo wataondolewa hili litakuwa ni kosa kubwa sana hasa kwa vile wananchi wanahitaji utulivu wakati wa kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, niunge mkono pia pendekezo la kuruhusu taasisi mbalimbali kutoa elimu juu ya masuala ya Katiba hapa nchini. Ni kweli watu wetu wengi hawaiielewi Katiba yetu. Elimu ya Katiba ni muhimu. Hata hivyo nashauri kwamba nakala za kutosha za Katiba ya sasa zichapishwe na kusambazwa nchi nzima. Elimu ya Katiba ya sasa ya kusaidia wananchi kuisoma haitafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono pendekezo la kura ya maoni ili kufikia maamuzi na kuwa na Katiba mpya. Hata hivyo, naiomba Serikali isikubaliane na pendekezo la Chama cha Wananchi (CUF) kwamba maamuzi lazima yawe ni theluthi mbili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, marekebisho yaliyoletwa yana maana kwa lengo la kuboresha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba pale ambapo inapendekezwa DC aondolewe tumweke Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya/Mji/Jiji, siungi mkono. Suala la Katiba ni suala la kisiasa zaidi kuliko ilivyo suala la kisheria. Ndio maana inatungwa na watu wote, sheria nyingine hutungwa na Bunge (na Rais) tu. Katiba hutungwa na watu wote kwa sababu hii, kumtoa DC na kumweka Mkurugenzi si sawa. Mkurugenzi hausiki na siasa. Siasa tumwachie mtu mwingine, naye ni DC. Huyu tangu hapo, kazi yake ya asili ni kuratibu ustawi wa watu katika Wilaya. Ni kusimamia jinsi ambavyo mambo yanakwenda kwa ujumla katika Wilaya yake, ana utaratibu huu tayari, ana uwezo, ana vyombo (usalama, polisi, na kadhalika), ambavyo Mkurugenzi hana. Tumwache DC afanye kazi hii na sio Mkurugenzi.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni yangu juu ya Muswada tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, nakishukuru Chama changu cha CHADEMA kwa juhudi kubwa walizofanya tangu Muswada huu ulipoletwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni, pale

tulipobainisha upungufu uliokuwepo katika Muswada huo ambao hata hivyo ulipitishwa na Bunge ambao baadaye ulisainiwa na Rais kuwa sheria. CHADEMA waliamua kumwona Mheshimiwa Rais kufanya majadiliano naye ambayo yameleta mabadiliko haya ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebisho katika kifungu cha 6(5)(a) ili kuruhusu wananchi ambao si wanasiasa, wananchi kutoka makundi mbalimbali ya jamii isipokuwa Wabunge na Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi kuwa Wajumbe katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuunga mkono marekebisho yanayomruhusu Mheshimiwa Rais kuadika Vyama Vya Siasa, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa wajumbe. Hii itatoa wigo mpana na uwakilishi mpana wa wananchi katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebisho yanayomwondoa Mkuu wa Wilaya katika kusimamia mchakato wa kusimamia ukusanyaji wa maoni ya wananchi katika kutunga Katiba mpya. Tunajua wote kuwa Wakuu wa Wilaya ni makada mahsusi wa Chama cha Mapinduzi na hivyo wanaweza wasiyatendee haki makundi mengine yanayoleta maoni yao juu ya Katiba mpya kwa kuegemea upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya kifungu 21(8) ili kupunguza adhabu kwa watu watakaokiuka masharti ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya 2011.

Mheshimiwa Spika, adhabu iliyokuwepo kwanza ya faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au kifungu kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka saba iliyokuwepo ilikuwa kubwa sana na isiyoundana na uzito wa kosa lenyewe ukilinganisha na sheria zingine na adhabu zilizopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naunga mkono mapendekezo yote ya marekebisho ya sheria hii kama yalivyolekwa na Serikali kwani sheria hii ilisainiwa ikiwa na upungufu mwingi sana ambao ulipitishwa na Wabunge wa CCM bila kujali upungufu huo na maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kupanua ushiriki wa wadau mbalimbali katika Muswada wa Katiba Mpya na hasa kurudisha Bungeni kuufanyia marekebisho. Naamini nia ni kufanya zoezi hili lililikiwe zaidi na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya katika Wilaya ni mwakilishi wa Rais, kwa msingi huo kumwondoa ni kuleta udhaifu mkubwa sana. Mkuu wa Wilaya anawajibika kuhakikisha zoezi zima linakwenda kwa amani hadi kukamilika kwake. Kwa hiyo, ni muhimu abakie kama mtekelezaji muhimu katika jukwaa kwa kuhakikisha tunapata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kuwahusisha wanasiasa na taasisi za kiraia. Naunga mkono hoja hiyo kwa vile inaongeza upana wa wahusika katika mchakato mzima na hatimaye tutapata Katiba yenye mshiko, Katiba ambayo itakuwa uzao wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweka historia ya kuwa na marekebisho ya Katiba ya nchi yetu tukiwa katika kusherehekea miaka 50 ya Uhuru wetu. Pia nampongeza kwa kuhakikisha ameshirikisha jamii katika ngazi mbalimbali kwenye kupokea mapendekezo yao wakiwemo Viongozi wa Dini, Vyama mbalimbali vya Siasa na Asasi Zisizo za Kiserikali. Marekebisho yanayohusu Mkuu wa Wilaya, nashauri kifungu cha Mkuu wa Wilaya kuwa msimamizi wa dola kiwepo kwani wao ndio wasimamizi wetu katika masuala mbalimbali ya kisiasa kwa maeneo husika. Kwani kama

hoja au wasiwasi nani atasimamia uchaguzi liko wazi sana. Hivyo Mkuu wa Wilaya ana nafasi yake pia.

Mheshimiwa Spika, Tume itakapoundwa na kupita kukusanya maoni ni vyema nakala za Muswada huu wa Sheria ziwe zimesambazwa na kuwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali ili waweze kutoa maoni yao kutokana na yaliyoandikwa kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, mengi yameshasemwa. Natoa pongezi nyingi kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa kwa kukubali kusikiliza makundi yote yaliyopeleka marekebisho ya Sheria ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kuwa Wakuu wa Wilaya wawepo, wasiwekwe pembeni, badala yake Wakurugenzi wasiwepo. Kwani Wakuu wa Wilaya ndio makamanda na wasimamizi wa kila kitu Wilayani.

Mheshimiwa Spika, naomba Tanzania ni moja na Katiba ni ya Watanzania. Kwa moyo mkunjufu naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja na kupendekeza yafuatayo:-

Tume ya Mabadiliko ya Katiba itakayoundwa kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba Mpya, ifanye kila linalowezekana kuwafikia Watanzania wote popote waliko ikiwa ni pamoja na jamii ya wafugaji ambao kwa mfumo wa nchi ulivyo maeneo yao yamekuwa yakitwaliwa na Serikali na kupewa wawekezaji au kufanya mashamba ya wanyamapori na wao wenyewe kulazimika kuhamahama kutafuta maeneo ya malisho kwa mifugo yao na hivyo kuwa vigumu kuwafikia katika mazingira yao magumu na yasiyokuwa na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, pili, napendekeza maneno Mkuu wa Wilaya katika kifungu cha 17(5)(a) yabaki kama ilivyokuwa mwanzo kwa hoja kuwa DC ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilayani, Mkuu wa Serikali (dola) na mwakilishi wa Rais Wilayani.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kuwa Wabunge na Wawakilishi ni wanasiasa kama wengine hakuna mantiki kuwanyima fursa ya kupendekezwa au kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume.

Pili, isemwe wazi kwamba Rais hawajibiki kuwateua waliopendekezwa na Vyama vya Siasa au Asasi za kijamii. La sivyo kutakuwa na malalamiko mengi kutoka taasisi hizi pale ambako waliyempendekeza hatateuliwa na Mheshimiwa Rais. Hili liongezwe kwenye *subsection (5)* au baada yake kadiri AG atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa hekima na busara kubwa aliyonayo ya kuwaunganisha Watanzania wote kupitia Vyama vya Siasa, Asasi mbalimbali na makundi mbalimbali ya kijamii ili kutoa maoni yao ya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa mvumilivu, msikivu na makini kusikiliza hoja mbalimbali za wananchi na kulijenga Taifa moja lenye mshikamano thabiti. Naunga mkono hoja ya Serikali ya kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ili kuboresha Sheria ya kuunda Tume ya kukusanya Maoni.

Mheshimiwa Spika, dhana ya wanasiasa kuwemo ndani ya Tume ni tendo la busara kwa sababu maoni mbalimbali yatazingatiwa ili kuunda Katiba imara inayowaunganisha Watanzania wote wenye itikadi mbalimbali na kutoka Jumuiya mbalimbali za Jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Muswada huo kwa kuunga mkono kwa mapendekezo yaliyoletwa na Serikali kwa sababu yamezingatia kupunguza mvutano wa kimitazamo wa vyama na hatimaye kuleta utulivu wa kisiasa katika jamii ya Watanzania. Ni muhimu sana wakati nchi inatengeneza Katiba mpya, ni vema hali ya amani ikazingatia kuwa, kuandika Katiba isiwe ndiyo kusingizio cha kufanya vurugu.

Hata hivyo, naomba mahali ambapo Mkurugenzi wa Maendeleo anatakiwa asimamie, sasa iendeleo kuwa DC kama ilivyokuwa imekusudiwa awali. Hii ni kwa sababu ya mgawanyo wa majukumu kwani suala la ulinzi na usalama lipo chini ya Mkuu wa Wilaya. Kimsingi pia Mkuu wa Wilaya ndiyo mwakilishi wa Rais ambaye ndiye mwenye dhamana ya kuhakikisha ulinzi na usalama wa eneo lake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ukweli jambo hili la marekebisho au ya mabadiliko ya Katiba yetu, katika hatua hii ya hivi sasa, inaonesha dhahiri kwamba, kuna mwelekeo mzuri katika kufikia mafanikio mema na hasa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Rais kwa busara sana amefanya kukubali kuwa msikivu na mwenye busara ya kusikiliza na kupokea maoni ya wadau mbalimbali jambo ambalo hupelekea hata wale ambao tulikuwa tukiangaliana kiundani, leo baada ya kusomwa marekebisho yenyewe na upande wa Serikali, Kamati ya Katiba na hata Kambi ya Upinzani wote kwa pamoja wameonesha kuridhika na kukubaliana na marekebisho au mapendekezo ya marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nami naomba kutamka kwamba nakubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yalivyoletwa. Tusipozingatia na kutafakari kwa busara ya kujali na kuzingatia Utaifa zaidi na tukajadili kwa kuongozwa na hisia za kiitikadi na mitazamo ya vyama vyetu, jambo hili jema tunaweza tukalipeleka Taifa hili mahali pabaya sana. Nashauri kwamba, tujadili na huku tukiangalia Kenya kama vile ipo mbele ya macho yetu, lakini tuiangalie kwa yale yaliyotokea kwa jambo kama hili tunalojijadili leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo ambayo yamepelekea Bunge hili katika kila upande kuungana na mapendekezo ya Serikali ni pamoja na kuondolewa Mkuu wa Wilaya kama vile kifungu cha 17(5)(a) ambacho kilikuwa kinaeleza hapo awali na kwamba sasa kinatamka neno Mkurugenzi badala ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hata mijadala hii inaonesha wazi kwamba, mivutano na mjadala mkubwa na sura ya kutofautiana baina ya wachangiaji hapa ni kifungu hicho cha 17 nilichokizungumzia.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kusema wazi na kwa kinywa kipana kabisa kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kama yalivyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja Muswada huu wa Sheria ili kuwezesha mchakato wa kumwezesha Mheshimiwa Rais aweze kuunda Tume itakayofanya kazi muhimu ya kukusanya maoni ya Watanzania juu ya kuundwa kwa Katiba mpya ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kujivunia kuona kwamba Bunge letu kwa sasa linakuwa kitu kimoja, Wabunge wakiwa wameungana kwa pamoja bila kujali itikadi za kivyama. Nia ya



kuundwa kwa Katiba mpya ni jambo ambalo litawajumuisha Watanzania kwa ujumla bila kujali rangi, kabila, ukanda au itikadi za vyama wala dini.

Katiba ni Sheria Mama ya nchi ambamo Sheria zingine zote zitatungwa kwa mujibu wa Katiba yetu. Kuingizwa kwa makundi mbalimbali ya kijamii ikiwemo wadau wa Vyama vya Siasa, makundi ya dini na kwa maana hiyo ni wazi kwamba, ushirikishwaji wa Watanzania walio wengi kuhakikisha kwamba yanapatikana maoni ya walio wengi. Uundwaji wa Katiba katika Mataifa mengi duniani zimetumbukia katika machafuko kutokana na kushindwa kuwa na uelewano.

Mabadiliko yaliyoletwa na Serikali ni kuwa na Tume ya kukusanya maoni itakayoleta umoja wa Kitaifa. Kinachotakiwa kufanyika hivi sasa ni kuhakikisha Watanzania walio wengi wapewe elimu ya uraia ili michango itakayotolewa wakati wa mchakato wa kupata maoni iwe ni yenye kuwezesha zoezi la kupata Katiba mpya yenye kulinda maslahi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TAUHIDA C.G. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja. Hata hivyo, napenda kuchangia kifungu cha asasi au kikundi chenye maslahi yanayofanana kuendesha programu za mafunzo. Kwa maoni yangu lazima Sheria itoe ufafanuzi zaidi kwani kifungu hiki kinaweza kuleta mgongano na Sheria nyingine za kuendesha mikutano ya hadhara.

Vile vile uamuzi wa kuwaondoa Wakuu wa Wilaya katika usimamizi wa zoezi hili na shauri utazamwe upya. Sababu ni kwamba, Wakuu wa Wilaya wao ndio wawakilishi wa Rais katika Wilaya zao na hivyo kuwaweka kuwa wasimamizi wa shughuli zote za Serikali katika Wilaya zao. Vile vile kwa upande wa Zanzibar suala la Mkurugenzi Mtendaji kuwa Mjumbe wa Bunge la Katiba haipo sawa kwani Bara na Zanzibar ni tofauti kiuwajibikaji na muundo wake wa Serikali. Kifungu cha kuzingatia na kwa kukumbushia ushirikishaji kwa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina bahati kwamba inakwenda kuandika Katiba yake ikiwa na utulivu bila ya kusubiri kusukumwa na nguvu za kutoka nje ya nchi. Ni uamuzi ambao kama nchi tumeufanya na tunastahili kupongezwa na wale wote wanaotutakia mema kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kifungu kinachonipa mashaka ni pale kifungu kinachotaka kuondolewa kwa Wakuu wa Wilaya katika kuitisha mikutano na badala yake kazi hiyo eti ifanywe na Mkurugenzi. Katika hali ya kawaida na mazoweya wenye kuitisha mikutano ni Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ninayopenda kuchangia ni juu ya kupiga marufuku suala la wanasiasa kutokuwepo katika Tume jambo ambalo kama Taifa lingetunyima fursa ya kutumia wale wanasiasa wenye ujuzi mkubwa na mchango wao ni wa muhimu katika uandikaji na ukusanyaji wa maoni.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunijalia kuwa mmoja wa waliojaliwa kupata nafasi ya kujadili na kuchangia mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusikiliza kilio cha Watanzania na kuleta marekebishi ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebishi yaliyoletwa na Serikali na naamini huu utakuwa sio mwisho na naomba Serikali izidi kuleta marekebishi mara inapotakiwa kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza uwepo wa Mkurugenzi Mtendaji Miji na Halmashauri kama alivyotajwa kwenye kifungu cha 17(c), Mkurugenzi atatumia watendaji wa Kata na Vijiji katika kukusanya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba kwa kuleta Muswada huu Bungeni kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutumia hekima na busara kukubali mabadiliko haya yaje hapa Bungeni. Hii ni ishara tosha kuwa Rais wetu anadamisha utawala bora.

Muswada huu unalenga kupanua wigo wa wajumbe wa Tume kwa kuruhusu wanasiasa kuwa wajumbe wa Tume ya kukusanya maoni ya wananchi isipokuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nashauri Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapewe nafasi ya kuingia kwenye Tume kwani nao kwa mujibu wa kazi zao ni wanasiasa. Pia Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamo wenye uwezo mkubwa wa kitaaluma katika masuala ya Katiba. Mfano tunao Waheshimiwa Wabunge wengi waliobobea katika masuala ya sheria. Tunaye Mheshimiwa Halima Mdee, Tundu Lissu, George Simbachawene, Andrew Chenge, Felix Mkosamali, Angellah Kairuki, Gosbert Blandes na wengineo.

Kuhusu kumwondoa Mkuu wa Wilaya na kumuingiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya siyo sahihi. Kiutawala Mkuu wa Wilaya ndiye Mtawala wa Wilaya. Pia ndiye mkuu wa ulinzi na usalama wa Wilaya na anavyo vyombo vya kuwasiliana navyo katika kuandaa ratiba ya Tume. Mfano, anao Makatibu Tarafa, Watendaji Kata na kadhalika, masuala ya itikadi za vyama hayana nafasi hata kama Mkuu wa Wilaya ni kada wa Chama cha Mapinduzi bado Katiba inamtambua kama Kiongozi Mwakilishi wa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Adhabu zinazorekebishwa naziunga mkono kwani adhabu zilizoko kwenye sheria ni kubwa mno na zinapingana na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ikiwa imebeba marekebisho mbalimbali kwa mfano, suala la nafasi ya Mkuu wa Wilaya ni muhimu awepo haliepukiki. Yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Naunga mkono na naomba maamuzi ya sheria iliyosomwa mwanzo yabakie.

Kwa nafasi iliyowekewa Mkurugenzi wa Halmashauri ibadilishwe 17(a, b, c, *et cetera*) awepo Mkuu wa Wilaya ni mfano wa nchi.

Nakubaliana kwa msingi kabisa naomba viongozi wa siasa wawepo katika Tume. Ni muhimu tuongozwe na dhana ya suala la Katiba kuwa ni suala la *social or political process*, sio la kisheria tu. Naunga mkono hayo marekebisho ya kuingiza wanasiasa katika Tume kwa kutambua pia tayari Rais ameshawekewa vigezo mbalimbali, ni wanasiasa wenye sifa zipi tusimfunge Rais mikono.

Nashukuru pia muono uliojitokeza kuona nafasi ya juu ya Rais kama kielelezo na muafaka wa Taifa letu hili. Muswada umetusaidia kutambua nafasi au *powers* za Rais. Suala la Rais kuunda Tume limekubalika vizuri.

Lakini pia kutambua nafasi ya Wabunge kama wawakilishi halali wa wananchi wa Tanzania kwa kusimamia na kukubali kubadilisha Bunge lililopo kuwa Bunge la Katiba, pamoja na wengine watakaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninayo furaha kwa kupata nafasi hii kuchangia Muswada huu wa Marekebisho. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwasikiliza wadau na kutuletea marekebisho haya.

Yafuatayo ni maoni yangu kuhusu marekebisho haya:-

Kifungu B 3(c) kifungu cha 17, nashauri katika kifungu hiki Mkuu wa Wilaya arudishwe baada ya uwepo wa Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nashauri hili kwa sababu zifuatazo:-

- (i) Mkuu wa Wilaya ni Mwakilishi wa Rais katika Wilaya.
- (ii) Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya yake.
- (iii) Mkurugenzi ni mjumbe tu wa Kamati wa Ulinzi na Usalama ya Wilaya.
- (iv) Mwenyekiti wa Wilaya ndiye mshauri na msimamizi wa shughuli za Serikali katika Wilaya yake.

Hivyo ni vyema Mkuu wa Wilaya asikilizwe hofu inayoelezwa na baadhi ya wachangiaji kuwa Mkuu wa Wilaya ametajwa katika Katiba ya CCM, hilo halina msingi wowote na hiyo ni kufananishwa suala la Katiba na itikadi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kukubali kuwaruhusu viongozi wa kisiasa, vyama na taasisi mbalimbali kuandaa mikutano yenye nia njema ya kukusanya maoni ya mabadiliko ya Katiba.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Watendaji wake, kwa kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sana Serikali imeona umuhimu wa kurekebisha yale ambayo Wabunge wengi tuliyasemea mwezi wa Oktoba 2011, lakini hayakusikilizwa. Nampongeza Rais, kwa kukubali kupokea mapendekezo ya Vyama vya Siasa na Wadau mbalimbali na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 17, Sheria inatamka kuwatumia Wakuu wa Wilaya kuendesha mikutano na kukusanya maoni ya Wananchi. Sikubaliani na hoja ya Wakuu wa Wilaya, hawa ni wateule wa Rais na ni wanasiasa kwa asilimia zote. Kwa kuwa ni wateule wa Rais, basi ni lazima watumikie bosi aliyewateua.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri watumiwe kuitisha na kuendesha mikutano hiyo. Watendaji watumike kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa na hata Wilaya.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona leo hii Wabunge wa Vyama vyote vya Siasa tumekaa kujadili mabadiliko haya. Nampongeza sana Rais, kwa kuyakubali maoni ya Viongozi wa Vyama vya Siasa ambao walikwenda kwake kutoa maoni yao na akayapokea na leo hii kayaleta hapa ili tuyajadili kwa pamoja. Ni dhahiri kuwa, Rais wetu ana uadilifu mzuri katika uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana mia kwa mia na marekebisho haya kwamba, Mkuu wa Wilaya asiwe Mjumbe wa Tume hii.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais, kwa busara za hali ya juu alizozitumia kwa kukubali kusikiliza maoni ya taasisi mbalimbali na kuuona umuhimu wa kuleta mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8

Mheshimiwa Spika, nami naomba nianze kutoa pendekezo kwa kuanzia Kifungu cha 17. Ukisoma kifungu hiki, sioni haja ya kifungu hiki kumtoa Mkuu wa Wilaya na kumuweka Mkurugenzi katika kipengele hicho. Kwanza kabisa, ieleweke kuwa Mkuu wa Wilaya Kikatiba ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na hata Mkurugenzi yupo chini ya Mkuu wa Wilaya na sioni mantiki ya kusema kuwa Mkurugenzi ni Kiongozi wa Kisiasa. Hakuna sababu kama ni hivyo hata Rais pia ni Kiongozi wa Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umempa fursa Rais kukaribisha Taasisi mbalimbali na Vyama vya Siasa kupeleka orodha ya majina ya watu wanaopendekezwa ili ateue kuwa Wajumbe wa Tume. Nimeshukuru kuona kuwa atateua Wajumbe nje ya orodha iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho unalenga Kupanua wigo wa Tume ya Kukusanya Maoni kwa kuwaongeza Viongozi wa Vyama vya Siasa isipokuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nakubali Viongozi wa Siasa kuwepo kwenye Tume lakini sikubali kuwabagua Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwani nao ni Wanasiasa wateuliwe katika Tume.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wabunge, kwa kupitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011. Nampongeza Rais, kwa kukubali kusaini Sheria hiyo tayari kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuipitia Sheria hiyo na kuona ipo tena haja ya kufanya mabadiliko ya Sheria hiyo kwa lengo la kuifanya itekelezwe kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa sababu Muswada huu endapo utapitishwa kuwa Sheria, utasaidia mchakato wa kupata Katiba Mpya uwe wenye ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba kutoa ushauri kidogo kama ifuatavyo:-

(1) Kifungu cha (7) kiongezwe isipokuwa kisimpe masharti Rais. Maneno yanayosomeka Rais atazingatia umoja unaosimamia Jumuiya au Asasi hizo, kwa sababu Kifungu cha (6) kinajitosheleza katika ukurasa wa saba.

(a) Kufuta neno Mkuu wa Wilaya katika aya ya (g), kifungu cha 5 na badala yake maneno "Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa."

(b) Kufuta maneno "Mkuu wa Wilaya" yanayoonekana katika aya ya B ya kifungu cha (5) na badala yake "Mkurugenzi wa Manispaa," mimi suingi mkono. Nashauri kifungu hicho kibaki kama kilivyo kwenye Sheria na neno "Mkuu wa Wilaya" liendelee kusomeka katika kila eneo linalotaja Mkurugenzi.

(c) Ukurasa wa nane Kifungu cha (10), makundi ya kukusanya maoni na kuyawasilisha kwa Tume kiondolewe na kazi ya kukusanya maoni tuiachie Tume, Kifungu hicho kiondolewe.

(d) Sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuelekea kwenye usawa wa kijinsia katika vyombo vyote vya maamuzi. Tayari Bunge na Serikali za Mitaa zimefikia asilimia 30 ya uwakilishi wa wanawake katika kutimiza lengo la usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Spika, napendekeza sheria ifanyiwe marekebisho katika Kifungu cha 6(3)(c) kwa kukiandika kwa uwazi zaidi kuonesha kwamba, kutakuwa na uwakilishi utakaozingatia uwiano wa kijinsia katika Tume - Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Viongozi wa Vyama vya Siasa, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kitaifa, Taasisi zisizo za Kiserikali, wakati wa kupeleka orodha wasisahau wanawake.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitangulize pongezi za kipekee kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuridhia kukutana na wadau mbalimbali ikiwemo Vyama vya Siasa na kujadili mapendekezo mbalimbali yenye kuleta Mwafaka wa Kitaifa katika suala muhimu hili la kufanyia marekebisho Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono marekebisho yote yaliyoletwa na Serikali. Hata hivyo, naomba nijielekeze kwenye Kifungu cha 12 juu ya Kamati itakayoundwa na Rais, endapo suala la kumwondoa Mjumbe kwa kukiuka Kanuni za Maadili. Kwa kifungu hiki, naomba nipendekeze kuwa kiongezwe kifungu cha kuipa Kamati itakayoundwa na Rais, muda maalum wa kufanyia uchunguzi suala lolote litakaloletwa mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 6(i), napendekeza Mbunge na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wawe pia miongoni mwa wanaostahili kuteuliwa katika Tume ya Kukusanya Maoni.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yote yaliyofanywa nayaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 17(5), amefutwa DC na kuwekwa Mkurugenzi. Mimi binafsi, napinga kwa kuwa DC ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. DC ni Taasisi siyo mtu. DC ni Mwakilishi wa Rais, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM na amekuwa na demokrasia pana. Naamini DCs hawa ndiyo wanatunza amani yetu na utulivu uliopo miaka yote.

Naomna DCs waendeleo kuwa na mamlaka ya kuitisha mikutano ya Wananchi kwa ajili ya kutoa maoni uzizingatia Mkurugenzi ana kazi nyingi za kufanya; hivi atasimamia mamilioni ya Serikali muda gani na muda gani afanye kazi ya Katiba? Mkurugenzi ni binadamu wa kawaida, yeye hana chama chochote mbona anapiga kura?

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, tutawajazia kazi hawa watu na tutashindwa kuwahibiti watajibu majukumu ni mengi. Mfumo pia Serikali Kuu na za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa busara zake za hali ya juu, kwa kuanzisha suala zima la Katiba Mpya ya Tanzania. Hayo yanatokana na Viongozi wachache Duniani ambao wanaweza kukubali mawazo ya Wananchi wake wote, kuchagua kutoa mawazo ya Katiba yao.

Kwanza, bila ubishi lazima tukubali Katiba ndiyo uti wa mgongo katika Taifa lolote Duniani na pili Rais wetu amewafunda wenzetu kuwa suluhisho lolote haliji kwa maandamano au kupinga. Tatizo lolote hutatuliwa kwa kukaa mezani na kusikilizana. Nashukuru upepo ule umepita, sasa tuungane tujenge nchi yetu na kutoa tofauti zetu ili tupate Katiba mwafaka.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache tu ya kuzungumzia hasa kuhusu Wakuu wa Wilaya. Mimi naungana na wasemaji waliopita kuwa, Wakurugenzi wa Wilaya wasiteuliwe kama wasimamizi badala yake Wakuu wa Wilaya ndiyo wachukue nafasi hizo kwa sababu Wakuu wa Wilaya ndiyo Marais wa Wilaya zao nao wanamwakilisha moja kwa moja Rais wa Jamhuri. Hawa Wakurugenzi ni watu wa mashaka, wanaweza kuhujumu mchakato mzima wa kutafuta Katiba;

kwanza, wao ndiyo wanahusika sana na ulaji au upotevu wa pesa za Halmashauri kwa hiyo wakae mbali ni rahisi kurubuniwa.

Jambo lingine, wanaomba ruhusa ya kutaka kuongelea na kuwapa elimu Wananchi. Lazima tuwe makini nao tusije tukawapa ruhusa watu ambao kazi yao kubwa kukipigia debe chama fulani. Hao watu lazima wawe na wasimamizi.

Yangu ni hayo tu, mengi yameongelewa na wachangiaji wenzangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, aliyewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani vizuri sana na kukubali kuunga mkono hoja. Aidha, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (Rais), kwa kukubali kuonana na vyama vyote au asasi zilizoomba kuonana nae na kujadili kiundani kabisa kuhusu Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kuzungumzia mabadiliko ya kifungu cha 17(5)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na badala yake kuweka maneno “Mkurugenzi” wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hii ni kutokana na tabia za ajabu ajabu zinayofanywa na hawa Wakuu wa Wilaya katika utendaji wao wa kazi huko katika makazi au sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Spika, Wajuu wa Wilaya katika nchi hii huwa wanafanya kazi kisiasa zaidi na kufuata maelekezo kutoka Chama Tawala na mfano mzuri juu ya hili ni Wakuu hawa wa Wilaya wanatambulika kama Wajumbe wa Vikao vyote Vikuu vya CCM katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Katiba hii ni kwa ajili ya Watanzania wote bila kujali itikadi za vyama tofauti na hivyo naomba Muswada huu upitishwe kama ulivyoletwa na Serikali. Napenda kukubaliana na Marekebisha ya Serikali ya Muswada wa Sheria hii ya Mabadiliko ya kuongeza kifungu kidogo cha (6) katika kifungu cha 18. Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume inaweza kumruhusu Taasisi au Asasi au Makundi mbalimbali, kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa maoni kuhusiana na Katiba kisha kuwasilisha maoni yao kwenye Tume. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, kutokana na ukubwa wa nchi yetu na wingi wa watu wake, haitawezekana kila Mwananchi kukutana na Tume na kuweza kuwasilisha maoni yake. Vilevile hili liendane sambamba na kuwepo na haki na uhuru wa kufanya mikutano kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Katiba yetu na wa maoni kwa mujibu wa Ibara ya 18.

Mheshimiwa Spika, naungana na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika kuyaunga mkono mapendekezo ya marekebisha ya Serikali katika Sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa usikivu wake na hivyo kuwarejesha Watanzania pamoja katika kujadili Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kwa kupata maoni zaidi kutoka kwenye mbari zote za Watanzania. Muswada uliopo mbele yetu umetanua michango ambayo imepatikana na maoni ya kuboresha Muswada kama ulivyopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Marekebisha yaliyopendekezwa na Serikali, yatasaidia kuiboresha Sheria hii. Naunga mkono ushirikishwaji wa Vyama vya Upinzani na hasa maoni yaliyotokana na mazungumzo yaliyofanyika chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wimbo wa Taifa huanza na Mungu na kwa kuwa Dua ya Kuliombea Bunge huanza na Mungu; naomba pendekezo langu

katika dodoso la hoja za kutolewa maoni ya Katiba Mpya Mungu awekwe kwanza. Kama Taifa halina dini sawa lakini lazima limtambue Mungu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono marekebisho haya ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, nafasi ya Mkuu wa Wilaya, ibaki kama ilivyo na Mkurugenzi aondolewe katika Kifungu cha 17. Pamoja na kwamba, Wakuu wa Wilaya wana upungufu wao, lakini bado uwepo wa Mkuu wa Wilaya unahitajika.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 12(4) cha Jwedwali la Marekebisho, hatuoni kwamba Wajumbe wa Tume itakayoteuliwa na Rais, kwa asilimia kubwa watatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano kutokana na nyadhifa zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya marekebisho.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kusisitiza kuwa, pendekezo la kuweka Wakurugenzi ni la msingi katika zoezi hili la mchakato wa Katiba Mpya. Nasema hivyo kwa sababu Wakurugenzi ndiyo Watendaji na wana uelewa wa utendaji na siyo rahisi kuegemea chama chochote cha siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia busara za Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, naamini alitumia busara hata akaafiki uamuzi huu wa busara. Nadhani ni busara tuungane na Mheshimiwa Rais na tuunge mkono mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuridhia tufanye marejeo kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Pia nawapongeza wenzetu wa Kambi ya Upinzani, kwa kutambua nafasi yao na matumizi bora ya nafasi tunazopewa na Wananchi ili kuwawakilisha na hivyo badala ya kususa Vikao ni vyema kutumia nafasi hizo vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunazidi mno kujiangalia kwa hofu ya itikadi zetu badala ya kusimama katika umoja wetu. Matatizo hayatatuliwi na cheo cha mtu bali na jinsi Mtanzania mwenyewe atakapoamua kutoheshimu Utaifa na Uzalendo wake.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na imani na DCs ni sawa na kutokuwa na imani na Wanasiasa kwa ujumla. Kama tunawaogopa DCs basi tuwaogope na Wanasiasa wote kwa ujumla; na wenzetu wasiseme kuwa hawakushirikishwa bali hawakutaka kutimiza wajibu wao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hivi Mwenyekiti wa Chama fulani akiwekwa kwenye Tume atakataa kwa vile ana Chama chake? Jamani tusivuruge nchi yetu.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adimu, kumshukuru Mwenyekiti Mungu, kuwa miongoni mwa Wabunge ambao wanachangia Muswada wa Marekebisho ya Katiba. Vilevile nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa busara, hekima, ujasiri na nia thabiti ya kuwaletea Watanzania Katiba Mpya, ambayo imekuwa ikizungumzwa siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais na Serikali yake, kwa uamuzi huu ambapo si aghalabu hasa kwa nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na Serikali juu ya Marekebisho haya, lakini nitazungumzia Kifungu cha (10) kinachosema Taasisi, Jumuiya au Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana, wanaweza kuandaa Mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa Wanachama wao kutoa maoni yao kuhusu Katiba na kisha kuyawasilisha kwenye Tume.

Mheshimiwa Spika, mimi sina wasiwasi mkubwa kwenye kipengele hiki, lakini naomba Taasisi ama Jumuiya au Kikundi chochote kile pamoja na fursa ya kutoa maoni kuhusu Katiba, kisha kuwasilisha kwenye Tume; lakini wanapotoa maoni yao katika Vikao vyao, basi wawepo Maafisa wa Tume ya Katiba. Wasiwasi wangu ni mtu mwingine kupata fursa ya kudanganya na kupotosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni yangu haya, naunga mkono hoja vizuri tu.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia kwa maandishi. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya ya kutosha na kuweza kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge na kupata nafasi ya kuchangia Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichangie katika Kifungu cha 17(a), maneno "Mkuu wa Wilaya" yabaki kama yalivyo na yasibadilike kama yanavyoonekana katika aya ya (a) ya Kifungu kidogo cha (5) na kuweka badala yake maneno "Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa." Hapana, sikubaliani na hili.

Mheshimiwa Spika, (b) maneno "Mkuu wa Wilaya" yanavyoonekana katika aya ya (b) ya Kifungu kidogo cha (5) yabaki kama yalivyo, yasifanyiwe marekebisho na kuweka "Mkurugenzi wa Manispaa, Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya." Sikubaliani kumtoa Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja na vifungu nilivyovitaja hapo juu vibaki kama vilivyo, kwa sababu Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya yake na huko tunakoelekea kwenye mchakato huu wa Katiba, ulinzi na usalama unatakiwa kwa kiwango kikubwa.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kitendo chake cha kukubali kukutana na Vyama vya Siasa katika kutafakari mustakabali wa nchi yetu. Pongezi sana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Katiba ni mali ya Wananchi na siyo mali ya Serikali na Chama chochote cha Siasa. Nampongeza sana Rais, kwa ujasiri huo. Tazama Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwamba, katiba ni mali ya Wananchi na Serikali hupata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali namna ya upatikanaji wa Wajumbe wa Tume. Hii inadhihirisha kuwa, tutapata Katiba tunayoitaka kwa kuwa na ushiriki mpana wa makundi mbalimbali katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Rais kwa kukubali Wakuu wa Wilaya kuondolewa na hii itatoa uhuru mpana wa kutoa mawazo kwani kwa mfumo wa sasa, Wakuu hao ni Makada wa Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, demokrasia pana ni muhimu katika kupata Katiba tunayoitaka Tanzania. *Let us agree to disagree and remain friends for the betterment of the nation.*

**SPIKA:** Sasa namwita Mtoa Hoja aje ahitimishe. Mtoa Hoja!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili ni moja ya vyombo muhimu sana katika Taifa letu. Naomba sana mnyenyekee kwa Spika. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kufanya majumuisho ya baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, waungwana. Wabunge wamechangia hoja hii kwa maandishi na wengine kwa kunena. Wabunge waliochangia hoja hii kwa kunena ni Wabunge 18. Waheshimiwa Wabunge waungwana waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 79. Wapo pia waliochangia kwa kunipongeza na sasa naongeza wengine Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, kwa hiyo jumla ni 81 waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruksa yako niwataje kwa sababu, naona ndio desturi ya wale Mawaziri wanaosimama hapa, kwangu mimi sio desturi. Mheshimiwa wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa Angellah Kairuki, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, ambaye aliwasilisha Maoni ya Kamati; namshukuru sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa pili aliyetoa maoni ni Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu; nampongeza sana kwa kuunga mkono hoja hii. Mheshimiwa Injina Mnyaa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Seleman Said Jafu, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa William Lukuvi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waungwana waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Pereira Silima, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Profesa wa Uchumi Anna Tibaijuka, Mheshimiwa Dokta Abdulla Juma Saadalla, Mheshimiwa Phillipa Mturano, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Dokta Fenella Mukangara, Mheshimiwa Jerome Bwanausi na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Umy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Joyce Nkya, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mheshimiwa Dokta Terezya Pius Luoga Huvisa, Mheshimiwa Dokta Titus Kamani, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa John Mnyika, tena; Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Chilligati, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Medrad Kigola, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Rita Kabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Azza Hillal Hemed, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Zaynabu Matifu Vullu, Mheshimiwa Dokta Cyril August Chami, Mheshimiwa Samia Suluhu, Mheshimiwa Salvatory Macheleli, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Zainabu Rashid Kawawa, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Riziki Omar Jumaa, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba,

Mheshimiwa Hamad Masauni, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege. *(Makofi)*

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waungwana mliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote hawa waliochangia, wanaiunga mkono hoja hii. Huu ni ushahidi wa kutosha kwamba tunataka zoezi la mchakato wa kupata Katiba Mpya nchini mwetu lianze. Baadhi yao wanapendekeza ama kviacha kama vilivyo vifungu vya sheria vinavyorekebisha.

Mheshimiwa Spika, sheria zinatungwa kwa njia ya maafikiano, ni jambo la kawaida katika nchi zinazofuata demokrasia ya Vyama Vingi. Kinachopaswa kutuongoza katika jambo hili ni busara na kwa kila upande kuelewa mantiki ya upande mwingine na kutafakari kwa makini kila hoja ili kuelewa athari zinazoogopwa. Wakati mwingine, unahitaji kutengeneza njia ya kati, njia ambayo inatoa haki nusu kwa kila mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nadhani ni vizuri Waheshimiwa Wabunge katika watu waliotumwa kuja Bungeni kuwakilisha Wabunge wetu, ninyi ndiyo mlionekana mnaafa na ninyi ndiyo mna busara. Aidha, nakubali ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba tunahitaji kutoa elimu ya Katiba, Katiba iliyopo hapa, nakubaliana pia na ushauri uliotolewa na Mbunge mmoja kwamba ipo haja ya kuanzisha utaratibu au kurejesha utaratibu wa matumizi ya *white paper* katika hatua za kutunga sheria. Nimeuliza swali katika makaratasi haya, kwamba hii Tume itafanya kazi kwa muda gani, naomba mrejee katika sheria kifungu cha 8(3) ambacho kinasema kwamba Tume itakamilisha kazi yake ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi na nane, kuanzia tarehe ya kuanza kazi. Ndiyo maana ni rai yangu, naomba Waheshimiwa Wabunge tofauti zetu ndogo hizi zisije zikazuia zoezi hili kuanza.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge wameshauri kwamba wanasiasa katika ngazi zote Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasizuiwe kuwa wajumbe wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo letu ni kwamba, tuwazuie Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Muswada wa Serikali unaowakilishwa hapa unasema hivyo. Hata hivyo, kama suala ni kufuta sharti hilo mamlaka ya uteuzi itashauriwa ipasavyo. Maoni yangu ni kwamba kama hatutafikia muafaka kwamba hawa waondolewe itakuwa vizuri hakutakuwa na athari. Kama hatutafikia muafaka kwamba hawa wazuiwe, basi utakuwa ni muafaka na kama hatutaelewana, basi ataamua kwa utaratibu wa kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nashauri ushauri wa kawaida kabisa, kwamba ukiacha Muswada ulivyo na sitegemei kuuondoa *unless* ninyi mnaniambia, kama Muswada ulivyo ukiondoa Wabunge pamoja na Baraza la Wawakilishi hakuna athari yoyote, ukiwaacha kwenye sheria kwamba wazuiwe, hakuna athari yoyote. Kwa sababu gani Waheshimiwa Wabunge, tunazungumzia mchakato, mchakato ambao hauishii kwenye Tume, mchakato ambao unaishia kwenye Bunge la Katiba. Hakuna mtu atakayehodhi mawazo katika ngazi ya Tume yakaenda, yakapita mpaka kwenye Baraza lile la Katiba, nafikiri niwaombe kwa imani zenu mtafakari kama vile mnasali au mnaswali kwamba hii niking'ang'ania athari yake ni nini? Tufikirie kama ni watu wazima, kama ni watu ambao tumeanika watu wenye busara. Pia naomba kumtambua kwamba Mheshimiwa John Momose Cheyo naye amechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo hili suala ambalo ni la ukakasi, suala la ma-DC na suala la Wakurugenzi wa Halmashauri. Naomba kuliweka suala hili sawa, kazi ambayo inazungumzwa katika kifungu cha 17(5), ni kazi ya kuitisha mikutano, si kazi ya kukusanya maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama unakubali wale wanaomsema DC sawa, DC kazi yake itakuwa kuitisha mikutano, kama ni DED wale ambao wanampigia chapuo DED, wajue kazi yake ni kuitisha mikutano, si kukusanya maoni. *(Makofi)*

Sasa wenzangu wanaoniona hapa wanafahamu kwamba mimi ni *mediator* na *negotiator*, naweza kusuluhisha watu wanaogombana na usuluhishi wangu, nilijifunza tangu nilipokuwa mtoto nikitaka kitu lazima nitapata. (Makofi)

*(Hapa Wabunge walikuwa wakishangilia baada ya Mwanasheria Mkuu kusema kuwa nikitaka kitu lazima nitapata)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nikitaka nakwenda, namwambia mama kwamba, Baba amesema unipe, mama ananipa kwa sababu hawezi kwenda kumuuliza baba. Nikienda kwa baba namwambia mama ndiyo unakataa nisipewe hiki anamuita mama anamwambia mama mpe.

**SPIKA:** Kwa hiyo, unawagonganisha. (Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nawagonganisha, nasema hivyo kwa sababu gani, hakuna *negotiator* mzuri kama mtoto mdogo hii *he or she knows to get to yes* na haya mafomu mliyokalia upande huu, hayo si hoja, hoja ni Tanzania iliyo kubwa kuliko ninyi. (Makofi)

Suala hapa ni uitishaji wa mikutano, upande mmoja unasema sisi hatuamini watu hawa kwa sababu wako kwenye Katiba yenu na upande mwingine unasema hakuna ushahidi kwamba wanatupendelea na nasikia mwingine anasema haya mapenzi...

**WABUNGE FULANI:** Mapenzi ya dharura.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mapenzi ya dharura, hakuna kitu kizuri kama mapenzi ya dharura. (Makofi/Kicheko)

*(Hapa Wabunge walishangilia sana baada ya Mwanasheria Mkuu kusema hakuna kitu kizuri kama mapenzi ya dharura)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa sababu alisema wale ambao mnasoma vitabu vya mashairi Mchungaji mmoja Mfaransa alitunga shairi, siwezi kulisema hapa kwa sababu lugha hii haileweki humu ndani. Lakini msingi wake ni utamu na urasharasha wa mapenzi ya dharura. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama mwenzako ameona umefanya kitu kizuri na siku zote umezoea kitu ambacho hapendi akakukumbatia na wewe ukamrudishia, mmesahau tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana pande zote, kila mtu ana hoja, tuangalie kazi za DC katika kuitisha mkutano, maana yake sheria ndivyo ilivyo sasa hivi na mwanzoni pale tuliona kwamba, ndiyo ana uharaka ana vyombo, ana *mechanism* ya kufanya mikutano, ndiyo tukaweka. Lakini sasa tuangalie tunatunga sheria ambayo tuna *compromise*, wale wanaongalia Bunge la America, ni *Republican* na *Democrat* wanazungumza wanaelewana. Hivi nini tatizo sisi tusielewane? Sasa nafikiria nikitumia uelewa wangu na ufahamu wangu wa kusuluhisha, Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kwa sababu maneno anavyosema kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi ni kwamba tumeyaweza basi tuwaweke wote, tuna *compromise*, jamani sikilizeni, sitaki, sitaki kumnyong'onyeza mtu yeyote...

*(Hapa Wabunge walikuwa wakinong'onanong'ona)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nilikuwa napendekeza, nilikuwa napendekeza...

**SPIKA:** Naomba tumsikilize tuweze kupima.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mapenzi ya dharura. (Kicheko)

Nilikuwa napendekeza kwamba tutumie maneno yote mawili kwa sababu ni Tume yaweza “may” na kwa upande wa Zanzibar, Zanzibar ambao wana maoni yao na utaratibu tukishabadilisha hapa na Zanzibar tutatafuta namna yake. Tutawa-engage Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nimependekeza hivyo, kuna hoja katika kifungu cha 6(8) ambacho nafikiri Mheshimiwa Halima Mdee amesema kwamba kwenye *schedule of amendment* yale maneno kwamba, *subsection six shall not be construed as precluding the President from appointing other persons to be members.* Kwamba Rais ateue tu kwa wale ambao wamechaguliwa kwenye hizo *organizations* ambazo ziko kwenye six na seven na naomba kufanya marekebisho kwenye *proviso* ya sita inasema: “*Provided that the list...*”, naomba isomeke: “*Provided that a list of names shall...*” halafu unaendelea na pale kwenye seven, kuna kitu umeomit, *Political parties.* Kwa hiyo, isomeke *in inviting* bila kuathiri hoja niliyoisikia kwamba kuna Mheshimiwa Mbunge ataleta mabadiliko. Kwenye *servicing* nitasema *in inviting Political Parties,* unaendelea kama kawaida...

Waheshimiwa Wabunge, Watanzania ambao hawako kwenye makundi hayo ni wengi sana, si Watanzania wote ambao wako kwenye *NGOs*, si wote wako kwenye *Mashirika aa Dini*, si wote ambao wako kwenye *professional boards au associations*, sasa hao utawatoa kwenye utaratibu huu? Huo ndiyo msingi wa kusema Rais hatalazimika tu kufuata ile orodha, atachagua watu wengine nje ya majina yale ambayo yameletwa na *associations.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nimelisikia nafikiri lilikuwa ni hilo la dhahabu, Vyama vya Siasa, suala la *DC*, hayo ndiyo masuala makubwa ambayo yamezungumzwa. Mengine yale tunaweza kwenda kwenye vifungu, tutatoa maelezo zaidi, lakini ombi langu kwenu Waheshimiwa Wabunge kupitia kwa Mheshimiwa Spika, ni kwamba, tunachofanya hapa ni kutunga sheria ambayo ina *compromise whether* au kama kuna mapenzi ya dharura. Lakini tunajua kwamba tunachotaka ni Tanzania tulivu ambapo mchakato huu wa Katiba utakwenda bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, siwezi kutaja kila mtu amesema nini, lakini wengine tutawaandikia, nafikiri wale ambao mmeuliza maswali magumu, tutawaandikia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la Kanuni. Nangojea Waheshimiwa Walioniandikia vi-note vya kanuni kwamba, wale walioleta *schedule of amendment* wametumia kanuni ambayo siyo yenyewe na kwamba kanuni ambayo ingetumika ni kanuni ya 88(6).

Mheshimiwa Spika, kwa kweli bila kumung'unya maneno na utaratibu ni kwamba zile *schedule of amendments* zimefuata utaratibu wa kanuni na kama Mheshimiwa Mbunge utakuwa hujaridhika, basi narudia tena kwamba, hapa tunakwenda kwa kanuni na msemaji wa mwisho kwenye kanuni ni Spika ambaye narudia tena, wale wanasheria ambao ni Wabunge tafadhali mnyenyekee mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, tunakwenda hatua inayofuata.

#### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011  
(The Constitutional Review (Amendments) Bill, 2011)**

**MWENYEKITI:** Katibu tuendeleel!

Ibara ya 1

(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)

Ibara ya 2

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peter Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mabadiliko kwenye *schedule of amendment* iliyoletwa na Serikali kwenye kifungu cha 6(7) ambayo kwenye jedwali la marekebisha ya Serikali ukisoma kifungu cha (6) na (7), unachokiona kifungu cha (7) ni marudio ya kifungu cha (6) nikawa napendekeza na naomba Wabunge waniunge mkono kifungu cha (7) tukifute na sasa kile kilichokuwa na (8) ndiyo kiwe cha (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hivi kwa sababu ukisoma kifungu chote cha (6), naipongeza Serikali kwani Rais ataweza kuwa-*invite* watu wote, Vyama vya Siasa, Makundi ya Kidini, *Civil Society* na watu binafsi wote wapeleke majina kwa ajili ya kuteuliwa kwenda kwenye Tume. Lakini unaona kwenye kifungu cha (7) nacho kinarudi kulekule yaani kinafanya *almost* kazi ile ile, lakini la msingi zaidi ni kwamba ziko *organizations* nyingi sana ambazo *umbrella bodies*, ukisoma kifungu cha (6) na (7) unaona kwamba watakaokuwa *considered* ni wenye *umbrella bodies* ingawaje namba (8) inasema Rais anaweza akaenda nje ya majina aliyopelekewa na kwa *spirit* hii ambayo tumeanza nayo itakuwa ni jambo la ajabu, tumeomba orodha halafu unaacha orodha yote unakwenda kutumia kifungu cha (8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili kifungu cha (7) chote kifutwe na sasa kifungu kilichokuwa cha (8) ndiyo kiwe cha (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, demokrasia ina gharama zake, tunafanya kazi za demokrasia hapa na siku zote kwenye demokrasia huwa lazima kuna upande mmoja utashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi ya Marekani wana Katiba ambayo imeundwa miaka mingi iliyopita, lakini siku wanapitisha Katiba yao, upande mmoja ulishinda kwa kura moja na hii ndiyo demokrasia inavyosema. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono ili tukitoe kifungu cha (7) ili tumfanye Rais awe na wigo mpana zaidi na aweze kuhakikisha yale aliyoletewa na vyote yaani wenye *umbrella* na wasio na *umbrella* wote aweze kuwaingiza kwenye mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

#### KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu gani? Wengine naomba mkae.

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge linapokaa kama Kamati ya Bunge Zima, limeweka utaratibu kwa mujibu wa Kanuni wa namna ya kutoa *schedule of amendments* kwa ajili ya kurekebisha Muswada.

Mtoa hoja ameleta mapendekezo ya mabadiliko yake mazuri tu, lakini ametumia Kanuni ya 86(10)(b) na ametumia Kanuni ya 86(11) na nitaomba kuzisoma.

Kifungu cha 10 kinasema: "Katika hatua hii iwapo mtoa hoja katika hoja hii tunayojadili ni Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anataka kufanya marekebisha au mabadiliko katika Muswada wa Sheria na Muswada wa Sheria ni huu siyo *schedule of amendment* ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameileta, Muswada tulionao ni *A Bill For an Act to Amend the Constitutional Review Act, 2011*.

Sasa Mheshimiwa Mbunge kutoka Kigoma Mjini ameleta kwa Kanuni ya 86 kama mtoa hoja na yeye si mtoa hoja. Lakini pili, mleta mabadiliko yaani Mbunge kutoka Kigoma Mjini ametumia Kanuni ya 86(11) ambayo naomba kuisoma, inasema: "Kamati au Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada." Narejea kwamba Muswada ni ule Muswada ambao ulikwenda kwenye Kamati na siyo *schedule of amendments*, ama Muswada huo wakati wa Bunge Zima akionyesha mabadiliko bayana yaani mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika kila Ibara inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya Kamati yako ya Bunge Zima, Kanuni ambayo inatuongoza katika kuleta mabadiliko ni Kanuni ya 88(2) ambayo inasema: "Mabadiliko yote yaliyopendekezwa kufanyika katika Muswada wa Sheria sharti yawekwe katika jedwali la mabadiliko..." na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kanuni ya 86(10)(b) na 86(11) haziendani na mabadiliko ambayo Mheshimiwa Mbunge anayataka kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hakuna *schedule of amendment* mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nadhani ungekwenda zaidi ukasoma kifungu cha 88(6) ambacho kinasema: "Endapo kuna mabadiliko mengine yamependekezwa kufanyika katika jedwali la mabadiliko basi mabadiliko haya yaliyopendekezwa awali na ambayo yamo katika jedwali la mabadiliko hayatahesabiwa kwamba yameondolewa hadi majadiliano juu ya mabadiliko haya yatakapokuwa yamefikwa mwisho au Waziri, Kamati ya Mbunge au Mbunge aliyetoa mapendekezo yaliyomo katika jedwali la mabadiliko atakapoomba kwa Spika mapendekezo yake yaondolewe."

Maana yake ni nini? Kuna *schedule of amendment* ambayo Serikali imeleta lakini kwa kifungu hiki unaweza kuleta tena *amendment* juu ya yale mabadiliko. Kwa hiyo, hii ni *given order*. Tunaendelea!

Sasa watu siyo kama mnasimama kuunga mkono...

#### KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Naomba niseme kwanza, halafu wewe baadaye. Kwa hiyo, mliosimama hamuungi mkono kama hiyo hoja nyingine, lakini nasema nitawapa nafasi ya kuzungumza, lakini sitatoa kwa ninyi wote. Wale nitakaowapa nafasi kuzungumza baada ya Mheshimiwa Serukamba watatumia dakika tatu halafu baada ya hapo nitamwita mtoa hoja ili aweze ku-*defend* hoja yake. Kisha nitamrudia Mheshimiwa Serukamba ambapo atakayosema kama tutaona hakuna haja, tunaendelea kubishana basi tunaweza kupiga kura.

Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti....

**MWENYEKITI:** Ni Mheshimiwa Tundu Lissu sasa! Ya nimeshasema ni kifungu cha 86.... (Kicheko)

Ni Mheshimiwa Tundu Lissu !

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jedwali la marekebisha ambalo limeletwa na Mheshimiwa Peter Serukamba linataka kubadili jedwali la marekebisha la Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ili jedwali la marekebisha libadili jedwali lingine la marekebisha inabidi liletwe kwa mujibu wa kanuni ya 88(6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa jinsi linavyoonekana hili jedwali la marekebisha la Mheshimiwa Serukamba limeletwa chini ya kanuni ya 86(10)(b) na kanuni ya 86(11), halijaletwa

kwa mujibu wa kanuni ya 88(6) ambayo ndiyo ingeruhusu marekebisho kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kweli kama angejielekeza kwenye kanuni ya 88(6) basi hili jedwali lingekuwa sahihi kabisa, lakini limeletwa chini ya kanuni isiyohusika. Kwa hiyo, haliwezi kuwa jedwali la marekebisho halali kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ni kweli kwamba kama jambo fulani limefanyika chini ya kifungu fulani, unapopeleka maombi ni lazima ufanye kwenye kifungu hicho na alichofanya mleta mabadiliko haya ingawaje ametumia kifungu kidogo cha 10 cha Kanuni ya 86 lakini amerefer au ameonsha kwamba anakitumia pia kifungu au kanuni ya 11 ya kanuni hiyo na katika lugha ambayo Mheshimiwa Lissu unafahamu unaweza kutenga 10 na 11 bado uka-serve mabadiliko au marekebisho ambayo Mheshimiwa Serukamba ameyaleta. Nafikiri hoja kubwa hapa ni kuangalia mantiki kwa sababu *procedure* ipo sawa.

**MWENYEKITI:** Jamani tusiendeleze ubishi, tuone tunasemaje.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongozwa kwa mujibu wa kanuni.....

**MWENYEKITI:** Endelea kutoa hoja yako.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Tunaongozwa kwa mujibu wa Kanuni, mabadiliko ya Kanuni namba 86(11) ukiisoma haelezi kabisa anachokieleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, haihusiani kabisa na wala hatuna haja ya kuendelea kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kanuni ya 88(6) kama jinsi ambavyo umeisoma, endapo kuna mabadiliko mengine yamependekezwa mantiki ya Kanuni ya 88 ni mabadiliko kwenye Muswada. Muswada tulionao hapa ni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria yaani *Constitutional Act*, Muswada wetu siyo *schedule of amendment* ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameleta. Kifungu cha 88(6) kinafanua utaratibu wa namna ambavyo hoja inatoka au kuingiza na namna ambavyo Mbunge anaweza akaiondoa hoja ambayo ameleta au Waziri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza kwamba mabadiliko ambayo yameletwa na Mbunge wa Kigoma Mjini Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba hayakidhi matakwa ya Kanuni yetu. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hakuna mabadiliko mbele yetu, tunaomba tuendelee na mabadiliko mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti kama Mheshimiwa Zitto Kabwe angesoma vifungu hivi akakamilisha basi utata huu wote ungekwisha.

Nakwenda kwenye Kanuni hiyo ya 86(11) ambayo inasema: "Kamati au Mbunge anaweza kuwasilisha kwa Katibu kwa maandishi mabadiliko anayokusudia kuyafanya katika Muswada huo wakati wa Kamati ya Bunge Zima akionesha bayana mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika kila Ibara inayohusika." Sasa, tuna Muswada mmoja lakini pamoja na mabadiliko yanayofanyika hii anayozungumza ya Kanuni ya 88(6), inaweka utaratibu tu wa namna ya kuenenda baada ya hatua hiyo. Kwa hiyo, uwasilishaji wa hoja ya Mheshimiwa Peter Serukamba umefuata utaratibu unaotakiwa.

Lakini sita inasema: "Endapo kuna mabadiliko mengine yaliyopendekezwa kufanyika katika jedwali la mabadiliko katika hilo lililowasilishwa, basi mabadiliko hayo yaliyopendekezwa awali na ambayo yamo katika jedwali la mabadiliko hayatahesabiwa kwamba yameondolewa hadi majadiliano juu ya mabadiliko hayo yatakapokuwa yamefikia mwisho au Waziri, Kamati ya

Bunge au Mbunge aliyetoa mapendekezo yaliyomo katika jedwali la mabadiliko atakapoomba kwa Spika mapendekezo yake yaondolewe." Hapa inazungumzia utaratibu katika kuondoa hoja au kuhitimisha hoja, kwa hiyo, kifungu hiki angekisoma akakimaliza, ataona wazi kwamba Mheshimiwa Serukamba, Mbunge wa Kigoma aliwasilisha hoja yake kwa mujibu wa taratibu kwa Katibu wa Bunge.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna ukakasi wa uelewa, unaposema Muswada, Muswada ni nini? Muswada ni pamoja na *schedule of amendments*.

Mheshimiwa Mbunge nimesomea Sheria...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto wanapozungumza wenzako, wasikilize, hakuna ubishi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Muswada ni pamoja na *schedule* ndiyo maana, *schedule* ile imewasilishwa chini ya Kanuni ya 84, soma kitabu chako hicho. Kanuni ya 84(1) na ya (3) na imejadiliwa katika Kamati ya Bunge. Sasa Mheshimiwa Serukamba alitoa taarifa wakati tumekaa hapa kwamba, anatarajia kuleta mabadiliko ya kwenye sehemu hiyo. Nafikiri *issue* kubwa hapa ni kuangalia maudhui ya mabadiliko yake. Utaratibu ndio huo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunatumia muda mwingi na hii sio mara ya kwanza kabisa sisi tunafanya *amendments*. Kanuni zetu zinaruhusu hata kama ungekuwa wewe ukaleta *amendment* wengine waka-*amend* ile kanuni yako. Sasa utaratibu unaosema yule anayeleta *amendment* baadaye ndiye anayesikilizwa kwanza wakati *amendment* iliyotangulia inabakia pale pale. *In case amendment* ya Mheshimiwa Serukamba inapita basi ile nyingine inafutika.

Kama itashindwa ya Mheshimiwa Serukamba tunaendelea na *amendments* zilizo, sio mara yetu ya kwanza kutunga hiki kitu. Isipokuwa ninachokisema waliounga mkono tena waliosimama sio lazima nyinyi tu hata upande wa pili wanaweza kujadili hili. Sio kwamba nyinyi mlisosimama ndio mtakaojadili peke yenu hata wengine nao wanafikiria kwamba, mawazo haya anayopendekeza Mheshimiwa Serukamba hayatakiwi, nao wanaweza kujadili katika kifungu hicho. Kwa hiyo sijui nani anataka kujadili, nimewasahau, mmekuwa wengi mno. Anayetaka kujadili asimame nimwone. Anayetaka kuunga mkono au kupinga mapendekezo ya Mheshimiwa Serukamba azungumze. Mheshimiwa Angella halafu atakuwa Mheshimiwa nafikiri Msafiri. Ngoja kwanza tuandike.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie na kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaomba tuwaandike wale waliosimama wachache. Tumesema yupo Mheshimiwa Kairuki, Mheshimiwa Msafiri, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Blandes basi.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona ili na mimi niweze kuchangia na kuunga mkono mabadiliko yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Serukamba hususan katika kifungu cha 6(7). Namwunga mkono kwa sababu katika kifungu hiki Serikali inapendekeza kwamba Rais atakapozialika Taasisi, Makundi ya Watu au Jumuiya za Kidini azingatie umoja wa Taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatolea tu mfano wa Taasisi za Kidini. Taasisi ya Kanisa la Kisabato haiipo popote inasimama yenyewe. Ukisema washirikiane na Muungano wa Umoja wa Taasisi zingine utakuwa kwa kweli hujawatendea haki, lakini naamini pia kuna Taasisi zingine za Kidini haziko katika Umoja. Lakini pili, hata katika Taasisi ambazo ziko katika umoja hutakuwa na uhakika kwamba vikao hivyo vya kuamua majina gani yanapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kama vitafanyika na hutakuwa na uhakika endapo majina hayo yatakapopelekwa kama kweli wote



walishirikishwa. Kwa hiyo, kwa kweli dhamira yangu kwenye hilo mimi ni hiyo. Kwa hiyo, kwa kweli namwunga mkono Mheshimiwa Serukamba kifungu hiki kiondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda kuunga mkono hoja mapendekezo ya Mheshimiwa Peter Serukamba. Naunga mkono kwa sababu moja tu. Kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaamini kabisa kwamba Serikali yetu haina dini na kwa misingi ya utawala wa sheria, tunaamini kwamba hakuna mtu anayelazimishwa kujiunga na Taasisi yoyote ile iwe ya kiraia au ya asasi yoyote. Kwa hiyo, tunasema kwamba si busara kumuwekea Rais masharti kwamba, lazima wawakilishi wa Tume watoke kwenye taasisi zilizotajwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tuna uzoefu kwamba kwa mfano, katika madhehebu ya dini hakuna chombo kinachounganisha madhehebu yote ya dini Kitaifa. Hakuna chombo chochote cha Kitaifa kinachounganisha Asasi za Kiraia. Kwa hiyo, tutakuwa tunambana Rais na baadaye kutakuja kuleta migogoro kwa sababu tunaamini kwamba hizi asasi zimejiunga kwa malengo maalum na hakuna chombo cha Kitaifa kinachounganisha wote. Tuna Waislam wana mahitaji yao, tuna Wakristo wana mahitaji yao na tuna madhehebu madogo madogo kwenye imani na tuna taasisi mbalimbali. Kwa hiyo, lazima tumpe fursa Mheshimiwa Rais kwamba asifungwe na vifungu hivi kwamba lazima atoke kupitia huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii wamemsifu sana Mheshimiwa Rais kwa busara alizotumia mpaka tumefika hapa. Sasa kifungu cha 6(7) ambacho mapendekezo ya mabadiliko ya Mheshimiwa Serukamba yanataka kukifuta. Sasa nasema *schedule amendment* ya Mheshimiwa Serukamba inataka *delete subsection (7)* na kubadilisha *subsection (8)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *subsection*...

**MWENYEKITI:** *Subsection (8)* kama kikitoka cha (7), kwa hiyo (8) inarudi juu nilivyoelwa mimi, si ndivyo? *The issue* ni kile cha (7). Naomba uzungumze.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu cha (7) inasema "*By deleting the subsection (7) halafu Roman (ii) inasema, deleting subsection (8) and substituting for it the following new subsection*". Kwa hiyo, *subsection (7)* inafutwa kabisa halafu *subsection (8)* inabadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *subsection (7)* inayofutwa inasema kwamba katika kualika Taasisi za Kidini, Kiraia, Jumuiya na Makundi mengine Rais atazingatia umoja wao. Nimesikia hoja hapa kwamba, hii inamfunga Mheshimiwa Rais. Sasa Mheshimiwa Rais mwenyewe alisema kwamba, kuna Mashirika ya Kiraia na ya Kidini zaidi ya 4,000, haitawezekana kuya-consult yote, ndiyo maana akasema kwamba twende kwenye *umbrella organizations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiki ambacho kinapendekezwa kubadilisha kinakwenda kinyume moja kwa moja na matakwa na ushauri wa Mheshimiwa Rais aliosema kwamba nendeni kwenye *umbrella organizations*.

**MWENYEKITI:** Haya saa yako imekwisha bwana. Kitu kimoja naomba tuelewane. Humu ndani tunatunga sheria, hayo mashauriano mliyofanya na Rais sijui wapi tunaomba msije mka-refer hapa. Kwa sababu hata kanuni zetu zinakataa kum-refer Rais kusudi watu wengine watetemeke hapa waache kutunga sheria. Ahaa! Tungeni sheria toeni hoja zenu za msingi tukubali ama tukatae. Naomba sana mlikuwa na Rais, mmeshaona hiyo ndiyo inayoleta kero hapa, Rais hatungi sheria huko.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kama nilimuelewa Mheshimiwa Serukamba vizuri alipokuwa anatoa maelezo ya kwa nini ameleta *amendment*. Alisema kwamba *section (7)* iwe *deleted* kwa sababu inafanana na *section (6)*. Lakini nataka nitoe tu maelezo vizuri kwamba, ibara ya 6 ni tofauti kabisa na ibara ya 7. Ibara ya 7 inajaribu kutoa namna sasa huo uteuzi unavyofanyika ni *check and balance*. Kwa mfano na *issue* hapa inavyoleta shida ni hii *umbrella organization*. Kwa mfano, hii sheria inasema, kwa hiyo *subsection (7)* inasema "*Inviting religious organizations, civil societies* ndio Rais a-consider *umbrella organization*."

Sasa unaposema *religious organizations* maana yake ni kwamba *you talk of bigger picture Christians* pamoja na Waislam. Sasa maana yake ni kwamba Rais asije akachukua majina ya watu waliotoka kwenye Viongozi wa Dini akateua Wakristo tu. Ni kwamba hii *section (7)* inampa afanye *check and balance* ahakikishe kwamba, kuna mwakilishi wa Waislam kuna mwakilishi wa Wakristo na unapokuja kwenye *civil organizations* kwa mfano kuna umoja wa NGO's kama labda ziko mbili anahakikisha kwamba labda nimem-pick mmoja kutoka huku na mmoja kutoka huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachojaribu kumwambia Mheshimiwa Serukamba ni kwamba *section (7)* na *(6)* ni vitu viwili tofauti. Hii *section (7)* inajaribu kutoa tu *check and balance*, ni ni kitu gani cha ku-consider Rais atakapokuwa anafanya huo uteuzi. Kwa hiyo kama hofu yake ilikuwa ni kwamba *section (6)* na *section (7)* zinafanana, hazifanani Mheshimiwa Serukamba. Kwa maana hiyo naomba u-withdraw hii *amendment* kwa sababu sasa umeelewa kwamba hizi *section* hazifanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Sio Mahakamani, wewe umetoa mchango wako, tuachie sisi tutahukumu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naungana na Mheshimiwa Serukamba kuondoa kifungu hiki kwa sababu hapa neno ambalo limetumika ni neno hasa "*shall*". Inasema: "*The President shall have regard to their respective umbrella organizations*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno "*shall*" linambana, linamlazimisha Mheshimiwa Rais hana mwanya mwingine wa kuwa huru. Kwa hiyo, kumtungia sheria Mheshimiwa Rais inayombana namna hii akakosa mwanya wa kuangalia kuwa huru nadhani sio sahihi ndiyo maana naunga mkono.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposimama, sikusimama mwanzo, lakini niliposimama ilikuwa ni kutoa taarifa tu kwa yale ya Mheshimiwa Tundu Lissu aliyoyasema kuhusu kifungu kidogo cha (7), kwamba mimi siko sehemu ya Ikulu, lakini niko sehemu ya Bunge hili kwenye Kamati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ni kwamba, kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria. Hoja ya Serikali haikuwa na kifungu hicho kama ingelikuwa ni maelekezo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yake ni watu sikivu sana, wanachukua *instructions* za Serikali. Haya yalikuwa ni mashauriano tu ndani ya Kamati kwamba kwa taasisi ambazo zina *umbrella organizations* labda tuangalie uwezekano huo. Lakini haya hayakutoka kwenye *quota* ambayo amesema humu Bungeni kwamba yalikuwa ni maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muhimu kusafisha hii hali ya hewa.

**MWENYEKITI:** Ni kujibu bwana, unasafisha kutoka wapi? (Makofi/Kicheko)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nimetumia lugha ya kishairi tu.

Mheshimiwa Rais hakuagiza kwamba ije mvua au kije kiangazi, nawaagiza kwamba hayo yapite. Mheshimiwa Rais alichosema nendeni mkawashawishi Wabunge, ndicho tunachofanya hapa. Kama utaalim wa kujadiliana ni vizuri kuacha kabisa maneno ambayo yanaweka ukakasi kwa mwenzio. Kwa hiyo, hapa tuna-*negotiate* na kwa hili mimi na Tundu Lissu hatutofautiani sana kwa sababu kwanza aliunga mkono, niliona alikuja hapa tukasalimiana vizuri kwa mapenzi ya dharura. Kwa hiyo, *issue* hapa ni nini?

Narudia tena twende kwenye busara kifungu hiki utakumbuka Mheshimiwa Tundu Lissu tuliki-*draft* mimi na wewe chumba 200 pale. Kwa hiyo, hiki hakitokani na vile vikao vyetu tulivyokuwa na Mheshimiwa Rais. Ni vizuri kusema ukweli tu, lakini kinachosemwa hapa ni nini? Tullilipeleka jambo hili kwenye Kamati, Kamati ikatukubalia, mimi na wewe, sasa tunakuja kubembebeza Wabunge wakubali. Lakini sasa na wenyewe mimi nachelea kwa sababu tusimtumie Rais, nachelea sana. Sasa hapo inabidi tuwabembebeze mimi na wewe, tuwabembebeze wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge tulichoelewana hapa samahani kidogo. Tulichoelewana hapa ni hivi, kweli Rais alisema kuna haya majitu yako mengi sana tuangalie namna gani ya kurahisisha. Sisi tukadhani kwamba tukifanya *umbrella* tutakuwa tume-*solve problem*. Sasa na mimi nimekuja hapa nimesikia Mheshimiwa Serukamba anasema na wengine wamemwunga mkono kwamba si wote ambao wako kwenye *umbrella*. Hiyo ndiyo hoja ambayo sasa mimi na wewe tumesoma sheria tutafute namna gani ya ku-*accommodate views* za Mheshimiwa Serukamba bila ya kumnyong'oneza na hii ndiyo kazi hasa ya Bunge. Kazi ya Bunge ni kutunga sheria. Ile ya Rais ni kuangalia Muswada uliotungwa na Bunge kule hakuna *debate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na nasema hivi kwa nia njema kabisa kwamba, ukiondoa ile *subsection (7)*, hakuna kitu ambacho utakuwa umepoteza. Kwa hiyo, nakushauri Mheshimiwa Tundu Lissu kupitia kwa Mwenyekiti, ukubali pendekezo hili ni *give and take*. Tuliondoe hili kwa sababu halileti athari yoyote. Halafu ile iliyobadilishwa, ile ambayo mwenzetu amekaa ame-*draft let us give him credit*. *I think that is a good drafting*. Unakumbuka ile *subsection (8)* iliyopo sasa tuliandika mimi na wewe wakati ambapo labda usiku ulikuwa umekwenda sana. Lakini Mheshimiwa Serukamba anasema ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba amalize kusema halafu nielewe.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Serukamba mabadiliko yake yanasema: "*Subsection (6) shall not be construed as precluding the President from appointing as Members persons outside the list of names submitted to him as provided for subsection (6)*."

Sasa ukisoma tum-*convince* na yeye kwamba maana ya maneno hayo mengi ni sawa sawa na ile *subsection (8)* ya sasa ambayo inasema "*Subsection (6) shall not be construed as precluding the President from appointing other persons to be Members*."

Maana ya kifungu hiki ni kwamba, Mheshimiwa Rais ana orodha tayari ile inayotoka kwenye Mashirika yale. Lakini pia kuna Watanzania wengi kama mimi hapa ambao hatuna vyama, anatumchagua na wenyewe humu ndani. Nafikiri hatuwezi kuwaacha hawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Serukamba nafikiri nakubali kwamba tufute ile (7), lakini tu-*retain* (8) ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa gani jamani, ya kutoka wapi?

Ngoja kwanza, naomba nimsikilize Mheshimiwa Sillinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazungumza, amejaribu kutupa taarifa mpya kwamba Muswada huu, maeneo mengi walijadili yeye na Tundu Lissu, wakati Muswada uliopo ama mabadiliko ya sheria yaliyopo ni ya Serikali.

Sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali arekebishe taarifa yake ama akubali kwamba huu Muswada ni wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnajua tabia yetu ni kutaka kuchelewesha wakati. Tulichokuwa tunakataa sisi ni kufanya *reference* kwa Rais. Hiyo tumekataa kwa sababu sisi ndio watunga Sheria. Ndiyo hilo tu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa busara ya Meza yako. Kuna watu wanataka kuonyesha hatukufuata utaratibu, lakini utaratibu tumefuata vizuri. Bado nasisitiza kifungu cha (7) kifutwe. Gharama za Demokrasia hatuwezi kufuata makundi hata yakiwa 5000. Hii ndiyo gharama ya demokrasia. Lakini ni dogo tu wakati unaanza mchakato huu. Tulianza mikutano Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. Wako watu walikuja hapa wakasema hamjaenda sehemu nyingi. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo hapana, hamjashirikisha watu wengi. Lakini leo wanasema huna haja ya kwenda kwenye watu 3000. Sasa ni nini hapo?

Ninachotaka kusema mimi, namshukuru *Attorney General* amelielewa, naomba namba (7) tuitoe, namba (8) ipande. Lakini namba (8) nilichofanya mimi ni kuiandika upya. Sio kwamba nimebadilisha, nimecheza na maneno ambapo nilikuwa nimesema: "*Shall not be construed as precluding the President from the appointing other persons out of the list of names submitted to him as provided for in subsection (6)*" na kuifanya namba (8) iwe na namba (7).

Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono, tukiondoe kifungu namba (7) na tubadilishe maneno haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na muda tulionao, naomba nitumie kifungu cha 28(5) tuongeze dakika 30 kusudi tuendelee na kazi hiyo kwamba: "Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa moja na 45, Spika anaweza akaahirisha Bunge, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao na Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado hajiamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge." Kwa hiyo, naomba niongeze dakika 30 kuanzia saa mbili kasorobo tuweze kuendelea. Sasa wote wamezungumza sasa napenda kuwahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuamuliwa)*

*(Ibara ya Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na mabadiliko mengine. Lipo suala la Mheshimiwa Ole-Sendeka. Wakati wa Kamati ya Bunge Zima huwa hakuna vitu vya kuvurugana, tunaendelea ku-concentrate on this. Mheshimiwa Ole Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nimeleta mabadiliko juu ya jedwali la mabadiliko kama inavyosomeka kwenye karatasi ambayo Wabunge wanayo pale kwenye *section (6)*. Nimeomba tufute sehemu ile ya (a) katika *subsection (5)* na kwa maana hiyo tunapaswa sasa kupandisha (b) iwe (a) na (c) iwe (b).

Sasa mantiki mazima kwa nini nimependekeza, kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho ni kwamba lilikuwepo pendekezo la Serikali la kuondoa kizuizi kwa wanasiasa kuweza kuteuliwa kuingia katika Tume. Lakini ikaondolewa pingamizi hilo, lakini ikabakiza pingamizi, kwa baadhi ya wanasiasa ambao na wao ni Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Nami naamini busara ya Rais itaendelea kutumika katika kuteua Wajumbe hawa wa Tume, kwa hiyo, nikasema niombe Wabunge waniunge mkono katika kuiondoa hiyo sehemu ya (a) ya kifungu kidogo cha

(5) katika kifungu cha (6) cha Sheria hiyo na katika mabadiliko hayo kama ambavyo nimependekeza.

Kwa hiyo, nilikuwa najaribu kuona kwamba kizuizi hiki ukisema tu kwamba unawaondoa Wabunge Wawakilishi, lakini unasema viongozi wa kisiasa waingie, Wabunge pia ni viongozi wa kisiasa, lakini na Rais atatumia busara kwa sababu nafasi ni 16 Bara, na 16 upande wa Tanzania Zanzibar. Kwa hiyo, bado nilikuwa naamini kwamba kifungu hicho kidogo cha (a) kikitoka wala haitaathiri jambo lolote na naomba nitoe hoja na Wabunge wenzangu waniunge mkono katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni haina pingamizi na mapendekezo ambayo Mheshimiwa Ole-Sendeka ameyaleta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unaunga mkono? Kambi ya Upinzani au ni Zitto mwenyewe? Hakuna Kambi ya Upinzani.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani siku zote imekuwa kwamba Wabunge, Wawakilishi, wanasiasa, wasomi, *provided* wana uwezo na kuwa na zile *qualification* za kitaaluma zinazotakiwa, wana haki ya kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Huu ndiyo ulikuwa msimamo wetu tangu mwanzo, na ndiyo ulikuwa msimamo wetu leo asubuhi na msimamo wetu sasa hivi. Kwa hiyo, pendekezo la Mheshimiwa Ole-Sendeka, tunaliunga mkono mia kwa mia.

**MWENYEKITI:** Mlikaa pamoja? Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Tumekubaliana kimsingi kwamba mchakato wa kutunga Katiba ni mchakato wa Watanzania na wakati mwingine unagundua kabisa kwamba hawa waliomo katika Ukumbi huu wanaoshiriki katika Sheria mbalimbali pale inapofikia hatua, Watanzania wengi wanakosa nafasi ya kutoa mawazo yao, mawazo hayo yanaweza yakapatikana kupitia wanasiasa wazoefu, walioboea katika maeneo mbalimbali ambao wanaweza wakapatikana ndani ya Bunge ama ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hatua hiyo, ninaomba kabisa kwa dhati Waheshimiwa Wabunge tuungane mkono na mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Ole-Sendeka. Nami kwa hatua hiyo, nawashukuru sana hata wenzetu wa upinzani kwa kuona umuhimu wa kuunga mkono katika eneo hili. Kwa hiyo, naomba tuunge mkono mabadiliko haya yaliyoletwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kuna *consensus* kwamba Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasizuiwe. Kwa hiyo, sisi tutaiondoa kama ndiyo *consensus*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka unahitaji kusema chochote? Maana ni kama umekubaliwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishukuru Bunge lako Tukufu.

**MWENYEKITI:** Nadhani wote wamekubaliana. Ngoja niwahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 3

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kupata nafasi hii ya kuleta mabadiliko kwenye mabadiliko ya Serikali kama ifuatavyo:-

Katika kifungu cha 17(6) nasoma pamoja na...

#### TAARIFA

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Simama, sema.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani hatujafika huko kwenye kifungu cha 17, bado kuna *section 12* ambayo iko kwenye jedwali la Mheshimiwa *Attorney General*.

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na Muswada huu utaona kuna *paragraph* mbili tu. Yaani ya kwanza na pili. Ambacho msaidizi wako anasema ni Ibara mpya ambayo haipo kwenye *Bill*.

**MWENYEKITI:** Kwa mapendekezo hayo baada ya kushauriana hapa, kutokana na kwamba Ibara mpya ambayo imeletwa, tukubali ina mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu.

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya (3) kuna rekebisho linaloletwa na Serikali kwenye *section* ya 12, halafu kuna rekebisho linaloletwa kwenye *section* ya 13 na 17, yote haya yamewekwa kwenye Ibara moja. Pendekezo la Mheshimiwa Tundu Lissu anafikiri kwamba tupitishie namba 12, 13 na 17 *individually* ili kusudi kama moja inakataliwa, basi nyingine ziendelee.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nimesema tumkubalie pendekezo alilotoa.

**NDG. JOHN JOEL - KATIBU MEZANI:** Kwenye Ibara mpya ya (3) *section* ya 12 na *section* ya 13 hazina mabadiliko yoyote.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MHE. ANNE K. MALACELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Section* ya 17 ambayo Serikali inamwondoa kabisa Mkuu wa Wilaya katika kusimamia shughuli za utaratibu za utendaji wa kazi wa Tume na inaleta marekebisho kufuta maneno Mkuu wa Wilaya na kumweka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, katika kifungu kidogo cha (a), (b) pia kinamfuta Mkuu wa Wilaya kinamweka Mkurugenzi wa Manispaa; (c) kinafuta kifungu kidogo na kusema "Yeyote atakayetaka kuendeleza program..." Kwa kifupi hapa tatizo lipo kwamba Serikali inamwondoa Mkuu wa Wilaya kwa ujumla wake kusimamia shughuli zote ambazo zitakuwa zinafanywa na Tume ya kukusanya maoni. Mimi naleta *amendment* ya kumrudisha Mkuu wa Wilaya kama ilivyokuwa kwenye Sheria mwanzoni kwa sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali iliposimama kujibu, mmekuwa katikati katika kitu ambacho siyo kizuri, ni kuwa katikati. Haikusema aidha ni Mkuu wa Wilaya au ni Mkurugenzi. Mimi naomba nitetee hoja yangu kama ifuatavyo:-

Ndugu zangu hili tendo la Katiba ni tendo kubwa sana. Ni kwamba kwanza anayeteua ile Tume ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni *Central Government*. Tume ile inakwenda kwenye Wilaya zetu, ikifika kwenye Wilaya ile Tume ni kama itapenda, lakini: Je, ikipenda imhusishe nani? Inakwenda kwenye Wilaya, inamkuta Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye anayesimamia Wilaya ile badala ya Rais kwa sababu Rais hawezi kuwa kwenye Wilaya zote kwa wakati mmoja. Inamwacha Mkuu wa Wilaya, inakuja kumchukua *Director of the Local Government Authority*. Inatoka kwenye mtiririko wa *Central Government*, sasa inakwenda inateremka kwenye *Local Government*. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hoja za wenzangu wanaokataa hazina mashiko. Kwa sababu moja, mtu anasema Mkuu wa Wilaya yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya. Lakini Rais ni Mwenyekiti wa Kamati ya Siasa ya Taifa, Kamati Kuu. Kwa hiyo, wote ni makada hawa. Huwezi kumkubali Rais, ukamkataa Mkuu wa Wilaya. Lakini hapo hapo kuna jambo sikulipenda. Wengi wanasema Mkuu wa Wilaya, hawakuwatendea haki wakati wa uchaguzi. Mnajuaje kama ma-DED wamewatendea haki watu wote wakati wa uchaguzi?

Kwa hiyo, ninavyoona, tunapomzungumzia DC na Mkurugenzi wa Wilaya twende kwenye uzito wa shughuli iliyopo mbele yetu. Tunakwenda kwenye Wilaya, tunamkuta Mkuu wa Wilaya ndiye Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye dola, ndiye mwenye vyombo vya ulinzi na hapo hapo hata Mkurugenzi anaweza akatumwa na Mkuu wa Wilaya. Lakini kosa kubwa hapa msichanganye mambo.

**MWENYEKITI:** Muda wako wa dakika tano umekwisha.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-move amendment, nimrudishe Mkuu wa Wilaya kama alivyokuwa na naomba Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono kwa faida ya Katiba, ambacho ni kitu kibwa sana.

**MWENYEKITI:** Haya ngojeni niwaorodheshe. Tunaanza na Mheshimiwa Wenje.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye marekebisho aliyowasilisha Mheshimiwa Anne Kilango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye sheria, hii *Principal Act*, alivyojaribu kueleza Mheshimiwa Lukuvi kwamba katika majukumu haya ambayo kwenye *section (5)* inasema: "Tume inaweza..."Maana yake ni kwamba hata Mkuu wa Wilaya akirudi hapa, siyo lazima Tume impe hii kazi ya kutengeneza hii mikutano. Hata tukimweka Mkurugenzi, mambo ni yale yale. Sasa nashindwa kuelewa, *where is the fear?* Uoga uko wapi tukimwacha Mkuu wa Wilaya, tukamweka Mkurugenzi jinsi Serikali ilivyopendekeza? *Where is the fear?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna *hidden agenda* kwenye hii sheria, tatizo liko wapi tukimwacha Mkurugenzi? Leo Watanzania wanaona tunapojadili hii sheria hatujagawana kwa misingi ya vyama vyetu vya siasa, lakini mgawanyo leo unakuja kati ya *reformers and non-reformers*. Watanzania wanaona ni akina nani wanataka mabadiliko ya kweli na akina nani wanataka *status quo*, yaani mambo yale yale. Kuna watu leo hapa wanaonekana kama *watermelon*, ndani ni *red*, nje ni *green*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba, kama kweli tuna nia njema, hii nia njema ambayo ameanza kuonyesha Rais toka mwanzo, hili suala la kuweka *Local Government Director* (Mkurugenzi wa Halmashauri) libaki hivyo hivyo. Hakuna uoga hapa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Hizi lugha hizi!

**MWENYEKITI:** Mimi shida yangu ni moja tu. Ninyi wote mngekuwa mnajadili mantiki ya kazi ya huyo mtu mnyemtaka ni nini, bila kumwingiza Rais, bila kutishana, bila kuwashirikisha watu ambao hawawezi kuingia humu ndani. Maana mnawashirikisha wananchi ambao hawawezi kuingia humu ndani! Tungeni sheria hapa, ndiyo ninachotaka. Naomba muwe *sober*.

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unayo hapo hii *schedule of amendment* ambayo Mheshimiwa Mbunge kutoka Same ameileta, ukiona (a) na (c); (a) inatutaka tu-substitute kwa *District Commissioner*, (c) inafuta kabisa (a) na (b) na ku-substitute kwa *District Administrative Secretary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa kina hapo ni kwamba *schedule* hii haiyo kwa sababu anachopendekeza kwenye (a) anakifuta kwenye (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba tuendelee na ibara nyingine kwa sababu tayari *schedule* hii inajifuta yenyewe. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Aah, siyo utaratibu! Hiyo *observation* uliyoifanya na wao watakujibu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ninaanza kupata wasiwasi. Naomba uelewe kitu kimoja na Bunge letu lielewe, kwamba tunapozungumza hapa, pamoja na kwamba sisi ni watunga sheria, tunatunga sheria kwa niaba ya watu na tunatunga sheria kwa niaba ya Watanzania wote wasio na vyama, wa dini zote, wa makabila yote, watu wote katika ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu kwenye kipengele hiki, ni kwamba tunakwenda kurudisha hofu ambayo tulikuwa tumeshakusudia wote kuiondoa. Narudia tena maneno niliyozungumza katika hatua za awali.

Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wote wanatuangalia, huwezi kupinga ukweli kwamba tukianza ku-politicize hii process ya katiba, hatutafika mwisho wa safari yetu salama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ulazima wa kuondoa vikwazo ambavyo tunavi-foresee, ni vyema tukafanya mapema. Tutashinda ndani ya Bunge, lakini tutashindana nje ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa nia njema kabisa, kwa nia njema kabisa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tu-argue kwa nini ibakie hivi au nini. Naomba tu-argue kwanza. Mheshimiwa Mbowe endelea. Ninachoomba ni kwamba tuzungumzie kwa nini kisikubaliwe hiki kifungu, ndiyo ninachoomba tuzungumze.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo tunajenga ambayo tunataka ieleweke, tunataka process ya kurekebisha na kuandika upya katiba yetu isiwe ni process ambayo ni partisan. Ukweli unabaki kwamba ma-DC by all standards ni ma-partisan katika process hii. Hilo ni moja.

La pili, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya wana-represent boards za Wilaya kwa misingi kwamba Baraza la Madiwani liko chini ya Mkurugenzi wa Wilaya. Kuondoa mamlaka haya kwa Mkurugenzi wa Wilaya na kuyapeleka kwa DC unawaondolea haki hata Madiwani na mfumo mzima wa utawala wa Wilaya. Ina maana tunapuza Local Government System.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 1982 inaeleza na Katiba ya mwaka 2010 inaeleza hata majukumu ya DC katika Kamati za Chama cha Mapinduzi na Kamati za siasa, kwamba ni pamoja na kusimamia interests za Chama cha Mapinduzi katika Wilaya. Kwa misingi hii, process itakuwa ni partisan. Sisi tunasema, jamani, kama tumekuja kuridhiana, kama tumefika hatua hii, ni kwa nini tunakuwa na hofu ambayo haina msingi kwenda kuchafua hali ya hewa katika nchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkumba.



**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Tunawaambia mtashinda kwa wingi hapa, lakini kwa *spirit* hii, hii safari ni ndefu, tunamhitaji kila mmoja wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkumba!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa katika *stage* hii! Mheshimiwa Nkumba, nimekuita!

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi narudi kwenye hoja, siendi mbali. Madhumuni ya maelekezo ya mabadiliko ambayo Mheshimiwa Mama Malecela hapa ameyaleta, yanaturudisha kutueleweshwa kazi hii ukubwa wake, lakini vile vile kutueleweshwa kazi za Mkuu wa Wilaya na kazi za Mkurugenzi, nani anaweza akafanya majukumu haya kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe wenzangu ambao pengine hawakai sana kule kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi ana vikao chungu nzima pale. Kwanza, ndiye msimamizi wa *Finance Committee*, yuko kwenye *Full Council*, yuko kwenye zabuni mbalimbali za pale Halmashauri, lakini pia ni msimamizi wa miradi mbalimbali, daraja likibomoka ni Mkurugenzi, Kamati ya LAAC ya Mzee Mrema huku anahitajika; muda huu wa kufanya kazi ya kusimamia hii Tume ataupata wapi huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapenzi ambayo tumempa Mheshimiwa Rais, naomba tuwape hawa Wakuu wa Wilaya. Kazi ni moja. Kazi ya Mkuu wa Wilaya pale ni kusimamia kwa karibu zaidi usalama na ulinzi wa amani na kusukuma shughuli za maendeleo basi. Ukimkabidhi kazi hii, hata hawa Wajumbe wa Tume watakuwa na usalama zaidi na mikutano hiyo itakuwa ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono maelezo. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Tuko kwenye Kamati, taarifa za wapi? Kila mtu aseme, tutampa nafasi.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Anakosea huyu! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, naomba ukae. Kwa sababu kila mtu hapa anaweza kutoa taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu hujanijibu!

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa kitu gani? Anaendelea kuzungumza, nitatoa mwongozo wa kufanya nini?

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Anne Malecela. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

Tupo kwenye Kamati ya Bunge Zima, kwa hiyo, hamwezi kupiga mwongozo, taarifa, nitatoaje tena!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kutokuunga mkono hoja iliyoletwa na Mheshimiwa dada yangu Anne Malecela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ambao umeletwa na Serikali kuweka kifungu cha kutoa Mkuu wa Wilaya na kuweka Mkurugenzi wametambua nafasi ya Wakurugenzi kwenye Halmashauri zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Wakurugenzi wana majukumu mengi sana, lakini pia ni Watendaji Wakuu wa shughuli zote za maendeleo kwenye Wilaya zetu, hilo tunalijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba baadhi ya Wakuu wa Wilaya wanatamka hadharani kwamba wao ni makada wa vyama. Wengi wanasema hivyo, ni makada, hawafichi! Hadharani kabisa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipeleka hili suala kisiasa, sidhani kama tutapata muafaka. Huu ni mwanzo tu wa mchakato wa kwenda kwenye katiba mpya. Tukianza kuingiza watu ambao wataleta *interest* za vyama, haitakuwa ni katiba ya wananchi wote, itakuwa ni katiba inayoangalia maslahi ya chama zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *spirit* ile ile ya kuanza vizuri kwenye mchakato wa kwenda kwenye katiba mpya, tuweke Watendaji wa Serikali na watumishi waweze kusimamia vizuri ili tuweze kupata katiba nzuri na Tume nzuri ya kuweza kuratibu maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sijaunga mkono hoja! (Makofi/Kicheko)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa nafuatilia hii, nilikuwa naona kwamba tunaleta mabadiliko kwenye *subsection (5)*. Sasa, napata matatizo kidogo. Nikisoma *subsection (5)* ambayo ndiyo sheria, inasema, Tume inaweza kwa Tanzania Bara, kumtaka Mkuu wa Wilaya, Afisa Mtendaji wa Kata ambaye yuko chini ya DED, Mtendaji wa Kata, Mtaa, Afisa Mtendaji wa Kijiji, *even at the bottom*, kuitisha mkutano. *Issue* hapa ni kuitisha mkutano. *I find it very difficult* kwamba tuna-*argue* kitu gani? *It's so difficult really* kwamba watu wazima tuna-*argue*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *practically*, hata kama ni Mkurugenzi umemtaja, bado Mkurugenzi hataitisha mkutano. Mkurugenzi kama anataka mkutano uitishwe, atawasiliana na Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa kitu gani na Kitongoji. Sasa, *I find it very difficult* kwamba tunatumia *five hours* ku-*discuss* kitu ambacho *in my opinion*, ni kidogo. Nakaa.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Shekifu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi namshukuru sana mzungumzaji aliyekaa sasa. Kwa kweli, kama ilivyosemwa, tunachohitaji kutumia hapa ni busara tu. Tukitumia busara sana, mimi sioni tatizo katika kifungu hiki. Yale mabadiliko yaliyoandikwa katika Muswada wenyewe ambao ulikuwa unawapa mamlaka Wakuu wa Wilaya yalifuata mfumo wa utawala. Mfumo wa utawala, Kiongozi Mkuu katika Wilaya ambaye anashika mamlaka na kuweza ku-*command* au kutoa maelekezo kwa walioko chini yake ni Mkuu wa Wilaya. Ukimchagua mwingine nje ya huyo, ina maana unavuruga utaratibu mzima.

Kwa hiyo, kinachozungumzwa hapa na Mheshimiwa Mama Anne Malecela ni kwamba hebu twende katika utaratibu na mfumo unaokubalika. Tukifuata hiyo, tutakuwa tumeleta kitu ambacho siyo kigeni. Kwa sasa sura inaonekana kwamba tunavutana kwa maslahi, lakini mimi siamini kwamba ni maslahi, kwa sababu mfumo unamtambua Mkuu wa Wilaya kama kiongozi katika ngazi ya Wilaya, tumpe heshima yake hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika sheria hii, imeandikwa: "inaweza" Kwa hiyo, inaweza isimchague Mkuu wa Wilaya, lakini kwa vyovyote kwa watu wenye busara, nami nilikuwa Mkuu wa Mkoa, wakija hawa watakuja kutoa heshima zao kwako. Sasa hawawezi kwenda kwa Mkurugenzi wakatoe heshima, halafu ndiyo waende kwa Mkuu wa Wilaya wakatoe heshima. Ni utaratibu tu wa kawaida ambao kwa kweli hautupeleki mahali popote pa kubadilisha jambo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Zanzibar hakuna Wakurugenzi, sasa tumweke nani ambaye ataandaa mkutano? Kwa hiyo, haya mambo tunaweza kuyaangalia katika ufinyu, lakini tukiyaangalia katika upana. Tunaona tunajenga nyumba moja, kwa nini tugombe fito?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba Wakuu wa Wilaya waendeleo kuwepo na hili suala ni dogo, tukubaliane. Ahsante sana. (Makofi)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sheria za maridhiano zina matatizo wakati fulani na ndiyo maana niliomba kwanza pale mwanzoni kama wanavyosema Wazee wanaonizidi umri kwamba tuwe na busara kwenye hili. Mimi nilipendekeza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, akasema kwamba nilikuwa katikati. Nilikuwa katikati kwa sababu ya kutafuta *compromise*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *option* ya pili, pengine kwa nia nzuri kabisa ni kutosema chochote pale kwa sababu maneno "yaweza" ni *discretion*. Hiyo *discretion* tuiachie Tume yenyewe kwa sababu naona kama hoja ya DC na DED ina matatizo kila upande. Aidha, tukubali kuangalia majukumu kwamba *okay*, katika mfumo wa Serikali tufuate mfumo wa Serikali au tufuate mfumo huu wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ni mshauri tu, watungaji wa sheria ni ninyi. Kwenye hili, lazima niseme ukweli kwamba kila upande una sababu nzito. Sasa hamwezi kung'ang'ania *positions*. Wazungu wanasema *don't negotiate from position*." Huwezi kumsalimia mtu aliyekunja ngumi, hamshikani mikono, itakuwa kama wakwezi. Anayekwea na anayeteremka, hawawezi kushikana mikono, maana mmoja ataanguka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba tukubali. Kama hatukubali, mimi ni mshauri tu, lakini pendekezo langu ni hili ambalo liko hapa. Lakini kama wengi wanafikiri kwamba DC ndiye anafaa, basi tumewasikiliza wachache, tumewasikia wanasema, lakini *let the majority have their way*, kitu ambacho kwa kweli wakati fulani kwenye sheria hizi siyo kizuri sana. Kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba mapendekezo yangu ni mawili na bado ninasema ninakuwa katikati, *either* tuwaweke wote wawili DC na DED, na Tume itafanya maamuzi kwa sababu neno tunalolitumia ni 'yaweza' au tuondoe yote mawili tuiachie Tume iamue nani ataisaidia.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu wote tutumie busara, kweli... (Kelele)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mnyamazeli! (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Tume kubwa kama hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango, naomba unisikilize. Mnapoongea, mkiniambia mimi inakuwa sawa sawa. Mkianza kuwaambia wengine huko mnaanza kufanya maudhi. Naomba uzungumze na wengine wasikilize. Endelea.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti sawa. Naomba niwasihi Wabunge, tuwe *practical*. Tume iliyoteuliwa na Mkuu wa nchi, inatoka inakotoka inafika Same, badala ya kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye Rais wa Wilaya ya Same, inateremka chini inakwenda kwenye Halmashauri. Ni kichekesho sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya ndiye Kiongozi wa Serikali Wilayani, hii Tume imeundwa na Mkuu wa Serikali ambaye ni Rais mwenye dola, Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, yeye ndiye yupo juu. Naomba kusema ukweli, hata Mkurugenzi anaweza akaagizwa jambo na Mkuu wa Wilaya. Tusiidhalilishe hii Tume ya Uchaguzi kiasi hicho. Bado naomba nisisimame kwamba Mkuu wa Wilaya ndiyo sahihi na ninaomba tupige kura.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha.

(Bunge lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Kwa sababu muda unafika mwisho namuomba Waziri wa nchi atuongeze kama dakika kumi ili kududi tuweze kufanya maamuzi ya busara.

Waheshimiwa Wabunge, ninachokusudia kufanya ni kwamba Kifungu hiki cha DC au Mkurugenzi nataka kukirejesha kwenye Kamati kwa sababu, kama nilivyosema, *the spirit* ya kupitisha Muswada imekuwa ni nzuri, na hapa tunapobishana, kwa sababu vichwani mwetu tumeweka mambo mengi sana ambayo hayapo katika dunia hii, lakini tumeyaweka wote pande zote, matokeo yake ni kila mtu anang'ang'aniana.

Nataka Kamati yangu iende ikazungumze mapendekezo aliyotoa Mwanasheria Mkuu kwamba ama tunaweza kuweka vifungu vyote, ama tunaondoa, maana yake inasema 'inaweza', siyo kwamba inasema 'ni lazima'. Kwa hiyo, ndiyo maana nataka kifungu hiki kiende kwenye Kamati tena, lakini nataka mnipe muda wa dakika kumi tupitisha kile kingine cha Mheshimiwa Simbachawene ili kusudi mwende mka-*negotiate intelligently* na busara. Hakuna cha ajabu hapa, ni ama mwondoe ama mwongeze.

Kwa hiyo, Waziri wa Nchi naomba niongezee muda dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako likubali kuongeza muda wa dakika kumi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Bunge liliongeza Muda wa Dakika Kumi ili Kuendelea na Kamati ya Bunge Zima)

#### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

##### **Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2011)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, tunapobadilisha vitu, mnatakiwa kutulia. Kama Wabunge hamna utulivu namna hiyo, hiyo siyo sahihi. Mimi sipendi kabisa tupige kura. Ndiyo maana nitatoa ruhusa kwa kifungu hiki, Kamati ikakae, mtoa hoja na wengine wanaopenda kuchangia waende ili mkasome vizuri. Kanuni ya Tano utawala bora. Mimi natumia Kanuni ya Tano kuendesha kikao vizuri. Tuendeleo na Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mimi nimeshafanya maamuzi, hamna taarifa tena.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu nadhani halina mgogoro mkubwa kwa sababu nilikuwa najaribu kuboresha tu kwenye Kifungu cha marekebisha ya Serikali sehemu ile ya (c) ambayo inazungumzia *in section 17* ukishuka unakwenda kwenye (c) kile cha (9) ni suala zima linalohusiana na utoaji wa elimu kwa umma. Hapa Serikali imekuja na *provision* nzuri tu inayotoa mwanya kwa watu wote kuhusika kutoa elimu wakiwepo hata watu mmoja mmoja. Lakini nimependekeza kwenye *schedule* yangu kwamba pale kwenye Kifungu kidogo cha (9) kinasema: "Any person who intends to conduct public awareness programme on the Constitution Review, pale yawekwe maneno 'and so recognised by the Commission shall in the case of...'"

Mantiki ya marekebisho haya ni kwamba angalau basi wawe wanajulikana, maana yake, kama kila mmoja atakuwa anakuja anasema mimi natoa tu taarifa halafu anakwenda kutoa elimu. Anakuja anasema nakwenda kutoa elimu, inaweza ikawa *chaos* kwamba isiwe rahisi kujua hawa wako wapi na wapi ikawa ni kitu kigumu kidogo.

Kwa hiyo, ndiyo maana nimetumia '*so recognised*', ningeweza kusema '*duly recognised*' lakini nimetumia neno '*so recognised*' ni kujulikana kwa kiasi cha kawaida tu cha kuorodheshwa tu, kwamba hawa wako mahali fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo na ile ya pili kabisa kwa sababu zipo kwenye kifungu kile kile. Napendekeza kwamba katika Kifungu cha 17 pale ukitoka tisa iongezee Kifungu cha 10 ambacho nakiongezee kipya na baadaye kile cha kumi kosomeke hivi: "*The notice referred to under sub paragraph (a) and (b) of sub section (9) shall specify time, date, place, venue and the nature of the subject matter of the awareness programme.*"

Hii itatusaidia kwamba unapokwenda kutoa elimu, tumesema hapa tuna zile tunu za Taifa. Kwanza nizungumzie kwenye muda na mahali, sehemu zetu za huko vijijini wakati mwingine unaweza kukuta watu wanafanyia shughuli hiyo kwenye mti mmoja tu katika sehemu ya Kijiji ndiyo ukumbi. Sasa kama hutasema lini utakuwa wapi, utafanya sehemu gani, mnaweza mkawa wengi mkagongana sehemu moja na huyu anayesimamia hili zoezi akapata shida sana.

Hii nyingine inayosema: "*The nature of the subject matter of the awareness programme*" mantiki yangu hapa ni kwamba, sasa basi angalau tuweze kulinda, maana mawazo yetu sisi ni *positive*, lakini anaweza akatokea mtoa elimu mwingine anakwenda kupotosha ile *positive thinking* tuliyonayo.

Tunasema tuna tunu hapa za Taifa, *National Values* tumezitaja kwenye *clause (9)* ambazo tunasema hapa kwamba Katiba yetu iweje. Mtu mwingine anaweza akaenda akazipinga hizi. Huyu tunasema *nature* ya elimu yake anayetaka kutoa sasa hapa inakwenda kinyume kabisa na ule utaratibu uliokuwa umewekwa.

Mantiki nyingine kwenye hii ni kwamba haiwezekani hata kama ni NGO'S au mtu binafsi ukawa mtalaam wa Katiba yote, basi angalau tuambiwe unataka kwenda kutoa elimu kuhusu haki za binadamu, unataka kwenda kutoa elimu kuhusu amani, maana kila mtu ana ujuzi wa jambo lake ndiyo mantiki ya haya marekebisho na mimi ningependa sana Wabunge katika hili mniunge mkono ili marekebisho yaweze kusaidia utendaji bora katika *level* hizo za chini za utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waliosimama ni Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi naunga mkono kabisa marekebisho ambayo Mheshimiwa Simbachawene ameyatoa, na hata katika mchango wangu niligusia eneo hilo la utoaji taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, tuna *experience* mbalimbali na hasa tukitolea mfano wa chaguzi zetu hapa. Taratibu zinakuwepo, lakini bado watu wanakiuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema mtu atoe taarifa halafu mpewa taarifa, ama DC, ama Mkurugenzi ambaye tumetoka kubishana hapa, hatujafikia muafaka, hana mamlaka ya kumwambia huyu mtu kwamba eneo fulani yupo Simbachawene kwa muda huu, wewe nenda kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tu, umeona hili zoezi lilivyo! Hapa kwenye hatua hii ya awali tu, huko mbele sijui itakuwaje! Tukiacha mambo bila kuweka uangalizi wa kutosha, haya mambo hayatafika. Ndiyo maana nimesema hivi, ni lazima kuwepo na angalizo na kitu ambacho

amesema Mheshimiwa Simbachawene hapa. Kama huku kuna watu wengine, huyu mwingine asubiri. Hapa tu tumeshindwa kuonyesha mfano, tukiacha hivi huko tunaweza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimuunge mkono Mheshimiwa George Simbachawene kwenye eneo hili la Muswada, amejaribu kuleta uwazi zaidi katika eneo hili. Mimi namuunga mkono, itasaidia sana wale ambao watashughulika na kuandaa ratiba ya ugeni huu kama kifungu hiki kitakuwa na uwazi unaopendekezwa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakuja kwa upande wa marekebisho ya Serikali kwamba ukishakubali aliyoyasema Mheshimiwa Simbachawene kwamba kile kilichokuwa Kifungu cha 10 na 11 sasa inakuwa Kifungu cha 11 na 12, mimi naangukia sasa Kifungu cha 11. Kwa upande wa Serikali kwenye *schedule of amendment* kipo kifungu kidogo cha 10. Ukikisoma Kifungu hiki cha upande wa Serikali wanasema: "*For the purpose of this section, an organisation...*" mpaka inafika mwishoni, "*to make their opinions on the Constitution.*" Sasa mimi natatizwa na *reference* hiyo. Watoe maoni yao kuhusu Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yenyewe, ukienda kwenye tafsiri ambazo zinatumiwa ukurasa wa saba...

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Tumwachie kwanza amalize.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachojadili Mheshimiwa Chenge hakipo kwenye *Schedule of Amendment* ya Mheshimiwa Simbachawene.

**MWENYEKITI:** Tukimsikiliza tunaweza kuelewa vizuri.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** No! Anajadili kitu ambacho hakipo kwenye mjadala!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, kila mtu tumsikilize na wewe una *opinion* zako. Tunagombana nini?

Mheshimiwa Chenge endelea. Uvumilivu kila wakati ni wa muhimu.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana ndugu yangu na mdogo wangu Lissu. Hiki ninachokisema kipo kwenye mapendekezo ya Mheshimiwa Simbachawene kwenye (c) ambayo inasema *renumbering sub-close* 10 ziwe 11 na 12, sasa hiyo huwezi ukakubali. Maana yake ni nini? Ni lazima uende sasa kwenye marekebisho yaliyoletwa na Serikali. Pale nilipata nafasi ya kusimama, sasa siwezi kusimama kila wakati kwa sababu nimepata nafasi sasa ya kuyasema haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yenyewe imetoa tafsiri ya neno *Constitution* kwa kutumia herufi kubwa (C) inasema: "*Means the Constitution of the United Republic of Tanzania of 1977,*" wananchi hawa hawaendi kutoa maoni kuhusiana na Katiba ya sasa, wanatoa maoni yao kuhusiana na ile Katiba mpya inayokusudiwa na ndiyo maana sheria inasema: "*Proposed Constitution, means an enactment of the Constitution Assembly which is the subject of the referendum.*"

Nilikuwa naomba Serikali, ili tusilite mkanganyiko katika eneo hili kwenye kifungu kidogo cha Mheshimiwa Simbachawene, namuunga mkono mapendekezo yake lakini katika ku-*re-number* nisingependa nisimame tena, lakini niseme kwamba tuseme *the Proposed Constitution*, watoe maoni yao kuhusu *Proposed Constitution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii inahusu ile *clause* iliyoongezwa namba Tisa, kwanza natoa angalizo tu kama bado tuna mjadala juu ya *DC* na *Local Government*, basi itabidi labda watakaokwenda kujadili pia wajadili hili eneo, maana yake limejaa *Director* na vitu kama hivyo. Hilo angalizo la kwanza.

La pili, ninavyoona hapa *tusi-over restrict* sana kutoa maoni. Unajua huu mchakato *is a political agenda! Whether* upende usipende, lakini Katiba ni siasa na maoni yatakuwa ni maoni mbalimbali ya watu mbalimbali. Kwa hiyo, watu wawe huru.

Mimi nimefurahishwa sana na ile *clause* namba 11 ambayo inatoa fursa kwa kundi lolote tu kuitisha mkutano kufuatana na utaratibu uliopo sasa hivi. Yaani unakwenda Polisi, unasema mimi nitakuwa na Mkutano Rugulu au Ng'wasinasi halafu unapiga mambo yako ya Katiba wananchi waseme hapana, ndiyo na wengine watakugunia. *To me is a political life*. Kwa hiyo, tusiwe tu *careful, too strict*, ili kuufanya mchakato wote uwe na fursa ya wananchi kuufurahia mambo haya na pia kutoa maoni yao. Hilo ndilo nilikuwa na-*suggest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiangalie ile *suggestion* yake siyo ku-*restrict* lakini *just is a mere information* watu wasigongane. Mimi sina tatizo nalo, lakini zaidi tuweke umuhimu kwa watu kuwa huru kama vile *clause* Na. 11 ya *section* inavyosema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *effect* ya mapendekezo ya Mheshimiwa Simbachawene ya kuongeza maneno, '*and so recognised by the Commission*' maana yake ni kwamba hawa wanaopeleka taarifa watambuliwe na Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with all due respect* kwa Mheshimiwa Simbachawene, haya mapendekezo yake hayaongezi chochote kwenye sheria, kwa sababu kifungu kidogo cha (9) kinachopendekezwa kwenye jedwali la marekebicho ya Serikali kinasema kwamba huyo anayetaka kufanya *programme* ya elimu kwa umma kama ni mtu binafsi apeleke taarifa kwenye Tume. Sasa kama ni mtu binafsi anapeleka taarifa kwenye Tume, si itabidi ajiandike jina jamani? Akijiandika jina si atatambuliwa na Tume? Sasa haya maneno '*and so recognised by the commission*', *is completely superfluous*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachozungumzwa hapa, watu wanafikiria mikutano, mikutano. Kinachozungumzwa hapa ni *program* ya elimu kwa umma. Inaweza kuwa kwa radio, kwa mabango, kwa *television*, kwa *seminar*, kwa *workshop* au kwa mikutano ya hadhara. Sasa wanafikiria hii maana yake ni mikutano ya hadhara, tutapigana huko. Hapana! *Is just a misconception*. Kinachozungumzwa hapa ni taarifa kwamba mimi nakwenda kufanya *seminar* kwenye Ukumbi wa Chimwaga tarehe fulani, basi. Haya maneno kwamba mpaka atambuliwe ni maneno ya watu ambao wanafikiria mikutano ya hadhara tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotezewa muda na watu ambao *they suffering from misconceptions*. Sasa pendekezo la 10 la kusema kwamba hiyo taarifa iseme mahali, siku, saa, *venue*, na nini, anayekwenda kutoa kwenye *television*, kwamba nitatoa *program* ya elimu kwenye *television* anasemaje kuhusiana na *place/venue*?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasheria hawana kiapo kama kile cha Madaktari. Lakini wana wajibu wa kufafanua vitu ambavyo havipotoshi. Kifungu ambacho Mheshimiwa Simbachawene anasema, nafikiri kinafanya *clarity*. Ni *clarity* kwa msingi kwamba hiki kifungu cha 10 sijakwenda bado kwenye yale ya juu pale. Kifungu cha 10 kama akifuta yale maneno '*sub paragraph (a) and (b) of*', akabakiza '*the notice refer to under subsection (9) shall specify time, date, place, venue and the nature of the subject matter of the awareness programs*', sasa Mheshimiwa Mbunge anatumia maneno ambayo mimi nilifundishwa nisiyatumie kwenye hadhara ya *misconception*. Nafikiri nitumie maneno ya kiungwana kwamba ukisema mtu anaugua maradhi ya *misconceive*, yaani hafikiri vizuri, kwa kweli ni lugha ambayo inaudhi na siyo vizuri kuitumia. Mimi nafikiri kwamba hii hai-*exclude* hizo ambazo wewe unataka ziwe *excluded*. Yaani hai-*exclude* hadhara. Unaweza kwenye *television*, sema basi utakwenda

wapi, useme *Hall* gani, ni sawa sawa kwa sababu kuna wave ya hasa vijana kufikiri kwamba unaweza kuwa na uhuru ambao hauna mipaka. Uhuru wako unaishia inapoishia pua yangu. Yaani ukiwa na uhuru mpaka hapa ni sawa sawa. Lakini *by the time* unagusa pua yangu sasa unaingilia haki zangu. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na utaratibu ambao unaleta vurugu. Wenzetu wamekaa wamefikiria mambo ambayo sisi hatukuwa tumeyafikiria, wameyaleta hapa, mimi naunga mkono hili. (Makofi)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilileta mapendekezo haya kwa dhamira njema. Sikusudii mapendekezo yangu yanifanye niwe na ugomvi na yeyote yule. Sikulelewa hivyo. (Makofi)

Kazi yetu ya Kibunge ni kutunga Sheria na mchango ndio huu na sababu yake nimeisema. Angalau huyu anayekuwa *notified* kwenye ile "(a) an individual notify the commission in writing or in that behalf, a director..." kama ilivyosema huku mbele, dhamira yake ni angalau basi wawe wanafahamika. Kwa sababu kila mmoja atajifanyia tu kwa vurugu, *you can not control*. Hawa watu, haya maoni yao, *these are just agents* tu wanakwenda kupeleka elimu. Hata hiyo elimu tuiwekee utaratibu basi, kwamba unakwenda pale, unasema bwana mimi naitwa fulani, nimetoka sehemu fulani. Ubaya wake uko wapi? *Where is the superfluous?* Iko wapi hiyo *the superfluous?* Kwa hiyo, niseme tu hiyo ndio ilikuwa *gist* ya hiyo. Lakini ya pili, ile mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwamba nitoe ile (a) na (b) kwa sababu inataja tu kile kitu kilichokuwepo, niendeleze tu pale kwamba *the notice referred to under subsection (9), shall specify time, date, place, venue and the nature of the subject matter of the awareness programs*. Lakini content yangu ya mwisho ni maneno yale, *shall specify time, date, place, venue and nature of the subject matter*. Nimeeleza msingi wangu na hauna mabadiliko yoyote. Naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Andrew Chenge alipokuwa anachangia, alipendekeza kwamba kwenye kifungu cha 11, yaani kifungu cha sasa kifungu kidogo cha 10 alipendekeza kuwe na maneno *Proposed Constitution* kwenye kifungu kidogo cha 10. Tunaomba marekebisho haya yaingizwe kwenye rekodi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina shida ya *time*. Nilioomba muda mfupi, nimepewa, sasa unaishiaishia. Ulitaka kusemaje Mheshimiwa Tundu Lissu? Kwa kifupi sana.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa *very brief*. Alichokisema Mheshimiwa Chenge hakipo kwenye *schedule of amendment* na namna pekee ya kurekebisha *schedule* au Muswada kwenye Kamati ya Bunge Zima *is by way of the schedule of amendment*. Haya yanayotakiwa kufanyika hapa ni mambo ya kienyeji. Tukianza kuruhusu mambo ya kienyeji wakati tuna Kanuni za Bunge, hili Bunge litakuwa *succours*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *succour, what it is* ndio kazi mliyonyayo. Katika taratibu zetu, mwenye hoja anaweza kuleta *amendment* hapa hapa. Lakini mtu mwingine yeyote inabidi alete kwa utaratibu huu. Kwa hiyo, ndio maana Mheshimiwa Chenge hakufanya *amendment*, *ali-caution* na aliposoma Mwanasheria Mkuu ambaye ndio mwenye hoja, akasema nakubaliana na maelekezo yale. Lakini yule haku-*amend* anayetoa *amendment*, ni huyu mwenye hoja yake kitu ambacho kinakubaliwa. (Makofi)

(Bunge lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hii hoja katika ngazi ya Kamati ya Bunge Zima, hatujaimaliza. Kwa hiyo, simwiti Mtoa Hoja aseme lolote kwa sababu hatujaimaliza. Sasa ombi langu kwa sababu, kama tulivyosema, Waheshimiwa Wabunge tunao wajibu wa kitaifa, tunayo *responsibility* ya kuweza ku-*guide* utaratibu mzima wa mchakato wa Katiba. Itakuwa ni kitu cha ajabu sana sisi tubishane kwenye kitu kidogo sana ndio maana sikubali kupiga kura hapa. Kwa sababu tutaipelekea nchi ielewe kwamba kuna jambo kubwa kabisa wakati halipo. Kama kweli mnasoma Sheria ninyi Wanasheria wote mlioko humu ndani, Tume inaweza, neno inaweza ina *options* nyingi sana.



Sasa napenda Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala Bora wakae tena jioni hii wakafanye makubaliano nini tuandike. Ama tuondoe kabisa ama tuweke vyote, lakini hapa hatupigi kura. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo haya, naomba Kamati yangu iende ikafanye kazi. Ndio gharama za demokrasia. Lakini tunataka umoja wa Taifa ubakie pale kwa sababu sisi ni mafundi sana wa kuwadanganya wananchi kama ni jambo kubwa kabisa la kutisha.

Hili jambo ni dogo kabisa na naomba mkasome Sheria. Siyo mkaanze kubishana, hizi fikra zenu za uchaguzi wa mwaka 2010 au vinginevyo. Hii tunazungumzia jinsi Tume itakavyofanya kazi yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Margreth Sitta, anaomba Wajumbe wa Kamati yake, wakakutane sasa hivi katika Ukumbi wa Pius Msekwa na hawa wengine tulikuwa tunapendekeza Ukumbi Na. 231.

Tafadhali Waheshimiwa Wabunge wanaohusika naomba mkafanye kazi hiyo na wengine wanaotaka kwenda kusaidia waende. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.55 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 10 Februari, 2010 saa tatu asubuhi)*